

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi na Nane- Tarehe 27 Aprili, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa TatuAsubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU WA MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MHE. VICK P. KAMATA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Swali letu la kwanza, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kadutu.

Na. 144

**Tatizo la Mawasiliano ya Simu Katika Jimbo la Ulyankulu**

**MHE. JOHN P. KADUTU** aliuliza:-

Jimbo la Ulyankulu linakabiliwa na tatizo la mawasiliano ya simu hasa katika Vijiji vya Ibambo, Mwongozo, Ichemba, Kanoge, Illege, Busanda, Bulela, Ikonongo, Igombemkulu na maeneo mengi:-

Je, ni lini kampuni za simu zitamaliza tatizo la mawasiliano katika Jimbo la Ulyankulu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliingia Makubaliano na Kampuni ya Mawasiliano ya Viettel ya Vietnam (*Halotel*) kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania yasiyokuwa na mvuto wa kibashara ikiwa ni pamoja na maeneo ya Vijiji vya Ibambo, Mwongozo, Illege, Bulela na Ikonongo. Utekelezaji wa kuleta mawasiliano ya simu kwa miradi hiyo umekamilika ambapo minara imejengwa katika Vijiji vya Ibambo, Keza na King'wangoko. Hata hivyo, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itahakikisha maeneo yote yanapata huduma hiyo muhimu kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Lihemba, Kanoge, Busanda na Igombemkulu vitaainishwa na kuingizwa katika orodha ya miradi ya kuwapatia mawasiliano inayosimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itakayotekelezwa siku za usoni kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kadutu.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kabla sijaauliza maswali mawili ya nyongeza, naomba tufanye marekebisho kidogo kwenye majina ya vijiji, kijiji kinaitwa Ichemba na wala siyo Lihemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile minara hii inajengwa kwa umbali mrefu karibu kilometa 30 kwenda mnara mwengine, je, Serikali kwa kushirikiana na makampuni haya iko tayari kuongeza minara mingine katikati ili kuongeza upatikanaji wa mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwenye jibu ametaja mchakato wa ujenzi au kutengeneza minara katika Vijiji vya Ichemba, Kanoge, Busanda na Igombemkulu utafanyika siku za usoni. Kwa Kiswahili rahisi ukisema siku za usoni maana yake haijulikani ni hata baada ya miaka 10, 15 ni siku za usoni. Je, Serikali sasa iko tayari kueleza muda maalum badala ya kutuambia habari za siku za usoni? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Kadutu kwa sababu pamoja na mambo mengine tumekwishawasiliana kuhusu masuala ya mawasiliano kwenye jimbo lake na nilimweleza vizuri tu hatua mbalimbali ambazo Serikali imeendelea kuzichukua. Kawaida umbali kati ya mnara na mnara katika eneo ambalo halina milima mlingi sana ni *radianc*e ya kilometra 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imeendelea kuweka umbali wa *radianc*e ya kilometra 60 kwa sababu umbali huo unarahisisha kuweka mnara mwingine umbali wa kilometra hata 60 kama hakuna millima. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Kadutu kwamba umbali wa minara kama ye ye anapata kwa kilometra 30 ni kwa sababu maeneo yaliyopo yana milima milima na tutajitahidi kuangalia sehemu zote ambazo hazipati mawasiliano tusogeze minara mingine ili wananchi waweze kupatiwa mawasiliano kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini miradi kwenye vijiji viliviyotajwa pale itapatiwa mawasiliano. Kwa sasa hivi tunaorodhesha vijiji na kata mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya nchini mwetu kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Hivi ninavyoongea tumeepanga tufanye ratiba ndefu ya miezi miwili baada ya Bunge la Bajeti kwa ajili ya kupima kwa kutumia *GPS* na kuweka alama ni wapi tutaweka minara kwa ajili ya kuwezesha wananchi wa Tanzania wote waweze kupata mawasiliano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kuna mwingiliano mkubwa wa njia za mawasiliano hasa *SafariCom* kwenye Jimbo la Vunjo, Rombo na maeneo yanayozunguka mipakani. Serikali ina mkakati

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

gani, labda washauriane ili kuweza kuona mwingiliano huu unaondoka namna gani kwa sababu wewe mtumiaji unalazimika kuingia kwenye *roaming* bila wewe mwenyewe kutaka na inasababisha gharama kubwa?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri majibu, Mheshimiwa Dkt. Kafumu na Mheshimiwa Shekilindi wajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maeneo mengisana ya nchi yetu hasa yale ya mipakani kumekuwa na mwingiliano mkubwa sana wa mawasiliano katika ya hizo nchi jirani na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na *TCRA* tumeendelea kuyaainisha maeneo hayo kwa ajili ya kuongeza nguvu minara yetu na kuzuia *frequency* ambazo ni mtambuka kutoka nchi moja kwenda nyingine kuhakikisha tunazidhibiti ili Watanzania wapate mawasiliano ya Tanzania na nchi jirani ziedelee kupata mawasiliano kutoka nchi hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kafumu ajiandae Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jimbo la Igunga kama liliyo Jimbo la Ulyankulu, tuna kata kadhaa ambazo bado hazina mawasiliano. Kata hizo ni pamoja na Kiningila, Isakamaliwa, Mwamashiga, Mtunguru na Kata ya Mwashiku Jimbo la Manonga. Ni lini basi Serikali itasaidia ili wananchi hawa waweze kupata mawasiliano? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE - NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Dalaly kwa sababu mara nyingi sana

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

tumekuwa tukikutana ofisini kwa ajili ya kuongelea kata zake  
hizo alizozitaja ambazo ni kweli hazina mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru vilevile  
kwamba ameshatuandikia hata kwa maandishi na hii taarifa  
yake tayari iko kwa watu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa  
Wote ambao tumekubaliana kwamba mwezi saba mpaka  
wa tisa tutakuwa na ziara nchi nzima kuhakikisha tunaweza  
mawasiliano ya eneo hilo. Namhakikishia tu Mheshimiwa Dkt.  
Kafumu kwamba nitakapokuwa nakwenda maeneo ya  
Igunga nitamtaarifu ili tuwe wote kutembelea maeneo haya.  
Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa  
Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona ili niweze kuuliza swali dogo  
la nyongeza. Kwanza kabisa nimshukuru Naibu Waziri,  
Mheshimiwa Nditiye kwa kutuma wataalam wake kwenda  
kubaini maeneo ambayo hayana minara katika Jimbo la  
Lushoto. Je, ni lini sasa utekelezaji utaanza ili wananchi wa  
Lushoto waweze kupata mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu,  
anataka kujua ni lini tu, halafu jiandae Mheshimiwa Joyce.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye swali la  
msingi na kama nilivyoeleza kwenye maswali mengine ya  
nyongeza, Mheshimiwa Shekilindi kuanzia mwezi wa Saba  
baada ya Bunge la Bajeti nitafanya ziara ndefu sana ya  
kutembelea maeneo yote yenye changamoto za  
mawasiliano nikiambatana na timu ya Mfuko wa  
Mawasiliano kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika nitafika jimboni  
kwake na pia nitafika kwa Mheshimiwa Nape naye ambaye  
najua kabisa anasumbuka sana kuhakikisha tu kwamba  
mawasiliano kwa nchi yetu yote yanapatikana bila tatizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joyce.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Tatizo hili linafafana kabisa na tatizo la Kijiji cha Ngarasero katika Jimbo la Ngorongoro, Mkao wa Arusha. Je, ni lini Serikali itapeleka minara katika eneo hilo ili wananchi waweze kupata mawasiliano katika Kijiji cha Ngarasero?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, kwa kifupi.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE - NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Ngorongoro ni moja kati ya maeneo ambayo nayo yana changamoto ya mawasiliano. Kwa baadhi ya sehemu ambazo zina changamoto, tayari tumekwishatuma watu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwenda kufanya tathmini ya mahali gani panatakiwa kwenda kuwekwa minara kwa ajili ya kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pindi watakapotuletea taarifa, tutatangaza tenda ili makampuni mbalimbali ya simu yajitokeze kwa ajili ya kujenga minara ili kutatua changamoto hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante ameshakuelewa. Tunaendelea na Wizara hiyohiyo na swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

Na. 145

**Kero ya Cable za TV**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Kumekuwa na kero kubwa kwa wananchi wanaotumia huduma za *Cable TV* hasa Dodoma *Cables*; wananchi wanalipia lakini hawapati huduma ipasavyo:-

Je, ni lini Serikali itawadhibiti na kwa namna gani baadhi ya *Service Providers* kama hawa ambao wamekuwa wakiwadhulumu wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) imetoa leseni ya kutoa huduma za *Cable* kwa kituo cha Dodoma *Cables* ambapo kinatakiwa kiendeshwe kwa kufuata sheria na kanuni zinazohusu masuala ya utangazaji. Ili kukidhi ubora wa huduma za *cable*, *TCRA* imekuwa ikifuatilia maudhui na inafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye vituo hivi kuangalia kama mitambo inakidhi vigezo vya utoaji wa huduma bora na ya uhakika kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la *Cable TV* linahusu kuwepo kwa mtandao wa waya kutoka kwa mtoe huduma (*cable operator*) kwenda kwa wananchi, kuna wakati kumekuwa na changamoto za kukatika kwa nyaya ambapo wananchi wanapaswa kutoa taarifa kwa mtoe huduma ili apate msaada wa kiufundi pindi anapokuwa hapati huduma za matangazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, *TCRA* imeweka mfumo wa kupokea malalamiko ambapo kama mwananchi atakuwa hapati huduma bora na stahiki anatakiwa kutoa taarifa kwa mtoe huduma na pindi asipopatiwa huduma kama alivyoahidiwa na mtoe huduma, mwananchi anatakiwa kupeleka malalamiko yake katika Ofisi za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ambayo kawaida huyapokea na kuyafanya kazi ili kulinda maslahi ya wananchi na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na stahiki kwa malipo waliyotoa kwa mtoe huduma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri. Nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa usumbufu umekuwepo kwa watumiaji wa hizi *cable* hasa hii *Cable* ya Dodoma, mtu ushaharibikiwa inabidi uende *trip* mara mbili, mara tatu kuripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu aliyonijibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba inabidi uende tena Ofisi ya Mamlaka ya Mawasiliano ukatoe ripoti, hizo ni gharama na ni usumbufu. Kwa nini Serikali isiweke kitu kama *hotline* ikiwa mtu unaposumbuliwa na mambo kama hayo unapiga ukapata ripoti ili kuhakikisha kwamba mtumiaji anapata haki kwa ile pesa yake aliyoitao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu lingine ni vile unavyokwenda kutaka kuijunga na hizi *cable* unaahidiwa utapata *channel* kama 200 au 300. Inapokuja kwenye hali halisi ukijaribu kutafuta *channel* nydingi unaambiwa *access denied*, sasa huu kweli si wizi wa kiwaziwazi? Je, Serikali inadhibiti vipi kuhakikisha kwamba mtumiaji anapata haki yake kwa pesa alioilipia? Nahisi bado Mamlaka ya Mawasiliano inatakiwa izidishe udhibiti kwenye vyombo hivi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumtaarifu tu Mheshimiwa Asha kwamba huwa zipo *hotline* lakini kwa kweli sasa hivi sipo nazo kichwani. Baada ya muda tukikuta tu hata pale *canteen* nitakuwa nimeshazipata kutoka kwa watu wa *TCRA CCC* na kumpatia ili kuweza kuwasiliana na watu ambao wako pale kwa ajili kuhudumia wateja.

Mheshimiwa Mwenyeki, swali lake la pili ni kuhusu *channel* chache kuliko zinavyopaswa, hiyo inahusika na masuala ya ving'amuzi. Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Asha kwamba Serikali kupia *TCRA* tunaendelea kuwahakiki hawa wanaotoa huduma za TV. Kuna leseni mbalimbali, leseni kama *DSTV* wale wako wazi kabisa kwamba *channel* za bure ni mbili au tatu lakini kwa mfano hivi ving'amuzi vingine kama *Dodoma Cable*, sijapata uhakika Mheshimiwa Asha wana *channel* za bure ngapi na kwa zipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakapopata uhakika nitakuwa na nafasi nzuri sana ya kukujibu lakini tuna uhakika na kama Serikali tunafahamu kwamba kuna baadhi ya *cables* ambazo zinatakiwa zitoe *channel* za bure na zile ambazo hazittoi *channel* za bure tunazifua tilia kwa karibu ili tuweze kuzifungia kama zinakiuka masharti.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyeki, nakushukuru kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kirefu cha LUKU ni Lipia Umeme Kadri Utumiavyo. Kwenye ving'amuzi kwa nini Serikali isikae na watoa huduma ili mtumiaji alipie kadri anavyotumia badala ya kulipia kwa mwezi awe ametumia au hajatumia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE - NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya makampuni yanayotoa huduma za *cable* kwa ufupi huwa yanafanya biashara na huwa yanalenga katika kupata faida. Nimhakikishie Mheshimiwa kwamba tumelipokea wazo lake hilo na tutalifanya kazi kama Serikali tuone namna nzuri ya kulitekeleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, swali namba 146 limeondolewa kwenye orodha ya maswali. Sasa, tunakwenda swali namba 147, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha.

Na.147

**Kiwanda cha Nguo cha MUTEX**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA (K.n.y. MHE. MARWA R. CHACHA)** aliuliza:-

Kiwanda cha Nguo cha *MUTEX* cha Musoma Mjini amepewa mwekezaji lakini mpaka sasa hakifanyi kazi vizuri:-

Je, ile ahadi ya Rais kurudisha viwanda visivyofanya kazi ipo katika hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *Musoma Textile Mills Limited* kilianza uzalishaji mwaka 1980 kikiwa na uwezo ulioewekezwa wa mita millioni 22 kwa mwaka. Bidhaa zilizokuwa zinazalishwa kwa kutumia pamba inayolimwa nchini ni kanga na kitenge. Kiwanda hiki kiliwekwa kwenye utaratibu wa kufilisiwa mwaka 1996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na madeni makubwa ya benki, zoezi la ufilisi lilichukua muda mrefu na kukamilika mwezi Juni, 2006 ambapo kiwanda husika kilibinafsishwa kwa utaratibu wa ufilisi kwa Kampuni ya *Lalani Group 2006*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Lalani Group* ilifanya ukarabati wa kiwanda na kuanza uzalishaji ambao haukudumu kwa muda mrefu. Mwezi Mei, 2008, Kampuni ya *Lalani Group* iliuzala mali za *MUTEX* kwa *Tanzania Commodities Trading Company* ambayo ni Kampuni tanzu ya Kampuni ya Mohamed *Enterprise Limited*. Mauzo hayo yalifanyika katika makampuni hayo mawili kutoka utaratibu ambao haukuhusisha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kilifanyiwa ukarabati na uzalishaji wa kanga na kitenge ukaanza mwaka huohuo wa 2008. Uzalishaji umekuwa siyo wa kuridhisha kutokana na kuwepo kwa ushindani mkubwa katika soko la bidhaa kama hizo zinazozalishwa na zinazotoka nje ya nchi. Ilipofika mwaka 2016, kiwanda cha *MUTEX* kilisitisha uzalishaji kutokana na ushindani kuwa mkubwa na hivyo kutokufanya vizuri katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto hiyo, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Kilimo, ziliandaa Mkutano wa Wadau wa Nguo na Mavazi tarehe 20 Aprili, 2018 ili kujadili changamoto zinazoikabili sekta hiyo ambayo ni muhimu sana kwa ajira na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muafaka ulifikiwa kuhusu suala la ushindani usio wa haki katika soko kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania iimarishe udhibiti wa bidhaa za nguo kutoka nje na kutoza kodi stahiki kwa mujibu wa sheria na viwango vilivyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza agizo la Rais, tumekubaliana na mmiliki wa kiwanda cha *MUTEX* na ameahidi kuwa katika kipindi cha miezi miwili uzalishaji utaanza. Aidha, kiwanda kimeandaa mpango wa kupanua shughuli zake kwa kuwekeza kwenye mitambo ya kuzalisha vitambaa vya aina ya *Denim* (*Integrated Denim Manufacturing Facilities*) vinavyotumika kutengeneza mavazi aina ya *jeans* katika kukabiliana na ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kumfuatilia mwekezaji huyu na kuhakikisha kuwa anazalisha kama alivyoahidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mara nyingi tunasema majibu ya Serikali yawe mafupi. Mnakuwa na majibu marefu sana na muda wetu leo saa 4.00 tunatakiwa tuwe tumemaliza maswali.

Tunaendelea na Mheshimiwa Salome na Mheshiniwa Boniface ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ya viwanda Tanzania ni gharama kubwa za uzalishaji katika viwanda hivi. Serikali ina mpango gani wa kuweka mazingira wezeshi ili kupunguza gharama kama kuboresha miundombinu na kutengeneza mazingira mazuri ya kilimo cha malighafi kama pamba kwa ajili ya uzalishaji wa viwanda hivi? Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira hayo ili wawekezaji hasa kwenye viwanda vya nguo waweze kupata gharama nafuu za uzalishaji zitakazopelekea wao kupata faida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, viwanda vingi vimekuwa vikikwama kwa sababu ya kukosa mitaji. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuzungumza na mabenki ambayo yanatoa mikopo kuweka riba nafuu kwenye viwanda ili waweze kupata pesa kwa ajili ya kufanya biashara? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza hapo awali, Serikali kwa kutambua changamoto

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

zilizopo ndiyo maana ilikuwa imeitisha kikao na wadau ili kujadili na kuweza kubaini changamoto hizo na hivyo ipo mbioni katika kuzifanya kazi ikiwemo kuangalia mazingira ambayo yanafanya bidhaa hizo zisiwe na ushindani wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mitaji, ni kweli kwamba kuna baadhi ambao wanahitaji kuwekeza lakini suala la mitaji hasa katika uwekezaji binafsi ni jukumu la mwekezaji mwenyewe. Kwa upande wa Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wanaweza kulima pamba iliyo bora zaidi, lakini pia wanastahili wapate faida inayostahili kutokana na kilimo chao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniface.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii. Wilaya ya Bunda ni moja ya wilaya zinazolima pamba sana kwa Mkoa wa Mara. *Ginneryya* Buramba na Ushashi baada ya kilichokuwa Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Mara kufa au kufilisika, zilikabidhiwa mufilisi. Ni lini sasa Waziri atafika kuangalia zile *ginnery* mbili ambazo zimekabidhiwa mufilisi muda mrefu na ziko taarifa kwamba mufilisi ameuza kila kitu na vile viwanda vimetelekezwa? Ni lini Waziri atafika pale kuangalia makabidhiano yaliyokuwepo ya *Mara Corp* na hali ilivyo kwa sasa kwa *ginnery* hizo mbili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Chumi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kumaliza Bunge. (*Kicheko/Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali

kwamba wawekezaji binafsi wafanye jitihada wenyewe za ku-access mikopo, naomba kuuliza ni lini Waziri atatembelea viwanda vya Mafinga ambavyo vimeitikia kwa wingi sana katika suala la uchumi wa viwanda ili kuzungumza na wenye viwanda kuhusu changamoto na fursa mbalimbali za mikopo ya riba nafuu inayopatikana kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi kama mwanzo. (*Kicheko/Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kwenda Mara nitaelekea Mufindi. (*Kicheko/Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Munira.

**MHE. MUNIRA M. KHATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kiwanda cha Urafiki hakizalishi kwa kiwango kinachotakiwa na kiwanda hiki kinamilikiwa na Wachina. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kiwanda hiki kinamilikiwa na Serikali ili kuongeza uzalishaji na kupata ajira kwa vijana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Urafiki kimsingi kinamilikiwa na Wachina na kuna hisa ambazo ni za Serikali. Tumekuwa tukiwasiliana juu ya uboreshaji wa kiwanda hiki na kuhakikisha kwamba tunazalisha kwa kiwango kikubwa zaidi, hata hivyo, bado uzalishaji hauridhishi. Kwa hiyo, Serikali bado inaendelea kulifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, muda wetu ni mdogo, tunakwenda Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa James Mbatia.

## **Huduma za Afya Zinazotolewa kwa Ubia Nchini**

**MHE. JAMES F. MBATIA** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa huduma ya afya nchini kwa ubia na Mashirika ya Dini na/au Taasisi Zisizo za Kiserikali:-

(a) Je, ni kwa asilimia ngapi ya ubia huo kwa kila upande kati ya Serikali na Mashirika ya Dini au Serikali na Taasisi nyingine Zisizo na Kiserikali?

(b) Kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita ubia huu umepata mafanikio kiasi gani na kwa kutumia vigezo gani kwa Hospitali ya Kilema?

(c) Kwa kipindi hicho tajwa hapo juu, je, ubia huo umepatwa na changamoto kiasi gani kwa kutumia vigezo gani kwa Hospitali ya Kilema?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania inatambua mchango wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya hapa nchini. Aidha, Serikali kwa kutambua mchango wa sekta binafsi ilitunga Sera ya Ubia kati za Sekta ya Umma na Binafsi, (*Public Private Partnership, 2009*) pamoja na Sheria Na.103 ya mwaka 2010 iliyorejewa mwaka 2014 na kanuni zake za mwaka 2011 ambazo zimerejewa mwaka 2015.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Machi 2018, jumla ya vituo vyatolea huduma vilivyopo ni 7,215 (vyatolea

umma vikiwa ni 5,361 sawa na asilimia 74 na sekta binafsi ni 1,854 sawa na asilimia 26). Aidha, kati ya vituo binafsi 1,854, vituo 900 sawa na asilimia 13 vinamilikiwa na Mashirika ya Dini. Kati ya vituo hivyo vinavyomilikiwa na Mashirika ya Dini ambavyo vimesaini makubaliano ya kutoa huduma za afya baina ya Serikali na Mashirika ya Dini ni 130 sawa na asilimia 1.8 ambapo hospitali ni 85, vituo vya afya na zahanati ni 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inadhihirisha kwamba sekta binafsi ina mchango mkubwa katika utoaji wa huduma za afya hapa nchini. Aidha, takribani asilimia 40 mpaka 70 ya gharama za uendeshaji wa Hospitali za Mashirika ya Dini zinatoka Serikalini kwa ajili ya mishahara ya watumishi, dawa, vifaatiba pamoja na gharama nyingine za uendeshaji wa hospitali hizi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Kilema ilianza kutumika kama Hospitali Teule ya Halmashauri ya Moshi Vijijini mwaka 1984. Katika kipindi hiki kuna mafanikio mengi yaliyopatikana ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi;

(ii) Kuongeza idadi ya vifaatiba ambavyo vimeboresha utoaji wa huduma;

(iii) Hospitali hii ina jumla ya watumishi 156 walioajiriwa na Serikali ambao wanafanya kazi katika hospitali hii;

(iv) Watoa huduma hususani Madaktari wameongezeka hadi kufikia watumishi tisa; na

(v) Wanapata mgao wa madawa kutoka *MSD*.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki chote ambapo Hospitali ya Kilema imekuwa ikitumika kama Hospitali Teule imekuwa ikipata changamoto ambazo zimekuwa zikitatuliwa kwa pamoja kati ya Serikali na mmiliki

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

ambaye ni Jimbo la Moshi la Kanisa Katoliki. Baadhi ya changamoto hizo pamoja na kufanyiwa kazi kwa kushirikiana ni ufinyu wa bajeti; upungufu wa watalaaam pamoja na uwekezaji katika hospitali hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama Mheshimiwa Waziri alivyosema ni kwa kweli hospitali hizi zinafanya kazi kubwa sana, lakini hali ilivyo sasa tangu Septemba, 2013, hospitali hizi hazijapewa ruhusa ya kufanya ajira mpya wala ajira mbadala na watumishi wapo pungufu zaidi ya asilimia 50. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuangalia hospitali hizi hasa Hospitali ya Huruma, Kilema, Machame mpaka kule Karatu ambazo zina upungufu wa watumishi kwa zaidi ya asilimia 50?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, mkataba kati ya Hospitali ya Rufaa ya *KCMC* na Bugando tangu Septemba, 2017 haujakamiliika au haujafanyiwa kazi ambapo hospitali hizi haziendeshwi vizuri inavyotakiwa na ni hospitali za rufaa. Je, ni lini Serikali itakamilisha utaratibu huu wa mkataba kati ya Serikali na Mashirika haya ya Dini hasa Hospitali ya Bugando na *KCMC*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana, wewe ni mtaalam wa kila kitu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba baadhi ya hospitali ambazo zimetajwa zimekuwa na changamoto ya rasilimali watu na kadri tunapopata uwezo tumekuwa tunapeleka watumishi. Tunatarajia baada ya Bunge hili la Bajeti tutapata watumishi wa ziada ambapo katika hospitali hizi za *DDH* na sisi tutapeleka watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swalii la pili ameongelea suala la mikataba. Ni kweli Serikali imekuwa inapeleka rasilimali watu na fedha, lakini tumekuwa

tunapata changamoto katika baadhi ya hizi hospitali katika usimamizi wa fedha na rasilimali watu ambao tumepeleka. Sasa hivi Serikali inafanya mapitio na pale mapitio haya yatakapokuwa yamekamilika, basi tutaingia mkataba ili tuweze kusimamia vizuri rasilimali fedha za Serikali na watumishi ambao tunawapeleka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali inatoa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi kwa vijana wetu wenye umri wa miaka tisa mpaka 14. Je, baada ya kupatiwa kinga hizo vijana wetu wasichana iwapo watakuwa wanafanya ngono zembe, kinga hiyo itaendelea kumkinga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nitoe maelezo kidogo kuhusiana na saratani. Serikali imezindua...

**MWENYEKITI:** Siyo sana Mheshimiwa Waziri, najua wewe ni mtaalam.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imezindua chanjo dhidi ya saratani ya shingo ya uzazi na tumejielekeza kwanza kwa mabinti wote wa miaka 14 na baada ya hapo tutakuja mabinti wa miaka tisa mpaka 13 na baada ya hapo tutakuja mabinti wa miaka tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zimejionyesha kwamba vijana wengi wanaanza kujamiiana wakiwa na umri mdogo, chanjo hii itawakinga mabinti dhidi ya saratani ya shingo ya uzazi, haitawakinga mabinti dhidi ya magonjwa mengine ya kuambukiza kama vile magonjwa ya kaswende, kisonono pamoja na UKIMWI.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wanaotusikiliza, chanjo hii ni salama na lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaondokana kabisa na saratani ya shingo ya kizazi ambayo inawaathiri wanawake walio wengi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye.

Na.149

**Kupeleka Madaktari Bingwa katika Hospitali  
ya Rufaa ya Mkoa - Kigoma**

**MHE. KIZA H. MAYEYE** aliuliza:-

Kukosekana kwa Madaktari Bingwa na wataalam wengine katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma kunafanya wagonjwa wengi kupewa rufaa ambazo zingeweza kushughulikiwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Madaktari Bingwa na wataalam wengine wa kutosha katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma inahitaji Madaktari Bingwa wa fani mbalimbali ili iweze kutoa huduma za kibingwa. Aidha, Wizara inatambua kuwa, katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma kwa sasa ina Daktari Bingwa mmoja tu katika fani ya watoto.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuzihamisha Hospitali za Rufaa za Mikoa kuwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Serikali inaendelea na zoezi la kufanya tathmini ya kina kujua hali halisi ya Madaktari Bingwa na fani zao katika hospitali zote za mikoa, kanda, hospitali maalum na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha tathmini hii, Wizara itawapanga upya Madaktari Bingwa kwa uwiano kulingana na mahitaji ya hospitali za mikoa, kanda maalum pamoja na Taifa. Lengo ni kuwa hospitali ya mkoa iwe na Madaktari Bingwa ikiwemo pamoja na Hospitali za Rufaa ya Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Serikali imegharamila mafunzo ya Madaktari Bingwa 125 ambao wameingia mkataba wa kutumikia katika maeneo watakayopangiwa baada ya kuhitimu masomo kwa lugha ya kitaalam *bonding*. Mkoa wa Kigoma utakuwa ni moja ya mikoa itakayonufaika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kiza.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, ametupa faraja watu wa Kigoma. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Hospitali hii ya Mkoa wa Kigoma ya Maweni ni hospitali kubwa ukizingatia Kigoma tuko mpakani, inahudumia wananchi zaidi ya milioni mbili, lakini mpaka sasa hatuna vifaa muhimu kama *CT-scan* na vile vya kupimia saratani ya kizazi kwa wanawake. Naomba majibu ya Waziri, ni lini mtatuletea vifaa hivi katika hospitali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mkoa wa Kigoma umekuwa ukikumbwa na changamoto nydingi za magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu hasa katika

Wilaya yangu ya Kigoma Vijijini. Nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha wanamaliza tatizo la kipindupindu ndani ya Mkoa wa Kigoma? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, S wali lake la kwanza ameuliza ni lini Serikali itapeleka mashine ya *CT-scan* na vipimo vya kupima saratani. Niseme tu kwamba kwa mujibu wa mpango wa Serikali na aina ya huduma ambazo zinatolewa, sasa hivi katika ngazi za Hospitali za Rufaa za Mikoa, hatuna mpango wa kuweka *CT-scan* kwa sababu, moja, mashine hizi kwanza ni za gharama kubwa lakini pili zinahitaji utaalam ambao kwa sasa hivi katika ngazi za rufaa za mikoa hatuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi katika mikakati yetu ni kwamba mashine za aina ya *CT-scan* upatikanaji wake unaanza katika Hospitali za Rufaa za Kanda. Hata hivyo, vipimo kwa ajili ya dalili za awali za saratani ya shingo ya uzazi vyote vinapatikana hadi katika ngazi ya vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi ambao wanatusikiliza kwamba huduma hizi zinapatikana. Kwa wale wanawake ambao hatujawagusa katika chanjo hizi, huduma hizi tumezisogeza, zaidi ya vituo 1,000 ndani ya nchi hii vifaa hivi vinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı lake la pili limehusiana na suala la kipindupindu. Ugonjwa wa kipindupindu ni mtambuka na sisi kama Wizara ya Afya ambao tunasimamia masuala yote ya afya, tunaendelea kushirikiana na mamlaka katika ngazi ya mkoa na halmashauri kuhakikisha kwamba mikakati yote ambayo sisi tumeiweka ya kutokomeza ugonjwa huu inatekelezwa kwa maana ya kutoa dawa, vipimo, kutibu maji na kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na ugonjwa wa kipindupindu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abood, Mheshimiwa Kapufi, Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro ipo katikati ya barabara za Iringa, Mbeya, Dodoma na ajali nyingi zinatokea lakini mpaka leo kuna matatizo ya *X-ray machine*. Je, ni lini Serikali itaipatia uwezo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro *X-ray machine* kwa sababu ajali nyingi huwa zinatokea katika barabara hizi? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro ni moja kati ya hospitali 10 ambazo tutazipatia mashine ya *X-ray*. Tunatarajia ifikapo mwezi Juni mwaka huu mashine hii itapatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi, jiande Mheshimiwa Susan.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kukosekana kwa Madaktari Bingwa na wataalam wengine katika Hospitali ya Kigoma kunaakisi hali halisi ilivyo katika Hospitali ya Manispaa ya Mpanda ambayo inafanya kazi kama hospitali ya mkoa. Je, ni lini Serikali itatusaidia Madaktari na wataalam wengine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, jiandae Mheshimiwa Susan Lyimo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze amekuwa anafuatilia sana masuala kuhusiana na afya katika eneo lake la Mpanda. Pia nimhakikishie tu kwamba kadri Serikali itakapokuwa tunapata watumishi na tunatarajia mwezi Julai mwaka huu tutapata watumishi wengine wa ziada, Hospitali ya Mpanda ambayo na mimi

nimeshaitembelea na natambua changamoto zake itakuwa ni moja ya hospitali zitakazopata watumishi. Sambasamba na hilo, Serikali imejielekeza sasa katika ujenzi wa hospitali mpya kubwa ya rufaa katika Mkoa wake wa Katavi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wizara ya Afya haijaanza jana wala juzi. Nimesikitika sana kusikia Mheshimiwa Waziri akisema sasa ndio wanafanya tathmini ya kujuu Madaktari Bingwa ni wangapi ili waweze kuwapanga. Swali langu, hawaoni huu ni uzembe mkubwa kwamba walipaswa kuwa na kanzidata au *database* ya Madaktari Bingwa ili kusiwe na tatizo hili kwa sababu kila siku tunauliza na tunaambiwa kuna tatizo? Hawaoni huo ni uzembe kwamba walipaswa kuwa nayo?

**MWENYEKITI:** Amekuelewa, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambao nao wanasimamia sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa maana ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekabidhiwa hospitali hizi za rufaa za mikoa mwishoni mwa mwaka jana wakati wa uzinduzi wa Hospitali ya Mloganzila. Tunatambua idadi ya Madaktari tuliokuwa nao na tunakuwa na mikakati ya kuhakikisha kwamba tunapata watumishi wa afya wa kutosha. Kwa hiyo, si uzembe, kila kitu ni mikakati ambayo Serikali tumeendelea kuijiwekea na tutaendelea kuzihudumia na kuwapatia watumishi wa kutosha kadri uwezo wa Serikali unavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, muda wetu ni mdogo, mwisho ni saa 4.00. Wizara ya Mifugo na Uvumi, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah.

**Kutokomeza Uvuvi Haramu**

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH** aliuliza:-

Mwaka 1974 Tanzania iliridhia Mkataba wa Kuzuia Uchafuzi wa Bahari na Usalama wa Bahari ambao lengo mojawapo ni kuzuia uvuvi haramu wa kutumia mabomu na kutoa misaada ya vifaa vya kuzuia uchafuzi wa bahari:-

(a) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuzuia uvuvi haramu wa kutumia mabomu ambao bado unaendelea?

(b) Je, Serikali inawasaidiaje wavuvi ili waachane na uvuvi haramu wa kutumia mabomu?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mikakati mbalimbali ya kupambana na uvuvi haramu ukiwemo uvuvi wa kutumia mabomu, mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia na kulinda rasilimali za uvuvi kuititia Halmashauri, Serikali za Vijiji na Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvu kwa maana ya *BMUs*;

(ii) Kuendelea kutoa elimu kuhusu athari za uvuvi haramu kwa mazingira, jamii na uchumi;

(iii) Kufanya maboresho ya sheria ili kuwa na sheria kali dhidi ya uvuvi haramu hasa uvuvi wa kutumia

mabomu ama milipuko ikiwa ni pamoja na kuweka kipengele cha kuonesha uvuvi haramu ni uhujumu wa uchumi; na

(iv) Kuimarisha Mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa kwa kushirikiana na nchi mbalimbali zikiwemo nchi za *SADC* katika kuzuia uvuvi usioratibiwa na usioripotiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kufanya operesheni ikiwa ni pamoja na Operesheni Sangara, Jodari na operesheni za Kikosi cha Kitaifa kwa maana ya *Mult Agency Task Team (Matt)* cha kuzuia uharibifu wa mazingira ili kulinda rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *MATT*, Serikali imefanya operesheni katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga na Dar es Salaam ambapo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kupungua kwa idadi ya milipuko kutoka asilimia 88 kwa mwezi hadi kufikia asilimia mbili mwezi Machi 2018, kukamatwa kwa vifaa vya milipuko na watuhumiwa 32 ambapo kesi 13 zimefunguliwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwasaidia wavuvi kuachana na uvuvi haramu ukiwemo wa kutumia mabomu, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wavuvi wa jamii za Ukanda wa Pwani kuhusu athari za uvuvi haramu kama vile uharibifu wa mazingira, matumbawe, mazalia na makulio ya samaki, kusababisha jangwa katika bahari, kuua viumbwe vingine visivyo kusudiwa, vifo, ulemavu ili waache kabisa vitendo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inaendelea kuwashimiza wavuvi kujejunga katika vikundi na kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Msingi, Vyama vya Akiba kwa maana ya *SACCOS* na *VICOBA* ili waweze kukopesheka na kuweza kununua zana na vyombo bora vya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye injini za kupachika, nyuzi

za kushonea nyavu pamoja na nyuzi kwa ajili ya nyavu za uvuvi na vifungashio kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2011na Sheria ya Mamlaka ya Mapato (VAT) ili kuwasaidia wavuvi kupata zana za uvuvi kwa bei nafuu. Aidha, Serikali inahamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vyta kutengeza boti na zana bora za uvuvi ili kuwezesha wavuvi kuzipata kwa bei nafuu na kwa urahisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamida.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu haya yenye kuleta matumaini kwa wavuvi wetu, lakini yametuelekeza namna ambavyo Serikali inaendelea kulinda mazingira ya bahari na kuendelea kulinda viumbe vilivyopo ndani ya bahari na kuendelea kuleta tija kwa wavuvi wetu. Sasa napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya Lindi Manispaa, Lindi Vijijini maeneo ya Kilwa, vijana sasa wameamua kujitengenezea ajira kupitia shughuli za uvuvi na tayari wamejiunga katika vikundi mbalimbali. Napenda kujua ni lini sasa Serikali itakuja kuwawezesha angalau kuwapa *fiber boat* na injini za boti ili vijana wale waendelee kuwa na uvuvi wa tija na kuongeza vipato vyao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, napenda sasa Serikali ituambie italeta lini mwongozo ambao utatuelekeza ni nyavu zipi zitatumika katika maziwa, mito na bahari. Unaposema kutumia nyavu ya nchi mbili, samaki wa baharini ni tofauti na samaki hao wa maziwa. Kwa mfano baharini kuna chuchungi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna dagaa, lakini unaposema tutumie nyavu ya nchi mbili maana yake samaki wale huwezi kuwapata. Napenda

Serikali iseme ni lini itatuletea mwongozo wa namna nyavu zitakavyotumika zile za bahari, maziwa pamoja na mito?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo ahsante sana.  
*(Makof)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nampongeza sana kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa masuala yanayohusua wananchi na hasa wavuvi wa kule Lindi. Anauliza lini Serikali itawawezesha vijana, nataka nimhakikishie tu kwamba Serikali iko tayari, tunapokea maombi hasa yanayohusu vifaa kwa maana ya injini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari wiki iliyopita tumeshapokea maombi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Lindi anayeitwa Mheshimiwa Hamidu Bobali akiomba mashine kwa vikundi viwili. Kwa hivyo, nafahamu Mheshimiwa Hamida ni Mbunge makini na yeye namkaribisha ofisini kutuletea hayo maombi na mashine zipo kwa ajili ya kuweza kuwasaidia vijana na vikundi vya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal lake la pili ni lini Serikali itaweka mwongozo wa matumizi ya nyavu katika maeneo mbalimbali. Tunafikiria mwaka huu kuleta maboresho ya sheria lakini kwa maelezo zaidi na kwa uelewa mpana zaidi wa sekta hii ya uvuvi Wizara yetu imeandaa semina kwa Wabunge wote ambayo itakwenda kujibu masuala yanayohusu tasnia nzima ya uvuvi siku ya Jumapili na tunawakaribisha Waheshimiwa Wabunge muweze kushiriki kikamilifu katika semina hii. Ahsante sana. *(Makof)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa zoezi hili la kuzuia uvuvi haramu linatumwiwa sasa na vikosi vya doria kunyanyasa, kudhalilisha

na kupora wananchi hasa wavuvi kwenye Visiwa vy  
Ukerewe kwa kuwadai pesa na malipo mbalimbali yasiyo  
halali. Nataka kujua Serikali iko tayari kutoa kauli kuzuia  
unyanyasaji huo lakini na Mheshimiwa Waziri kufika Ukerewe  
kukaa na wavuvi na kupata ushahidi wa haya yaliyotokea ili  
Serikali iweze kuchukua hatua kwa wahusika? Nashukuru.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi  
jiandae Mheshimiwa Dau.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa  
Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge wa  
Ukerewe. Naomba kusema kwamba kama kuna  
changamoto yoyote ambapo watendaji wetu kwa namna  
ile wameenda kinyume na misingi na taratibu tulizowapa,  
watendaji wetu wote wanapoenda doria wanapewa  
mwongozo wa makosa gani ambayo yanatakiwa  
kuchukuliwa hatua na kwa kiasi gani. Mheshimiwa Mbunge  
kama anayo hiyo orodha ya watu ambaa anasema kwamba  
hawakutendewa haki atuletee sisi tutalishughulikia mara  
moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mimi kwenda  
Ukerewe...

**MWENYEKITI:** Swali lake moja tu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa  
Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
matatizo ya uvuvi haramu katika maeneo ya Lindi  
yanafanana sana na matatizo ya uvuvi haramu katika Kisiwa  
cha Mafia. Taasisi iliyopewa mamlaka ya kushughulika na  
uvuvi haramu Mafia imejitwika majukumu mengi zaidi ya  
uhifadhi kwa maana ya wanaiza maeneo ya vivutio na  
kukusanya mapato. Je, ni lini sasa Serikali itahakkisha

kwamba Taasisi ya Hifadhi ya Bahari ya Mafia wanabaki na kazi ya uhifadhi peke yake badala ya kujishughulisha na kukusanya mapato? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa MwenyeKITI, Mamlaka ya Hifadhi ya Bahari kwa Kiingereza tunaiita kwa kifupi *MPRU* ipo kwa mujibu wa sheria za nchi. Miongozo ya kuanzishwa kwake *MPRU* kwa maana ya hifadhi ya bahari inawaelekeza kufanya kazi kadha wa kadha.

Moja ya kazi hizo ni uhifadhi lakini mbili ni kusimamia masuala yanayohusu wanaokuja katika maeneo yale ya hifadhi ikiwa ni pamoja na kuwatoza ushuru ambao kwa pamoja unarudishwa katika vijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kwa mfumo wa asilimia 30. Asilimia 10 inakwenda katika halmashauri ya wilaya na asilimia 20 inakwenda moja kwa moja katika vijiji vinavyohusika na uhifadhi ule.

Mheshimiwa MwenyeKITI, swali la Mheshimiwa Mbunge ni lini sasa *MPRU* itajielekeza katika kusimamia uhifadhi tu badala ya kukusanya ushuru. Masuala haya ni ya kisheria na kikanuni tunamkaribisha Mheshimiwa Dau kwa hoja hiyo mahsusii kabisa ya kutaka kwamba *MPRU* ijielekeze na uhifadhi tu badala ya kufanya shughuli zingine ikiwemo hiyo ya kukusanya mapato. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

Na. 151

### **Ujenzi wa Majosho**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA** aliuliza:-

Wilaya ya Ulanga ina ongezeko la mifugo; ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe lakini hakuna huduma za mifugo kama vile majosho:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa majosho?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu ongezeko la mifugo katika wilaya mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Ulanga inayokadiriwa kuwa na idadi ya mifugo kama ifuatavyo: Ng'ombe 70,000; mbuzi 16,000 na kondoo 6,373.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imepokea ombi la Mheshimiwa Goodluck Mlinga na kwa kushirikiana na wadau wengine litazingatiwa katika bajeti ya mwaka 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri machachari na kijana, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo kuongezeka kwa wingi Ulanga limeanza tangu miaka ya 90 na tumepiga kelele lakini Serikali kwenye ujenzi wa majosho wako nyuma lakini kwenye kupiga chapa kwa sababu inawaingizia mapato wamekuwa wako mbele. Naomba *commitment* ya Serikali iseme kuwa mwaka huu 2018/2019 tutajenga majosho. Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa kuwa kumekuwa na tatizo la masoko ya mifugo, masoko yaliyoko ni minada ya kienyeji ambapo wafugaji wanauzwa mifugo kwa bei nafuu. Je, lini Serikali itaweka utaratibu maalum wa masoko ili wafugaji wauze mifugo yao kwa bei ya faida? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika, kwa kifupi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge wa Ulanga kwamba tutajenga josho katika jimbo lake mwaka huu ujao wa fedha pamoja na kisima, siyo josho tu ni pamoja na kisima cha kunyweshea mifugo maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunajua kuna tatizo la uanzishaji wa masoko ambapo watu wengine wanaanzisha masoko bila utaratibu na wengine wanakosa mwongozo. Kwa hiyo, hili tunalismamia vizuri na katika mwaka huu wa fedha tutayamaliza yote haya. Tutahakikisha kwamba miongozo ipo ya kutosha kuhakikisha kwamba masoko mahali popote yanapoanzishwa yanazingatia miundombinu mahsusini inayotakiwa na eneo mahali linapohitajika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mponda.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Ulanga na Malinyi ni walewale. Suala hili la miundombinu la mifugo tumelipigia kelele muda mrefu na tumeielekeza na kuishauri Serikali watumie Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (*Livestock Development Fund*) ambayo inakusanywa kutokana na minada waweke *percentage* ili kuwa na uhakika wa kuhudumia miundombinu hiyo pamoja na malambo na majosho. Ni lini Serikali watatekeleza maagizo haya ambayo mara nyingi tumetoa hapa Bungeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu, anataka kujuua ni lini tu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni muda mfupi sana sasa hivi Waziri wa Mifugo na Mvvi atawasilisha hotuba yake, masuala yote yamesheheni humo ataona mipango yetu madhubuti kabisa ambapo sasa mifugo nchi hii haiwezi kufa tena kwa kukosa malisho na maji. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi. Kilwa ni miiongoni mwa eneo ambalo mifugo inakuja kwa wingi na Serikali hajaandaa kabisa miundombinu. Serikali ina mpango gani kutujengea malambo Kilwa ile mifugo iliyopo pale iweze kupata afya inayostahili? (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaanza na kisima kimoja mwaka huu ujao wa fedha kwa Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante amekuelewa. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Balozi Kamala.

Na. 152

### **Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera**

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi - Gera ni muhimu katika kuchochaea maendeleo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha utendaji wa chuo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*) vilihamishwa kutoka iliyokuwa Wizara ya

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika mwaka wa fedha 2016/2017 kuja Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kufuatia uhamishio huo Wizara ilitoa kandarasi kwa vyuo vitatu ambavyo ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundji Arusha na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa kina wa hali halisi ya miundombinu na vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi kabla ya kuanza taratibu za kuvifanyia ukarabati ikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera. Vilevile Wizara inaendelea kufanya tathmini ya rasilimali watu kwa vyuo vyote kwa lengo la kujuu hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tathmini kuhusu hali ya vyuo hivyo, Wizara itabaini mahitaji ya wafanyakazi, miundombinu, vitendea kazi na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuvipatia ufumbuzi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa vyuo hivyo kikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji utakaofanyika utalenga kuimarisha utoaji wa mafunzo ya ufundji stadi kwa fani zilizopo kwa sasa. Aidha, fani na stadi nyinigne mpya tofauti na za sasa zitaanza kutolewa katika vyuo hivyo kulingana na mahitaji ya soko la ajira na mahitaji ya jamii husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kamala, jiandae Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa mwaka 1975 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kushirikiana na Shirika la *SIDA* alianzisha vyuo vya *FDC* kwa nia ya kutoa ujuzi kwa akina mama wajasiriamali na vijana ili waweze kuongezewa ujuzi na hivyo kuweza kujaijiri; na kwa kuwa Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Nkenge imeandaa mpango mkubwa wa kutoa ujuzi kwa wajasiriamali akinamama na

vijana, je, Wizara iko tayari kushirikiana na Ofisi ya Mbunge wa Nkenge katika kutekeleza mpango huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alitembelea Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera na akakuta zaidi ya shilingi milioni 100 zilizotolewa kwa ajili ya kukarabati zilifanya kazi ndivyo sivyo; na kwa kuwa alitoa maelekezo palepale wale waliofanya kazi chini ya viwango warejee tena kwa gharama yao, je, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri yametekelawa au imebaki kama ilivyokuwa kabla ya kutoa maelekezo yake? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kama tuko tayari kushirikiana na Ofisi ya Mbunge, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko tayari kushirikiana naye kwa sababu lengo letu ni moja, tunataka vile vyuo viweze kufanya kazi ili tuendelee kupata nguvukazi ya ufundi na stadi mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kuhusu maelekezo yaliyotolewa juu ya ukarabati uliofanyika ambao haujakkenda vizuri. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maelekezo na uamuzi wa Wizara uko palepale, tutaendelea kufuatilia kuhakikisha kwamba maelekezo yale yanatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona na naomba niulize swali dogo la nyongeza kuhusiana na mada hii iliyoko mezani.Kwa kuwa Wilaya ya Longido haina chuo hata kimoja, chuo chochote cha Serikali; na kwa kuwa Wilaya hii ya Longido ni ya wafugaji kwa karibu asilimia 100 na ni wilaya ya uhifadhi wa wanyamapori kwa sababu tuna maeneo ya WMA na ya

uwindaji, je, Serikali haiwezi kuja kutujengea VETA hasa inayolenga tashia ya ufugaji mifugo na uhifadhi wa wanyama na mazingira na ikiwezekana Chuo cha Walimu wa Sayansi kwa sababu kuna uhaba mkubwa wa Walimu wa sayansi nchini na tuna ardhi ya kutosha na maji ya Kilimanjaro yanakuja?

**MWENYEKTI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi. Waheshimiwa muda wetu umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba mikoa na wilaya zote nchini zinakuwa na vyuo vya VETA. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeanza kwenye baadhi ya maeneo ambako tayari kuna ujenzi unaendelea na kuna mipango ya kuhakikisha kwamba wilaya zote zinakuwa na vyuo vya VETA. Kwa hiyo, hata Longido tutafika na wakati tunafanya hivyo, tutaangalia zile fani ambazo zitawasaidia wananchi wa pale kuweza kuijendeleza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali la Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, kwa niaba yake, Mheshimwa Shangazi.

Na. 153

#### **Vyuo Vikuu Kutozingatia Miongozo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI (K.n.y. MHE. ESTER M. MMASI)** aliuliza:-

Baadhi ya vyuo vikuu nchini vimeduwa na utamaduni wa kutozingatia miongozo ya Serikali Kuu katika kuongoza na kusimamia vyuo vikuu nchini na hata kupeleka kupuuzwa kwa stahiki za wafanyakazi wa elimu ya juu kwa kisingizio cha elimu ya juu inajiongoza na kujisimamia yenyewe chini ya *University Charter*:-

Je, ni nini kauli ya Serikali katika hili?

## **NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji na usimamizi wa elimu ya juu nchini unasimamiwa na Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura 346 na Kanuni zake za mwaka 2013. Kupitia sheria hiyo, vyuo vikuu vyote nchini vinaelekezwa kuweka mifumo ya usimamizi wa vyuo na kuunda Mabaraza na Kamati za Kitaaluma ili kuhakikisha kuwa usimamizi wa taaluma vyuoni unaenda sambamba na ubora unaotarajiwa. Hivyo, hakuna chuo chenye Hati Idhini (*University Charter*) ambayo inatekelezwa kinyume na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda ifahamike kwamba msimamizi mkuu wa Sheria ya Vyuo Vikuu ni Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*) ambayo imepewa jukumu kisheria kusimamia ithibati na udhibiti ubora wa elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TCU*imekuwa na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa vyuo vikuu mara kwa mara ili kuona kama vinazingatia sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya uendeshaji kulingana na madhumuni ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *TCU*imetoa Miongozo ya Ajira kwa Wafanyakazi wa Vyuo Vikuu nchini yaani *Minimum Guidelines For Employment, Staff Performance Review and Career Development, 2014* ambayo inatoa dira kuhusu ajira (*recruitment*), upandaji vyeo (*promotion*) na uwiano wa kazi (*workload*) ambazo waajiri wa vyuo vikuu wanatakiwa kuzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine chuo kikuu kinapobainika kukiuka sheria, taratibu, kanuni na

miongozo iliyopo, hatua za kinidhamu zimekuwa zikichukuliwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sheria hii, ajira katika vyuo vikuu husimamiwa pia na sheria nyingine zinazohusu kazi na ajira hapa nchini. Hivyo, kama kuna malalamiko yoyote kuhusu watumishi kutopatiwa haki zao za ajira katika baadhi ya vyuo vikuu yawasilishwe Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, napenda kuiuliza Serikali, je, imepangaje kusaidia vyuo vikuu vijendeshe kwa mujibu wa sheria za nchi lakini bila kuathiri uhuru wa utoaji wa taaluma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, ubora wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu vyetu imekuwa ni ya kutia mashaka na inashindwa kuwaandaa vijana kujajiri lakini pia kushindana kimataifa. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuboresha mitaala ya elimu ya vyuo vikuu? (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaheshimu uhuru wa vyuo vikuu (*academic freedom*) na mara nyingi sana Serikali haitaingilia namna vyuo vikuu vinavyoendeshwa. Hata hivyo, uhuru huo lazima ufanyiwe kazi ndani ya sheria. Kwa hiyo, vyuo vyote vinatakiwa viwe na uhuru lakini uhuru wake uko kwenye mipaka ambayo imewekwa na sheria, kanuni na taratibu. Ndiyo maana chuo kikuu chochote, kiwe cha Serikali au binafsi ambacho hakifuati sheria, kanuni, taratibu na miongozo hatutasita kukichukulia hatua. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalii lake la pili kwamba ni namna gani tunajaribu kuboresha *quality* ya elimu katika vyuo vikuu vyetu, jibu lake linafanana na hilo ambalo nimeshatoa kwamba Tume ya Vyuo Vikuu ambayo ndiyo hasa imepewa kazi ya kuhakikisha kwamba inadhibiti ubora wa elimu katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia itaendelea kuhakikisha kwamba taratibu zile zinafuatwa na ndiyo maana tunafanya tathmini ya kila mara na vyuo vikuu vile ambavyo havitakuwa vimefuata taratibu zile vitafungiwa. Ndiyo maana kwa mwaka huu vyuo 19 vimefungiwa na programu 75 za vyuo 22 zimesitishwa. Tunachosema tu ni kwamba ili tuweze kuwa na ubora unaotakiwa, tutaendelea kuchukua hatua ili elimu yetu iendelee kuwa bora.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, najua kuna maswali mengi ya nyongeza lakini Kiti nacho kinabanwa na kanuni. Wakati wa bajeti, maswali ni saa moja tu na mwisho ni saa nne asubuhi.

Nina Taarifa nydingine kwenu Waheshimiwa Wabunge, bajeti ya Wizara ya Habari na Utamaduni ni siku moja. Kwa maana hiyo, hapatakuwa na miongozo baada ya kutangaza majina ya wageni. Sitegemei kuona Mbunge yeoyote asimame baada ya tangazo hili.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Spika ambaa ni Mheshimiwa Hanne-Marie Kaarstad, Balozi wa Ufalme wa Norway Nchini Tanzania. *Welcome to the Parliament.* Ndugu Victor Mlunde, Meneja Miradi Ubalozi wa Norway. (*Makofii*)

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mheshimiwa Juliana Shonza, Naibu Waziri, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaa ni Ndugu Suzan Mlawi - Katibu Mkuu; Ndugu Nicholas William - Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Hassan Abbas - Mkurugenzi wa Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali; Dkt. Ayoub Ryoba Chacha - Mkurugenzi Mkuu *TBC*;

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Dkt. Jim Yonaz - Mtendaji Mkoo *TSN*; Mhandisi James Kilaba, Mkurugenzi Mkoo wa *TCRA*. (*Makofi*)

Wameambatana na Wenyeviti wa Bodi ambao ni Dkt. Ponera - Mwenyekiti wa Bodi *BAKITA*; Ndugu George Yambesi - Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya *TaSuBa*; Ndugu Leodgar Tenga - Mwenyekiti wa *BMT*; Mheshimiwa Balozi Hebert Mrigo - Mwenyekiti wa Bodi ya *TBC*. Pamoja na Watendaji Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na vitengo mbalimbali kutoka Wizarani. (*Makofi*)

Wageni wengine ni Askofu Andrew Kasyaju - Askofu wa Kanisa la Morovian Rungwe na Shekhe Nuhu Mwafilango - Shekhe Mkoo wa Wilaya ya Kyela. Pia wapo Machifu saba wa makabila mbalimbali wakiongozwa na Mtemi Fredrick Ntobi, Katibu Mkoo wa Umoja wa Machifu Tanzania na Mtemi wa Masanza. Karibuni Dodoma. (*Makofi*)

Wasanii wa filamu waliopata tuzo hivi karibuni wakiongozwa na Ivony Cherry (Monalisa). Karibuni sana. (*Makofi*)

Wasanii wanne wa muziki wa kizazi kipyta ambao ni Nasib Abdul (*Diamond*), Faustina Charles (Nandi) na Mrisho Mpoto (Mjomba). Karibuni Dodoma. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wasanii wa Kikundi cha Kakau kutoka Bukoba Mkoa wa Kagera. (*Makofi*)

Wageni kutoka Kyela Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Nabii Charles Mkuvasa. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Wizara ni kutoka Sekta ya Habari, Sekta ya Michezo, Sekta ya Sanaa, *TCRA* na Sekta ya Utamaduni. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni Dkt. Julius Clement Mashamba - Wakili Mkoo wa Serikali; Dkt. Ally Possi - Naibu Wakili Mkoo wa Serikali; Ndugu Biswalo Mganga - Mkurugenzi

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wa Mashtaka; Ndugu Edson Makallo - Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka; na Ndugu Evaristo Longopa - Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambaao ni viongozi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Wageni hao ni Mheshimiwa Shamata Khamis - Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI Zanzibar; Mheshimiwa Mmanga Mjawiri - Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali; Mheshimiwa Shadya Suleiman - Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto; Mheshimiwa Juma Mkakungu Juma - Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati; na Ndugu Haji Salum Haji Askari wa Idara Maalum. (*Makofi*)

Wageni watano wa Waheshimiwa Wabunge wa *CUF* ambaao ni Profesa Ibrahim Lipumba - Mwenyekiti wa *CUFTAifa*. Ameambatana na... (*Makofi/Vigelegеле*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Kiboko yao, kiboko yao huyo.

**WABUNGE FULANI:** CCM, CCM, CCM.

**MWENYEKITI:** *Order, order, order.*

**WABUNGE FULANI:** CCM, CCM, CCM.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamba...

**MBUNGE FULANI:** CCM Juu.

**MWENYEKITI:** Nitaanza kutaja majina sasa. Mnapofanya hivi mnachukua muda wenu wa kuchangia, hii ni bajeti ya siku moja tu.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni watano wa Mheshimiwa Musa Ntimizi kutoka Shirika la *UPF* - Senegal. *Welcome to the Parliament.* (*Makofi*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Wageni 34 wa Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ambao ni wanafunzi na Walimu kutoka Chuo cha Ukutubi. (*Makofi*)

Wageni 35 wa Mheshimiwa Omary Badwel ambao ni wanafunzi 29 na Walimu sita kutoka Shule ya Sekondari ya Mitaa iliyopo Bahi, Mkoa wa Dodoma. Karibuni. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Masoud Khamis ambaye ni mtoto wake, Ndugu Aziza Ali kutoka Mfenesini Zanzibar. (*Makofi*)

Wageni 25 wa Mheshimiwa Pascal Haonga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mkoa wa Songwe. (*Makofi*)

Wageni 22 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma. (*Makofi*)

Wageni 18 wa Mheshimiwa Lucy Magereli ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Kitivo cha Tiba. (*Makofi*)

Wageni 43 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanakwaya ya Uvuke kutoka Kanisa la *Anglican* Dodoma. (*Makofi*)

Wageni 27 wa Mheshimiwa Felister Bura ambao ni wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Susan Lyimo, Ndugu Filipo Filbert. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Bonnah, Ndugu Juma Haji Ambari, Ndugu Hosea Mbuza, Ndugu Milly Almasi, wadau wa *social media* kutoka Dar es Salaam. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Wageni 42 wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni Madiwani kutoka Halmashauri ya Jiji la Mwanza. (*Makofî*)

Mgeni wa Mheshimiwa Tauhid Cassian ambaye ni baba yake mzazi Ndugu Cassian Gallos Nyimbo. (*Makofî*)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 75 na Walimu wanne kutoka Shule ya Awali na Msingi ya Feza ya Jijini Dar es Salaam. (*Makofî*)

Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada, *Chapel* ya Bunge, anawatangazia Wabunge wote kuhudhuria ibada katika ukumbi wa Pius Msekwa, ghorofa ya pili leo siku ya Ijumaa tarehe 27 Aprili, 2018 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana. Katika ibada hiyo kutakuwa na mtumishi wa Mungu Mchungaji Marko Kinyau wa Kanisa la KKKT Ilazo. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilishatoa mwongozo kwamba siku ambayo bajeti ya Wizara ni siku moja hakuna mwongozo. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa maneno haya, yejote anayesimama inamaanisha anadharau mamlaka ya Kiti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Nassari, kaa chini, Katibu. (*Makofî*)

**NDG. BAKARI KISHOMA- KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

### **WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kwa kupokea, kujadili na hatimaye kuitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2018/2019 kuitia kikao chake cha tarehe 26 Machi, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu imezingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa maendeleo ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa naomba nimpongeze kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyositisiza uzingatiwaji wa uzalendo, maadili, mila na desturi za Mtanzania katika Taifa letu. Ni muhimu sote tukakumbuka wosia wa Baba wa Taifa kuwa Taifa lisilokuwa na utamaduni wake ni Taifa mfu na maendeleo ya Taifa lolote yanahitaji uadilifu, uzalendo, nidhamu, weledi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia, kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, kukupongeza wewe pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna ambavyo mnalisimamia vyema Bunge hili ambalo ni mhimili muhimu kwa maendeleo ya watu na Taifa letu kwa ujumla. Aidha, niwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wabunge waliochaguliwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Sija); Mheshimiwa Said Maulid Mtulia (Kinondoni); Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro (Songea Mjini) na Mheshimiwa Justin Joseph Monko (Singida Kaskazini). (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Kyela kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Ubunge. Ni matarajio yangu kuwa Wanakyela watatumia kikamilifu fursa za kibiashara zinazoanza kujitokeza wilayani kutokana na kuanza kukamilika kwa miradi mikubwa ya miundombinu ya bandari, uchukuzi ziwani na barabara ya Kikusya-Matema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru wanangu kwa kuyakubali matokeo na mapenzi ya Mungu bila kinyongo pamoja na umri wao mdogo, kwa kurejesha amani, nuru na matumaini katika maisha yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Mheshimiwa Julianne D. Shonza, Naibu Waziri; Bibi Susan P. Mlawi, Katibu Mkuu; na Bw. Nicholas B. William, Naibu Katibu Mkuu. Niwashukuru pia Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma, tija na ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018, Bunge lako Tukufu lilipatwa na simanzi kubwa kwa kuondokewa na Mheshimiwa Leonidas Gama, Mbunge wa Songea Mjini. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, wananchi wa Jimbo la Songea Mjini na wanafamilia kwa kumpoteza kiongozi huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim M.

Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2017/2018 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makusanyo ya Maduhuli; mwaka 2017/2018, Wizara ilikadiria kukusanya Sh.1,574,602,000 kutokana na viingilio katika viwanja vya Taifa na Uhuru; malipo ya usajili wa magazeti na majarida; tozo ya matumizi ya Ukumbi wa Mikutano wa Idara ya Habari-MAELEZO; utoaji wa vitambulisho vya waandishi wa habari na mauzo ya picha mbalimbali za Viongozi wa Kitaifa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara ilikusanya Sh.556,360,778 sawa na asilimia 35 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Taasisi saba zilizo chini ya Wizara kiasi kilichokadiriwa kukusanya ni jumla ya Sh.36,912,939,000 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Sh.14,047,934,461 zilikusanya sawa na asilimia 38 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Uwanja wa Taifa ulifungwa kwa miezi minne ili kuruhusu ukarabati katika uwanja huo ikiwemo upandaji wa nyasi mpya katika eneo la kuchezea. Aidha, Serikali ilianza upya usajili wa magazeti na majarida nchini ikiwa ni utekelezaji wa Sheria Mpya ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kumekuwepo na ongezeko la ushindani kwa huduma za redio, televisheni na magazeti pamoja na kukua kwa teknolojia ya mawasiliano kunakorahisisha na kuwezesha njia mbalimbali mbadala, nafuu na za haraka kutumika katika uhabarishaji na utoaji wa matangazo ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha; mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliidhinishiwa Sh.28,212,695,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

(a) Matumizi ya Kawaida: Sh.21,892,695,000 zikijumuisha Mishahara Sh.17,276,616,000 na Matumizi Mengineyo Sh. 4,616,079,000; na

(b) Miradi ya Maendeleo: Sh.6,320,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi mwezi Machi, 2018 Wizara ilipokea Sh.18,113,422,942 ambayo ni sawa na asilimia 64 ya bajeti yote kwa mchanganuo ufuatao:-

(a) Matumizi ya Kawaida: ni Sh.13,755,422,942 ambayo ni sawa na asilimia 62, ambapo Sh.9,728,184,426 ni mishahara sawa na asilimia 56 na Sh.4,027,238,516 ni matumizi mengineyo sawa na asilimia 87; na

(b) Miradi ya Maendeleo: kiasi kilichopokelewa ni Sh.4,358,000,000, sawa na asilimia 69.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/2018. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/2018 hadi mwezi Machi, 2018 imeelezewa kwa kina kwa Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika sehemu ya 3.2 ukurasa wa tisa hadi 56 katika Kitabu cha Hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako hotuba yangu yote ambayo iko kwenye kitabu liingizwe kwenye *hansard* na mimi nasoma muhtasari tu kwa kiasi nitachowea kutokana na muda. Kwa muhtasari naomba kutoa taarifa hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya habari, sekta hii inahusisha Idara ya Habari-MAELEZO, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*). Katika Sekta hii hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2017/2018 ni kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya mikutano minane (8) kati ya Msemaji Mkuu wa Serikali na Waandishi wa Habari ilifanyika na

kuwezesha kutolewa kwa mrejesho kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo zinazotekelvezwa na Serikali;

(b) Jumla ya vipindi 49 vya televisheni vya Tunatekeleza viliratibiwa kupitia Idara ya Habari-Maeleo na kurushwa hewani kupitia *TBC1*;

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipindi hivi vinatoa fursa kwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Watendaji Wakuu wa Mashirika, Taasisi, Wakala na Idara Zinazojitegemea za Serikali kutoa taarifa kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya maeneo wanayosimamia ikiwemo kutatua changamoto za wananchi, maboresho katika utoaji wa huduma na mikakati inayotekelvezwa ya kuwaletea wananchi maendeleo.

(c) Mkutano wa Maafisa Habari ulioshirikisha zaidi ya Maofisa Habari 300 ulifanyika Mkoani Arusha tarehe 12-16 Machi, 2018. Mkutano huo pamoja na mambo mengine, ulilenga kuimarisha uwezo wa utendaji wa Maafisa Habari wa Wizara na Taasisi za Serikali katika kuuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Serikali na kupokea mrejesho kutoka kwa wananchi kwa lengo la kufanyiwa kazi;

(d) Nakala 5,000 za Jarida la Nchi yetu lenye kuainisha Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha miaka miwili (2016-2017) zilichapishwa na kusambazwa katika Wizara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na kwa wananchi kwa ujumla. Aidha, toleo maalum la Jarida la Nchi Yetu la Miaka 56 ya Uhuru wa Tanzania Bara lilichapishwa na nakala 4,000 kusambazwa; na

(e) Jumla ya magazeti na majarida 169 yalipatiwa Leseni ya Uchapishaji ambapo 21 ni ya Serikali na taasisi zake na 148 ya binafsi hadi kufikia Machi 31, 2018. Leseni hizi zilitolewa kufuatia kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) Shirika hilo lilitokeleza miradi minne iliyolenga kuboresha usikivu na huduma ya utangazaji kama ifuatavyo:-

(a) Uwekaji wa mitambo ya kuongeza usikivu wa radio *TBC Taifa* na *TBC FM* katika maeneo ya mipakani, ikiwemo Rombo, Longido, Tarime, Kibondo na Nyasa. Hatua hii kwa upande wa Rombo imewezesha *TBC* kusikika katika eneo lote la Tarakea, Vijiji vya Olele, Miembea, Usseri, Mashima, Kibaoni na Mashati na katika baadhi ya maeneo ya Rombo Mkuu na Rongai. Aidha, kwa upande wa Longido, *TBC* inasikika katika maeneo ya Namanga, Kitombeine, Vijiji vya Oldonyosambu, Mirow na Engarnaibo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Tarime, *TBC* inasikika katika maeneo ya Tarime Mjini, Sirari, Nyamuuhonda, Nyamuigura na maeneo mengine jirani na wilaya hiyo. Vilevile, Wilaya za Kibondo na Kakonko usikivu unapatikana katika maeneo ya Kibondo Mjini, eneo lote la Wilaya ya Kakonko na Vijiji vya Nyakanazi, Kifura, Kumhasha, Kumbanga, Mabamba, baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Biharamulo na Vijiji vya jirani mpakani na Tanzania katika nchi ya Burundi. Kwa upande wa Wilaya ya Nyasa usikivu unapatikana katika Mji wa Mbambabay, Vijiji vya Kilosa, Kipwili, Nangombo na Chinula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, usikivu wa mtambo wa Redio katika Wilaya ya Nachingwea umeongezwa kutoka *Watt 100 (TBC FM)* hadi *Watt 1,000* na *TBC Taifa* kutoka *Watt 250* hadi *Watt 1,000* na hivyo kuwezesha kupanuka kwa usikivu katika wilaya na maeneo ya Nachingwea, Ruangwa na sehemu za Wilaya ya Masasi. Miradi yote hii imetekelezwa na mafundi wa *TBC* na hivyo kuliwezesha Shirika kuokoa fedha nydingi ambayo ingelipwa kwa wakandarasi na kwa miradi michache;

(b) Ujenzi wa studio ya kisasa ya Redio Jamii katika Mkoa wa Arusha kwa ufadhili wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Services Access Fund*-

*UCSAF) ambayo ilizinduliwa tarehe 11 Machi, 2018. Kukamilika kwa studio hizi kutatoa fursa mbalimbali kwa wananchi wa Mkoa wa Arusha ikiwemo kurusha matangazo ya Utalii, Biashara, Elimu, Burudani, Mila na Desturi, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na*

(c) Uboreshaji wa mifumo ya urushaji matangazo kwa njia ya kidijiti ambapo *TBC* ilinunua mtambo wa Satelaiti (*Satelite Uplink*) na kuufunga katika Studio zake za Mikocheni. Hatua hii imewezesha mtambo huo kurusha mawimbi kwa kutumia njia mbili tofauti na hali iliyokuwepo awali ya kuwa na njia moja tu ambayo mbali na kuathiri muonekano wa *TBC*, ilitishia Televisheni ya Taifa kutoweka hewani endapo hitilifu yoyote ya kiufundi ingetokea;

(d) Ununuzi wa magari tisa (9) kwa ajili ya shughuli za utangazaji pamoja na ununuzi wa vifaa vyta kisasa vya kidijiti vya kurusha matangazo mubashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuboresha mifumo ya urushaji matangazo kwa njia ya kidijiti, tathmini ya sasa ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) imebainisha ubora wa picha za televisheni ya *TBC* umeongezeka kutoka asilimia 52 hadi 88;

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kufuatia agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, hatua ya uanzishwaji wa chaneli ya utalii inayoratibiwa na *TBC* kwa kushirikiana na wadau wakuu wa utalii nchini, zimefikia hatua nzuri. Matarajio ni kuanza kurusha matangazo hayo ya majaribio katika chaneli hiyo mwezi Mei, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* na Kampuni ya *Star Communication Network Technology* ya China, ambao ni wabia wa Kampuni ya *StarMedia* waliweka saini makubaliano yanayolenga kurekebisha kasoro za kimkataba na za kiuendeshaji zilizosababisha Kampuni ya *StarMedia* kushindwa kupata faida tangu ilipoanzishwa miaka saba

iliyopita. Makubaliano hayo yaliwekwa saini tarehe 3 Aprili, 2018, Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) iliedelea kusimamia na kufuatilia maudhui yanayorushwa na vituo vya utangazaji ikiwa ni pamoja na yale ya Kielektroniki, Maudhui Mitandaoni ambapo utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

(a) Kusajili jumla ya vituo 12 vya Redio na sita vya Televisheni na kufanya idadi ya vituo vya Redio kufikia 158 na Televisheni 34;

(b) Kwa kushirikiana na Wizara, kuratibu utungaji wa Kanuni za Maudhui ya Redio na Televisheni na Kanuni za Maudhui ya Mitandaoni za mwaka 2018 chini ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010, ambazo zimeanza kutumika rasmi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa wadau wa huduma za utangazaji, wanahabari na wananchi kwa ujumla kuzielewa Kanuni hizo, zinazoweka utaratibu wa uendeshaji bora wa redio na televisheni na matumizi bora ya mitandao yanayozingatia maadili ya Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*), hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kuimarisha ubora wa magazeti yanayozalishwa na kampuni hiyo ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuboresha maudhui na mwonekano wa magazeti; kutenga kurasa maalum katika magazeti ya *Daily News* na *HabariLeo* kwa ajili ya habari za Makao Makuu ya nchi yaani Jiji la Dodoma;

(ii) Kuchapisha matoleo maalum ya Afrika Mashariki kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kukamilisha muonekano mpya wa gazeti la *HabariLeo* kwa kulifanya kuwa na mvuto kupitia habari za Kikanda, Miji Mikuu na pia makala maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine zilizochukuliwa ili kuimarisha utendaji na mapato ya Kampuni ni:-

(i) Kuzindua mauzo ya gazeti la HabariLeo nchini Rwanda tarehe 18 Desemba, 2017 uliopokelewa kwa msisimko mkubwa;

(ii) Kuimarisha habari mtandao kwa kununua vifaa vyta kisasa na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Kitengo cha Habari Mtandao;

(iii) Kuendesha majukwaa matatu ya fursa za biashara na uwekezaji katika Mikoa ya Shinyanga, Tanga na Zanzibar na mwezi Mei, 2018, jukwaa hilo litafanyika Mkoani Arusha. Aidha, maandalizi yanaendelea kwa upande wa Mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Mara na Songwe pamoja na majukwaa ya kisekta kama Madini, Utalii na Ujenzi. Mipango inafanyika pia ili jukwaa hili lifanyike katika nchi za Afrika Mashariki na ughaibuni kwa lengo la kutangaza fursa zilizopo na hivyo kuvutia biashara na uwekezaji nchini.

(iv) Kuagiza karatasi moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji ikiwa ni hatua ya kupunguza gharama za uendeshaji ambapo shehena ya kwanza yenye uzito wa tani 150 imewasili kiwandani tarehe 19 Machi, 2018; na

(v) Kuendelea na mchakato wa ununuzi wa mtambo wa uchapaji ambapo mtambo huo unatarajiwa kuzinduliwa mwezi Juni, 2018. Mtambo huu utaiwezesha *TSN* kutekeleza mradi wa uchapaji ambao utaimarisha mapato ya kampuni kupitia uchapaji wa machapisho mbalimbali ikiwemo vitabu, kalenda, shajara, mabango, taarifa mbalimbali, majarida na vipeperushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maendeleo ya utamaduni. Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni inahusisha kuenzi, kulinda, kuhifadhi na kuweka kumbukumbu za urithi wa utamaduni usioshikika ikiwa ni pamoja na historia,

mila, desturi, sanaa, lugha, maadili na uzalendo. Utekelezaji katika Sekta hii katika mwaka 2017/2018 ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara iliendelea kufanya mapitio ya Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 kwa kuzingatia maoni ya Wadau yaliyopokelewa na Wizara. Aidha, kwa kushirikiana na Wadau, Wizara iliendelea kuratibu uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu wenyewe lengo la kuwawezesha Wanatasnia ya Sanaa kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa mitaji ikiwa ni pamoja na mikopo yenyе masharti na riba nafuu;

(ii) Taarifa na takwimu za maeneo ya kihistoria, utamaduni, mila na desturi zilikusanywa katika Halmashauri za Wilaya za Babati, Morogoro, Tunduru na Ulanga na uchambuzi wa awali wa taarifa hizo umebalini maeneo yenyе vyanzo vya maji ambavyo hutumika kwa shughuli za uvuvi na vivutio vya utalii; mapango na maboma yaliyotumiwa na wenyeji na Askari wa Jeshi la Kijerumanii kujificha wakati wa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia;

(iii) Wizara iliratibu Mkutano na Viongozi wa Madhehebu ya Dini uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2017, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Wajumbe zaidi ya 140, wakiwemo Viongozi wa Serikali, Viongozi wa Dini na Vyombo vya Habari. Mkutano huo uliazimia mambo mbalimbali ikiwemo Viongozi hao kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha vita dhidi ya rushwa, ukwepaji wa kulipa kodi na matumizi ya dawa za kulevy;

(iv) Wizara kwa kushirikiana na wadau iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (*JAMAFEST*) liliofanyika nchini Uganda tarehe 7 - 17 Septemba, 2017 na kushirikisha jumla ya wajasiriamali wa Kitanzania wa kazi za kitamaduni, filamu, sanaa na ubunifu wapatao 396. Wajasiriamali hao walipata fursa ya kutangaza na kuuza kazi zao pamoja na kuanzisha mitandao ya kibiashara itakayoimarisha masoko ya kazi zao katika ukanda wa Afrika Mashariki; na

(v) Wizara iliratibu Kampeni ya Kitaifa ya Uzalendo iliyozinduliwa tarehe 8 Desemba, 2017 Mkoani Dodoma na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na kuhudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Kitaifa akiwemo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamjeni hii ambayo ni endelevu, itakuwa inafanyika tarehe 14 Oktoba kila mwaka, Siku ya Kumbukumbu ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na tarehe 7 Aprili ya kila mwaka, Siku ya Kumbukumbu ya Mzee wetu Abeid Amani Karume, ikiwa ni hatua ya kuenzi uzalendo uliooneshwa na Waasisi hawa wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2011, nchi yetu ilipewa dhamana kubwa na Umoja wa Afrika (*AU*) ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na vilevile kuwa mwenyeji wa Kituo Kikuu cha Makumbusho na Utafiti wa Harakati za Ukombozi Barani Afrika. Taifa letu ilipewa heshima hii kubwa kutokana na kuwa kiongozi, ngome na kinara wa kuongoza harakati na mapambano ya kulikomboa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu inalenga kubaini, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote kuhusu harakati za ukombozi wa Bara la Afrika ikiwa ni pamoja na vifaa, maeneo, majengo, nyaraka, kazi za sanaa, mahandaki, maelezo, sare, silaha, magari na hotuba kwa matumizi ya vizazi vyaa sasa na vijavyo. Katika kipindi hiki Programu ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Kuorodhesha maeneo 25 yaliyotumika wakati wa harakati za ukombozi wa Bara la Afrika ili yakaratibiwe na kutumika katika kukuza utalii wa kiutamaduni na kuhifadhi urithi wa ukombozi. Hadi sasa jumla ya maeneo hayo ni 161 ambayo yamebainishwa;

(ii) Kufanya mahojiano na wazee 82 walioshiriki au kushuhudia harakati za ukombozi wa Bara la Afrika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Pwani na Ruvuma na hivyo kuwezesha idadi ya wazee waliohojiwa hadi sasa kufikia 201.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinazopatikana kupitia mahojiano hayo zitatumika katika kazi mbalimbali ikiwemo utafiti na uandishi wa majorida na vitabu vyta historia na uraia kwa madhumuni ya rejea na kufundishia. Wizara iliratibu mkutano kati ya Tanzania na Afrika Kusini uliofanyika tarehe 16 hadi 19 Septemba, mwaka jana Mjini Dodoma na kujadili masuala mbalimbali kuhusu uhifadhi wa urithi wa ukombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkutano wa Mawaziri wa Utamaduni wa Nchi za SADC uliofanyika Afrika Kusini tarehe 27 hadi 29 Machi, mwaka huu ulijadili utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika katika nchi za SADC na kuazimia pamoja na mambo mengine, kuendelea kufanya utambuzi na utunzaji wa maeneo na kumbukumbu zilizotumika katika harakati za ukombozi, kubadilishana utaalama katika masuala mbalimbali ikiwemo utafiti na mafunzo yanayohusiana na urithi wa ukombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuipongeza na kuishukuru sana Serikali ya Afrika Kusini kwa kufanikisha mkutano huo wa Mawaziri wa Utamaduni wa Nchi za SADC chini ya Uenyekiti wa Tanzania na kufikia maamuzi muhimu ya kuendeleza Programu hii. Namshukuru sana vilevile Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Balozi Ali Karume kwa uwezo mkubwa alioonyesha kuendesha mkutano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili la Taifa liliendelea kuratibu na kusimamia matumizi ya fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili pamoja na maendeleo ya lugha hiyo kwa ujumla ndani na nje ya nchi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuandaa vipindi 56 vya Lugha ya Kiswahili vilivyorushwa kupitia *TBC* Taifa, vipindi 55 vya Kumepambazuka vilivyorushwa kupitia *Radio One* na vipindi 13 vya ufanuzi wa Msamati wa Kiswahili vilivyorushwa kupitia *Redio Clouds FM* na Idhaa ya Kiswahili ya Redio ya Umoja wa Mataifa;

(ii) Kutoa huduma ya ukalimani wa lugha kwa Idara mbalimbali za Serikali, mashirika, kampuni, taasisi na watu binafsi ikiwemo katika Mkutano wa Bunge la Afrika uliofanyika Afrika Kusini mwezi Oktoba, mwaka jana na katika Mkutano na Mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika uliofanyika nchini Ethiopia mwezi Julai, 2017 na Januari, 2018;

(iii) Kuendesha semina kwa Watangazaji na Wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari ili kuhilmiza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari, ikiwemo matumizi ya lugha yenye staha;

(iv) Kuandaa mfumo wa kielektroniki (kanzidata) wa kutunza kumbukumbu za Wataalam wa Lugha ya Kiswahili, yaani Walimu, Wafasiri, Wakalimani wa lugha za alama na lugha ya kawaida, Wahariri na wanataaluma nyingine husianifu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa wanataaluma wote wa lugha ya Kiswahili kujisajili katika kanzidata hii ili wanufaike na fursa mbalimbali zinazojitokeza ndani na nje ya nchi, tena kwa ada ndogo tu ya usajili wa 10,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), baadhi ya majukumu yaliyotekelizwa ni:-

(i) Kuwajengea uwezo wasanii na wadau wa Sanaa 50 kuhusu matumizi ya mitandao katika kutangaza na kuuza kazi za sanaa ndani na nje ya nchi;

(ii) Kwa kushirikiana na kampuni ya *Data Vision International* na Shirikisho la Sanaa za Ufundi (*TAFCA*), kuanzisha mradhi wa utambuzi wa wasanii wa sanaa za ufundi nchini unaotambulika kwa jina la *TACIP (Tanzania Art and Crafts Identification Project)*, wenyewe lengo la kuwaunganisha wanasanaa za ufundi kupitia kanzidata mahsusii itakayowawezesha kujipanga vyema na kuuza kazi zao kupitia mifumo ya TEHAMA bila kumhitaji mtu wa kati;

(iii) Kupitia uratibu wa *BASATA*, Umoja wa Wanamuziki (*Tanzania Music Foundation – TAMUFO*) kwa kushirikiana na kampuni ya *CogsNet Technologies* wanaendelea na uandaaji wa mfumo wa uhifadhi wa taarifa mtandaoni na kanzidata ya wasanii wa muziki ambapo kila mwanamuziki atakuwa na ukurasa wake kwa lengo la kujitangaza na kuongeza soko la kazi zao na mwisho;

(iv) Kuendelea kutoa elimu kuhusu maadili na weledi katika kazi za sanaa kwa njia mbalimbali ikiwemo: kupitia tovuti yake, [www.basata.go.tz](http://www.basata.go.tz), kurasa za *twitter* – basatatanzania, *facebook* – baraza la sanaa la Taifa na *Instagram* – basata.tanzania. Aidha, elimu pia imeendelea kutolewa kupitia Jukwaa la Sanaa linalofanyika kila Jumatatu ya kwanza na ya Jumatatu ya mwisho ya kila mwezi Jijini Dar es Salaam na mikoani na kupitia vyombo vyahabari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Filamu Tanzania ilitekeleza majukumu mengi, baadhi yake ni:-

(i) Kuwajengea uwezo wanatasnia wa filamu pamoja na Makatibu wa Bodi za Filamu za Mikoa na Wilaya kuhusu namna ya kuboresha utayarishaji, usambazaji, uwekaji wa tafsiri, uoneshaji na ithibati kwa wanatasnia;

(ii) Ikiwa ni hatua ya kuhakikisha filamu zinazoingia sokoni zinafuata taratibu, jumla ya operesheni 22 zilifanyika na kuwezesha kukamatwa kwa jumla ya filamu 51 zilizoingia sokoni kinyemela;

(iii) Kuendelea kuhamasisha wadau wa filamu kutumia njia mbalimbali za usambazaji na uoneshaji wa kazi za filamu ikiwemo usambazaji kwa njia za mtandao. Miradi mbalimbali ya kusambaza kazi hizo imeanzishwa ili kazi za filamu zimfikie mlaji moja kwa moja na kwa urahisi, kama vile *Barazani Entertainment*, *Max Burudani*, na *Cogsnet* kupitia channel maalum ya kuonesha filamu za kitanzania inayoitwa *JTV* inayopatikana katika king'amuvi cha *Startimes* kupitia *Channel Number 126* ambayo inamwezesha mmiliki wa filamu inayooneshwa kulipwa kulingana na idadi ya watazamaji. Chaneli nyengine mahsusi zinazoonesha filamu za Kiswahili ni pamoja na *Maisha Magic Bongo*, *Sinema Zetu*, *Sibuka* na *EATV*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unisamehe nimetumia neno king'amuvi, neno sahihi ni kisimbuzi;

(iv) Wadau wa filamu waliendelea kuhamasishwa kushiriki katika matamasha, tuzo na maonesho ya bidhaa za filamu kitaifa, kikanda na kimataifa ili kujitangaza na kupanua masoko ya kazi zao. Tamasha la Filamu la Kalasha – Kenya, Tamasha la Filamu la Kimataifa la Zanzibar – *ZIFF, Forum for Animation Films* – Misri, Tamasha la Kimataifa la Filamu za *Sinema Zetu* (*ZIFF*), Tamasha la Kimataifa la Filamu la Mashariki (*Mashariki International Film Festival* – Rwanda), *Zimbabwe Women International Films Festival*, *Twelve Months Films Festival* ya Romania na *African Prestigious Awards* – Ghana;

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matamasha hayo Filamu za Kitanzania, Waigizaji wa Kitanzania walipata tuzo mbalimbali. Tutayataja majina ya filamu zilizoshinda na waigizaji waliopata tuzo wa Kitanzania baadaye itakapolazimu tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongezeka kwa dhati washindi wote na wale wote walioshiriki lakini hawakufanikiwa kupata tuzo. Ushiriki wao umedhihirisha kuwa wao ni chachu ya maendeleo ya Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (*TasUBa*) yenyeye jukumu la kutoa mafunzo ya sanaa na utamaduni, utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya wanachuo wa Astashahada 64, stashahada 53 na kozi fupi 112 walidahiliwa; na

(ii) Tamasha la 36 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni liliofanyika mwezi Septemba, mwaka jana na kushirikisha jumla ya Vikundi 104, Sanaa za Maonesho 75 na Sanaa za Ufundu 29, ambapo vikundi 101 ni vya ndani ya nchi na vitatu vilitoka Kisiwa cha Mayote, Ufaransa na Zimbabwe liliratibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tamasha hili huendeshwa na *TasUBa* kwa lengo la kutunza na kuenzi sanaa na utamaduni wa Mtanzania. Hukutanisha watu wa tamaduni mbalimbali kutoka sehemu nydingi duniani, ili kuonesha kazi zao za sanaa na utamaduni wao pamoja na kuwawezesha wanafunzi wa Kitanzania kuanzisha na kuimarisha uhusiano na wasanii wa ndani na njie ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maendeleo ya Michezo. Sekta ya Michezo nchini inasimamiwa na Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995. Malengo ya Sera hiyo ni pamoja na kuhamasisha umma wa Watanzania kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo. Kuwezesha upatikanaji wa viwanja na zana bora na za kutosha kwa ajili ya kuimarisha maendeleo ya michezo nchini; na kuandaa na kutayarisha wataalam wa kutosha katika fani na taaluma mbalimbali za michezo ili kuhakikisha timu na wachezaji wanafanya vizuri katika mashindano na michezo mbalimbali ya kimataifa.

Mheshimiwa mwenyekiti, katika sekta hii sehemu ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Zoezi la mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 liliendelea na Rasimu ya Sera hiyo imekamilika

na ipo katika hatua za kuwasilishwa kwenye ngazi za maamuzi kwa ajili ya kuidhinishwa;

(ii) Maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Vijana Wenye Umri chini ya Miaka 17 (*AFCON U-17*) mwaka 2019 yaliendelea kwa kuunda Kamati ya Maandalizi na Kamati za Kitaalam ambazo zinakutana mara kwa mara kwa lengo la kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika kwa ufanisi mkubwa; na

(iii) Maandalizi ya maandalizi ya ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Mkoani Dodoma yaliendelea ambapo zaidi ya ekari 168 katи ya ekari 328 za eneo la uwanja huo zimesafishwa pamoja na kufanya maandalizi ya awali ya kuandaa michoro ya kitaalam ya uwanja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limetekeleza majukumu yafuatayo, baadhi yake:-

(a) Kuandaa mashindano ya riadha kwa wanawake yaliyohusisha wanariadha 123 kutoka mikoa 26 ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (*JICA*);

(b) Kuendesha Mashindano ya Taifa kwa watu wenye mahitaji maalum yaliyofanyika Zanzibar mwezi Disemba, mwaka jana kwa kushirikiana na Kamati ya Olimpiki Maalum. Mashindano hayo yalishirikisha wachezaji 497 kutoka mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na mikoa mitano ya Zanzibar;

(c) Kusajili Mashirikisho/Vyama 24, Vilabu vya Michezo 233, Vituo vya Michezo 17 na wakuzaji wa michezo 18;

(d) Kuratibu maandalizi ya Timu ya Tanzania iliyoshiriki michezo ya Jumuiya ya Madola *Gold Coast*, Australia mwezi Aprili, mwaka huu, ambapo wachezaji wanne wa ngumi za ridhaa, kuogelea mchezaji mmoja, mpira wa meza wachezaji wanne na riadha wachezaji sita walishiriki; na

(e) Kwa kushirikiana na asasi ya *Joe's Gym* kuratibu pambano baina ya bondia Mtanzania Ibrahim Class dhidi ya bondia Koos Sibiya kutoka Afrika Kusini. Katika pambano hilo Mtanzania Ibrahim Class aliweza kutetea ubingwa wake wa Dunia wa *Global Boxing Council* wa uzito wa kati kwa kumshinda mpinzani wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, chini ya usimamizi wa Baraza, mabondia wengine wa Kitanzania waliendelea kushinda; Bondia Maono Ali tarehe 22 Februari, mwaka huu nchini Afrika Kusini alishinda ubingwa wa Dunia wa Vijana uzito wa kati (*WBC Youth*) dhidi ya Luka Tutek wa Croatia, bondia Bruno Tarimo aliyetwaa Mkanda wa Dunia wa Uzito wa kati wa *WBA Oceania* nchini Australia tarehe 24 Machi, 2018 kwa kumshinda bondia Billel Dib nyumbani kwao na Bondia Salehe Mkalekwa aliyetwaa Ubingwa wa *African Boxing Union (ABU)* baada ya kumsinda Bondia Andreas (*King Cheater*) Valavanis wa Misri katika pambano liliofanyika Jijini Nairobi, tarehe 21 Aprili, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuwa hatufanyi vizuri sehemu nyingine, lakini huku tunatamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/2018, changamoto zilijitokeza ambapo hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi zinaelezwu kwa kina katika sehemu ya 4.0, ukurasa wa 56 hadi 58 wa Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo ni pamoja na kuendelea kuongezeka kwa mmomonyoko wa maadili ya Kitanzania, kuongezeka kwa maudhui hasi mitandaoni pamoja na kuwepo kwa vipindi vyta redio na television visivyozingatia weledi na maadili ya utangazaji. Magazeti kutozingatia weledi na sheria za nchi na hivyo, mara kwa mara kurudia makosa ya kitaaluma na kukiuka sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kukabiliana na changamoto hizo kwa kuelimishana na

kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili, mila na desturi ya Mtanzania, kuendelea kukutana na wamiliki wa vyombo vyaa habari na kuandaa Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Maudhui ya Mitandaoni na Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Maudhui ya Redio na *Television* zote za mwaka 2018 ambazo zinazelekeza namna bora ya uendeshaji wa redio na *television* pamoja na matumizi sahihi ya mitandao yanayozingatia utamaduni na maadili ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naomba sasa kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa kutekeleza majukumu yaliyofafanuliwa kwa kina kisekta na kwa takwimu katika sehemu ya tano, ukurasa wa 59 hadi 73 wa Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO itaendelea kuisemea Serikali kwa kukusanya, kusambaza na kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa Sera, Mpango, Miradi na Programu mbalimbali za Maendeleo, kuratibu uanzishwaji wa vyombo vipyaa vyaa usimamizi wa masuala ya habari kama vile Dawati la Matangazo ya Serikali, Bodi ya Ithibati na Baraza Huru la Habari vilivyoanzishwa chini ya Sheria Namba 12 ya Huduma za Habari ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) litaanza ujenzi wa jengola Makao Makuu yake Mkoani Dodoma litakalotosheleza mahitaji ya shughuli za utangazaji na utawala Makao Makuu ya Nchi. Kununua

magari 11 kwa ajili ya shughuli za utangazaji, utafutaji na uandishi wa habari, uandaaji wa vipindi na ufundi wa mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, TBC itaanzisha *Channel* ya Utalii itakayorusha na kutangaza vipindi vinavyohusiana na maliasili na fursa mbalimbali zilizopo nchini na hivyo kukuza utalii wa ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*), Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro (*NCAA*), Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*), Bodi ya Filamu Tanzania (*TFB*) na Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyama Pori (*TAWA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Magazeti (*TSN*) itaendelea kupanua mauzo ya gazeti la Habari Leo katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kukuza lugha ya Kiswahili na kutangaza fursa za kibashara zillizopo nchini. Watajiimarisha zaidi kimtandao ili kuboresha mauzo ya magazeti pamoja na kupanua zaidi wigo wa majukwaa ya fursa za bishara ikiwemo kuyaendesha katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nje ya Jumuiya hiyo ili kutangaza fursa za kibashara na uwekezaji zilizopo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kusimamia na kufuatilia maudhui yanayorushwa na vituo vya Televisheni na Redio, ikiwa ni pamoja na yale ya kielektroniki, maudhui ya mtandaoni. *TCRA* itaendelea na mashauriano na wadau kuhusu uanzishwaji wa mfumo wa utangazaji wa redio za kidijiti ili kukabiliana na upungufu wa masafa ya kidijiti ya redio. Aidha, *TCRA* itaendelea kuhamasisha utengenezaji na uzalishaji wa maudhui ya ndani yanayozingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Mamlaka itaendelea kutoa elimu juu ya Kanuni mpya ya Maudhui Mitandaoni na Kanuni mpya ya Maudhui Redioni na kwenye luninga zilizotungwa chini ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroni na Posta ya mwaka 2010 ambazo pamoja na mambo mengine, zinasisitiza yafuatayo:-

- (i) Zinazuia usambazaji wa kauli chafu, matusi, picha mgando na jongevu za utupu na zenyе maudhui yasiyofaa kwa watoto;
- (ii) Zinawaingiza kwenye mfumo rasmi wa kutambulika kisheria, kama wanahabari na kuwajibika kulipa kodi watoa huduma wa picha jongevu za habari na burudani na kutoa matangazo kwa njia za mitandao (*bloggers*);
- (iii) Zinamtaka kila mtumiaji wa mitandao (kwa faida yake mwenyewe) awe na namba yake ya siri ili wajanja wasitumie kiurahisi chombo chake cha mawasiliano na kutenda matendo hasi kinyume na sheria;
- (iv) Zitaweka muda maalum (*watershed period*) ambaо picha jongevu zote za filamu au muziki zenyе maneno na maeneo yasiyo mazuri kwa watoto zirushwe au kuoneshwa kwenye luninga katika muda maalum tu. Tuliweka muda huo maalum kuanzia saa 4.00 usiku hadi saa 11.30 asubuhi lakini wadau wamekuwa wakali sana, wanataka picha na nyimbo za aina hiyo zianze kurushwa saa 6.00 usiku wakati watoto wamelala na mwisho saa 11.00 asubuhi kabla watoto hawajaamka; (*Makofi*)
- (v) Zinatambua Kiswahili na Kiingereza tu kuwa lugha rasmi zitakazotumika kwenye matangazo ya redio na runinga;
- (vi) Zinataka kila redio na luninga kutoa kipaumbele kwa muziki wa Kitanzania kati ya saa 11.30 alfajiri hadi saa 3.00 usiku. Muziki wa Kitanzania uchukue asilimia 80 ya muda huo;
- (vii) Zinataka mamlaka husika kutengeneza Kanuni zinazotawala uingiaji wa mikataba ya kununua haki, kurusha matangazo (*airtime*) kama vile michezo, utaratibu ambaо bila kuwekewa masharti unaweza kuwanyima wananchi haki yao ya msingi ya kupata taarifa na hata burudani kutoka vyombo vya utangazaji vya umma ambavyo vina wajibu wa kurusha matangazo bure kwa wananchi; na

(viii) Zinataka madaraja yawekwe kwa kila filamu, video, wimbo au albamu kutoka ndani au nje ya nchi ndipo kazi hiyo itumike kwenye vyombo vyatangazaji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi msingi wa Kanuni hizi ni kuhakikisha teknolojia inatutumikia badala ya kututumikisha na kuvuruga mustakabali wa maadili ya Taifa letu. Ni Kanuni zilizozingatia mazingira yetu halisia kama Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Utamaduni na Sanaa, Wizara itaendelea na zoezi la kuhuisha Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 na kuendelea na utungaji wa Sera Mpya ya Filamu na uanzishaji wa Mfuko wa Sanaa pamoja na kuratibu na kusimamia Mjadala wa Kitaifa kuhusu Maadili na Kampeni ya Kitaifa ya Uzalendo yenye Kauli Mbiu "Nchi Yangu Kwanza". Aidha, Wizara itaratibu maandalizi ya Tamasha linaloitwa (*JAMAFEST*) ambalo Tanzania itakuwa mwenyeji mwaka kesho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama zinatarajia kuleta katika Tamasha la *JAMAFEST* wajasiriamali na wadau wa sekta za utamaduni, sanaa na ubunifu zaidi ya 1,200. Aidha, zaidi ya washiriki 20,000 wanatarajiwu kutoka nchini Tanzania. Hivyo, Tamasha hili ni fursa muhimu sana katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiutamaduni na pia ni njia mahususi ya kukuza viwanda vyatangazaji na kuteka soko la kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) litaendelea kuandaa na kurusha vipindi vyatangazaji ya lugha ya Taifa kupitia vyombo mbalimbali vyatangazaji ya lugha ya Kiswahili. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wenye ubobezi katika lugha ya Kiswahili watajitokeza kwa wingi kujisajili katika kanzidata ya Kiswahili ili kuchangamkia fursa zinazozidi kujitokeza ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Filamu itaendelea kuititia Miswada ya kutengeneza filamu, makala za filamu, matangazo ya biashara na michezo ya kuigiza na kutoa vibali kwa watayarishaji na wapiga pitcha kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi itaendesha operesheni dhidi ya kazi za filamu na michezo ya kuigiza zinazoingia sokoni bila kufuata taratibu na kuanzisha, kuendesha na kuwezesha Tamasha la Tuzo la Kimataifa (*Serengeti International Film Festival Award*). Bodi pia itaratibu utungwaji wa kanuni za usajili, mwonekano na uendeshaji wa vibanda vyta kuoneshea filamu nchini ambavyo vinakadiriwa kuwa zaidi ya 3,800 sasa hivi nchini ili kuhakikisha maadili yanazingatiwa katika uendeshaji wa shughuli katika vibanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Sanaa la Taifa litaendelea na zoezi la uibuaji na ukuzaji wa vipaji vyta sanaa kwa wanafunzi, kukuza soko la kazi za sanaa, kuratibu na kuitangaza Sekta ya Sanaa kwa kuendesha matamasha mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Michezo, Wizara itakamilisha uhuishwaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995, kuratibu ukarabati wa miundombinu Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru na maandalizi kwa ajili ya michezo wa (AFCON-U17) wa mwakani, kuratibu ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Manispaa ya Dodoma, kuchimba kisima cha maji safi, kujenga mifumo yake katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) litaendelea kusajili vyama na michezo na vituo mbalimbali na kutoa mafunzo ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Michezo kwa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda naomba sasa niongelee Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Makusanyo ya Mapato; mwaka 2018/2019 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Sh.1,077,804,000 kuititia vyanzo

vyake vinavyokusanya na Idara za Habari-MAELEZO na Maendeleo ya Michezo. Aidha, kwa upande wa Taasisi saba zilizo chini ya Wizara kiasi kinachokaridiriwa kukusanya na jumla ya Sh.32,761,620,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo; mwaka 2018/2019, Wizara imetengewa bajeti ya Sh.33,349,675,000/= Kati ya fedha hizo Mishahara ni Sh.15,253,265,000/=; Matumizi Mengineyo ni Sh.9,396,410,000/= na Miradi ya Maendeleo ni Sh.8,700,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2018/2019; ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2018/2019 naomba sasa niliombe Bunge Iako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2018/2019 ya jumla ya Sh.33,349,675,000/= . Kat i ya fedha hizo Mishahara ni Sh.15,253,265,000/=; Matumizi Mengineyo ni Sh.9,396,410,000/= na Miradi ya Maendeleo ni Sh. 8,700,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wadau mbalimbali walioshiriki katika kuwezesha kufikiwa kwa mafanikio mbalimbali katika mwaka 2017/2018. Wadau hao ni pamoja na nchi za Afrika Kusini, Australia, China, Cuba, India, Iran, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Misri, Morocco, Norway, Sweden, Ubelgiji, Uganda, Ujerumani na Urusi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni Umoja wa Ulaya (*EU*), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (*JICA*), *UNESCO* na *UNDP*. Wengine ni *AZAM TV*, *CRDB*, *NBC*, *Bank of Africa*, Kampuni ya *Coca-Cola*, *Geita Gold Mine*, *Multichoice Tanzania Limited*, Kampuni ya Bia ya Serengeti, *SportPesa*, *Startimes*, *Universal Communication Services Access Fund (UCSAF)* na wengine wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Waandishi wa Habari, Wanamichezo na Wasanii kwa mchango wao katika kufikia mafanikio ya Wizara. Aidha,

naishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia "Press A" kwa kuchapa Kitabu cha Hotuba yangu kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana vilevile katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: [www.habari.go.tz](http://www.habari.go.tz) na [www.maelezo.go.tz](http://www.maelezo.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## **1.0 UTANGULIZI**

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2018/19.

2. *Mheshimiwa Spika*, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya uenyekiti wa Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kwa kupokea, kujadili na hatimaye kuitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2018/19 kuititia Kikao chake cha tarehe 26 Machi, 2018. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu

imezingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa maendeleo ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**3. *Mheshimiwa Spika*,** kwa namna ya pekee kabisa naomba nimpongeze kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyosisitiza uzingatiwaji wa uzalendo, maadili, mila na desturi za Mtanzania katika Taifa letu. Ni muhimu sote tukakumbuka wosia wa Baba wa Taifa kuwa Taifa lisilokuwa na utamaduni wake ni taifa mfu na maendeleo ya Taifa lolote yanahitaji uadilifu, uzalendo, nidhamu, weledi na uwajibikaji.

**4. *Mheshimiwa Spika*,** nitumie nafasi hii pia, kukupongeza wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna ambavyo mnalisimamia vyema Bunge hilli ambalo ni mhimili muhimu kwa maendeleo ya watu na Taifa letu kwa ujumla. Aidha, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwawakilisha wananchi.

**5. *Mheshimiwa Spika*,** nawapongeza Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu: Mhe. Dkt. Godwin Mollel (Siha); Mhe. Said Maulid Mtulia (Kinondoni); Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Songea Mjini) na Mhe. Justin Joseph Monko (Singida Kaskazini).

**6. *Mheshimiwa Spika*,** nitumie fursa hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Kyela kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu ya ubunge. Ni matarajio yangu kuwa wana-Kyela watatumia kikamilifu fursa za kibiashara zinazoanza kujitokeza wilayani kutokana na kuanza kukamilika kwa miradi mikubwa ya miundombinu ya bandari, uchukuzi ziwani na barabara ya Kikusya-Matema. Aidha, nawashukuru wanangu kwa kuyakubali matokeo na mapenzi ya Mungu bila kinyongo pamoja na umri wao mdogo, kwa kurejesha amani, nuru na matumaini katika maisha yetu.

7. ***Mheshimiwa Spika***, sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Mhe. Juliana D. Shonza, Naibu Waziri; Bibi Susan P. Mlawi, Katibu Mkuu na Bw. Nicholas B. William, Naibu Katibu Mkuu. Niwashukuru pia Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma, tija na ufanisi.

8. ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2017/18, Bunge lako Tukufu lilipatwa na simanzi kubwa kwa kuondokewa na Mhe. Leonidas Gama, Mbunge wa Songea Mjini. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, Wananchi wa Jimbo la Songea Mjini na wanafamilia kwa kumpoteza Kiongozi huyo.

9. ***Mheshimiwa Spika***, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb), na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2017/18 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2018/19.

## **2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2017/18 Makusanyo ya Maduhuli**

10. ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2017/18, Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Sabini na Nne, Mia Sita na Mbili Elfu (Sh.1,574,602,000) kutokana na viingilio katika viwanja vya Taifa na Uhuru; malipo ya usajili wa magazeti na majarida; tozo ya matumizi ya Ukumbi wa Mikutano wa Idara ya Habari-MAELEZO; utoaji wa vitambulisho vya waandishi wa habari na mauzo ya picha mbalimbali za Viongozi wa kitaifa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Wizara ilikusanya Shilingi Milioni Mia Tano Hamsini na Sita, Mia Tatu Sitini Elfu, Mia Saba Sabini na Nane (Sh.556,360,778) sawa na asilimia 35 ya lengo la mwaka.

11. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Taasisi saba (7) zilizo chini ya Wizara kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni jumla

ya Shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni Mia Tisa Kumi na Mbili, Mia Tisa Thelathini na Tisa Elfu (Sh.36,912,939,000) ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Arobaini na Saba, Mia Tisa Thelathini na Nne Elfu, Mia Nne Sitini na Moja (Sh.14,047,934,461) zilikusanya sawa na asilimia 38 ya lengo la mwaka.

**12. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi hiki, Uwanja wa Taifa ulifungwa kwa miezi minne ili kuruhusu ukarabati katika uwanja huo ikiwemo upandaji wa nyasi mpya katika eneo la kuchezea. Aidha, Serikali ilianza upya usajili wa magazeti na majarida nchini ikiwa ni utekelezaji wa Sheria Mpya ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016. Vilevile, kumekuwepo na ongezeko la ushindani kwa huduma za radio, televisheni na magezeti pamoja na kukua kwa teknolojia ya mawasiliano kunakorahisisha na kuwezesha njia mbalimbali mbadala, nafuu na za haraka kutumika katika uhabarishaji na utoaji wa matangazo ya biashara.

#### **Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha**

**13. *Mheshimiwa Spika*,** mwaka 2017/18, Wizara iliiidhinishiwa Shilingi Bilioni Ishirini na Nane, Milioni Mia Mbili Kumi na Mbili, Mia Sita Tisini na Tano Elfu (Sh.28,212,695,000) kwa mchanganuo ufuatao:-

(a) **Matumizi ya Kawaida:** Shilingi Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Nane Tisini na Mbili, Mia Sita Tisini na Tano Elfu (Sh.21,892,695,000) zikijumuisha Mishahara Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Mbili Sabini na Sita, Mia Sita Kumi na Sita Elfu (Sh.17,276,616,000) na Matumizi Mengineyo Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Sita Kumi na Sita, na Sabini na Tisa Elfu (Sh.4,616,079,000); na

(b) **Miradi ya Maendeleo:** Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tatu Ishirini (Sh.6,320,000,000).

**14. *Mheshimiwa Spika*,** hadi mwezi mwezi Machi, 2018 Wizara ilipokea Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Moja Kumi na Tatu, Mia Nne Ishirini na Mbili Elfu, Mia Tisa Arobaini

na Mbili (Sh.18,113,422,942) ambayo ni sawa na asilimia 64 ya bajeti yote kwa mchanganuo ufuataao:-

(a) **Matumizi ya Kawaida:** Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Saba Hamsini na Tano, Mia Nne Ishirini na Mbili Elfu, Mia Tisa Arobaini na Mbili (Sh.13,755,422,942) ambayo ni sawa na asilimia 62, ambapo Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Saba Ishirini na Nane, Mia Moja Themanini na Nne Elfu, Mia Nne Ishirini na Sita (Sh.9,728,184,426) ni mishahara sawa na asilimia 56 na Shilingi Bilioni Nne, Milioni Ishirini na Saba, Mia Mbili Thelathini na Nane Elfu, Mia Tano Kumi na Sita (Sh.4,027,238,516) ni Matumizi Mengineyo sawa na asilimia 87; na

(b) **Miradi ya Maendeleo:** kiasi kilichopokelewa ni Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tatu Hamsini na Nane (Sh.4,358,000,000) sawa na asilimia 69.

### **3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2017/18**

**15.** *Mheshimiwa Spika*, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/18 hadi mwezi Machi, 2018 imeelezewa kwa kina kwa Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika sehemu ya 3.2 ukurasa wa 9 hadi 56 katika Kitabu cha Hotuba yangu. Kwa muhtasari naomba kutoa taarifa hiyo kama ifuatavyo:-

#### **SEKTA YA HABARI**

**16.** *Mheshimiwa Spika*, Sekta hii inahusisha Idara ya Habari-MAELEZO, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN). Katika Sekta hii hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu katika mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya mikutano minane (8) kati ya Msemaji Mkuu wa Serikali na Waandishi wa Habari ilifanyika na kuwezesha kutolewa kwa mrejesho kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo zinazoteklezwa Serikali;

(b) Jumla ya vipindi 49 vya televisheni vya TUNATEKELEZA vilitatibiiwa kupitia Idara ya Habari-MAELEZO na kurushwa hewani kupitia TBC1;

**17.** *Mheshimiwa Spika*, vipindi hivi vinatoa fursa kwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Watendaji Wakuu wa Mashirika, Taasisi, Wakala na Idara zinazojitegemea za Serikali kutoa taarifa kwa Umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya maeneo wanayosimamia ikiwemo kutatua changamoto za wananchi, maboresho katika utoaji wa huduma na mikakati inayotekeliza ya kuwaleta wananchi maendeleo.

(c) Mkutano wa Maafisa Habari ulioshirikisha zaidi ya Maofisa Habari 300 ulifanyika Mkoani Arusha tarehe 12-16 Machi, 2018. Mkutano huo pamoja na mambo mengine, ullenga kuimarisha uwezo wa utendaji wa Maafisa Habari wa Wizara na Taasisi za Serikali katika kuuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Serikali na kupokea mrejesho kutoka kwa wananchi kwa lengo la kufanyiwa kazi;

(d) Nakala 5,000 za Jarida la NCHI YETU lenye kuainisha Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha miaka miwili (2016-2017) zilichapishwa na kusambazwa katika Wizara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na kwa wananchi kwa ujumla. Aidha, toleo maalum la Jarida la NCHI YETU la Miaka 56 ya Uhuru wa Tanzania Bara lilichapishwa na nakala 4,000 kusambazwa; na

(e) Jumla ya magazeti na majarida 169 yalipatiwa Leseni ya Uchapishaji ambapo 21 ni ya Serikali na taasisi zake na 148 ya binafsi (hadi kufikia Machi 31, 2018). Leseni hizi zilitolewa kufuatia kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016.

**18.** *Mheshimiwa Spika*, Kwa upande wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) Shirika hilo lilitekeleza miradi minne (4) iliyolenga kuboresha usikivu na huduma ya utangazaji kama ifuatavyo:-

(a) Uwekaji wa mitambo ya kuongeza usikivu wa redio (TBC Taifa na TBC FM) katika maeneo ya mipakani, ikiwemo Rombo, Longido, Tarime, Kibondo na Nyasa. Hatua hii kwa upande wa Rombo imewezesha TBC kusikika katika eneo lote la Tarakea, Vijiji vya Olele, Miembea, Usseri, Mashima, Kibaoni na Mashati na katika baadhi ya maeneo ya Rombo Mkuu na Rongai. Aidha, kwa upande wa Longido, TBC inasikika katika maeneo ya Namanga, Kitombeine, Vijiji vya Oldonyosambu, Mirow na Engarnaibo.

Katika Wilaya ya Tarime, TBC inasikika katika maeneo ya Tarime Mjini, Sirari, Nyamuhonda, Nyamuigura na maeneo mengine jirani na wilaya hiyo. Vilevile, Wilaya za Kibondo na Kakonko usikivu unapatikana katika maeneo ya Kibondo Mjini, eneo lote la Wilaya ya Kakonko, na Vijiji vya Nyakanazi, Kifura, Kumhasha, Kumbanga, Mabamba, baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Biharamulo na Vijiji vya jirani mpakani na Tanzania katika nchi ya Burundi. Kwa upande wa Wilaya ya Nyasa usikivu unapatikana katika Mji wa Mbambabay, Vijiji vya Kilosa, Kipwili, Nangombo na Chinula.

Vilevile, usikivu wa mtambo wa Redio katika Wilaya ya Nachingwea umeongezwa kutoka *Watt* 100 (TBC FM) hadi *Watt* 1,000 na TBC<sub>Taifa</sub> kutoka *Watt* 250 hadi *Watt* 1,000 na hivyo kuwezesha kupanuka kwa usikivu katika wilaya na maeneo ya Nachingwea, Ruangwa na sehemu za Wilaya ya Masasi. Miradi yote hii imetekelizwa na mafundi wa TBC na hivyo kuliwezesha Shirika kuokoa fedha nydingi ambayo ingelipwa kwa makandarasi na kwa miradi michache;

(b) Ujenzi wa studio ya kisasa ya Redio Jamii katika Mkoa wa Arusha kwa ufadhili wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Services Access Fund-UCSAF*) ambayo ilizinduliwa tarehe 11 Machi, 2018. Kukamilika kwa studio hizi kutatoa fursa mbalimbali kwa Wananchi wa Mkoa wa Arusha ikiwemo kurusha matangazo ya Utalii, Biashara, Elimu, Burudani, Mila na Desturi, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

- (c) Uboreshaji wa mifumo ya urushaji matangazo kwa njia ya kidigitali ambapo TBC ilinunua mtambo wa Satelaiti (*Satellite Uplink*) na kuufunga katika Studio zake za Mikocheni. Hatua hii imewezesha mtambo huo kurusha mawimbi kwa kutumia njia mbili tofauti na hali iliyokuwepo awali ya kuwa na njia moja tu ambayo mbali na kuathiri muonekano wa TBC, ilitishia Televisheni ya Taifa kutoweka hewani endapo hitilifau yoyote ya kiufundi ingetokea;
- (d) Ununuzi wa magari tisa (9) kwa ajili ya shughuli za utangazaji pamoja na ununuzi wa vifaa vyta kisasa vyta kidijitali vyta kurusha matangazo mubashara.

**19.** *Mheshimiwa Spika*, kutokana na kuboresha mifumo ya urushaji matangazo kwa njia ya kidigit, tathmini ya sasa ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imebainisha ubora wa picha za televisheni ya TBC umeongezeka kutoka asilimia 52 hadi 88;

**20.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kufuatia agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, hatua ya uanzishwaji wa chaneli ya utalii inayoratibiwa na TBC kwa kushirikiana na wadau wakuu wa utalii nchini, zimefikia hatua nzuri. Matarajio ni kuanza kurusha matangazo ya majaribio katika chaneli hiyo mwezi Mei, 2018.

**21.** *Mheshimiwa Spika*, TBC na Kampuni ya *Star Communication Network Technology* ya China, ambao ni wabia wa Kampuni ya *StarMedia* waliweka saini makubaliano yanayolenga kurekebisha kasoro za kimkataba na za kiuendeshaji zilizosababisha Kampuni ya *StarMedia* kushindwa kupata faida tangu ilipoanzishwa miaka 7 iliyopita. Makubaliano hayo yaliwekwa saini tarehe 03 Aprili, 2018 Mjini Dodoma.

**22.** *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iliendelea kusimamia na kufuatilia maudhui yanayorushwa na vituo vyta utangazaji ikiwa ni pamoja na

yale ya Kielektroniki (Maudhui Mitandaoni) ambapo utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

(a) Kusajili jumla ya vituo 12 vya Redio na sita (6) vya Televisheni na kufanya idadi ya vituo vya Redio kufikia 158 na Televisheni 34;

(b) Kwa kushirikiana na Wizara, kuratibu utungaji wa Kanuni za Maudhui ya Redio na Televisheni na Kanuni za Maudhui ya Mitandaoni za mwaka 2018 chini ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010, ambazo zimeanza kutumika rasmi;

**23.** *Mheshimiwa Spika*, natoa wito kwa wadau wa huduma za utangazaji, wanahabari na wananchi kwa ujumla kuzielewa Kanuni hizo, zinazoweka utaratibu wa uendeshaji bora wa redio na televisheni na matumizi bora ya mitandao yanayozingatia maadili ya Kitanzania.

**24.** *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kuimarisha ubora wa magazeti yanayozalishwa na kampuni hiyo ikiwa ni pamoja na: kuboresha maudhui na mwonekano wa magazeti; kutenga kurasa maalum katika magazeti ya Daily News na HabariLeo kwa ajili ya habari za Makao Makuu ya nchi, Dodoma; kuchapisha matoleo maalum ya Afrika Mashariki kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kukamilisha muonekano mpya wa gazeti la HabariLeo kwa kulifanya kuwa na mvuto kuititia habari za Kikanda, Miji Mikuu na pia makala maalumu. Hatua nydingine zilizochukuliwa ili kuimarisha utendaji na mapato ya Kampuni ni:-

(a) Kuzindua mauzo ya gazeti la HabariLeo nchini Rwanda tarehe 18 Desemba, 2017 uliopokelewa kwa msisimko mkubwa;

(b) Kuimarisha habari mtandao kwa kununua vifaa vya kisasa na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Kitengo cha Habari Mtandao;

- (c) Kuendesha majukwaa matatu ya fursa za biashara na uwekezaji katika Mikoa ya Shinyanga, Tanga na Zanzibar na mwezi Mei, 2018 jukwaa hilo litafanyika Mkoani Arusha. Aidha, maandalizi yanaendelea kwa upande wa Mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Mara na Songwe pamoja na majukwaa ya kisekta kama Madini, Utalii na Ujenzi. Mipango inafanyika pia ili jukwaa hili lifanyike katika nchi za Afrika Mashariki na ughaibuni kwa lengo la kutangaza fursa zilizopo na hivyo kuvutia biashara na uwekezaji nchini. Kupitia majukwaa haya, TSN inatumia magazeti yake kuhabarisha na kuhamasisha wananchi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zilizopo na vilevile kupanua wigo wa biashara ya Kampuni;
- (d) Kuagiza karatasi moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji ikiwa ni hatua ya kupunguza gharama za uendeshaji ambapo shehena ya kwanza yenye uzito wa tani 150 imewasili kiwandani tarehe 19 Machi, 2018; na
- (e) Kuendelea na mchakato wa ununuzi wa mtambo wa uchapaji ambapo mtambo huo unatarajiwa kuzinduliwa mwezi Juni, 2018. Mtambo huu utaiwezesha TSN kutekeleza mradi wa uchapaji ambao utaimarisha mapato ya kampuni kupitia uchapaji wa machapisho mbalimbali ikiwemo vitabu, kalenda, shajara, mabango, taarifa mbalimbali, majarida na vipeperushi.

**25. *Mheshimiwa Spika***, jitihada hizi zimekuwa na mafanikio mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa matangazo sokoni kwa TSN kwa kupata asilimia 37.05 ya matangazo yote yanayochapishwa kwenye magazeti nchini ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.15 ikilinganishwa na asilimia 34.9 katika kipindi kama hiki mwaka 2016/17.

#### **SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI**

**26. *Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni inahusisha kuenzi, kulinda, kuhifadhi na kuweka kumbukumbu za urithi wa utamaduni usioshikika ikiwa ni pamoja na historia, mila, desturi, sanaa, lugha, maadili na uzalendo. Utekelezaji katika Sekta hii katika mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo:-

(a) Wizara iliendelea kufanya mapitio ya Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 kwa kuzingatia maoni ya Wadau yaliyopokelewa. Aidha, kwa kushirikiana na Wadau, Wizara iliendelea kuratibu uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu wenye lengo la kuwawezesha Wanatasnia ya Sanaa kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa mitaji ikiwa ni pamoja na mikopo yenyé masharti na riba nafuu;

(b) Taarifa na takwimu za maeneo ya kihistoria, utamaduni, mila na desturi zilikusanya katika Halmashauri za Wilaya za Babati, Morogoro, Tunduru na Ulanga na uchambuzi wa awali wa taarifa hizo umebaini maeneo yenyé vyanzo vya maji ambavyo hutumika kwa shughuli za uvuvi na vivutio vya utalii; mapango na maboma yaliyotumiwa na wenyeji wa Afrika na Jeshi la Kijerumani kujificha wakati wa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia;

(c) Ikiwa ni hatua ya kukuzaji na kuendeleza misamiati ya lugha ya Kiswahili na fasihi zake, taarifa na kumbukumbu za Khanga za kale zipatazo 150 zenyé maandishi ya lugha ya Kiswahili na misemo 120 iliyotokana na michezo ya timu za mpira wa miguu za Simba na Yanga zilikusanya kwa njia ya utafiti wa maktabani na kuhifadhiwa kwa njia ya kielektroni;

**27.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu Mkutano na Viongozi wa Madhehebu ya Dini uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2017, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Wajumbe zaidi ya 140, wakiwemo Viongozi wa Serikali, Viongozi wa Dini na Vyombo vya Habari. Mkutano huo uliazimia mambo mbalimbali ikiwemo Viongozi hao kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha vita dhidi ya rushwa, ukwepajji wa kulipa kodi na matumizi ya dawa za kulevya;

(d) Wizara kwa kushirikiana na wadau iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (*JAMAFEST*) liliofanyika nchini Uganda tarehe 7 - 17 Septemba, 2017 na kushirikisha jumla ya wajasiriamali wa Kitanzania wa kazi za kitamaduni, filamu, sanaa na ubunifu

wapatao 396. Wajasiriamali hao walipata fursa ya kutangaza na kuuza kazi zao pamoja na kuanzisha mitandao ya kibashara Itakayoimarisha masoko ya kazi zao katika ukanda wa Afrika Mashariki; na

(e) Wizara iliratibu Kampeni ya Kitaifa ya Uzalendo iliyozinduliwa tarehe 8 Desemba, 2017 Mkoani Dodoma na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na kuhudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Kitaifa akiwemo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa.

**28. *Mheshimiwa Spika*,** Kampeni hii ambayo ni endelevu, itakuwa inafanyika tarehe 14 Oktoba kila mwaka, Siku ya Kumbukumbu ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere na tarehe 7 Aprili ya kila mwaka, Siku ya Kumbukumbu ya Abeid Amani Karume ikiwa ni hatua ya kuenzi uzalendo ulioonyeshwa na Waasisi hawa wa Taifa.

**29. *Mheshimiwa Spika*,** tangu mwaka 2011, nchi yetu lilipewa dhamana kubwa na Umoja wa Afrika (AU) ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na vilevile kuwa mwenyeji wa Kituo Kikuu cha makumbusho na utafiti wa harakati za ukombozi barani Afrika. Taifa letu lilipewa heshima hii kubwa kutohana na kuwa kiongozi, ngome na kinara wa kuongoza harakati na mapambano ya kulikomboa Bara la Afrika.

**30. *Mheshimiwa Spika*,** Programu inalenga kubaini, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote kuhusu harakati za ukombozi wa Bara la Afrika ikiwa ni pamoja na vifaa, maeneo, majengo, nyaraka, kazi za sanaa, mahandaki, maelezo, sare, silaha, magari na hotuba kwa matumizi ya vizazi vyta sasa na vijavyo. Katika kipindi hiki Programu ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Kuorodhesha maeneo 25 yaliyotumika wakati wa harakati za ukombozi wa Bara la Afrika ili yakarabatiwe na

kutumika katika kukuza utalii wa kiutamaduni na kuhifadhi urithi wa ukombozi. Hadi sasa jumla ya maeneo 161 yamebainishwa; na

(ii) Kufanya mahojiano na wazee 82 walioshiriki au kushuhudia harakati za ukombozi wa Bara la Afrika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Pwani na Ruvuma na hivyo kuwezesha idadi ya wazee waliohojiwa hadi sasa kufikia 201.

**31.** *Mheshimiwa Spika*, taarifa zinazopatikana kuitia mahojiano hayo zitatumika katika kazi mbalimbali ikiwemo utafiti na uandishi wa majorida na vitabu mbalimbali vyta historia na uraia kwa madhumuni ya rejea na kufundishia.

**32.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu mkutano kati ya Tanzania na Afrika Kusini uliofanyika tarehe 16 hadi 19 Septemba, 2017 mjini Dodoma na kujadili masuala mbalimbali kuhusu uhifadhi wa urithi wa ukombozi. Aidha, mkutano wa Mawaziri wa Utamaduni wa Nchi za SADC uliofanyika Afrika Kusini tarehe 27 hadi 29 Machi, 2018 ulijadili utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika katika nchi za SADC na kuazimia pamoja na mambo mengine, kuendelea kufanya utambuzi na utunzaji wa maeneo na kumbukumbu zilizotumika katika harakati za ukombozi, kubadilishana utaalamu katika masuala mbalimbali ikiwemo utafiti na mafunzo yanayohusiana na urithi wa ukombozi;

**33.** *Mheshimiwa Spika*, nitumie nafasi hii kuipongeza na kuishukuru Serikali ya Afrika Kusini kwa kufanikisha mkutano huo wa Mawaziri wa Utamaduni wa Nchi za SADC chini ya uenyekiti wa Tanzania na kufikia maamuzi muhimu ya kuendeleza Programu hii. Namshukuru vilevile Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo wa SMZ, Mhe. Balozi Ali Karume kwa uwezo mkubwa alioonesha kuendesha mkutano huo.

**34.** *Mheshimiwa Spika*, Baraza la Kiswahili la Taifa liliendelea kuratibu na kusimamia matumizi fasaha na sanifu

ya lugha ya Kiswahili pamoja na maendeleo ya lugha hiyo kwa ujumla ndani na nje ya Nchi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

- (i) Kuandaa vipindi 56 vya Lugha ya Kiswahili vilivyorushwa kupitia TBC Taifa; vipindi 55 vya Kumepambazuka vilivyorushwa kupitia Radio One na vipindi 13 vya ufanuzi wa Msamati wa Kiswahili vilivyorushwa kupitia Redio Clouds FM na Idhaa ya Kiswahili ya Redio ya Umoja wa Mataifa;
- (ii) Kutoa huduma ya ukalimani wa lugha kwa Idara mbalimbali za Serikali, mashirika, kampuni, taasisi na watu binafsi ikiwemo katika Mikutano wa Bunge la Afrika uliofanyika Afrika Kusini mwezi Oktoba, 2017 na katika Mikutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika uliofanyika nchini Ethiopia mwezi Julai, 2017 na Januari, 2018;
- (iii) Kuendesha semina kwa watangazaji na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari ili kuhimiza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari, ikiwemo matumizi ya lugha yenye staha; na
- (iv) Kuandaa mfumo wa kielektroniki (kanzidata) wa kutunza kumbukumbu za Wataalam wa Lugha ya Kiswahili (walimu, wafasiri, wakalimani wa lugha za alama na lugha ya kawaida, wahariri na wanataaluma nyingine husianifu) nchini.

**35.** *Mheshimiwa Spika*, ninatoa wito kwa wataalamu wote kujisajili katika kanzidata hii ili wanufaike na fursa mbalimbali zitakazojitokeza ikiwemo fursa za kazi zinapojitokeza ndani na nje ya nchi kwa ada ndogo ya usajili ya Sh. 10,000 tu!

**36.** *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), majukumu yafuatayo yalitekelezwa:-

- (i) Kuwajenyea uwezo Wasanii na wadau wa Sanaa 50 kuhusu matumizi ya mitandao katika kutangaza na kuuza kazi za sanaa ndani na nje ya nchi;

- (ii) Kwa kushirikiana na kampuni ya *Data Vision International* na Shirikisho la Sanaa za Ufundi (TAFCA), kuanzisha mradi wa utambuzi wa wasanii wa sanaa za Ufundi nchini unaotambulika kwa jina la TACIP (*Tanzania Art and Crafts Identification Project*), wenyе lengo la kuwaunganisha wanasanaa za ufundi kupitia kanzidata mahsusii itakayowawezesha kujipanga vyema na kuuza kazi zao kupitia mifumo ya TEHAMA bila kumhitaji mtu wa kati;
- (iii) Kupitia uratibu wa BASATA, Umoja wa Wanamuziki (*Tanzania Music Foundation - TAMUFO*) kwa kushirikiana na kampuni ya *CogsNet Technologies* wanaendelea na uandaaji wa mfumo wa uhifadhi wa taarifa mtandaoni na kanzidata ya wasanii wa muziki ambapo kila mwanamuziki atakuwa na ukurasa wake kwa lengo la kujitangaza na kuongeza soko la kazi zao;
- (iv) Jumla ya wasanii binafsi 183, vikundi vyia Sanaa 151, wakuzaji 51 na kumbi 127 walisajiliwa na kuhuisha vibali vyao. Aidha, jumla ya kazi 448 za muziki ziliidhinishwa;
- (v) Kuendesha mafunzo ya siku tano (5) katika fani ya upigaji na uchezaji wa ngoma na midundo ya asili kwa watoto katika Wilaya ya Kisarawe, Mkoani Pwani. Mafunzo hayo ambayo yalilenga kuibua na kuendeleza vipaji vyia Sanaa kwa watoto yalishirikisha jumla ya watoto 100 na walimu sita (6) kutoka shule za msingi tano (5) Wilayani humo; na
- (vi) Kuendelea kutoa elimu kuhusu maadili na weledi katika kazi za sanaa kwa njia mbalimbali ikiwemo: kupitia tovuti yake, [www.basata.go.tz](http://www.basata.go.tz); kurasa za *twitter*; "basatatanzania"; *facebook*; "baraza la sanaa la taifa" na *Instagram*; "basata.tanzania". Aidha, elimu pia imeendelea kutolewa kupitia Jukwaa la Sanaa linalofanyika kila Jumatatu ya kwanza na ya mwisho ya kila mwezi jijini Dar es Salaam na mikoani na kupitia vyombo vyia Habari.

**37. *Mheshimiwa Spika*, Bodi ya Filamu Tanzania ilitekeleza majukumu yafuatayo:-**

- (i) Kutoa vibali 160 vya utayarishaji wa picha jongeve na michezo ya kuigiza ambapo 130 ni kwa waombaji kutoka nje ya nchi na 30 ni kwa Watanzania;
- (ii) Kuhakiki, kupanga madaraja na kutoa vibali kwa DVD 844 za filamu ambapo DVD 689 ni za Kitanzania na 155 ni kutoka nje ya nchi;
- (iii) Kuendelea kuwajengea uwezo wanatasnia ya filamu pamoja na makatibu wa Bodi za Filamu za Mikoa na Wilaya kuhusu namna ya kuboresha utayarishaji, usambazaji, uwekaji wa tafsiri, uoneshaji na ithibati kwa wanatasnia;
- (iv) Ikiwa ni hatua ya kuhakikisha Filamu zinazoingia sokoni zinafuata taratibu, jumla ya operesheni 22 zilifanyika na kuwezesha kukamatwa kwa jumla ya filamu 51 zilizoingia sokoni kinyemela;
- (v) Kuendelea kuhamasisha wadau wa filamu kutumia njia mbalimbali za usambazaji na uoneshaji wa kazi za filamu ikiwemo usambazaji kwa njia za mtandao. Miradi mbalimbali ya kusambaza kazi hizo imeanzishwa ili kazi za filamu zimfikie mlaji kwa urahisi, kama vile *Barazani Entertainment*, Max Burudani (kupitia Max Malipo) na *Cogsnet* kupitia Chaneli maalumu ya kuonesha filamu za kitanzania inayoitwa JTV inayopatikana katika king'amuza cha Startimes kupitia *Chaneli Na. 126* ambayo inamwezesha Mmiliki wa filamu inayooneshwa kulipwa kulingana na idadi ya watazamaji. Chaneli nyingine mahsusini zinazoonesha filamu za Kiswahili ni pamoja na Maisha Magic Bongo, Sinema Zetu, Sibuka na EATV;
- (vi) Jumla ya maeneo 3,863 yalibainishwa kwa ajili ya urasimishaji sawa na asilimia 77.26 ya maeneo 5,000 yaliyokusudiwa kwa mwaka 2017/18 ili kupanua wigo wa soko la kazi za filamu; na
- (vii) Wadau wa filamu waliendelea kuhamasishwa kushiriki katika matamasha, tuzo na maonesho ya bidhaa za filamu kitaifa, kikanda na kimataifa ili kujitangaza na kupanua

masoko ya kazi zao. Ushiriki wao umewezesha kupatikana kwa tuzo mbalimbali nchini na Kimataifa ikiwemo zifuatazo:-

- Yvone Cherry (Monalisa), aliyeshinda Tuzo ya *African Prestigious Awards* nchini Ghana mwaka 2018 katika kipengele cha *Best Female Actress*;
- Vincent Kigosi aliyeshinda Tuzo ya *African Prestigious Awards nchini* Ghana mwaka 2018 katika kipengele cha *Best Male Actor*;
- Moiz Hussein aliyeshinda Tuzo ya *African Prestigious Awards nchini* Ghana mwaka 2018 katika kipengele cha *Best Photographer*;
- Filamu ya T-Junction kuitia mtayarishaji Amil Shivji iliyoshinda Tuzo ya *Best African Feature at Women International Films Festival* nchini Zimbabwe nwaka 2017;
- Filamu ya Kiumeni kuitia mtayarishaji Nicholas Marwa iliyoshinda Tuzo ya *Best Director* katika Tamasha la *Zanzibar International Film Festivals (ZIFF)* mwaka 2017;
- Flamu ya Binti Zanzibar kuitia mtayarishaji Salum Maulid Stika iliyoshunda tuzo ya *Best Film (short film)* katika Tamasha la *SZIFF* mwaka 2018; na
- Filamu ya Harusi ya Teja kuitia mtayarishaji Musa Kitale iliyoshinda Tuzo ya *Best Comedian (Feature Films)* katika Tamasha la *Sinema Zetu International Film Festival* mwaka 2018.

**38.** *Mheshimiwa Spika*, nichukue fursa hii kuwapongezeka kwa dhati washindi wote na wale wote walioshiriki lakini hawakufanikiwa kupata tuzo. Ushiriki wao umedhihirisha kuwa wao ni chachu ya maendeleo ya Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini.

**39.** *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) yenye jukumu la kutoa

mafunzo ya sanaa na utamaduni, utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

- (i) Jumla ya wanachuo wa Astashahada 64 (wanawake 12, na wanaume 52); stashahada 53 (wanawake 8 na wanaume 45) na kozi fupi 112 (wanaume 86 na wanawake 26) walidahiliwa; na
- (ii) Tamasha la 36 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni liliofanyika mwezi Septemba, 2017 na kushirikisha jumla ya Vikundi 104 (Sanaa za Maonyesho 75 na Sanaa za Ufundu 29) ambapo vikundi 101 ni vya ndani ya nchi na vitatu (3) vilitoka Kisawa cha Mayote, Ufaransa na Zimbabwe liliratibiwa. Tamasha hili huendeshwa na TaSUBa kwa lengo la kutunza na kuenzi sanaa na utamaduni wa Mtanzania, kukutanisha watu wa tamaduni tofauti kutoka sehemu mbalimbali duniani ili kuonyesha kazi zao za sanaa na utamaduni wao pamoja na kuwawezesha wanafunzi wa Kitanzania kuanzisha na kuimarisha uhusiano na wasanii wa ndani na nje ya nchi.

#### **SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO**

**40. *Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Michezo nchini inasimamiwa na Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995. Malengo ya Sera hiyo ni pamoja na kuhamasisha Umma wa Watanzania kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo; kuwawezesha upatikanaji wa viwanja na zana bora na za kutosha kwa ajili ya kuimarisha maendeleo ya michezo nchini, kuandaa na kutayarisha wataalam wa kutosha katika fani na taaluma mbalimbali za michezo ili kuhakikisha timu na wachezaji wanafanya vizuri katika mashindano na michezo mbalimbali ya kimataifa. Katika Sekta hii utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

- (i) Zoezi la mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 liliendelea na Rasimu ya Sera hiyo imekamilika na ipo katika hatua za kuwasilishwa kwenye ngazi za maamuzi kwa ajili ya kuidhinishwa;

- (ii) Maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Vijana Wenye Umri chini ya Miaka 17 (AFCON U-17) mwaka 2019 yaliendelea kwa kuunda Kamati ya Maandalizi na Kamati za Kitaalamu ambazo zinakutana mara kwa mara kwa lengo la kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika kwa ufanisi mkubwa;
- (iii) Uwanja wa Taifa umefanyiwa ukarabati kwa kupanda nyasi eneo la kuchezea pamoja na kuvifanya marekebisho vyumba vya wachezaji kwa mujibu wa vigezo vya FIFA. Ukarabati umefanyika pia katika Uwanja wa Ndani wa Taifa katika maeneo ya mabenchi ya kukalia pamoja na kuwekwa zulia maalumu katika sakafu;
- (iv) Maandalizi ya ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Mkoani Dodoma yaliendelea ambapo zaidi ya ekari 168 kati ya ekari 328 za eneo la uwanja huo zimesafishwa pamoja na kufanya maandalizi ya awali ya kuandaa michoro ya uwanja;
- (v) Huduma ya kinga na tiba ilitolewa kwa wachezaji 645 ikihusisha wachezaji wa mpira wa miguu 320, mpira wa wavu 167, mchezo wa ngumi 48 na riadha 110. Aidha, waamuzi 400 na watazamaji 262 walipatiwa kinga hiyo; na

- (vi) Jumla ya Wanafunzi 124 walidahiliwa katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 78 ikilinganishwa na wanafunzi 46 waliodahiliwa mwaka 2016/17.

**41. *Mheshimiwa Spika*, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) lilitokeleza majukumu yafuatayo:-**

- (a) Kuandaa mashindano ya riadha kwa wanawake yaliyohusisha wanariadha 123 kutoka Mikoa 26 ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (*Japan International Cooperation Agency-JICA*);
- (b) Kuendesha Mashindano ya Taifa kwa watu *wenye mahitaji maalum yaliyofanyika* Zanzibar mwezi Desemba,

2017 kwa kushirikiana na Kamati ya Olimpiki Maalum. Mashindano hayo yalishirikisha wachezaji 497 kutoka mikoa 26 ya Tanzania Bara na mikoa mitano (5) ya Zanzibar;

(c) Kusajili Mashirikisho/Vyama 24, Vilabu vya Michezo 233, Vituo vya Michezo 17 na wakuzaji wa michezo 18;

(d) Kuratibu maandalizi ya Timu ya Tanzania iliyoshiriki michezo ya Jumuiya ya Madola Gold Coast, Australia mwezi Aprili, 2018, ambapo wachezaji wanne (4) wa ngumi za ridhaa, kuogelea mchezaji mmoja (1), Mpira wa Meza wachezaji wanne (4) na riadha na wachezaji sita (6) walishiriki; na

(e) Kwa kushirikiana na asasi ya *Joe's Gym* kuratibu pambano baina ya bondia Mtanzania Ibrahim Class dhidi ya bondia Koos Sibiya. Katika pambano hilo Mtanzania Ibrahim Class aliweza kutetea ubingwa wake wa Dunia wa *Global Boxing Council* (CBG) wa uzito wa kati kwa kumshinda mpinzani wake. Aidha, chini ya usimamizi wa Baraza, mabondia wengine wa Kitanzania waliendelea kushinda: Bondia Maono Ali tarehe 22 Februari, 2018 nchini Afrika Kusini alishinda ubingwa wa Dunia wa Vijana uzito wa kati (*WBC Youth*) dhidi ya Luka Tutek wa Croatia, bondia Bruno Tarimo aliyetwaa mkanda wa Dunia wa uzito wa kati wa WBA Oceania nchini Australia tarehe 24 Machi, 2018 kwa kumshinda bondia Billel Dib nyumbani kwao na Bondia Salehe Mkalekwa aliyetwaa Ubingwa wa *African Boxing Union (ABU)* baada ya kumsinda Bondia Andreas (*King Cheater*) Valavanis wa Misri katika pambano liliofanyika Jijini Nairobi, tarehe 21 Aprili, 2018.

#### **4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

**42.** *Mheshimiwa Spika*, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/18, changamoto zilijitokeza ambapo hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi kama inavyoelezewa kwa kina katika sehemu ya 4.0, ukurasa wa 56 hadi 58 wa Kitabu cha Hotuba.

43. *Mheshimiwa Spika*, changamoto hizo ni pamoja na kuendelea kuongezeka kwa mmomonyoko wa maadili ya Kitanzania; kuongezeka kwa *maudhui hasi ya mtandaoni pamoja na kuwepo kwa vipindi vya redio na Televisheni visivyozingatia weledi na maadili ya utangazaji na vyombo vya habari vya magazeti kutozingatia weledi wa taaluma na sheria za nchi na hivyo mara kwa mara kurudia makosa ya kitaaluma na kukiuka sheria. Wizara imeendelea kukabiliana na changamoto hizo kwa kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania, kuendelea kukutana na wamiliki wa Vyombo vya Habari na kuandaa Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni) na Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Redio na Televisheni) zote za mwaka 2018 ambazo zinaelekeza namna bora ya uendeshaji wa redio na televisheni pamoja na matumizi sahihi ya mitandao yanayozingatia utamaduni na maadili ya Mtanzania.*

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

44. *Mheshimiwa Spika*, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2017/18, naomba sasa kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2018/19.

45. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa kutekeleza majukumu yaliyofafanuliwa kwa kina Kisikta na kwa takwimu katika sehemu ya 5.0 ukurasa wa 59 hadi 73 wa Kitabu cha Hotuba.

46. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO itaendelea kuisemea Serikali kwa kukusanya, kusambaza na kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa Sera, Mipango, Miradi na Programu mbalimbali za Maendeleo; kuratibu uanzishwaji wa vyombo vipyta vya usimamizi wa masuala ya habari kama vile Dawati la Matangazo ya Serikali, Bodi ya Ithibati na Baraza Huru la

Habari vilivyoanzishwa chini ya Sheria Na.12 ya Huduma za Habari ya mwaka 2016. Aidha, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) litaanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu yake Mkoani Dodoma litakalotosheleza mahitaji ya shughuli za utangazaji na utawala; kununua magari 11 kwa ajili ya shughuli za utangazaji, utafutaji na uandishi wa habari, uandaaji wa vipindi na ufundi wa mitambo. Aidha, TBC itaanzisha Chaneli ya Utalii itakayorusha na kutangaza vipindi vinavyohusiana na maliasili na fursa mbalimbali zilizopo nchini na hivyo kukuza utalii wa ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro (NCAA), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) na Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyama Pori (TAWA).

**47.** *Mheshimiwa Spika*, Kampuni ya Magazeti Tanzania (TSN) itaendelea kupanua mauzo ya gazeti la HabariLeo katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kukuza lugha ya Kiswahili na kutangaza fursa za kibiashara zilizopo nchini; watajimarisha zaidi ki-mtandao ili kuboresha mauzo ya magazeti pamoja na kupanua zaidi wigo wa majukwaa ya fursa za biashara ikiwemo kuyaendesha katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nje ya Jumuiya hiyo ili kutangaza fursa za kibiashara na uwekezaji zilizopo Tanzania. Aidha, kampuni itaanza rasmi uchapaji wa machapisho mbalimbali kibiashara kwa kutumia mtambo mpya.

**48.** *Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kusimamia na kufuatilia maudhui yanayorushwa na vituo vya Televisheni na Redio, ikiwa ni pamoja na yale ya kielektroniki (maudhui ya mtandaoni)*, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itaendelea na mashauriano na wadau kuhusu uanzishwaji wa mfumo wa utangazaji wa redio za kidijiti ili kukabiliana na upungufu wa masafa ya kidijiti ya redio. Aidha, TCRA itaendelea kuhamasisha utengenezaji na uzalishaji wa maudhui ya ndani yanayozingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania. Vilevile, Mamlaka itaendelea kutoa elimu juu ya Kanuni mpya ya Maudhui Mitandaoni na Kanuni mpya ya Maudhui Redioni na kwenye luninga zilizotungwa chini ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 ambazo pamoja na mambo mengine:-

- (i) Zinazuia usambazaji wa kauli chafu, matusi, picha mgando na jongevu za utupu na zenyе maudhui yasiyofaa kwa watoto;
- (ii) Zinawaingiza kwenye mfumo rasmi wa kutambulika kisheria na kuwajibika kulipa kodi watoa huduma wa picha jongevu za habari na burudani na kutoa matangazo kwa njia za mitandao (bloggers);
- (iii) Zinamtaka kila mtumiaji wa mitandao (kwa faida yake) awe na namba yake ya siri ili wajanja wasitumie kiurahisi chombo chake cha mawasiliano kutenda matendo hasi kinyume na sheria;
- (iv) Zinaweka muda maalum (*watershed period*) ambao picha jongevu zote za filamu au muziki zenyе maneno na maeneo yasiyo mazuri kwa watoto zirushwe au kuoneshwa kwenye luninga katika muda maalumtu. Tuliweka muda huo maalum kuanzia saa 4:00 usiku hadi saa 11:30 asubuhi lakini wadau wamekuwa wakali sana, wanadai picha na nyimbo za aina hiyo zianze kurushwa saa 6:00 usiku wakati watoto wamelala na mwisho saa 11:00 asubuhi kabla watoto hawajaamka;
- (v) Zinatambua Kiswahili na Kiingereza tu kuwa lugha rasmi zitakazotumia kwenye matangazo ya redio na runinga;
- (vi) Zinataka kila redio na luninga kutoa kipaumbele kwa muziki wa Kitanzania kati ya saa 11:30 alfajiri hadi saa 3:00 usiku. Muziki wa Kitanzania uchukue asilimia 80 ya muda huo;
- (vii) Zinataka mamlaka husika kutengeneza Kanuni zinazotawala uingiaji wa mikataba ya kununua haki za kurusha matangazo (*airtime*) kama vile michezo, utaratibu ambao bila kuwekewa masharti unaweza kuwanyima wananchi haki yao ya msingi ya kupata taarifa na hata burudani kutoka vyombo vya utangazaji vya umma ambavyo vina wajibu wa kurusha matangazo bure kwa wananchi; na

(viii) Zinataka madaraja yawekwe kwa kila filamu, video, wimbo au albamu kutoka ndani au nje ya nchi ndipo kazi hizo zitumike kwenye vyombo vyatangazaji.

**49.** *Mheshimiwa Spika*, kwa kifupi msingi wa Kanuni hizi ni kuhakikisha teknolojia inatutumikia badala ya kututumikisha na kuvuruga mustakabali wa maadili ya Taifa letu. Ni Kanuni zilizozingatia mazingira yetu halisia kama Watanzania.

**50.** *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Sekta ya Utamaduni na Sanaa, Wizara itaendelea na zoezi la kuhuisha Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997; kuendelea na utungaji wa Sera Mpya ya Filamu na uanzishaji wa Mfuko wa Sanaa pamoja na kuratibu na kusimamia Mjadala wa Kitaifa kuhusu Maadili na Kampeni ya Kitaifa ya Uzalendo yenyewe Kauli Mbiu "Nchi Yangu Kwanza". Aidha, Wizara itaratibu maandalizi ya Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) ambalo Tanzania itakuwa mwenyeji mwaka 2019. Tamasha hili linahusisha maonesho ya kazi za Kiutamaduni na Ubunifu, Ujasiriamali, Filamu, Utalii, Historia; Makongamano na Midahalo na pia ni njia ya masoko ya kibiashara.

**51.** *Mheshimiwa Spika*, nchi wanachama zinatarajiwa kuleta katika Tamasha hili wajasiriamali na wadau wa sekta za utamaduni, sanaa na ubunifu zaidi ya 1,200. Aidha, zaidi ya washiriki 20,000 wanatarajiwa kutoka nchini. Hivyo, Tamasha hili ni fursa muhimu sana katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiutamaduni na pia ni njia mahususi ya kukuza viwanda vya ndani na kuteka soko la kikanda na kimataifa. Ni dhahiri Tamasha hili litahitaji gharama kubwa katika kuliendesha, hivyo kupitia Bunge lako Tukufu, nawaomba Wadau, Washirika wa Maendeleo na Watanzania kwa ujumla kushirikiana na Wizara katika kufanikisha tamasha hili kwa hali na mali ili kuendelea kuitangaza nchi yetu kama kitovu cha utajiri wa rasilimali mbalimbali na vilevile kutangaza bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu.

**52.** *Mheshimiwa Spika*, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) litaendelea kandaa na kurusha vipindi vya lugha ya Taifa

kupitia Vyombo mbalimbali nya Habari; kufanya tafsiri na ukalimani pamoja kusajili wataalamu wa Lugha ya Kiswahili. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wenye ubobezi katika lugha ya Kiswahili watajitokeza kwa wingi ili kuchangamkia fursa zinazozidi kujitokeza ndani na nje ya nchi.

**53. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi ya Filamu itaendelea kupitia Miswada ya kutengeneza filamu, makala za filamu, matangazo ya biashara na michezo ya kuigiza na kutoa vibali kwa watayarishaji na wapiga picha kutoka ndani na nje ya nchi; kuhakiki kazi za filamu; kubaini, kuimarisha, kuendeleza na kutolea ithibati za uendeshaji wa shughuli za filamu kwa makampuni na maeneo au/na miundombinu; kuendesha operesheni dhidi ya kazi za filamu na michezo ya kuigiza zinazoingia sokoni bila kufuata taratibu na kuanzisha, kuendesha na kuwezesha Tamasha na Tuzo la Kimataifa (*Serengeti International Film Festival and Award*). Bodi pia itaratibu utungwaji wa kanuni za usajili, muonekano, na uendeshaji wa vibanda nya kuoneshea filamu nchini ambavyo vinakadiriwa kuwa zaidi ya 3,800 kwa sasa ili kuhakikisha maadili yanazingatiwa katika uendeshaji wa shughuli katika vibanda hivyo.

**54. *Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa la Taifa*** itaendelea na zoezi la uibuaji na ukuzaji wa vipaji nya sanaa kwa wanafunzi; kukuza soko la kazi za sanaa; kuratibu na kuitangaza Sekta ya Sanaa kwa kuendesha matamasha mbalimbali na kusimamia na kuboresha udhibiti wa maadili katika Sekta ya Sanaa. Kwa upande wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni (TaSUBa), taasisi hiyo itadahili wanachuo 350; kuimarisha ubora katika kujifunza na kufundisha; kukarabati baadhi ya majengo ikiwemo maktaba pamoja na kuratibu Tamasha la 37 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo litakalofanyika mwezi Oktoba, 2018.

**55. *Mheshimiwa Spika*,** Katika Sekta ya Michezo, Wizara itakamilisha uhuishwaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995; kuratibu ukarabati wa miundombinu Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru kwa ajili ya maandalizi ya

mashindano ya mpira wa miguu ya vijana chini ya umri wa miaka 17 (AFCON-U17); kuratibu ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Manispaa ya Dodoma; kuchimba kisima cha maji safi na kujenga mifumo yake katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) litaendelea kusajili Vyama/Mashirikisho, Vilabu ya michezo na Vituo mbalimbali vya Michezo; kutoa mafunzo ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Michezo kwa Jamii na kusimamia utawala bora katika michezo ikiwemo kusimamia chaguzi za viongozi katika Vyama/Mashirikisho mbalimbali ya Michezo.

## **6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 Makusanyo ya Mapato**

**56.** *Mheshimiwa Spika*, mwaka 2018/19 Wizara inarajia kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Sabini na Saba, Mia Nane na Nne Elfu (Sh. 1,077,804,000)** kuitia vyanzo vyake vinavyokusanya na Idara za Habari-MAELEZO na Maendeleo ya Michezo. Aidha, kwa upande wa Taasisi saba (7) zilizo chini ya Wizara kiasi kinachokaridiriwa kukusanya ni jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Mbili, Milioni Mia Saba Sitini na Moja, Mia Sita Ishirini Elfu (Sh.32,761,620,000)**.

**Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

**57.** *Mheshimiwa Spika*, mwaka 2018/19 Wizara imetengewa bajeti ya Shilingi **Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Tatu Arobaini na Tisa, Mia Sita Sabini na Tano Elfu (Sh.33,349,675,000)**. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tatu, Mia Mbili Sitini na Tano Elfu (Sh.15,253,265,000)**, Matumizi Mengineyo ni **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Mia Nne Kumi Elfu (Sh.9,396,410,000)** na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Saba (Sh.8,700,000,000)**.

## **7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2018/19**

**58.** *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2018/19 naomba sasa niliombe Bunge Iao

Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2018/19 ya jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Tatu Arobaini na Tisa, Mia Sita Sabini na Tano Elfu (Sh.33,349,675,000)**. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tatu, Mia Mbili Sitini na Tano Elfu (Sh.15,253,265,000)**, Matumizi Mengineyo ni **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Mia Nne Kumi Elfu (Sh.9,396,410,000)** na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Saba (Sh.8,700,000,000)**.

## **8.0 SHUKRANI**

**59.** *Mheshimiwa Spika*, kwa niaba ya Wizara, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Wadau mbalimbali walioshiriki katika kuwezesha kufikiwa kwa mafanikio mbalimbali katika mwaka 2017/18. Wadau hao ni pamoja na nchi za Afrika Kusini, Australia, China, Cuba, India, Iran, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Misri, Morocco, Norway, Sweden, Ubelgiji, Uganda, Ujerumani na Urusi. Wadau wengine ni Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Wengine ni AZAM TV, Benki ya CRDB, Benki ya Taifa ya Biashara, Bank of Africa, Kampuni ya Coca-Cola, Geita Gold Mine, Multichoice Tanzania LTD, Kampuni ya Bia ya Serengeti, SportPesa, Startimes, Universal Communication Services Access Fund (UCSAF) na wengine wengi.

**60.** *Mheshimiwa Spika*, nichukue fursa hii pia kuwashukuru Waandishi wa Habari, Wanamichezo na Wasanii kwa mchango wao katika kufikia mafanikio ya Wizara. Aidha, ninaishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia "Press A" kwa kuchapa Kitabu cha Hotuba yangu kwa wakati.

**61.** *Mheshimiwa Spika*, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: [www.habari.go.tz](http://www.habari.go.tz) na [www.maelezo.go.tz](http://www.maelezo.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati au kwa niaba. (*Makofii*)

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa fasili ya 6(5)(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu yote ya kisera yanayotekelizwa na Wizara hii. Aidha, majukumu ya Kamati katika Wizara kuhusiana na uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka yameelekezwa katika fasili ya 7(1), Kamati Inatekeleza ipasavyo majukumu hayo. Taarifa hii imejielekeza zaidi katika masuala makubwa matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza ya 8(6)(5)(c) iliyochini ya Kanuni ya 18 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Kwa mujibu wa Fasili ya (7)(1)(a) ya Nyongeza ya Nane, imetaja Majukumu ya Kamati kisekta ikiwemo kushughulikia Bajeti ya Wizara. Hivyo Kamati hii kama

zilivyo Kamati nyingine za kisekta imetekeliza jukumu hili ipasavyo.

(i) Uchambuzi wa Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti na maoni ya kamati kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018. Pamoja na maelezo mengine, uchambuzi huu umejielekeza pia katika ukusanyaji wa maduhuli na mwenendo mzima wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 na hali ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo;

(ii) Uchambuzi wa mpango wa Wizara kuhusu makadirio ya mapato na matumizi yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Uchambuzi huu umejielekeza katika aina na kiasi cha mapato ikilinganishwa na mwaka uliotangulia na matumizi yanayokusudiwa;

(iii) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mapendekezo hayo yatajielekeza pia katika suala la Bajeti ya Wizara; Usimamizi wa michezo mashulenii; Taratibu za hatua za kinidhamu kwa wasanii; Ufanisi wa Shirika la Utangazaji la Taifa (*TBC*); Mapato ya Wizara katika Uwanja wa Taifa; Ufanisi wa timu ya Taifa ya mpira wa miguu; Vyuo vya Michezo nchini; Ujenzi wa viwanja vya michezo; kazi za wasanii; pamoja na lugha ya Kiswahili na Ukalimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 wakati Kamati inawasilisha taarifa yake kuhusu Bajeti ya Wizara hii ilioa jumla ya maoni tisa kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Wizara. Kamati imepitia taarifa ya utekelezaji wa maoni hayo na inaona kwa kiasi kikubwa yametekeliza. Aidha, baadhi ya maoni bado hayajatekelezwa kikamilifu na Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inakamilisha utekelezaji wa maoni hayo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara imetekeliza shughuli mbalimbali kama

zilivyoelezwa kwa kina na Mheshimiwa Waziri. Kamati imejiridhisha kuwa Utekelezaji wa shughuli hizo umezingatia Mpango kazi wa Wizara, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 pamoja na Miongozo mbalimbali ya Wizara na Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo yenye Fungu 96 ilipanga kukusanya Sh.38,881,541,000/= . Kati ya makadirio hayo, Sh.1,574,602,000/= ni kutoka katika makusanyo ya Idara na Sh.36,912,939,000/= ni kutoka katika makusanyo ya Taasisi saba zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Wizara ilifanikiwa kukusanya Sh.12,520,368,792/= sawa na asilimia 32 ya malengo. Kati ya fedha hizo, Sh. 515,889,316/= sawa na asilimia 32.8 ya lengo zilikusanya kutoka katika Idara zilizo chini ya Wizara na kiasi cha Sh.12,004,479,476/= sawa asilimia 32.5 ni kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara, Rejea Kielelezo Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesikitishwa na ukusanyaji huu wa kiwango cha chini kabisa wakati tukiwa tayari tupo kwenye robo ya tatu ya mwaka wa fedha. Pamoja na maeleo ya Wizara kuhusu sababu zilizosababisha makusanyo yashuke ikiwemo usajili wa magazeti na majarida kujitokeza kwa kiwango cha chini yaani 163 ikilinganishwa na Makadirio ya usajili wa magazeti na majarida 400. Kamati inaitaka Wizara kuendelea kuhamasisha wamiliki wa magazeti kusajili magazeti na majarida yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Fungu 96 iliidhinishiwa Sh.28,212,695,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake. Kati ya fedha hizo, Sh.21,892,695,000/= sawa na asilimia 77.5 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo pia Sh.17,276,616,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Idara na

Taasisi na Sh.4,616,079,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, kiasi cha fedha cha Sh.6,320,000,000/= sawa na asilimia 22.5 kilitengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hadi kufikia Februari 2018, Wizara ilikuwa imepokea Sh.16,722,577,401/= tu sawa na asilimia 59 ya Bajeti yote. Kati ya Fedha hizo, Sh.12,364,577,401/= sawa na asilimia 73.9 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.8,659,390,884/= kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Idara na Taasisi na Sh.3,706,484,866/= kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilipokea Sh.4,358,000,000/= sawa na asilimia 68.9 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hivyo, pamoja na kwamba mipango ilikuwa ikitekelezwa kwa mujibu wa miongozo ya kitaifa, kiasi cha utekelezaji kimekuwa ni cha kusuasua kutokana na mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa fedha zilizotengwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kielelezo Na. 2(a), (b) na (c) kinaonesha Mchanganuo wa Upatikanaji wa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyobainika katika ziara ya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo; Kamati imebaini kuwa kati ya Miradi iliyotengewa fedha katika Mwaka wa fedha 2017/2018 ni Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa *TBC* uliotengewa Sh.3,000,000,000/= na zote zimetolewa na Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha zote za Mradi kutokana na umuhimu wake katika kutoa taarifa kwa umma. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha za Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na za Miradi wa Eneo Changamano la Michezo Dodoma ili miradi hii nayo iweze kukamilika kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019; Kamati iliipata fursa ya kuchambua na kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama inavyoelezwa kwa kina kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) inakadiria kukusanya Sh.33,839,424,000. Kati ya makadirio hayo Sh.1,077,804,000 sawa na asilimia 3.1 ya Makadirio kitakusanya kutoka katika Idara zilizo chini ya Wizara. Aidha, Sh.32,761,620,000 sawa na asilimia 96.8 kitakusanya kutoka katika taasisi zilizo chini ya usimamizi wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa, makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa fedha ni pungufu kwa asilimia 12 ya kiasi kilichokadiriwa katika mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati ilielezwa kuwa upungufu wa makadirio haya ni kutokana na taasisi za Wizara kutokutana na Msajili wa Hazina kwa ajili ya kuidhinishiwa viwango vya makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kutoa maelezo kama tayari Taasisi hizi zimeshakutana na Msajili na Makadirio yakoje ili Wizara iweze kukusanya maduhuli hayo. Mchanganuo wa ulinganisho wa makadirio haya ni kama unavyoonekana katika kielelezo Na.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara inaomba kuidhinishiwa Sh.33,349,675,000 kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake. Matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha mishahara na matumizi mengineyo yanaombewa Sh.24,649,675,000 sawa na asilimia 73.9 ya bajeti yote ya Wizara. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo inaombwa Sh.8,700,000,000 sawa na asilimia 26.1 ya bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka huu na ile iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na imebaini yafuatayo:-

(a) Bajeti ya mwaka 2018/2019 imepungua kwa Sh.5,136,980,000 sawa na asilimia 15.4 ya bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018;

(b) Bajeti ya mishahara ya mwaka 2018/2019 imepungua kwa asilimia 11.7 kutoka Sh.17,276,616,000 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 hadi kufikia Sh.15,253,265,000 zilizoombwa katika mwaka wa fedha wa 2018/2019;

(c) Bajeti ya matumizi mengineyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imeongezeka kwa Sh.4,780,331,000 na kufikia Sh.9,396,410,000 sawa na ongezeko la asilimia 50.8 la Sh.4,616,079,000 zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha wa 2017/2018;

(d) Bajeti ya Miradi ya Maendeleo imeongezeka kutoka Sh.6,320,000,000 mwaka 2017/2018 hadi kufikia Sh.8,700,000,000 sawa na ongezeko la asilimia 27.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara hii na ina amini kabisa kuwa fedha zote hususan za kutekeleza Miradi ya Maendeleo zitatolewa kabla ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati, baada ya uchambuzi wa Kamati naomba sasa kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti, kama ambavyo imeonekana katika uchambuzi wa Kamati, hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 59 tu ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kamati inaamini kabisa asilimia 41 iliyobaki

ni muhimu sana kwa kuwa pia inajumuisha fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo zimekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Kamati. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa, kiasi kilichobaki cha asilimia 41 kinatolewa kwa Wizara kabla mwaka huu wa fedha kwisha ili iweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Huduma za Habari. Sheria hiyo ili itekelezwe kikamilifu, suala la utungaji wa Kanuni ni muhimu sana. Kamati imebaini kuwa Kanuni bado hazijatungwa lakini pia vyombo muhimu kama vile Baraza Huru la Habari na Bodi ya Ithibati ya Wanahabari nazo bado hazijaundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwa tupo kwenye kipindi cha mpito katika kuelekea kutekeleza sheria hili, hata hivyo kipindi hili cha mpito hakizui kuundwa kwa vyombo hivi muhimu. Kamati inaitaka Serikali kueleza Bunge lako Tukufu ni lini itakamilisha kutunga kanuni hizi lakini pia lini itakamilisha kuunda vyombo hivi muhimu kwa maendeleo ya tasnia ya habari nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua umuhimu wa michezo na inaona ipo haja kabisa kwa Serikali kuweka usimamizi thabiti wa Michezo kwa kushirikishiana na TAMISEMI ili kuinua michezo shulenii kupitia UMITASHUMTA na UMISETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha michezo shulenii kutasaidia kuibua vipaji vya vijana. Si hivyo tu, wote tunafahamu michezo ni afya, kama kweli tunataka kuwa Taifa imara lenye vijana hodari na chapakazi yatupasa kuzingatia michezo kuanzia ngazi ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha wa 2018/2019 moja ya mipango ya Wizara ni kuendeleza mpango wa michezo kwa jamii ikiwa ni pamoa na kusimamia mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA kwa kushirikiana na TAMISEMI ili zoezi hili liweze kutekelezwa upatikanaji wa fedha ni jambo la msingi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya Baraza la Michezo la Taifa

ambalo ndilo lenye wajibu wa kusimamia michezo zinatolewa zote na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Wizara ilifungia nyimbo na wasanii kwa maelezo kuwa baadhi ya nyimbo zao haziendani na maadili yetu. Kamati inatambua umuhimu wa kuzingatia maadili ya Mtanzania lakini hata hivyo utaratibu unaotumika siyo mzuri na unaleta changamoto kwa wasanii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(a) Vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sanaa nchini kuhakikisha vinatimiza majukumu yao kwa kukagua nyimbo zote za wasanii kabla hazijatoka ili kuhakikisha hakuna wimbo unaotoka kama haujazingatia maadili;

(b) Kuangalia nyimbo ambazo ni za kimataifa na kuzipa kibali maalum kwa maana ya muda na mahali pa kuutumia wimbo huo kabla haujaanza kutumiwa na vyombo vya habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji la Taifa (*TBC*), pamoja na Serikali kutoa bajeti yote ya miradi ya maendeleo ya *TBC* kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kiasi cha shilingi billioni tatu, lakini fedha hizi bado hazitosh. Itakumbukwa katika maoni ya Kamati kuhusu bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa msingi huo basi, Kamati inashauri Serikali kulifanya kazi andiko la *TBC* lenye kuonesha mahitaji muhimu ya Shirika ambapo inakadiriwa kiasi cha shilingi billioni 80 zinahitajika na kutoa fedha ili *TBC* Radio iweze kusikikia nchi nzima kwani kuna baadhi ya mikoa haipati matangazo ya *TBC* kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya Uwanja wa Taifa; Kamati inatambua kuwa mapato ya uwanja wa Taifa na uhuru ni makubwa na yamekuwa yakichanganywa kwa

makusudi ili kuchanganya wadau. Aidha, kumekuwepo na fedha zinazojulikana kwa jina la fedha za Mchина kwa kila mchezo kwa kuwa wamekuwa wakilipwa Wachina wanaohudumia uwanja. Kamati inahojи kuhusu suala hili, lakini hajapata maelezo ya kuridhisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Mapato ya Uwanja wa Taifa na Uhuru yasichanganywe, yatenganishwe;

(b) Uchunguzi ufanywe kuhusu fedha za Mchина zinazokatwa katika kila mchezo na Bunge lako Tukufu lipewe taarifa;

(c) Uwepo udhibiti wa mapato yatokanayo na uuzaji wa tiketi kwa njia ya kielektroniki wakati wa mechi za mpira wa miguu kwa kuwa fedha nyingi zimekuwa zikiibwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ya Taifa ya mpira wa miguu, Kamati imebaini kuwa bado Timu zetu hazifanyi vizuri katika mashindano mbalimbali. Kamati imebaini moja ya sababu inayochangia kutofanya vizuri ni kutoandaliwa vizuri kwa timu zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inashauri kuanzia sasa timu zetu ziandaliwe vyema ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi za masomo makocha wetu wa ndani ili wawe na viwango vinavyokubalika kimataifa na muda wa maandalizi wa kutosha uwepo kwa kuwaweka katika kambi moja ili ziweze kushiriki kikamilifu kwenye mashindano na kurudi na ushindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Michezo Nchini; Kamati imebaini kuwa kwa sasa hakuna vyuo vinavyozalisha Walimu wa Michezo kutokana na vyuo hivyo kufungwa. Kamati inaitaka Serikali kufufua vyuo hivyo ili viweze kuendelea kutoa mafunzo kwa Walimu ambao ni nyenzo muhimu katika michezo yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa viwanja vya michezo; kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo Kamati imekuwa ikiongelea suala la ujenzi wa viwanja vya michezo nchini. Kamati inaendelea kusisitiza ujenzi wa viwanja vya michezo ambapo kwa kuanzia inaitaka Wizara hii pamoja na TAMISEMI kukaa pamoja ili kuainisha mahitaji halisi ikilinganishwa na viwanja vilivyopo ili kubaini upungufu. Kamati inatambua bila uwepo na viwanja, mafanikio katika michezo hayawezi kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za wasanii; tatizo la wizi wa kazi za wasanii ni tatizo la muda mrefu na Kamati imekuwa ikilisemea mara kwa mara. Kamati bado inaendelea kusisitiza suala hili na kuwataka wale wote wanaohusika katika udhalimu huu kuacha mara moja. Aidha, Kamati inawashauri wasanii waboreshe kazi zao na hususan filamu kutokana na maendeleo ya teknolojia ili ziweze kuteka soko la ndani na nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lugha ya Kiswahili na Ukalimani, lugha ya Kiswahili ni mionganini mwa lugha za kimataifa kwa maana ya kwamba inatumika hata katika mikutano mikubwa ya kimataifa ambako mara nyingi viongozi wetu wa kitaifa wanakwenda kuhudhuria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya lugha hiyo kutumika katika mikutano hiyo ya kimataifa, kiswahili hutumika katika majadiliano ya mikataba mbalimbali ya kimataifa ambapo ili kukubaliana vyema katika hadidu za rejea (*terms of reference*) mbalimbali lugha inaweza kusaidia au kuwa sehemu ya changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua tatizo hilo hapa nchini la kutofahamu ipasavyo lugha ya Kiingereza hasa katika mikutano inayohusisha masuala mbalimbali. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iweke mkakati wa kuwa na kanzidata ya wataalam wote wa lugha ya Kiswahili nchini ili watumike kama Wakalimani katika maeneo mbalimbali hasa katika mikutano ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imetoa fursa ya ajira kwa Watanzania lakini pia fursa kubwa ya kuikuza lugha ya Kiswahili nje ya mipaka ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti. Aidha, namshukuru pia Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee zaidi naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mzuri walionao na wameonesha umahiri na weledi wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara hili. Naomba majina ya Wanakamati wote yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe; Naibu Waziri, Mheshimiwa Juliana Shonza; na watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Susan Mlawi na Naibu wake Ndugu Nicholaus Benjamin Benjamin kwani Wizara imekuwa ikitoa ushirikiano mzuri kwa Kamati muda wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa uongozi mahiri na kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Namshukuru pia Ndugu Athuman B. Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge; na Ndugu Dickson Bisile, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru sana Makatibu wa Kamati hii Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Agnes Nkwera kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pamoja nao namshukuru Msaidizi wa Kamati

Ndugu Modester Kipiko na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa uchambuzi mzuri ambao umewezesha sisi kama Kamati kutekeleza majukumu yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Fungu 96, Sh.33,349,675,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***SEHEMU YA KWANZA***

---

**1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Fasili ya 6(5)(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu

yote ya kisera yanayotekelawa na Wizara hii. Aidha, majukumu ya Kamati katika Wizara kuhusiana na Uchambuzi wa Bajeti ya kila mwaka yameelekezwa katika Fasili ya 7(1), Kamati imetekeleza ipasavyo majukumu hayo. Taarifa hii imejielekeza zaidi katika masuala makubwa matatu (3) yafuatayo;

Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane (6) (5) (c) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Kwa mujibu wa Fasili ya (7) (1) (a) ya Nyongeza ya Nane, imetaja Majukumu ya Kamati za Kisekta ikiwemo la kushughulikia Bajeti za Wizara. Hivyo Kamati hii kama zilivyo Kamati nyininge za Kisekta imetekeleza jukumu hili ipasavyo.

1.1 Uchambuzi wa Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti na maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha wa 20117/2018. Pamoja na maelezo mengine, uchambuzi huu umejielekeza pia katika ukusanyaji wa maduhuli na mwenendo mzima wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 na hali ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo;

1.2 Uchambuzi wa mpango wa Wizara kuhusu makadirio ya mapato na matumizi yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Uchambuzi huu umejielekeza katika aina na kiasi cha mapato ikilinganishwa na mwaka uliotangulia na matumizi yanayokusudiwa;

1.3 Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara pamoja na Makadirio ya Mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mapendekezo hayo yatajielekeza pia katika suala la Bajeti ya Wizara, Usimamizi wa Michezo mashulenii, Taratibu za hatua za kinidhamu kwa wasanii, Ufanisi wa Shirika la Utangazaji la Taifa TBC, Mapato ya Wizara katika uwanja wa taifa, Ufanisi wa timu ya Taifa ya mpira wa miguu, Vyuo vya Michezo nchini, Ujenzi wa viwanja vya michezo, Kazi za wasanii pamoja na Lugha ya Kiswahili na Ukalimani.

***SEHEMU YA PILI***

**2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO  
WA BAJETI NA UZINGATIWAJI WA MAONI YA KAMATI  
KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 wakati Kamati inawasilisha Taarifa yake kuhusu Bajeti ya Wizara hii ilioa Jumla ya Maoni Tisa (9) kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Wizara. Kamati imepitia Taarifa ya utekelezaji wa maoni hayo na inaona kwa kiasi kikubwa yameteketelezwa. Aidha, baadhi ya maoni bado hayajatekelezwa kikamilifu na Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inakamilisha utekelezaji wa maoni hayo ya Kamati.

**2.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa  
Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara imetekeleza shughuli mbalimbali kama zilivyoolezwa kwa kina na Mheshimiwa Waziri. Kamati imejiridhisha kuwa Utekelezaji wa shughuli hizo umezingatia Mpango kazi wa Wizara, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021), Ilani ya Uhcaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 pamoja na Miongozo mbalimbali ya Wizara na Kitaifa.

**2.2 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo yenye **Fungu 96** ilipanga kukusanya shilingi **38,487,541,000/=**. Kati ya makadirio hayo, shilingi **1,574,602,000/=** ni kutoka katika makusanyo ya Idara na shilingi **36,912,939,000/=** ni kutoka katika makusanyo ya Taasisi 7 zilizo chini ya Wizara.


**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Mwezi Februari, 2018, Wizara ilifanikiwa kukusanya shilingi **12,520,368,792** sawa na **asilimia 32.5** ya malengo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 515,889,316/=** sawa na **asilimia 32.8** ya lengo zilikusanywa kutoka katika Idara zilizo chini ya Wizara na kiasi cha shilingi **12,004,479,476/**

= sawa **asilimia** 32.5 kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara Rejea Kielelezo Na. 1.

*Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na ukusanyaji huu wa kiwango cha chini kabisa wakati tukiwa tayari tupo kwenye robo ya tatu ya mwaka wa fedha. Pamoja na maelezo ya Wizara kuhusu sababu zilizosababisha makusanyo yashuke ikiwemo ya usajili wa magazeti na majarida kujitokeza kwa kiwango kidogo (163 ikilinganishwa na Makadirio ya usajili wa magazeti na majarida 400). Kamati inaitaka Wizara kuendelea kuhamasisha wamiliki wa magazeti kusajili magazeti na majarida yao.*

### Kielelezo Na. 1

#### MAKADIRIO NA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2017/2018



**Chanzo: Usanifu wa Kamati kwa Randama ya Wizara**

### 2.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Fungu **96** iliidhinishiwa shilingi **28,212,695,000/=** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake. Kati ya fedha hizo, shilingi

**21,892,695,000/=** sawa na **asilimia 77.5** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo pia shilingi **17,276,616,000/=** zilikuwa ni kwaajili ya mishahara ya Watumishi wa Idara na Taasisi na shilingi **4,616,079,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, kiasi cha shilingi **6,320,000,000/=** sawa na **asilimia 22.5** kilitengwa. Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Februari 2018, Wizara ilikuwa imepokea shilingi **16,722,577,401/=** tu sawa na **asilimia 59** ya Bajeti yote. Kati ya Fedha hizo, shilingi **12,364,577,401/=** sawa na **asilimia 73.9** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Shilingi **8,659,390,884/=** kwaajili ya mishahara ya watumishi wa Idara na Taasisi na shilingi **3,706,484,866/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo)

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ilipokea shilingi **4,358,000,000/=** sawa na **asilimia 68.9** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hivyo, pamoja na kwamba milango ilikuwa ikitekelezwa kwa mujibu wa miongozo ya kitaifa, kiasi cha utekelezaji kimekuwa ni cha kusua kutokana na mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa fedha zilizotengwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kielelezo Na. 2 (a), (b) na (c) kinaonesha Mchanganuo wa Upatikanji wa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

#### Kielelezo Na. 2 (a)

IDARA	KILICHOIDHINSHWA	KILICHOPOKELEWA	ASILIMA
MSAHARA	4,389,869,000	2,397,785,484	54.6
MATUMIZI MENGINEYO	3,405,783,000	2,839,197,366	83.4
MRADI YAMAENDELEO	3,320,000,000	1,358,000,000	40.9
<b>JUMA</b>	<b>11,115,652,000</b>	<b>6,594,982,850</b>	<b>59.3</b>
TAASISI	KILICHOIDHINSHWA	KILICHOPOKELEWA	ASILIMA
MSAHARA	12,886,747,000	6,261,605,400	48.6
MATUMIZI MENGINEYO	1,210,296,000	867,287,500	71.7
MRADI YAMAENDELEO	3,000,000,000	3,000,000,000	100
<b>JUMA</b>	<b>17,097,043,000</b>	<b>10,128,892,900</b>	<b>59.2</b>

*Chanzo: Randama ya Wizara*


## Kielelezo Na. 2 (b)

**Chanzo: Usanifu wa Kamati kwa Randama ya Wizara**

### UPATIKANAJI WA FEDHA ZA IDARA KWA MWAKA

2017/2018

### UPATIKANAJI WA FEDHA ZA TAASISI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018



**Chanzo: Usanifu wa Kamati kwa Randama ya Wizara**

## 2.4 Yaliyobainika Katika Ziara ya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kati ya Miradi iliyotengewa fedha katika Mwaka wa fedha 2017/2018 ni Mradi wa Upanuzi wa Usikivu – TBC ilitengewa **shilingi 3,000,000,000/=** na zote zimetolewa na hazina.

*Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha zote za Mradi kutokana na umuhimu wake katika kutoa taarifa kwa umma.* Aidha, Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha za Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na za Mradi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma ili miradi hii nayo iweze kukamilika kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha.

### ***SEHEMU YA TATU***

---

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama inavyoelezwa kwa kina kwenye Taarifa hii.

### 3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato


**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**) inakadiria kukusanya shilingi **33,839,424,000/=**. Kati ya makadirio hayo shilingi **1,077,804,000/=** sawa na **asilimia 3.1** ya Makadirio kitakusanya kutoka katika Idara zilizo chini ya Wizara. Aidha, shilingi **32,761,620,000/=** sawa na **asilimia 96.8** kitakusanya kutoka katika Taasisi zilizo chini ya usimamizi wa Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka huu wa fedha ni pungufu kwa **asilimia 12** ya kiasi kilichokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kamati ilielezwa kuwa upungufu wa Makadirio haya ni kutokana na Taasisi za Wizara kutokutana na Msajili wa Hazina kwaajili ya kuidhinishiwa viwango vya makusanyo ya maduhuli. *Kamati inaitaka Serikali kutoa maelezo kama tayari Taasisi hizi zimeshakutana na Msajili na Makadirio yakoje ili Wizara iweze kukusanya maduhuli hayo.*

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa ulinganisho wa Makadirio haya ni kama unavyoonekana katika **Kielelezo Na.**

**3**

#### Kielelezo Na. 3:



**Chanzo: Usanifu wa Kamati kwa Randama ya Wizara**

### **3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.**


**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara inaomba kuidhinishiwa **shilingi 33,349,675,000/=** kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Majukumu yake. Matumizi ya Kawaida ambayo yanajumuisha Mishahara na Matumizi mengineyo yanaombewa **shilingi 24,649,675,000/=** sawa na **asilimia 73.9** ya bajeti yote ya Wizara. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo inaombwa **shilingi 8,700,000,000/=** sawa na **asilimia 26.1** ya bajeti yote ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka huu na ile iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na imebaini yafuatayo:-

- a) Bajeti ya Mwaka 2018/2019 imepungua kwa shilingi **5,136,980,000/=** sawa na **asilimia 15.4** ya bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018;
- b) Bajeti ya Mishahara ya Mwaka 2018/2019 imepungua kwa **asilimia 11.7** kutoka shilingi **17,276,616,000** zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 hadi kufikia shilingi **15,253,265,000/=** zinazoombwu katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019;
- c) Bajeti ya Matumizi mengineyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 imeongezeka kwa **shilingi 4,780,331,000/=** na kufikia **shilingi 9,396,410,000** sawa na ongezeko la **asilimia 50.8** la **shillingi 4,616,079,000/=** zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018;
- d) Bajeti ya Miradi ya Maendeleo imeongezeka kutoka shilingi **6,320,000,000/=** Mwaka 2017/2018 hadi kufikia shilingi **8,700,000,000/=** sawa na ongezeko la **asilimia 27.3.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Wizara hii na ina amini kabisa kuwa fedha zote hususan za kutekeleza Miradi ya Maendeleo zitatolewa kabla ya Mwaka wa fedha wa 2018/2019 kuisha.**

**Kielelezo Na. 4:**



*Chanzo: Usanifu wa Kamati kwa Randama ya Wizara*

**SEHEMU YA NNE**

---

**4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya uchambuzi wa Kamati naomba sasa kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu Wizara hii kama ifuatavyo:-

#### 4.1 Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo imeonekana katika uchambuzi wa Kamati, hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 59** tu ya Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kamati ina amini kabisa **asilimia 41** iliyobaki ni muhimu sana kwa kuwa pia inajumuisha fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo zimekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Kamati. *Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuw, kiasi kilichobaki cha asilimia 41 kinatolewa kwa Wizara kabla Mwaka huu wa Fedha kuisha ili iweze kutekeleza majukumu yake kama iliyopangwa.*

#### 4.2 Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016

**Mheshimiwa Spika**, mwaka 2016, Bunge lako Tukufu liliptitsha Sheria ya Huduma za Habari. Sheria hiyo ili itekelezwe kikamilifu suala la utungaji wa Kanuni ni muhimu sana. Kamati imebaini kuwa Kanuni bado hazijatungwa lakini pia vyombo muhimu kama vile Baraza Huru la Habari na Bodi ya Ithibati ya Wanahabari nazo bado hazijaundwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa tupo kwenye kipindi cha mpito katika kuelekea kutekeleza Sheria hii, hata hivyo kipindi hiki cha mpito hakizuii kuundwa kwa vyombo hivi muhimu. *Kamati inaitaka Serikali kueleza Bunge lako Tukufu ni lini itakamilisha kutunga kanuni hizi lakini pia lini itakamilisha kuunda vyombo hivi muhimu kwa maendeleo ya Tasnia ya Habari nchini.*

#### 4.3 Usimamizi wa Michezo Mashulenii

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua umuhimu wa Michezo na inaona ipo haja kabisa kwa Serikali kuweka usimamizi thabiti wa Michezo kwa kushirikishiana na TAMISEMI ili kuinua michezo shuleni kuitia UMITASHUMTA na UMISETA.

**Mheshimiwa Spika**, kuimarisha michezo shuleni kutasaidia kuibua vipaji vya vijana. Si hivyo tu, wote

tunafahamu michezo ni afya, kama kweli tunataka kuwa Taifa imara lenye Vijana hodari na chapakazi yatupasa kuzingatia michezo kuanzia ngazi ya chini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka huu wa Fedha wa 2018/2019 moja ya mipango ya Wizara ni kuendeleza Mpango wa Michezo kwa jamii ikiwa ni pamoja na kusimamia mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA kwa kushirkiana na TAMISEMI Ili zoezi hili liweze kutekelezwa upatikanaji wa fedha ni jambo la msingi. *Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya Baraza la Michezo la Taifa ambalo ndilo lenye wajibu wa kusimamia michezo zinatolewa zote na kwa wakati.*

#### 4.4 Ufungiaji wa nyimbo na Wasanii

**Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni Wizara ilifungia nyimbo na wasanii kwa maelezo kuwa baadhi ya nyimbo zao haziendani na maadili yetu. Kamati inatambua umuhimu wa kuzingatia Maadili ya Mtanzania lakini hata hivyo utaratibu unaotumika siyo mzuri na unaleta changamoto kwa Wasanii. Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

- a) *Vyombo vinavyohusika na Usimamizi wa Sanaa nchini kuhakikisha vinatimiza majukumu yao kwa kukagua nyimbo zote za Wasanii kabla hazijatoka ili kuhakikisha hakuna wimbo unaotoka kama haujazingatia maadili;*
  
- b) *Kuangalia nyimbo ambazo ni za Kimataifa na kuzipa kibali maalum kwa maana ya muda na mahali pa kuutumia wimbo huo kabla hazijaanza kutumiwa na Vyombo vyta Habari.*

#### 4.5 Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kutoa Bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo ya TBC kwa Mwaka wa Fedha

2017/2018 kiasi cha shilingi **Bilioni 3**, lakini fedha hizi bado hazitoshi. Itakumbukwa katika Maoni ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Ni kwa msingi huo basi, Kamati inaishauri Serikali:-

*a) Kulifanyia kazi andiko la TBC lenye kuonesha mahitaji muhimu ya Shirika ambapo inakadiriwa kiasi cha shilingi Bilioni 80 zinahitajika.*

*a) Kutoa fedha ili TBC Radio iweze kusikikia nchi nzima kwani kuna baadhi ya mikoa haipati matangazo ya TBC kabisa.*

#### 4.6 Mapato ya Uwanja wa Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa Mapato ya Uwanja wa Taifa na Uhuru ni makubwa na yamekuwa yakichanganywa kwa makusudi ili kuchanganya wadau. Aidha, kumekuwepo na fedha zinazouljikana kwa jina la fedha za Mchина kwa kila mchezo kwa kuwa wamekuwa wakilipwa Wachina wanaohudumia Uwanja. Kamati imehoji kuhusu suala hili lakini haijapata maelezo ya kuridhisha. Kutokana na hali hii Kamati inashauri yafuatayo:-

*a) Mapato ya Uwanja wa Taifa na Uhuru yasichanganywe;*

*b) Uchunguzi ufanywe kuhusu Fedha za Mchина zinazokatwa katika kial mchezo na Bunge lako Tukufu lipewe Taarifa; na*

*c) Uwepo udhibiti wa mapato yatokanayo na uuzaaji wa tiketi kwa njia ya kielektroniki wakati wa Mechi za Mpira wa miguu kwa kuwa fedha nyngi zimekuwa zikiibwa.*

#### 4.6 Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa bado Timu zetu hazifanyi vizuri katika mashindano mbalimbali. Kamati imebaini moja ya sababu inayochangia kutofanya vizuri ni kutoandaliwa vyema.

*Kamati inashauri:-*

- a) *Kuanzia sasa Timu zetu ziandaliwe vyema ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi za masomo makocha wetu wa ndani ili wawe na viwango vinavyokubalika Kimataifa;*
- b) *Muda wa maandalizi wa kutosha uwepo kwa kuwaweka katika kambi moja ili ziweze kushiriki kikamilifu kwenye mashindano na kurudi na ushindi.*

#### **4.7 Vyuo vya Michezo nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kwa sasa hakuna vyuo vinavyozalisha Walimu wa Michezo kutokana na Vyuo hivyo kufungwa. *Kamati inaitaka Serikali kufufua vyuo hivyo ili viweze kuendelea kutoa mafunzo kwa walimu ambao ni nyenzo muhimu katika Michezo yetu hapa nchini.*

#### **4.8 Ujenzi wa Viwanja vya Michezo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo Kamati imekuwa ikiongelea suala la ujenzi wa Viwanja vya Michezo nchini. Kamati inaendelea kusisitiza ujenzi wa viwanja vya michezo ambapo kwa kuanzia inaitaka Wizara hii pamoja na TAMISEMI kukaa pamoja ili kuainisha mahitaji halisi ikilinganishwa na viwanja vilivyopo ili kubaini upungufu. Kamati inatambua bila uwepo na viwanja mafanikio katika michezo hayawezi kupatikana.

#### **4.9 Kazi za Wasanii**

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la wizi wa kazi za Wasanii ni tatizo la muda mrefu na Kamati imekuwa ikilisemea mara kwa mara. Kamati bado inaendelea kusisitiza suala hili nakuwataka wale wote wanaohusika katika udhalimu huu kuacha. Aidha, Kamati inawashauri wasanii waboreshe kazi zao na hususan filamu kutokana na maendeleo ya Teknolojia ili ziweze kuteka soko la ndani na nje ya nchi.

#### **4.10 Lugha ya Kiswahili na Ukalimani**

**Mheshimiwa Spika**, Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Kimataifa kwa maana ya kwamba inatumika hata katika mikutano mikubwa ya kimataifa ambako mara nyingi viongozi wetu wa kitaifa wanakwenda kuhuduria. Licha ya lugha hiyo kutumika katika mikutano hiyo ya kimataifa, Kiswahili hutumika katika majadiliano ya mikataba mbalimbali ya kimataifa ambapo ili kukubaliana vyema katika hadidu za rejea (*terms of reference*) mbalimbali lugha inaweza kusaidia au kuwa sehemu ya changamoto.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua tatizo hilo hapa nchini la kutofahamu ipasavyo lugha ya Kiingereza hasa katika mikutano inayohusisha mataifa mbalimbali. *Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iweke mkakati wa kuwa na kanzi data ya wataalamu wote wa lugha ya Kiswahili nchini ili watumike kama wakalimani katika maeneo mbalimbali hasa katika mikutano ya kimataifa.*

**Mheshimiwa Spika**, kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imetoa fursa ya ajira kwa watanzania lakini pia fursa kubwa ya kuikuza lugha ya Kiswahili nje ya mipaka ya Tanzania.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti. Aidha, namshukuru pia Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee zaidi naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mzuri walionao na wameonyesha umahiri na weledi wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

- |                                    |               |
|------------------------------------|---------------|
| 1. Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb | Mwenyekiti    |
| 2. Mhe. Juma S. Nkamia, Mb         | M/ Mwenyekiti |

3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Peter Ambrose P. Lijualikali, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Bernadetha K. Mushashu, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Deogratius Francis Ngalawa, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Khalifa Mohamed Issa , Mb	Mjumbe
13. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
14. Mhe. John Peter Kadutu, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Mch. Dkt. Getrude P.Rwakatare, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Seleman Said Bungara, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
24. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb	Mjumbe
25. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb), Naibu Waziri Mhe. Juliana Shonza (Mb), Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Susan Mlawi na Naibu wake Ndg. Nicholaus Benjamin kwani Wizara imekuwa ikitoa ushirikiano mzuri kwa Kamati wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai - Katibu wa Bunge kwa uongozi mahiri na kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Namshukuru pia Ndg. Athuman B. Hussein - Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndg. Dickson M. Bisile – Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati yetu.

Aidha, Nawashukuru sana Makatibu wa Kamati hii Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pamoja nao namshukuru msaidizi wa Kamati Ndg. Modester Kipiko na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa uchapakazi mzuri ambao unatuwezesha sisi kama Kamati kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**) shilingi **Bilioni Thelathini Na Tatu, Milioni Mia Tatu Arobaini Na Tisa Na Laki Sita Sabini Na Tano (33,349,675,000/=)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono Hoja.

Peter J. Serukamba, Mb  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA**  
**NA MAENDELEO YA JAMII**  
27 Aprili, 2018

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kuna tangazo muhimu limekuja sasa hivi; Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba kuwatangazia au kuwapa taarifa kuwa matokeo ya mpira uliochezwa jana kati ya *Bunge Sports Club (Ndugai Boys)* pamoja na Bunge la Afrika Mashariki matokeo yalikuwa ni tatu kwa tatu na kwa upande wa Ndugai Boys Mheshimiwa Ali King alifunga magoli mawili na Mheshimiwa Aeshi Hillary alifunga goli moja. (*Makofi*)

Mchezo wa *netball* haukuchezwa kama ilivyopangwa baada ya wenzeni wa *EALA* kutokutokea uwanjani kwa kuogopa magoli mengi ya kufungwa. Ndugai Boys inawashukuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu

ambaye alikuwa mgeni rasmijana na Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kutuunga mkono katika kufanikisha michezo. (*Makofii*)

Pamoja na taarifa hiyo anaomba vilevile kuwatangazia tena kwamba tarehe 28 Aprili 2018, kutakuwa na mbio za mwendo wa pole (*jogging*) na matembezi chini ya udhamini wa *NMB* zitakazoanza saa 12 asubuhi kwenye lango kuu la kuingilia Bungeni na kumalizikia Uwanja wa Jamhuri.

Vilevile kutakuwa na mechi ya kirafiki za mpira wa miguu na mpira wa kikapu kati ya Ndugai Boysna *NMB*. Mpira wa kikapu utachezwa kuanzia saa 8.30 mchana hadi saa 9.45 na mpira wa miguu utachezwa kuanzia saa 10 hadi saa 11.30. Michezo yote itakuwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma na itarushwa mubashara na *Azam TV*. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kuanzia saa 1.30 jioni kutakuwa na mchapalo utakaohusisha Waheshimiwa Wabunge na wafanyakazi wa *NMB* katika Ukumbi wa Jengo la *PSPF*. Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote mnaalikwa.

Tarehe 6 Mei, kutakuwa na mechi kabambe kati ya Ndugai Boys na *Ilala Veterans* katika uwanja huo huo wa Jamhuri.

Semina kwa Wabunge wote, ndugu Athuman Hussein kwa niaba ya Katibu wa Bunge anaomba kuwapa taarifa Waheshimiwa Wabunge kuwa mnaombwa kuhudhuria semina itakayoendeshwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu athari za uvuvi haramu nchini siku ya Jumapili tarehe 29 Aprili, 2018, kuanzia saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa tunaanza kuchangia na sasa namwita Mheshimiwa Devotha Ninja dakika kumi, ajiandae Mheshimiwa Chumi.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Kivuli, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ambaye kwa sasa anatumikia kifungo cha miezi mitano jela, tunampa pole kwa anayopitia. Kambi ya Upinzani ikiungana na Watanzania ambao wananalitakia mema Taifa hili, wanaungana naye na wanasema kwamba yampasa apitie hayo anayopitia ili aweze kupata ukombozi kwa Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza sana maoni ya Kamati ya Wizara hii ambayo inasema kwamba inashangazwa, tangu kuundwa kwa Sheria hii ya Huduma za Vyombo vya Habari, ni kwa nini mpaka sasa hivi Mheshimiwa Waziri anaona klgugumizi kutunga kanuni? Ili sheria iweze kufanya kazi yake vizuri ni lazima iwe na kanuni ambazo zitaongoza sheria ile iweze kufanya kazi. Matokeo yake hivi sasa kinachoendelea, Mheshimiwa Waziri anachokifanya sasa hivi ni kufungia magazeti kazi ambayo siyo yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anafungia magazeti kwa kusema ni kosa la uchochezi. Tunaelewa kosa la uchochezi ni kosa la jinai na Mahakama pekee ndiyo ya kutoa hukumu hiyo. Tuliomba kanuni hizi ziundwe ili kuwe na yale mabaraza likiwemo la ithibati ambalo ndilo litakuwa na *room* ya kuzungumza na Mwandishi na kutoa adhabu inayostahili kulingana na alichokifanya. Siyo kama hivi sasa Mheshimiwa Waziri akilala, anaamka asubuhi ni kufungia gazeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha na wakati mwingine kunakuwa na *double standard*. Yale magazeti ambayo yanaandika habari mbaya za kupiga Upinzani, za kutukana viongozi wa Upinzani likiwemo Gazeti la *Tanzanite*, Mheshimiwa Waziri sijui halioni? Ikifika kwenye magazeti kama hayo, anavaa miwani ya mbao, lakini ikifika Tanzania Daima anavaa miwani yake ya kawaida na anayafungia magazeti. Tunasikitika sana kama kunakuwa na *double*

*standard katika matukio haya na tunataka atupe majibu ni kwa nini kanuni hazitengenezwi mpaka sasa? (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa tuliambiwa hapa *Bunge Live* halitakiwi kwa sababu kutakuwa na msongamano wa waandishi na nini, hawataweza kufanya kazi yao vizuri, tukaambiya mwarobaini itakuja *Bunge TV* na itakuwa na uwezo wa kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata habari, tukakubaliana na hilo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, toka hiyo *Bunge TV* ianze mpaka sasa *outreach* yake ni wapi? Kwa sababu hata pale barabarani haifiki. Yaani hii *Bunge TV* inakuwa kama kioo cha ndani, tunakaa hapa ndani tunajitazama tukitoka nje hatuwezi kujiona. Hivi kwa nini hii *Bunge TV* isiunganishwe ikaingia mpaka kwenye ving'amuzi Watanzania wakaona kinachoendelea ndani ya *Bunge lako*? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni *issue* ya bajeti, tulitegemea hata Mheshimiwa Waziri angeizungumzia sasa hii *Bunge TV* iweze kupewa, ifanye kazi yake vizuri, iweze kufikisha habari kwa Watanzania. Kwa sababu walitupa mifano, wakatuambia angalia hata *South Africa* kuna *channel* ya *Bunge*. Ni sawa hatujakataa, lakini tunataka tuione kwenye *frequency*, watu wenye ving'amuzi waione. Hata ikiwezekana wale wenye *TV* za *local* wawe na uwezo wa *ku-access*, wakati mwингine wa-*relay* kwenye *Bunge TV* wawaoneshe Watanzania kinachoendelea. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu waandishi kukosa *access*, pamoja na hii *Bunge TV* kuwepo. Tunaelewa kwamba lipo Kikanuni, Mbunge anapozungumza hapa yapaswa kila kitu kiingie kwenye *Hansard*, lakini Mbunge akiongea jambo ambalo lina ukakasi kwa Serikali linakuwa-edited.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri, ni vigezo vipi vinavyotumika? Kwa sababu ukienda kwenye written *Hansard* utakuta kila kitu

kinaandikwa vizuri kabisu, lakini kile ambacho kinachukuliwa hapa kinarekodiwa, wanapewa waandishi huko, hawana access na baadhi ya *information* zinakatwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi upo Mheshimiwa Waziri akitaka nitamwonesha.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## TAARIFA

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa dada yangu, Mheshimiwa Devotha Minja kuwa taarifa zote zinazotoka Bungeni hazichujwi, zinaenda hivyo hivyo. Ushahidi, nilipomwita Mheshimiwa Profesa Ndalichako Waziri wa masifuri illenea nchi nzima. Kwa hiyo, taarifa zinafika kama zilivyo.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwandishi *professional*, siwezi kumjibu, naendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kuhusu suala la usajili wa magazeti. Wote tunaelewa usajili ni kitu ambacho ni *permanent*. Usajili wa magazeti hivi sasa kuna sheria eti kila mwaka magazeti lazima yasajiliwe, tumewahi kuona wapi? Katiba yetu Ibara ya 18 inasema, ni haki na ni uhuru kwamba kila mwananchi ana uwezo wa ku-access *information*. Sasa wanapokuja na vigezo kwamba kila gazeti, kila mwaka lisajiliwe upya tunaomba watuambie, hivi Serikali wakati inapitisha bajeti zake, *TRA* ilionesha kwamba moja ya vyanzo vyake ni usajili wa magazeti? Ina maana hapa kuna ukiukwaji wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua usajili ni *permanent* na hii tunajua ni makusudi tu. Yale magazeti ambayo hayataandika mapambio ya kuitukuza na kuisifu Serikali hii

ya CCM baada ya mwaka yatafungiwa, hayatapewa usajili. Hali hii inasababisha wamiliki wa vyombo vyahabari kuwa na uwoga. Watu ambao wanataka hata kuingia kwenye biashara hii ya vyombo vyahabari, wanashindwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kuhoji, hii wamei-copy wapi? Nimejaribu kufuatilia nchi za Afrika Mashariki, nimeona ni Rwanda pekee yenyne *element* ya namna hiyo, kwamba kila mwaka wanasajili magazeti. Ni kwa nini tunachukua utaratibu ambao siyo utamaduni wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata *blogs* nazo eti zinaambiwa zinatakiwa zisajiliwe na zilipe, tena kwa hela nyangi; kati ya laki moja mpaka laki mbili. Mtu kafungua *blog* yake ambayo anategemea Watanzania watapata taarifa, lakini shilingi 200,000/= anaipata wapi? Haya ni masharti ambayo wanawawekea watu, wananchi watakwenda kuumia kwa sababu hawatakuwa na *access* ya kupata *information*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCRA* tulitegemea wangesaidia kusimamia sheria iliyopo ya kuhakikisha habari zinawafikia Watanzania, lakini *TCRA* imekuwa kama ni *barrier* sasa. Yaani kitu kidogo *TCRA* tayari ni kupiga faini magazeti, ni kupiga faini *TV*, ni kupiga faini redio, hali ambayo wakiangalia, na wao wana takwimu, waangalie tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano, ni watu wangapi wameingia kwenye ku-invest kwenye *media*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna kasi kubwa sana ya watu ku-invest kwenye *media* katika kipindi cha Awamu ya Nne, lakini siyo sasa hivi. Ni kwa nini? Masharti magumu, lakini tunajua *behind* ni kuangalia vile vyombo ambavyo haviimbi mapambio, ndiyo vipewe fursa ya kuhakikisha kwamba vinaendelea kufanya kazi, vile vinavyokosoa Serikali kuhakikisha kwamba havipati fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo tunajiuliza, nimemsikiliza sana Mheshimiwa Waziri kwenye

hotuba yake. Katika hotuba yake tulitegemea angetuambia ni nini kinachoendelea katika matukio haya ya Waandishi wa Habari kupotea, kutekwa, kunyanyaswa na waandishi wa habari wamekuwa kama vifaranga vya kuku ambavyo havina mchungaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi, hata mwezi haujapita, Mwandishi wa Gazeti la *The Guardian* alitekwa, alipigwa, alinyanyaswa, lakini hata Mheshimiwa Waziri hana habari. Hawa ndio watu wake ambao anafanya nao kazi. Kwa nini hawasemei Waandishi? Serikali kwa nini haitoi matamko kuhusu matukio ambayo Waandishi wa Habari wanafanyiwa, ikiwemo Azory ambaye sasa hivi amepotea ni miezi mingi mpaka sasa hatujasikia hata tamko la Serikali. Tumemsikia Mheshimiwa Waziri akizungumza habari za sanaa, za nini, lakini kuzungumza habari za Azory ambaye amepotea sijawahi kumsiklia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahoji haya matukio ambayo Waandishi wa Habari wamekuwa wakiyarioti, Serikali inaendelea kukaa kimya. Tunashuhudia watu wanapigwa risasi mchana kweupe, *media* zinarioti, lakini hakuna kinachoendelea. Tunashuhudia watu wanatolewa bastola, Waandishi wa Habari wamepiga picha zinaonekana kabisa, mpaka sasa hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maiti zinaokotwa tunaoneshwa kwenye *media*, kwenye kila namna ya magazeti, lakini hakuna chochote kinachoendelea. Sasa ifike mahali Mheshimiwa Waziri, Wizara yake itambue mchango mkubwa wa kazi ya Wanahabari ambao wana kazi ya kulielimisha Taifa hili, kazi ya kutoa taarifa za Taifa hili ili Serikali iweze kufanya kazi na kutoa matamko ya mambo yanayoendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuhusu suala...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili. Ulianza kasoro dakika ishirini na moja.

Mheshimiwa Chumi, halafu Mheshimiwa Kadutu, Mheshimiwa Musukuma dakika tano na Mheshimiwa Sixtus, dakika tano.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Dakika zangu ni ngapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi dakika kumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kwa kupata nafasi na kama mdau wa michezo napenda kuishukuru Wizara na Watendaji wake wote kwa maandalizi ya hii hotuba yao. Pia napenda kushukuru vyombo vyaa habari vyaa Serikali, hasa *Daily News* kwa sababu sasa hivi wamekwenda *digital*, wanatusaidia kueneza Kiswahili kwa kuchapisha lile jarida lao linalotoka kwa ajili ya nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kupongeza Idara ya Habari Maelezo kwa wepesi wake wa kutoa taarifa mara kwa mara kwa Umma wa Watanzania. Nawaomba waendelee kwa sababu hii ndiyo idara ambayo inategemewa kutoa matamko na maelezo mbalimbali, kinyume chake kutakuwa na *vacuum* ambayo inaweza kujazwa na taarifa ambazo zinaweza zikapotosha wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, niende kwa haraka sasa katika michezo unaopendwa na watu wengi duniani, michezo wa mpira wa miguu. Hapa naipongeza *TFF*, angalau baada ya mwaka 2017 kuchangia na kutoa takwimu za ushiriki wa Timu ya Taifa katika michezo ile kulingana na kalenda ya *FIFA*, naona *TFF* angalau walizingatia ule ushauri na sasa hivi Timu ya Taifa inashiriki kadri ya kalenda ya *FIFA* katika mechi za majaribio au za kujipima nguvu au za kirafiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesaidia mpaka wiki iliyopita angalau tumeponda kutoka nafasi ya 146 mpaka 137. Hata hivyo, bado kuna kazi inatakiwa ifanyike, tuendelee kukutana na timu ambazo angalau ziko kwenye viwango vya hamsini bora kwenye *FIFA ranking* maana yake ile inatusaidia sisi kupata angalau *points* nydingi na hivyo kuisogeza Timu yetu ya Taifa katika viwango bora vya *FIFA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mojawapo ya vitu vilivytusaidia ni kuwafunga *Congo DRC* ambao wako nafasi ya 38 katika *FIFA World Rankings*. Kwa hiyo, tusiandae mechi kucheza tu na ambao niseme ni kama wachovu wenzetu, hapana. Tukabiliane na hao *ma-giant* kama tulivyofanya kwa Algeria, hata kama tulipoteza. Maana yake ni kwamba tunaendelea kuijengea uwezo Timu yetu ya Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Timu ya Ngorongoro, Timu ya Serengeti na Timu za Wanawake. Kimsingi *TFF* naona inajitahidi kuhakikisha kwamba timu zetu zinashiriki katika michuano ya Kimataifa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, la pili ambalo linaweza kusaidia Timu yetu ya Taifa iwe na ushindani, ni ligi yetu kuwa na ushindani. Sasa hivi kanuni inasema timu inaweza ikaajiri wachezaji saba wa kigeni, lakini je, ni wachezaji wa kiwango gani? Kwa hiyo, napenda kushauri *TFF*, mfano Ligi Kuu ya Uingereza ili ucheze, lazima uwe umethibitisha ubora yaani lazima uwe timu yako iko katika viwango.

Kwa mfano, kiwango cha kwanza mpaka nafasi ya kumi mchezaji lazima awe amecheza angalau asilimia thelathini (30) ya mechi za Timu ya Taifa kwa miaka miwili. La, kama unatoka katika timu ambayo kwenye *FIFA Ranking* iko nafasi ya 21 mpaka 30, lazima mchezaji uwe umecheza angalau asilimia 60 katika timu yako ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi inawezekana kuna wachezaji wanatoka nchi za Afrika Magharibi kweli kiasi fulani zimepiga hatua, lakini hata wachezaji wanaotoka kwenye Ukanda wetu wa Afrika Mashariki na Kati hebu basi *TFF* iwe vigezo, isiwe tu bora mchezaji. Maana yake nimefuatilia kalenda ya *FIFA*, hakuna wachezaji walioitwa kwenda kuchezea timu zao za Taifa lakini hapa tunawaita ma-*professional*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha Juuko Murushid, Emmanuel Okwi, ukiacha Dany Usengimana na yule wa *Singida United* na ukiacha, siku za nyuma, Haruna Niyonzima, hakuna mchezaji ye yote ameitwa kwenye timu yake ya Taifa, lakini sisi hapa tunamlipa fedha nyingi. Kwa hiyo, naiomba *TFF*-set standard kwamba ili mchezajiacheze Ligi Kuu hapa nyumbani, lazima kuwe na vigezo fulani, hatuwezi kuwa na vigezo kama vya *Spain* au vya *England* au vya *Italy*, lakini lazima tu-set standard ili hapa isiwe soka ambayo imekuwa kama vile ni soka holela holela tu, kwamba watu wanakuja kujifunzia mpira hapa. Hilo litasaidia kuleta ligi yenye ushindani, lakini kutokana na ligi yenye ushindani maana yake tutakuwa na timu ya Taifa ambayo ni bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, Uingereza sasa hivi kuelekea Kombe la Dunia 2022 wameamua kuongeza kwamba kila timu lazima iwe na wachezaji wa ndani kutoka nane mpaka 12. Sisi tunasema wachezaji wa kigeni wawe saba; ni vizuri, hatuwezi kuiga kila kitu kutoka kwa wenzetu waliopiga hatua sana, lakini angalau tu-set hizo standards. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Kamati imezungumzia hapa kuhusu Timu ya Taifa kwamba maandalizi yanakuwa ni duni; naiomba Serikali, pamoja na kwamba mambo haya yanasmamiwa na *TFF*, lakini hakuna namna. Kama tunataka kufanya kweli michezo ni biashara, tutangaze utalii kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, kwamba Serikali ikakaa pembeni katika uandalizi wa timu za Taifa. Tumeona tumeenda juzi Jumuiya ya Madola imeendelea kuwa vichekesho vilevile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tufanye hivyo hakuna namna, ni lazima Serikali kwa kushirikiana na wadau kwa namna yoyote, ni lazima *i-take lead*, tusiviachie Vyama vya Michezo, lazima Serikali *i-take lead* ndiyo tutavuna matunda mema. Vinginevyo tutajadili hapa, tutapiga madongo vyama vya michezo, bila Serikali kuweka mkono wake hakuna namna tutapiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, napenda kuhoji Mheshimiwa Waziri, wakati Serikali ikijibu swalii Na. 62 hapa, ilieleza masuala ya udhamini ambao inaupata *TFF* kutoka kwa vyombo mbalimbali hapa nchini. Kama hii taarifa ni kweli na naiamini, kwa sababu ni ya Serikali, katika sehemu ya jibu ilisema; "aidha, *TFF* iliingia mkataba na Kampuni ya Bia ya *TBL* mwaka 2013 - 2017 kwa thamani ya Dola za Kimarekani milioni kumi kwa ajili ya Taifa. Mkataba huo ulishamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFF* imeingia mkataba wa ufadhilli na Kampuni ya Bia ya Serengeti kwa miaka mitatu; 2017 - 2019, wenye thamani ya shilingi milioni 700 na milioni 450 kwa ajili ya Ligi Kuu ya Wanawake. Maana yake kimahesabu kati ya 2013 - 2017 ilikuwa dola milioni kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya 2017-2019 ni dola milioni moja. Hivi gharama za maisha zinapanda au zinashuka? Maana yake hii nimeitoa kwenye *Hansard*, kwamba mwaka 2013 - 2017 unaingia udhamini wa dola milioni kumi, 2017 - 2019 unaingia udhamini wa dola milioni moja. Sijui, yaani najaribu kufikiri, kwa kweli sipati picha na ningependa kwenye majumuisho Mheshimiwa Waziri atusaidie kutueleza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, *entertainment and media industry*, kwa mujibu wa PWC, Tanzania ni kati ya nchi tano ambazo *entertainment industry* inakuwa kwa kasi sana. 2016 mapato yalikuwa dola milioni 504, sawa na shilingi trilioni 1.1. Kufikia 2021 inatarajiwaa mapato yatakuwa dola bilioni 1.1, sawa na shilingi trilioni 2.4. *Where is our stake?* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii wetu wananaufaikaje katika hizi trillioni zinazoingia? Au ni fedha tu zinaishia kwenye makampuni ya kuza *data*, kwenye makampuni ya promosheni? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hii *vacuum* ambayo inatokea kwenye *media and entertainment industry* naomba atakapokuja ku-*wind up*, atusaidie, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba wasanii wanaendelea kunufaika na hizi trillioni ambazo Taifa linaingiza? Kwa sababu katika *2.4 trillion* mpaka mwaka 2021 hapa wasanii wakipata japo asilimia 20 tu, maana yake ni kwamba utakuwa umeongeza ajira ngapi katika Taifa? Wengi wanaofanya shughuli hii ni vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, *this entertainment and media industry is very potential*. Hebu tutazame, tukae na hawa wasanii, tuwaelekeze tamaduni zetu, tuwape milongozo ili waendane na tamaduni na mila zetu lakini *at the same time* waweze kunufaika na kile kinachopatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya, napenda kuunga mkono hoja na nawatakia wapenzi wote na mashabiki wote wa Simba na Yanga mchezo bora Siku ya Jumapili. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kadutu, jiandae Mheshimiwa Musukuma dakika tano na Mheshimiwa Mapunda dakika tano na Yussuf Hussein dakika kumi.

**MHE.JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata fursa hii. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wa Taasisi zote zinazoshughulika na michezo na bila shaka wanajua mimi ni mwanamichezo niliyekubuhi na nashughulika na michezo zaidi ya miaka 40 sasa. Kwa hiyo, najua kila kitu kilichoko ndani ya Wizara hii na ndani ya michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii na sehemu

kubwa, maoni yetu ni yale ambayo tuliyajadili kule, nami nikiwa mdau pia, maoni yetu tuliyatoa kwenye Kamati na Serikali tulieleza kila kitu, kwa hiyo, hapa nitakuwa na mchango mdogo tu wa kusisitiza. La kwanza ni juu ya michezo mashulen. Kwa hulka Watanzania hatuna *Academy* za michezo nyingi kwa sababu ya gharama za uendeshaji. Sasa vituo vyetu hivi kwa maana ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo ndiyo *Academy* zetu zinazoweza kutoa wanamichezo wazuri na hasa kwa kuzingatia historia huko nyuma, UMISETA tulikuwa na wachezaji wazuri waliotutetea vizuri kwenye timu za Taifa na pia UMITASHUTA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maoni yangu ni kwamba Serikali hebu ijaribu kurejea huko nyuma tulifanyaje kwenye michezo shulen. pamoja na kwamba hapa katikati kuna watu walilewa madaraka wakafuta, nadhani tuwaache tu na mambo yao, lakini turudi nyuma kabla ya kufutwa, nini kilifanyika na nini tulifanikiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni juu ya ruzuku kwa Vyama vya Michezo. Huko nyuma Serikali ilikuwa na mkono wake kwenye Vyama vya Michezo na tuliona faida zake, lakini sasahivi imebaki tunasifia tu, timu ikifanya vizuri tunasifia lakini kwa sasa naona msaada wa Serikali au mkono wa Serikali uko mbali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweke mkono kwenye Vyama vya Michezo ili iwe na *power* ya kuwaambia *no*, hiki wanachokifanya siyo. Kama tunasubiri tu mafanikio, mtu tukafanikiwa huko anakuja hapa Bungeni tunapiga makofi na nini, mkono wa Serikali kama haupo, maana yake ni kwamba hata kuwagusa watu hawa hatutaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chumi amezungumzia ushiriki wa timu zetu za Taifa, siyo kwa maana ya mpira wa miguu tu peke yake. Juzi tumeona kwenye madola, tunaondoka kwa mbwembwe lakini tunarudi hata haijulikani timu imerudi au haijarudi. Maana yake hatuna

maandizi. Ikifika mahali tunashindwa, turudi kwenye ushauri ule, tuache kwenda kucheza ili tujitengeneze vizuri tukaporejea, turudi na nguvu nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni juu ya mapato ya Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru. Kamati imetoa maoni yake, lakini mimi nakuja na kitu kingine kabisa. Mapato ya Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru, Baraza la Michezo linachukua asilimia 15, *TFFinaambulia* asilimia tano. Nadhani jambo hili siyo sawa. Tutoe asilimia tano ya wenye uwanja, tuwape *TFF* kwa maana ya kuimarisha Mfuko wa Timu ya Taifa, angalau watakuwa na pesa nyingi za kuweza kuhudumia. Vinginevyo, Timu ya Taifa ni mzigo mkubwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unajua Timu ya Taifa ni mzigo. Tunaweza kufikiri kwamba mapato yapo ni mengi ya kuweza kuhudumia, lakini wakati mwingine hata kucheza mechi za Kimataifa timu inashindwa kwa sababu ya gharama. Kwa hiyo, wazo langu, tuangalie, ukiacha viwanja vingine hatuwezi kuvisemea viwanja vile vinavyomilikiwa na Chama cha Mapinduzi mimi siwezi kuwasemea, lakini nazungumzia viwanja vinavyomilikiwa na Serikali; asilimia tano tuito kule ili iende kwenye asilimia za *TFF*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, sitaki kutumia dakika nyingi. Nimekuwa nasema hapa toka 2010 tunayo Timu ya Vijana Wanaoishi katika Mazingira Magumu kule Mwanza. Timu hii 2010 ilikwenda kushiriki Kombe la Dunia la Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu kule South Afrika. Tumetoka kule tukawa washindi wa pili. Mwaka 2014 tumekwenda Brazil, tukawa mabingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata ubingwa, watu wakafurahi, wakaja hapa wakatupokea Bungeni, tukaona raha na ahadi nyingi, mpaka leo hakuna jambo lilitotekelezwa. Serikali ijaribu kurudi wapi imejikwaa, kwa nini itoe ahadi ya zawadi hewa? Mpaka leo vijana hawajapewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wiki ijayo tunakwenda Urusi kama mabingwa watetezi wa Kombe la Dunia la Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu. Nini msaada wa Serikali juu ya timu hii? Wakati mwingine hapa Tanzania hakuna bingwa wa dunia isipokuwa wale watoto, hatuoni fahari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia, tukipata ubingwa kama hamtusaidii ni afadhalii msituite Bungeni. Bungeni hapa tutakuja kwa utartaibu mwingine. Habari ya kuahidi hapa kila siku, watoto tunawaahidi wanatoka hapa wanasema tumeahidiwa moja, mbili, tatu, sijui viwanja, sijui maisha bora kule kwenye kambi yetu; kama hamtusaidii, wala msianze kufurahia tutakacholeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kawaida, maneno yangu huwa hayapasi papasi. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma dakika tano, Mheshimiwa Mapunda dakika tano, jiandae Mheshimwa Yussuf.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nilikuwa najaribu kuangalia kumbukumbu yangu kichwani, Serikali imewekeza pesa nydingi sana kwenye michezo hasa mchezo wa mpira. Nikirudisha *memory* zangu naona kama mpira wa miguu na michezo hiyo mingine haitusaidii sisi kama Serikali kutangazwa kwenye nchi nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijabu kuangalia, sisi inawezekana tuna bahati sana ya kutangazwa na wasanii hasa wa muziki na filamu. Wamefanya vizuri, tumeona leo hata ukienda huko nje kwenye *clubs* za Wazungu inapigwa miziki ya Kiswahili unapata morali hata wewe wa kuingia *club* na kucheza. Ila kwa *style* zinazoendelea kwa Mheshimiwa Waziri na yenewe hii tasnia tunaenda kuipoteza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia sana hapa kipindi cha katikati fungia fungia. Msanii anafanya kazi yake

nzuri; na wewe ni mpenzi wa muziki, nakufahamu. Kinachomfanya mtu ahamasike kulipa kiingilio kwenda kwenye muziki ni pamoja na matangazo mazuri atayokuwa ametangaza msanii. Kwa sasa kinachoendelea, msanii anafanya kazi nzuri, kwenye kushuti akikosea tu kidogo mpasuo, Mheshimiwa Waziri huyo, amefunga. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kumwuliza, anafungia miziki ya Tanzania au anawafungia wasanii wa Tanzania kupasua sketi kuonesha mpasuo, hebu aangalie miziki ya akina Rihanna na ndiyo wanakaa wanaangalia humu kwenye *youtube* kila saa. Hii ya Tanzania ambayo mnataka wasanii wetu wavae sijui dela, sijui wavae pekozi, hakuna mtu aliye na *hobby* na miziki ya pekozi kwa sasa. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia msanii anafanya kazi nzuri, ana-/invest hela kwa mkopo na nini, akikosea tu mpasuo anafunga. Tukienda Samora, mbona akinamama tunaona kama zile nguo wanazovaa kule Samora Samora zinafafana tu na Wanamuziki, kwa nini kule hawapeleki kifungo? (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshauri Waziri Mheshimiwa Mwakyembe, hebu tujifunze wasanii wetu wanaiga miziki ya Ulaya, halafu wanaiga na *style* za Ulaya na miziki Ulaya huwezi ukapeleka muziki mtu amevaa kanzu au dela haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie faida tunazopata kwa hawa wasanii wetu. Ni bora wakatafuta muda wakawapa semina kuliko kuwaacha, mtu anafanya kazi nzuri, anagharamika, halafu anakosea kosa moja tu, unamfungia miezi sita. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize swali lingine, mwanamuziki ameimba muziki mwaka mzima na nusu, halafu Mheshimiwa Waziri anaibuka anasema huu muziki umekiuka maadili, anafungia. Sasa huko vijijini watu wameshaweka kwenye simu, kwenye *computer*, unapambana nao vipi? Anatupa shida sana sisi wenzake wa

vijijini kwa sababu wana- *create* ujinga kwa watu walioko vijijini huko, Watendaji, akina nani, akikosa kazi tu anaanza kukamata *computer* zina miziki imefungiwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pia ye ye ni mtu wa zamani kidogo ninavyomwona umri wake, hebu nataka anisaidie, vazi halisi la utamaduni wetu sisi la Kitanzania ni lipi? Kwa sababu nakumbuka wale wenye umri kama wangu wanafahamu, hata ngoma za utamaduni za Kitanzania akinamama hasa Wasukuma na Wagogo, wanafunga tu kwenye maziwa hapa, wanafunga na hapa chini, huku chini inakuwa kivutio. Sasa mbona hii miziki ya sasa hivi wanaleta figisu ambayo hatuwaelewī?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli namwomba sana Mheshimiwa Waziri ajitahidi kukaa na wasanii, asitumile muda mwingi sana kufunga, ni bora kutumia muda mwingi kuwafundisha na kukemea yale mambo madogo madogo ili hii tasnia iendelee. Wanaona wanamsumbuwa Diamond hapa masikini wa Mungu, wanaona yaliyofanyika Kenya? Wenzenu wamempokea, wanamwambia imba kila kitu ulichozuiliwa. Wamempa kiwanja, wamempangia nyumba. Tutapoteza hizi bahati tubaki kung'ang'ana na mipira ambayo imeshakuwa kichwa cha mwendawazimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri kidogo atakapokuja kuhitimisha anisaidie. Waganga wa Kienyeji kule vijijini, ukiwa Wilayani Halmashauri wako chini ya Afisa Utamaduni. Naamini Waganga wa Kienyeji ni watu wazuri sana, tumeshindwa tu jinsi gani ya kuwatumia. Kwa kuwa Mhehimiwa Rais ameanza utaratibu wa kutoa tuzo kwa wale waliovumbua vitu, nadhani hata huku kwa Waganga wa Kienyeji aingie kidogo ili aone mambo yalivyo. Shida iliyoko, kwa nini wanawazuia kufanya matangazo wakati Wazungu wakileta chanjo za Polio wanawaruhusu watangaze kwenye.... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sixtus, dakika tano, jiandae Mheshimiwa Yussuf dakika kumi.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi hii ya kuchangia asubuhi kwenye Wizara hii. Kwa sababu nina dakika tano, nitajitahidi niende haraka sana ili mambo yangu haya mtatu niweze kuyawasilisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naipongeza hii Wizara kwa hatua ya kupitia ile sera ya mwaka 1995 na kuja ile ya mwaka 2017 ili iboreshe Sekta ya Michezo. Namwomba Mheshimiwa Waziri aikimbize sana, kwa sababu kwa hali jinsi iliyo tukakaa kama tulivyo kwa muda mrefu, Sekta ya Michezo itazidi kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo ningependa niliseme asubuhi ya leo ni kuhusu kuwawezesha wale ambao wana nia ya kujenga viwanja vya michezo au *sports facilities* mikoani ili waweze kuifanya kazi hii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kuna taasisi nyingi zina nia ya kujenga viwanja hasa kwa kutumia nyasi bandia, lakini changamoto kubwa wanayokutana nayo ni gharama ya kuweza kulipia ushuru ili zile *facilities* zije.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara, ukienda pale Kidongo Chekundu, ukiangalie zile *facilities* zilizojengwa, tukipata vilabu vyenye uwezo wa kufanya hivyo, vikatengeneza, vikapewa msamaha wa zile nyasi bandia, nina uhakika viwanja vitakuwa bora zaidi na michezo itakua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka niliseme, nchi yetu sisi hatuna *Sports Academy*, lakini ni wajibu wa Serikali sasa kuona namna gani tunatoka. Mimi nina ushauri, umefika wakati sasa Serikali ichague shule moja ya sekondari ya mkoa iipatie *facilities* na iwe na *curriculum* ya michezo tu, iwe na masomo saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masomo hayo saba, ziwe lugha zote ikiwepo Kiswahili, Kifaransa, Kiingereza na Kispaniola halafu na somo la Historia, Geografia na Uraia. Yanatosha kabisa. Halafu vyama vya soka vikishirikiana na Maafisa Utamaduni watafute wachezaji kuititia UMITASHUMITA na UMISETA, hao waingie kwenye ile shule maalum ya michezo ya Mkoa. Tukifanya hivi, nina imani baada ya muda siyo mrefu, mambo yatakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, naomba niliseme kwa kifupi tu. Hii wiki kuna sintofahamu iliyokuwa ikiongelewa humu Bungeni kuhusu umiliki wa viwanja vya michezo vinavyomilikiwa na Chama cha Mapinduzi. Naomba nitumie fursa hii kuliambia Bunge lako Tukufu, sera ya TANU mwaka 1957 ilikuwa ni kuboresha michezo. Pamoja na hilo, katika harakati zetu za kupata uhuru, Chama cha TANU kiliishirikisha Yanga na Simba katika vuguvugu la kuleta uhuru mpaka uhuru ukapatikana mwaka 1961. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka ule mpaka leo Chama cha Mapinduzi kimekuwa na sera kila kwenye tawi lao au kwenye Ofisi ya Mkoa kutenga eneo kwa ajili ya michezo. Hiyo kazi hawakuwahi kuicha. Kwa kukuthibitishia hilo, mlezi wa Yanga kwa kipindi kile alikuwa ni Mzee Karume na mlezi wa Simba alikuwa Mzee Kawawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1961 Tanzania ilikuwa katika mfumo wa vyama vingi, wala hakikuwa chama kimoja. Katika kipindi cha mfumo wa vyama vingi 1961 mpaka 1965 bado TANU iliendelee kuhimiza ukuaji wa michezo na maazimio ya kujenga viwanja vya mpira halikuwahi kuwa azimio la Serikali, bali liliikuwa ni azimio la Halmashauri Kuu ya TANU na baadaye Halmashauri Kuu ya CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuwaambia, mwaka 1992 tulipokwenda kwenye mfumo wa kurudisha vyama vingi kwa mara ya pili, waliotaka kwenda kwenye vyama vingine walikwenda kwa hiari yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipata swali la kuijuliza, hebu tuulizane hapa Mheshimiwa Lwakatare alianza na *CUF*. Je, alipojenga zile Ofisi za *CUF* baada ya kuhamia CHADEMA anadai matofali ya Ofisi zake? Ni kitu ambacho hakiingii akilini. Ninachotaka kusema, sera ya michezo ni sera ya CCM. (*Makofi*)

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

### **TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka *record* sawa, Ofisi Kuu ya Chama pale Buguruni, hazikujengwa, chama kilinunua. Kwa hiyo, siyo kwamba kuna mtu alijenga, hapana. Chama kilinunua.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, tatizo ni tafsiri tu. Kujenga au kununua ni wazi ilitokana na michango ya Wanachama. Hela za wanachama ndizo zilizojenga. Mchang wa mwanachama mmoja mmoja ndiyo uliojenga hizi *facilities*. Hii siyo hoja ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ni kwamba *from day one*, TANU ikiazishwa na CCM ilikuwa na sera mahususi ya michezo, ndiyo maana mpaka leo kila kwenye Ofisi ya CCM kuna kiwanja cha michezo. Hebu tuwaalize nyie wenzenetu, kwenye Ofisi zenu mna hatu yadi mbili za watoto kucheza kitenesi? Sasa kwa nini leo mnataka kudai viwanja? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaambieni kitu kimoja, kukuthibitishieni kwamba michezo ni sehemu ya Chama cha Mapinduzi mpaka mwaka

1998 kwenye Katiba ya Yanga na Simba, viongozi wao, Marais wao walikuwa wanateuliwa na Kamati ya Utekelezaji ya Umoja wa Vijana wa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yussuf, jiandae Mheshimiwa Machano Said na Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
*Bismillah Rahman Rahim.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na leo nilikuwa nichangie kwa ukali sana, lakini Mheshimiwa Waziri ashukuru kwamba hotuba yake imekuja katika siku Tukufu na katika siku ya leo sisi Waislam huwa tunahusiana *uusi kum ibada-Allah wanafsi-bitakuwa-Allah*. Kwa hiyo, nitamshauri zaidi kuliko kwenda katika yale mambo ambayo nilikuwa nimeyapanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza sana katika nchi yetu kuhusu kuporomoka kwa maadili. Maadili yanaporomokaje? Vijana wetu tunasema hawana maadili, nyimbo hazina maadili, michezo haina maadili; sasa nani hana maadili? Ni sisi wenyewe ndio hatuna maadili. Hatuna kwa sababu gani? Kwa sababu tumekubali kuwa watumwa tukaacha mila na utamaduni wetu na tukaiga mila nytingine. Mheshimiwa Waziri pale kila siku anaenda na nyimbo za kizazi kipyga, sijui nini, lakini hujamsikia akihamasisha ngoma za asili au tamaduni zetu za kiasili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati wa ngoma zile jando na unyago, misondo, akinamama wanavunja ungo wanawekewa ngoma, wanafundishwa, pale ndiyo tunafundishwa maadili. Leo katika hao wasanii wa kizazi kipyga, ukimwondoa Mr Ebbo ni nani anavaa kivazi cha asili cha Mtanzania kuitangaza Tanzania yetu? Hakuna. Wote wanaiga. Ni suruali chini ya matako, anajishika hapa, anajikunjakunja; kwa nini tusiende katika mila na destuli zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri ahamasishe ngoma zetu za asili ili vijana wetu angalau wajue mila na desturi na asili yao. Leo humu ndani ya Bunge ukiondoa katika hawa watoto wangu, ukimwondoa Mheshimiwa Mtemi Chenge, ukimwondoa Mheshimiwa Musukuma labda na Mheshimiwa Ndassa, ni Mnyamwezi gani anayeweza kucheza Lizombe humu? Mheshimiwa Kigwangalla hawezhi.

Kwa hiyo...

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## **TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba tu nimpe taarifa kwamba, nakubaliana na ushauri wake anaoutoa. Nataka tu niweke katika *records* kwamba alipozungumza kusema, ukimwondoa Mr. Ebbo kwamba ni nani sasa hivi anayetukuza huo utamaduni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yangu ni kwamba Mr. Ebbo kwa sasa ni Marehemu. Kwa hiyo, taarifa ziwekwe kwamba ukimwachcha Mr. Ebbo ambaye sasa hivi ni Marehemu: Je, ni nani mwingine ambaye amerithi, anafuata utamaduni aliokuwa anafanya Mr. Ebbo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Changu ni hicho tu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana shemeji yangu. Napokea taarifa yake. Mwenyezi Mungu amweke Mr. Ebbo mahali panapostahili kwa kazi yake aliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, turudi katika mila na desturi zetu. Hata utalii tunapoutangaza huko nje, tunapotumia mila na desturi zetu, basi watalii wanavutika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa katika utalii. Wageni wanapokuja, tunapowawekea ngoma za kiasili wanafurahi zaidi, wanacheza na mpaka wanakwambia sasa tutafutie tena utuwekee. Wanapenda mchezo wa ng'ombe, wanapenda ngoma za kiasili, lakini leo sisi tumeingia katika kizazi tu hiki. Sasa unasema maadili yamepotoka, ni sisi wenyewe ndiyo tunayapotoa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kila mwanamichezo hapa amelalamika kwamba michezo inakufa, tunapeleka watu haturudi na medali, tunarudi na aibu, tunatoka kwa shangwe, tunarudi na msiba; ndiyo. Kwa sababu wanamichezo wazuri walikuwa wanapatikana mashulen. Leo katika shule hakuna huo utamaduni wa hii michezo kuendelezwa, ikafika kipindi ikafungiwa kabisa ikawa haipo, mara inarudishwa. Kwa hiyo, hatujui tunafanya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la michezo katika mashule jamani, michezo ni afya. Watoto wanapocheza, utakuta wale watoto wanaofanya michezo mashulen ndiyo wanakuwa *active* vilevile katika masomo. Kwa hiyo, pale ndiyo sehemu ambapo tunajenga michezo, lakini ndiyo sehemu ambapo tunapata vipaji. Sasa hapo Mheshimiwa Waziri ukishapata kutoka shulen: Je, una vyuo vya kuwapeleka na kuwaendeleza? Hili nalo ni swalii ambalo Mheshimiwa Waziri aliweke katika kichwa chake, leo nimemwambia na namsaidia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, limezungumzwa sana, Mheshimiwa Waziri anafungia nyimbo, lakini nyimbo inafungiwa baada ya kuwa imeshatoka baada ya mwaka mmoja, mwaka mmoja na nusu au miezi sita. Tayari kile kibaya ambacho unakiona wewe kipo pale anakifungia kimeshakwenda huko katika Jamii. Sasa kwa niniaunafungia nyimbo? Mimi sijui labda atanisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa shulenii nilikuwa msanii vilevile. Nilikuwa siendi hewani mpaka kuna *Board of Sensor* inapita, inasikiliza kile ambacho nitakipeleka hewani na panafanya wa marekebisho; aah, hili ondoa, hili peleka, hili fanya hivi. Nikimaliza wanarudi tena ndiyo unaruhusiwa sasa kutoka hewani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anakwenda kumfungia msanii ameshapata gharama, nyimbo imeshatoka, kama ni maadili yamepotoka, ndiyo leo anakuja kuifungia nyimbo wakati ujumbe umeshatoka? Sasa Mheshimiwa Waziri katika hili naomba hizi *Board of Sensors* ziwe zinafanya kazi zake kabla ya wimbo kutoka kama ni mavazi, kama ni maneno yenye we yaliyotumika, kama ni kitu gani, kifanyike kwanza. Sasa unakuja kufunga banda, farasi ameshatoka, sijui unafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, anafungia magazeti, redio; sasa hivi vitu kwetu ni vipyta. Hapa ilikuwa magazeti ni ya Serikali tu, *Redio ni za Serikali tu*, hata hiyo *television* yenye we ilikuwa hakuna, alikuwanayo Mwalimu pekee, anaangalia, kesho anakwambia nimeota Urusi kuna vita. Sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu Mheshimiwa Waziri anatakiwa avilee. Sasa wakati anavilea hivi vitu anatakiwa aweke utaratibu, havikuwa katika tamaduni zetu. Sasa kama havikuwa katika tamaduni zetu, ni kitu kipyta, lazima Mheshimiwa Waziri akae, atulie, aone namna gani atakwenda navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni changamoto ambazo zitakuwepo nyingi kwa sababu vyombo vilikuwa vinamilikiwa na Serikali, leo watu binafsi wanamiliki vyombo, kila mmoja ana mtazamo wake, ana fikira yake, unaona? Kwa hiyo, Waziri ambaye anasimamia hili anatakiwa avilee. Sasa leo Mheshimiwa Waziri mwenyewe amegeuka kama kuku mvia; anataga yai lake, halafu analila mwenyewe. Sijui tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kingine ambacho kimetokea hapa, kimezungumzwa na wachangiaji baadhi hapa kwamba Waandishi wa Habari wanapotea; Serikali haitoi taarifa yoyote. Sasa akitokea mtu na mtandao wake, akatoa taarifa, hata kama ni ya upotoshaji, hiyo ndiyo itaaminika, kwa sababu wewe kama Waziri hujafanya kazi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshauri kwamba linapotoka tatizo kama hilo, wakati hao ni watu wake, tuwahi kutoa taarifa hii. Sasa taarifa nydingine itakayokuja itakuwa hiyo sasa ni ya upotoshaji au Serikali imeshasema, lakini kama Mheshimiwa Waziri ananyamaza, akitokea mwingine akisema, anakwenda kusema huyo ni mchochezi, huyo fisadi, huyo hivi; nani hakufanya kazi yake? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Waziri atoe taarifa kwa wakati. Waandishi wa Habari wanapotea na Waandishi wa Habari hawa, kusema na kuandika ndiyo kazi yao. lazima watasema! Sasa wakisema sivyo, kosa siyo lao, kosa ni lako ambaye hukutoa taarifa kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kingine ambacho nataka kukzungumza cha mwisho kuhusu mapato ya *TFF* na *ZFA*. Kuna mgao ambaou huwa *TFF* inapata kila mwaka kutoka *FIFA*. Zanzibar ukiondoa kiwanja cha Gombani kuwekewa nyasi tokea kuanzishwa haya, ikaondolewa Zanzibar, inategemea *TFF* haijawahi kupata mgao mwingine. Kwa hiyo, hizi pesa zinakwenda wapi? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunalotaka kujuu, hapo zamani tulikuwa tunapata Dola laki 2.5 kwa mwaka kutoka *FIFA*, lakini hapo katikati hizi pesa wakazizua, wakawa hawazileti kwa sababu ya mambo yaliyojiteze hapo, ujisadi, *accounts* zenyewe haziko sawa na kadhalika, kwa hiyo, hizi pesa zikazuwa. Je, hizo pesa zimeanza kurudi? Sasa zimefikia hiyo laki 7.5 tunayoambwiwa au vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yote yanatakiwa kuwekwa wazi. Mheshimiwa Waziri atakapoweka wazi; atakapozungumza haya mambo kwa wakati, hawezi kusikia malalamiko. Hata yakitoka yale malalamiko, itakuwa tayari Mheshimiwa Waziri ameshayasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo nimezungumza kwa upole sana na Mheshimiwa Waziri kumwonesha namna gani aweze kufanya kazi vizuri katika hii Wizara. Hii Wizara inaonekana kama ni Wizara tu hivi nyepesi nyepesi na nini, lakini Wizara hii ndio inabeba maisha yetu. Kinapopotea kizazi chetu, inapotoka taarifa ya upotoshaji, inaweza ikaligharimu Taifa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Machano dakika 10 na Mheshimiwa Abdallah Bulembo dakika 10.

**MHE. KHAMIS YAHYA MACHANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku njema. Pia nachukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kuwasilisha bajeti yao leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo kama matatu ambayo nitayazungumza kwa sababu leo siku ya Ijumaa. Jambo la kwanza ambalo nitaanza kuzungumzia ni kuhusu *TBC*. Kwa upande wa *7V* nawapongeza sana kwamba wako makini na wanaonekana karibu katika nchi nzima. Kwa *TBC Radio* hasa kwa upande wa Zanzibar, usikivu wake ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri ajiimarishe katika Kitengo chake cha *TBC Radio* Zanzibar ili iweze kusikika na kushindana na Redio nyingine kwa sababu *TBC* ni Redio ya Kitaifa na ina umuhimu sana katika shughuli za maendeleo ya wananchi,

kuwaelimisha lakini pia burudani kwa wananchi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri akiangalie kitengo chake cha Zanzibar katika *TBC Radio*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nami kama Waheshimiwa wenzangu nizungumzie michezo; na nitazungumzia mpira wa miguu, riadha na ndondi. Hii miwili naizungumzia zaidi Kimataifa, yaani riadha na ndondi. Kwa muda mrefu tunashiriki katika mashindano mbalimbali lakini ushiriki wetu unakuwa hauna mafanikio sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi uliopita au mwisho wa mwezi huu tulikwenda katika Jumuiya ya Madola, lakini hatukurudi hata na medali moja. Kosa kubwa ambalo tumelifanya, baadhi ya wanariadha wanaotegemewa ambao wengi wanatoka katika vikosi vyetu vya ulinzi hawakushiriki na hatimaye Tanzania imerudi mikono mitupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wakae na Wizara ya Ulinzi ili waangalie taratibu gani zitawezekana ili wanamichezo wetu waweze kushiriki katika mashindano haya ya Kimataifa. Ni aibu kwa nchi yetu kwenda katika mashindano yale na tukarudi mikono mitupu wakati majirani zetu Kenya na Uganda wamerudi na medali kibao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kusikitisha katika riadha, kuna baadhi ya wanamichezo hawakwenda Jumuiya ya Madola na waliruhusiwa ili wajiandae na *London Marathon*, lakini hatua ya mwisho wanariadha hawa nao hawakuruhusiwa na hawakwenda na Tanzania ikakosa tena medali katika *London Marathon* ambayo tunaipata kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hili nalo Serkali waliangalie, waweke utaratibu ili tujiandae kwa mwakani kwa sababu kutokushiriki kwetu, kwanza tunakosa medali lakini pili, tunawavunja moyo wale wanariadha wenywewe kwa sababu hili nalo ni suala la ajira yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie mpira wa miguu. Kwanza nianze kwa kuzipongeza timu zetu za vijana za *Serengeti Boys na Ngorongoro Heroes*. Tumeweza kuingia fainali katika Mashindano ya Vijana wa Afrika Mashariki na Kati, lakini pia timu yetu ya Ngorongoro nafikiri inakwenda katika mechi ya mwisho kabla ya kwenda *AFCON* kwa vijana chini ya miaka 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwapongeze sana Wizara na *TFF* kwa mafanikio ambayo tumefikia. Kwa bahati nzuri, timu zote mbili hizi ziko chini ya makocha Wazalendo. Kwa hiyo, kama alivyosema Mheshimiwa Chumi, kama Serikali itapanga mpango mkakati wa kuwasomesha makocha Wazalendo, mimi naona kwamba faida kubwa inaweza kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uendeshaji wa *TFF*; *TFF* wamefanya uchanguzi mwishoni mwa mwaka 2017, wamepata viongozi wapya. Wapenzi wa mpira wote wana matumaini makubwa na uongozi huo, lakini hapa katikati tumeanza kusikia migogoro ya kufukuzana na mambo mengine. Naomba Mheshimiwa Waziri ukae nao hawa wakae vizuri kwa sababu tukiwa na uongozi mzuri, imani ya wananchi ya Serikali na mashirikisho ya Kimataifa yanakuwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mwenyewe ni shahidi kwamba mwaka huu tulipata ugeni mkubwa wa Rais wa *FIFA* na akifuatana na Rais wa *CAF* yaani Shirikisho la Mpira la Afrika. Wamekuja Tanzania, wamezungumza, wametoa ahadi nydingi lakini ahadi zile haziwezi kutekelezeka kama uongozi wenyewe utakuwa wa kuyumba na wa kubabua babua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo pia tetesi za upotevu wa mapato katika mpira kama alivyosema Mheshimiwa Cosato Chumi kwa uwanja mkuu wa Taifa na uwanja wa uhuru. Kamati imesema kwamba mapato haya yachanganuliwe, kila uwanja uwekewe mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lipo tatizo katika uwanja Mkuu wa Taifa. Wakati wa mechii kubwa katika uwanja ule kunakuwa na uuzaaji wa madawa ya kulevyaa na zaidi bangi. Sasa kwa bahati nzuri *TFF* wanaye Mkuu wa Usalama wa Viwanja. Tatizo hili linalotokea, Mheshimiwa Waziri tunaomba alifanyie kazi ili suala hili lisiweze kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nizungumzie kwa uchache kuhusu wasanii kwa sababu leo ni siku ya Ijumaa nami nataka kukimbilia Msikitini kama wenzangu, kwanza nawapongeza wasanii wote wa Tanzania kwa juhudii zao za kuendeleza sanaa, tumetoka katika burudani, lakini sasa tumeingia katika ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ni vyema wasanii wakawa na maadili, lakini taratibu zifuatwe. Kama BASATA wamepewa fursa hii kikanuni, basi na wao watumie nafasi yao kufanya kazi kikanuni ili tuepuke kuwabebesha Mheshimiwa Waziri au Viongozi wa Wizara kufanya kazi ya BASATA ambalo limeundwa kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wapo wasanii wengine wanapotoka, wanazidisha mambo yao, lakini ni ukweli ulio wazi kwamba tunachelewa sana kuwaelimisha na kuwachukulia hatua. Wakati mwingine tunapochukua hatua ni kama tunawazindua watu kwamba kumbe ile nyimbo nayo ina maudhui mabaya. Watu wengine walikuwa hata hawajui kama kuna maudhui mabaya katika hiszo nyimbo, lakini tunapowazindua ndiyo tunakuwa tumewazindua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vyema, kwa sababu BASATA kazi yake inashughulikia, inaangalia na kadhalika, tuchukulie kama Baraza la Michezo la Taifa. Katika mchakato wa *club* kuingia ubia na wafadhili mbalimbali, wametoa mwongozo wao kwamba ili ukubaliwe kufanya hili, lazima uwe na moja, mbili, tatu. Kwa hiyo, vile vilabu vinalelewa kwamba tukikubaliana katika jambo hili tutafikia

hatua hii; tukikosana hapa, hatuwezi kwenda ingawa bado kuna maoni kwamba hata ingekuwa *fifty, fifty* katika uwekezaji ingekuwa siyo jambo baya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo, naomba niunge mkono bajeti hii ya Wizara ya Habari kwa asilimia mia moja na nawaomba wenzangu waipitishe bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bulembo, halafu ajiandae Mheshimiwa Mussa Sima na Mheshimiwa Tauhidha. Kutegemea na muda utakavyokwenda.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nami nafasi hii ya kuchangia eneo muhimu sana hili la michezo. Pongezi zangu nizipeleke kwa kaka yangu Mheshimiwa Harrison Mwakyembe na Mheshimiwa Naibu wake, Katibu Mkuu, Watendaji wote na Ma-CEO wote waliokuwa katika taasisi zake. Pongezi zaidi nisisahau kuzipeleka kwenye timu yangu ya Simba ambayo inakaribia kuwa bingwa wa nchi hii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Hebu rudia tena hapo! (*Kicheko*)

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, pongezi zaidi zipelekwe kwa timu yangu ya Simba ambayo inakaribia kuwa bingwa wa nchi hii. (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mataifa yaliyoendelea, katika eneo la michezo wamekuwa wakiwapa nafasi wachezaji wao. Ni eneo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi zao. Mfano, kwenye bajeti zetu hapa tunatafuta hela nyingi za barabara,

maji na afya. Mataifa yaliyoendelea yanawekeza kama tunavyowekeza kwenye barabara, afya na elimu. Nini maana yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mtoto aweze kuandaliwa, lazima uanze naye chini. Huyu anaweza kuikimbia, huyu anaweza kucheza mpira, anaweza ngumi, anaweza kutupa tufe; lakini wanaowekeza hivyo kila mwaka wanapofika kwenye mashindano ya Kimataifa utaona wanapokelewa na medani nyingi, wanaongeza uchumi wa nchi yao, wanaongeza pato la nchi yao. Kwa hiyo, katika michezo hii ni ajira, ni mapato, nchi inapata. lakini kwetu hapa sijui sana tunakwendaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye michezo ya Madola, ukienda kwenye michezo ya Olimpiki nchi nyingi, angalia jirani zetu Kenya wanakuja na medali. Hakuna medali inakwenda bure. Kila ukiona medali ni pesa zimeingia kwenye nchi yao. Sasa sisi ukiangalia historia ilivyo, tumeweza kupata medali kama sikosei, ilikuwa mwaka 1980, tulipoenda kushiriki Olimpiki Urusi na medali mbili ndiyo tulipata hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *sports* ni 1992 kama sikosei kushiriki mashindano ya Afrika. Kuanzia hapo, shughuli hii ni kama haipo. Ni kwa nini? ni kwa sababu hatujakubali kuwekeza kwenye Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachezaji walikuwa wengi ni sawasawa na waimbaji walivyo. Anajitokeza mchezaji mmoja kwa hiari yake, wanajitumikisha, anafanya nini, anapatikana, anafikia viwango tunaiambia Wizara anaondoka kesho njoo umkabidhi bendera. Huyu mchezaji katengenezwa na nani? Nani anajua alipo? Nani kamfanyia maandalizi? Thamani yake ni ipi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu katika eneo hili la mchezaji mmoja mmoja ndiyo tunashiriki naye, nchi yetu itaendelea kuwa kichwa cha mwendawazimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili, tuelekee kwenye vyuo. Katika nchi yetu Chuo cha Michezo ni Malya na Kaole kinachoitwa Chuo cha Sanaa. Ukiangalia kwenye bajeti ya maendeleo Malya ni shilingi milioni 150. Tuko *serious?* Tuna nia njema? Chuo hiki kinakufa. Mheshimiwa Mama Ndalichako nataka baadaye anijibu, Chuo hiki ni lini kitawezeka kutoa *degree* katika nchi hii? Kwa nini kinachechemea? Kwa nini hawakithamini? Tunapendaje michezo ambako hatuwezi kuwekeza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende TAMISEMI. Kila mwaka wana UMISETA na UMITASHUMTA. Wanaokwenda kuratibu mashindano haya na kuwapata wachezaji, mnawatoa wapi? Au unamchukua Mwalimu kwenye darasa, anajua kufunga goli, unamwambia wewe ni Mwalimu wa Michezo? Haiwezekani. Chama changu na Serikali yangu tumetamka ndani ya llani kuendeleza michezo. Tunaendeleza michezo kwa kusababisha Malya kupata shilingi milioni 150? Chuo pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michezo hii, ukitoka hapo Mzee Mkuchika simwoni humu ndani, lakini naomba wanijibu wakati wanajibu; katika ajira 52,000 nataka aniambie Maafisa Utamaduni ni wangapi? Maafisa Michezo ni wangapi katika ajira hiyo? Katika Halmashauri, Maafisa Utamaduni hawa wapo? Wanafanya kazi hii? Au tunapenda michezo watu wamejishindia wenye we tunawaita Bungeni kuwapigia makofi hapa! Tumewaandaaje? Tunawaandaa vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Serikali yangu, haiwezekani. Kama tunataka kusimamia michezo, tuweke msingi kwenye michezo. Michezo hii ni ajira sana. Naomba niwapongeze *TFF*, bora kidogo wanachokipata tunakiona, wanaandaa timu za vijana *under 17, under 20* wanashiriki, bora wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hebu aniambie *TOC* hela zao ziko wapi? Mashirikisho yoyote yaliyosajiliwa hapa nchini yanapata pesa kutoka nje. Pamoja

na kwamba zile pesa zinatoka nje, wanaziratibu vi? Wanamsaidia nani? Au ni meza tu watu wemekaa, ukishajili NGO yako, noti zinaingia, mambo yanaendelea? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumempata kwa Mheshimiwa Waziri pale mtu mmoja, nilisikia anamteua Mwenyekiti, Mheshimiwa Leodegar Tenga, mimi namkumbuka kama Mwalimu wangu. Wakati nagombea *FAT* alikuwa ananihoji, nashinda. Baadaye naye ameenda *FAT, TFF*, leo amekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu kwa Mheshimiwa Waziri, naomba Baraza la Michezo atakalolizindua alipe kazi ya kwenda kupitia sera hii. Sera ya Michezo ni butu. Mpira na riadha katika Tanzania siyo mchezo peke yake. Kuna ngumi, karate, *boxing* na vitu vingi sana viro, vinapatikanaje? Vinapatikana wapi? Wanaviandaa vi? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri wakati mwingine akatae kwenda kutoa bendera, kwa sababu haiwezekani Serikali inatoa bendera, haimwandai anayeenda kushiriki michezo hiyo. Anamwandalia wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kunijibu, aje na maelezo mazuri ya kuniambala kama yuko tayari, wanaposema Sera ya Michezo ipo, imekuja lini hapa tukaipitisha ili wakatayarische kanuni watu wakajua? Kwa sababu ipo ndani ya makomputa, iletwe hapa kwenye Bunge lijalo tuambiwe tunataka kufanya hiki na hiki kwenye michezo ili tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tupate mabadiliko ya kweli kwenye michezo. Lazima tukubali kuwekeza kwenye michezo, lakini hatuwezi kuipata michezo bila kuwekeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri; haiwezekani bajeti ya maendeleo ikawa

shilingi bilioni nane. Kamati inasema tumeongeza. Wameongeza nini? Wameongeza asilimia 20. Nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC*, nataka nitoe mfano. Nilibahatika kutembea kwenye nchi hii nikiomba kura na Mheshimiwa Rais wa nchi hii. Tulikuwa na chombo kimoja kinaitwa *Star TV*. Tukisema mukutano saa 4.00 anaweka chombo, tunarusha nchi nzima; tukisema saa 7.00, anaweka tunarusha nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* leo, Mheshimiwa Rais leo yuko Kondo, Mheshimiwa Waziri Mkuu leo aende Nyasa, Makamu wa Rais aende Zanzibar, *TBC* Chaiwezi. Haina vyombo kwamba unaweza kumwona Mheshimiwa Rais ukamwona Waziri Mkuu na Makamu wa Rais. Kwa nini? Chombo hiki ndiyo cha nchi. Hizi hela amepewa hapa shilingi bilioni tano hazitoshi kabisa, yaani hawezi kuiweka *TBC ika-compete* na watu wengine kwa shilingi bilioni tano. Ni hela ndogo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tutailamu *TBC*, tutawafukuza kila wanaokwenda kila siku, lakini kama hatukuwawezesha, tunategemea lini wafanye kazi vizuri? Nilitaka kusahau pale kwa Mheshimiwa Waziri Jafo, naye anijibu hapa ndani. UMITASHUMTA na UMISETA, wale Walimu wanaoenda kuchuja, wanawapata wapi? Wanawapatajaje? Au wazazi wanatoa hela, watoto wanaenda kule, majibu hayapatikani? Kwa sababu Wizara hizi ni mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akifika hapa anijibu, lini Wizara inayohusiana na michezo walikutana kikao? Walikutana wapi? Waliamua nini? Wanaendeleza nini? Kwa sababu hapa kuna elimu, hapa kuna utumishi, hapa kuna TAMISEMI na Wizara yake. Lini wanakutana au kila mtu anafanya lake? Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihadie hapa Bungeni, kwenye michezo niliuliza swali, kiti hicho alikuwa amekalia Mheshimiwa Mtemi Chenge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ABDALLAH M. BOLEMBO:** Imeisha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo imeisha. Ahsante kwa mchango mzuri na maneno mazuri uliyozungumza. Sasa namwita Mheshimiwa Mussa Sima, ajiandae Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Pia nami nachukua fursa hii kuwapongeza sana mabingwa wa Tanzania Dar Yanga Afrika, wameweza kutuwakilisha vyema Kimataifa na sasa wameingia kwenye makundi. Pia nichukue fursa hii kuwapongeza vijana wetu wa *Singida United* ambao wamefanya vizuri na sasa wameingia fainali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa nzuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nampongeza yeye na Naibu wake; pia yako maeneo tuna kila sababu ya kushauri. Wizara kama ambavyo wameeleza wenzangu, kwa sasa kuna eneo muhimu sana, tunazungumzia *entertainment industry*. Kwenye eneo hili la kiwanda, nilitarajia kuiona Wizara inatambua kwamba hapa tuna kiwanda. Tukishazungumza kiwanda, *content* za kiwanda zinajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya vizuri, iko Bodi ya Filamu ya Tanzania, iko Baraza la Sanaa (BASATA), lakini iko BMT. Vyombo vyote hivi vyaya Serikali havijaonesha ni namna gani vinawekeza kwenye kiwanda hiki? Havijaweka mazingira wezeshi ya wawekezaji kuja kuwekeza, badala yake kwa asilimia kubwa vime-deal/sana na maadili ambalo ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe kidogo. Kwenye tasnia hii ya filamu, tulikuwa na Marehemu Kanumba, alifanya kazi kubwa sana kuitangaza Tanzania; lakini hata baada ya kutangulia mbele ya haki, kazi zake zinaonekana. Leo nilitaka kuona Mpango Kazi wa Serikali wa kutuwezesha

sasa kuwa na akina Kanumba wengine ili kuweza kui-promote Tanzania. Hatujauona Mpango Kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukumbuke, sasa hivi kijana wetu Diamond anakwenda kutumbuiza kwenye *World Cup*. Ni fahari ya Tanzania. Najua wakati anaondoka tutamkabidhi bendera na wakati anarudi tutampokea vizuri, tutapiga picha na vitu vingine. Tunajifunza nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Diamond haendi kuwakilisha *Wasafi Record*, anaenda kuwakilisha Tanzania. Tunatarajia kwa uwakilishi wake duniani wawekezaji watataka kuja Tanzania. Je, mazingira ya kuwekeza tumeyaweka? Wale wawekezaji hawawezi wakaja wakaenda *Wasafi Record*, watakuja kwenye Wizara ya Habari na Utamaduni kujua mazingira ya kuwekeza kwenye sanaa hili yakoje? Hakuna mazingira yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *consistency*hii haipo. Maana yake hatuna watu wengine ambao tunaweza kuwaandaa wakaweza kuitangaza Tanzania, lakini badala yake tumeweza kusimamia kwenye eneo la maadili ambalo mimi naliunga mkono. Ila tulipaswa kutambua, tusitazame tulipoangukia, tunatakiwa tutazame tulikojikwaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka maadili yamepotoka, mpango huu wa maadili kupotoka Serikali ilipaswa iangalie wapi ambapo maadili yamepotoka? Siyo kurudi kuanza kufunga tu kuangalia maadili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ni ushindani na mazingira haya ya ushindani yanawapa wakati mgumu sana wasanii. Ili aweze kutoka na mazingira magumu aliyopitia, ni lazima aangalie nchi nyingine wamefanya nini ili aweze kushindana na hilo soko. Katika ushindani huo, lazima tuingie kwenye mazingira haya. Nasi Watanzania tunataka kuangalia kwa sababu tayari jamii yetu imekuwa ina mtazamo huo, lazima turudi, Serikali ikae na wasanii hawa, ikae na wanamichezo wote, izungumze nao. Wanapitia mazingira magumu sana! Kwa mazingira hayohayo, iwekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia kazi ya Bodi ya Filamu, eneo kubwa sana ni tamasha, makongamano na kadhalika. Sijaona mahali ambapo inaenda kuwekeza kwa hao wasanii. Itatupa mazingira magumu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie eneo hili la soka. Sisi wadau wa soka, tunafika mahali tunajivunia eneo ambalo Shirikisho la Michezo la Taifa imelisimamia, tumewapa mzigo mkubwa sana na *TFF* wanafanya kazi kubwa sana, lakini taarifa yote hii ya Serikali haijatambua hata mchango wa *TFF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipaswa kwenye bajeti hii na taarifa ya Serikali ioneshe ni namna gani inaweza kuwasaidia *TFF* kufikia malengo yaliyotarajiwa. Sasa *TFF* haiwezi kufika mahali ikaandaa na viwanja ama ikajenga viwanja. Serikali ilipaswa ituoneshe mpango thabiti hapa wa kujenga viwanja, lakini ilipaswa itoe maelekezo kwenye Halmashauri zetu, itenge maeneo ya viwanja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo viwanja ambavyo unaviona, vingi ni vya Chama cha Mapinduzi. Nilitarajia kuiona Serikali iingie ubia na CCM katika uboreshaji wa vile viwanja ili viweze kusaidia kwenye eneo hili la soka. Sasa kama huna viwanja na viwanja vimesimamiwa na mapato ya kiwanja kwenye *gate collection* ni asilimia 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana Baraza la Michezo la Taifa lenyewe linapata asilimia moja na wanaridhika. Kwenye *gate collection* wanapata asilimia moja wanaridhika. Sasa utaendeleza michezo Tanzania? Maana yake inaonesha kabisa hakuna *link* hapa ya Serikali na Chama cha Mpira kwa maana ya Chama cha Soka. Hamna *link* yoyote! Serikali lazima ilitazame hili; inawezajie kusaidia kwenye eneo hili la soka? Tofauti na hapa, hatutaweza kufanikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wa *Ngorongoro Heroes* na *Serengeti Boys*, nichukue fursa hii kuwapongeza

sana. Hizi ni juhudini binafsi za wazalendo, wanafanya kazi kubwa sana. Nilitarajia kuona mpango wa Serikali utakaowezesha vijana hawa *under 17* wengine *under 21* kwa miaka ijao tuwe na timu ya Taifa bora. Sijaona mpango wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri kama inawezekana, ni vizuri vijana hawa tukawapeleka nje hata kwenye *Academy* za wenzetu ambako soka limeendelea, lakini tukawapeleka kwa mkopo kwenye timu za nje hata kama ni za daraja la nne na kuendelea wakapikwa kule, hata kama Serikali ikigharamia wale vijana wakaa kule. Wakiwaacha huku wakaja kwenye timu zetu, watakuwa *polluted* na wala hawatawaona. Nasi Timu yetu ya Taifa hata siku moja hatuwezi kufika mahali tukaweza kuingia kwenye mashindano makubwa tukasema sasa timu yetu ya Taifa itafanya vizuri, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iliangalie eneo hili. Kwa mazingira haya tunazungumzia uchumi wa nchi. Uchumi wa nchi, hauwezi kujengwa tu na viwanda vingine. Natarajia kumwona na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, anatambua kwamba kuna *entertainment industry* katika viwanda vyake 3,600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanda kikubwa kuliko viwanda vyote; na kwa sababu najua huwa anaweka machanganuo mzuri kwamba kuna viwanda vikubwa, vyakati, vidogo na vidogo sana, maana hata kiwanda cha juisi anakiita kiwanda kidogo. Sasa *entertainment industry* ni kiwanda kikubwa sana. Kimeajiri vijana wengi. Lazima tuwe na mpango kazi na lazima tujitathimini wenywewe kabla ya kuamua kukwamisha kazi zao. Ndugu zangu, kazi hii ni ngumu mno. Sisi wanamichezo tunajua huko tunakoelekea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejikita kwenye UMISETA na UMITASHUMTA. Sisi Walimu tunajua lile ni somo, lakini je, Serikali kama inajua hili ni somo na imesimamia kule, imewezesha kwa kiwango gani maeneo haya hizi shule

zikafanya vizuri? Siyo tu kufanya vizuri, mwisho wake nini? Wale vijana wanapoenda kwenye mashindano yale wakamaliza, mwisho wake nini? Maana siyo wanaenda kwenye mashindano wanarudi, biashara imeisha. Ni lazima kuwe na mpango kazi wa Serikali utakaoendeaza michezo mashulenii. Watoto wale wakimaliza wanaenda wapi? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitarajia kuona hata kama hatuwezi kujenga *Academy*, uwepo mpango tu kwamba Serikali imeweka mpango wa kuwa na *Academy*, watoto wanatoka shule wanaingia kwenye *Academy* tunaendeaza vipaji vyao. Leo tutakuwa tunazungumza habari ya eneo hili la michezo, tutalizungumza tu, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lijualikali dakika tano.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampa pole Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Heche kwa kufiwa na mdogo wake ambaye ameuawa akiwa Kituo cha Polisi. Kauawa ndani ya mikono ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, Wizara yetu ya Michezo pamoja na mambo yake yote inayofanya; na leo ameongea mwenzangu hapa, anasema viwanja ambavyo CCM ilivichukua kwa kuwa wameshindwa kuvifanyia kazi iwasaidie kuiendeaza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, huyu ana dakika tano tu. Sasa mtakapoanza *confusion*... Kaa chini, endelea wewe.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala kwanza haliwezekani. Kama mmeshindwa kuviendeleza viwanja ambavyo mmepora kwa wananchi, tena mpaka sasa wananchi tuwape fedha za kuviendeleza, *this is not fair*. Kama vimewashinda, mvirudishe kwetu tuviendeleze kwenye Halmashauri zetu ili wananchi wetu waweze kufanya michezo na Taifa liendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hata kule kwangu Ifakara, nina kiwanja kikubwa sana, CCM wamekipora. Kile kiwanja kimejengwa na wananchi kwa jasho la wananchi. Leo hii eti ni cha CCM. CCM hawana nyaraka yoyote, wame-forge nyaraka, haiwezekani. Kwa hiyo, naomba kwamba kama vimewashinda, mvirudishe kwetu tuvifanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Taifa lolote linatakiwa liwe na taswira ambayo inajenga heshima kwake. Taifa kama lina mambo ambayo hayaeleweki linakosa heshima kama ambavyo sisi kama hatueleweki tunakosa heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye Taifa letu tumeweka kanuni mpya za mitandao. *bloggers* leo wanaambiwa wachangie Sh.100,000/= ili waweze kupeleka habari. Sisi kama Taifa kama tunashindwa kuwasaidia wananchi wetu wapate taarifa kama Taifa, watu wanajitegemea wenyewe, wanaweka mipango yao, tunakuja tunawakatisha tamaa, hatuvezi kuendelea. Juzi hapa Mheshimiwa Rais amesema hatuvezi kuwa na mitandao kama China. Kama tunaweza kuiga ya China hayo, tuige pia na kunyonga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, China kule kama mtu anafanya makosa ya rushwa mashtaka yao ni kifo tu. Hukumu ni kifo. Sasa kama hili la China ni zuri, pia wachukue na hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wananchi wetu wanashindwa kupata taarifa za kimsingi, magazeti wanayafungia, tena wanayafungia kwa jambo hilo hilo ambalo linafanywa na mtu wa kawaida. Likifanywa kwa ajili ya kuisema Serikali jambo hilo hilo Mheshimiwa Waziri anasimama anachukua hatua; jambo hilo hilo likisemwa kwa ajili kumtukana Mwenyekiti ama Kiongozi wa Upinzani, Serikali wanakaa kimya. *This is not fair.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kujenga Taifa ambalo watu wanakuwa *treated* kwa mujibu wa matakwa ya kiongozi aliyeleo madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu linaongozwa kwa mujibu wa sheria; Taifa letu haliongozwi kwa mujibu wa maneno ama kwa mujibu wa kauli za klongozi yeoyote yule. Tuna sheria zetu, lazima tuzifanyie kazi. Haiwezekani tu mtu anasimama anasema kuanzia leo... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu ya mchana imekwisha. Jioni tutaanza na Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Profesa Jay na Mheshimiwa Mwamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri, jioni kwenye majibu hebu nielimishe kidogo kuhusu hii nyimbo Mwanaume Mashine mmeikataza kwa nini? Maana yake nyimbo hiyo inamtaja Kichuya, inamtaja Msuva na Jumapili tunataka tuisikie. Hebu mtuambie sababu yake ni nini?

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00. (*Kicheko/ Makofii*)

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilsitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa tunaendelea. Niliwataja wachangiaji watatu wa kwanza ambaye tunaanza na Mheshimiwa Ng'eleja, Profesa Jay na Balozi Mwamoto.

Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo wako nadhani kwa Kanuni ya 68(7) kuhusiana na jambo ambalo lilitokea leo mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba kuna maneno wakati mchangiaji anazungumza yalikuwa yamezungumzia kwamba mdogo wake Mheshimiwa Heche amepelekwa kituo cha Polisi yanayofanania kwamba amekufa akiwa katika Kituo cha Polisi. Kwa hiyo, naona kama ni maneno ambayo pengine siyo mazuri kwa sababu wote tunategemea sana vituo hivi vya Polisi na pale kituo cha Polisi kinapoonekana siyo chombo sahihi cha kukimbilia, pengine itakuwa siyo jambo jema likabakia kama liliivo kama utanikubalia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ulikuwepo hapa wakati inazungumzwa hiyo kitu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama lakini mwishoni sikubahatika kupata nafasi.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, sawa nitakujibu baadaye.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hatutaki kuanza mjadala.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo mijadala.

## T A A R I F A

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtaarifu tu kwamba Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Rarya amethibitisha kwamba huyo kijana amefia katika Kituo cha Polisi na amekufa kwa kuchomwa kisu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaanza na michango. Mheshimiwa Ngeleja, jiandae Profesa Jay, jiandae Balozi Mwamoto.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Nami naungana na wachangiaji wengine kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wasaidizi wake akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wa Wizara hii. Wizara hii ina bajeti ndogo sana lakini tunaona kazi kubwa wanayoifanya kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni sehemu ya utangulizi wa mchango wangu, niungane na Watanzania walio wengi sana katika nchi yetu kuitakia kheri na kuipongeza timu ya Simba *Sports Club* ambayo sasa iko kwenye maandalizi ya kukabidhiwa ubingwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ambavyo tunafahamu ukilinganisha, kwa sababu soka ni shughuli ya sayansi na inaweza kulinganishwa kwa kupimwa, kulinganishwa na ligi zinazochezwa duniani kote....

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, muda wetu ni mdogo. Mheshimiwa Boni kaa chini. Msianze mijadala ya kutaka kuvuruga Bunge sasa hivi hapa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Nilitaka kusema kwamba Yanga ndiyo bingwa.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya kweli ambayo ninaizungumza kwamba hapa duniani kwenye ligi ngumu ni timu mbili tu ambazo zimebaki hazijafungwa, iko Barcelona kwenye ligi ya LaLiga na iko Simba *sports Club* Tanzania. Kwa hivyo mambo yanaenda vizuri na Wanasimba tuko vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma dira kwenye ukurasa wa nne wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo kimsingi naiunga mkono, dira ya Wizara hii inasema ni kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri, lilishamirika kiutamaduni na lenye kazi bora za sanaa na lenye umahiri mkubwa katika michezo ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 49 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hasa kile kipengele kinachozungumzia sekta ya maendeleo ya michezo, kinaelezea, pamoja na mambo mengine kwamba kinazungumzia Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 ambayo sasa hivi nafahamu Serikali inaipitia, pale yameelezwa malengo makuu ya sekta ya maendeleo ya michezo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya lengo ambalo limeelezwa katika kipengele hicho kuhusu sera ya michezo ni kuhamasisha umma wa Watanzania kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo, kuwezesha upatikanaji wa viwanja na zana bora kuhusu michezo lakini pia kuandaa na kutayarisha wataalam wa michezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kuchangia kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri kwenye eneo hili. Nianze kwa kulipongeza sana Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Mheshimiwa Job Ndugai, kwa sababu sisi kama watunga sheria na wasimamizi kimsingi wa utekelezaji wa sera za nchi yetu tumeshiriki kwa vitendo.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Bunge Sports Club inawakilisha, kwamba tumekuwa tukishiriki katika masuala ya michezo na hasa kufanya mazoezi viwanjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesho nawaalika Wabunge wote tushiriki kuanzia saa 12 asubuhi kwenye lango kuu kama tuliviotangaziwa asubuhi, Wadhamini wetu *NMB* watashirikiana na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye matembezi ya mwendo wa pole, kwenye shughuli ya kukimbia kwa mwendo wa taratibu lakini pia na matembezi kuanzia hapa mpaka uwanja wa Jamhuri. Hii ni mojawapo ya utekelezaji wa sera ya michezo Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa letu iko michezo mingi kwa sababu hatuvezi kuzungumzia yote kwa pamoja kwa mtu mmoja kwa dakika kumi, nataka njielekeze kwenye michezo unaopendwa sana duniani. Siyo kwamba najielekeza huko kwa sababu michezo mingine haipendwi, hapana! Nazungumzia soka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa. Nimesoma dira ya Serikali inasema kufikia mwaka 2025 tuwe Taifa ambalo limeshapiga hatua kubwa sana kimichezo, lakini leo ukiwauliza Watanzania toka miaka ya 1980 ambapo timu yetu ya Taifa ilifanikiwa kushiriki kwenye mashindano ya kombe la Afrika kwa kipindi chote hiki tumekuwa tukiugua maumivu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itufungulie na ijifunue wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya *winding up* atusaidie kuelezea mikakati ya Serikali ya kututoa hapa tulipo kwenda kulifikisha Taifa lilipokuwa miaka ya 1980, miaka ya 1970 na hata mwanzoni mwa miaka ya 1990. Tuna uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona maelezo ya ujumla ya kisera na kisheria lakini kwakweli ukiangalia soka letu ilipo hapa sasa hivi tuko mahututi. Sasa hivi kwenye *ranking* za *FIFA* tuko 130 na kitu. Ni jambo ambalo linatia aibu lakini

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

naamini kabisa juhudhi anazozifanya Mheshimiwa Waziri zinaweza kututoa hapa na kutusogezza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiona changamoto kwenye Baraza la Michezo ni tatizo, hapa nataka niseme ambacho nimekiona kwa sababu mwaka kesho tumepewa heshima ya kuandaa, tutakuwa wenyehi wa mashindano ya vijana walio chini ya miaka 17 kwenye mpira wa soka, mashindano yanafanyika hapa Tanzania, lakini kuna Kamati ya Maandalizi ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja katika ukurasa wa 49 na 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona hapa tunafanya yale yale kwa miaka yote. Nataka nishauri, hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema imizingatia maelekezo na maudhui ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyotoa hapa wiki mbili au tatu zillzapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Kamati ilivyooundwa hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisisitiza kwamba katika kufanya mambo yetu Kitaifa lazima tuishirikishe Sekta Binafsi. Sasa ukiangalia hapa kilichopo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijaona hata kipengele kimoja ambacho kinalezea kwa dhamira ya dhati kabisa kuishirikisha sekta binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo rahisi sana tukafanikiwa bila kuishirikisha sekta binafsi, kwa sababu ukurasa wa 71 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu anaizungumzia sekta binafsi ishiriki katika kuendeleza habari ya shughuli zetu za maendeleo na michezo ni mojawapo. Kwa hivyo, ushauri wangu ni kwamba tushirikishe sekta binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazungumzia habari ya maendeleo ya michezo na sanaa kwa ujumla, yako maeneo ambayo lazima tuyape kipaumbele, 'Bongo Fleva' sasa hivi imetutoa. Tunazungumzia Msanii kama Diamond, tunaungana na Watanzania wote kumpongeza kwa hatua aliyofikia kutambuliwa kwamba awe mojawapo ya watu

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

wanaotunga wimbo maalum kwa ajili ya Kombe la Dunia mwaka huu, hii ni heshima kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusudii kusema kwamba hatuthamini sanaa zingine, lakini muziki wa Bongo Fleva, nafahamu akiwemo 'Profesa Jay' ambaao wameshiriki sana kuufikisha muziki hapo ulipo, Diamond, Ali Kiba na wengine wote lazima tuwape kipaumbele katika shughuli hii ya kuendeleza sanaa hii kwa sababu ni heshima kwa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini na naishauri Serikali kwamba huko tunakoelekeaa sasa hivi ambapo Diamond atakwenda kutuwakilisha, Wizara ya Maliasili na Utalii itam-package kwenda kuitangaza nchi yetu, Diamond kwa sababu ye ye ni nembo ya Taifa. Kwa hiyo ni muhimu sana kuwapa ushirikiano watu kama hawa kwa sababu kuna faida kubwa kuwa nao katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera inazungumzia kujenga viwanja na kuimarisha miundombinu ya michezo. Tumezungumzia Chuo cha Malya hapa. Kwa bajeti ya Serikali kama ilivyo hatuwezi kufanikiwa lakini tutakuwaje na Wataalam waliobobeaa kama hatuna vyuo ambavyo vinaendeleza na kutengeneza weledi maalum kuendeleza michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu tena kwa mara nyingine, kama tulivyozungumza kwenye Kamati kwamba Mheshimiwa Waziri aendelee kushirikisha sekta binafsi aone, wapo watu wanapenda tu. JK *Youth Park* pale Dar es Salaam Kidongo Chekundu umejengwa uwanja mzuri kwa ufadhili na udhamini wa kampuni binafsi. Tuendelee kushirikiana tuone namna gani sekta binafsi inaweza kutusaidia katika kuboresha viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kwamba kwenye ile ruzuku ambayo tunaipata kila mwaka kutoka FIA pengine tuitumie pia kujenga, kuimarisha viwanja huko Wilayani kwa sababu nafahamu kwa ngazi ya mkoa angalau

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

tuna viwanja, lakini wachezaji wengi siyo lazima watoke Makao Makuu ya Mikoa tu. Ombi langu ni kwamba hili fungu ambalo tunapata kutoka *FIFA* kila mwaka tulitumie pia kuendeleza viwanja vya vijijini na Wilayani ambako tunaamini kwamba pia kuna uwezekano wa kuwapata wachezaji wengi wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ngeleja. Profesa Jay, jiandae Balozi Mwamoto.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niungane na wenzangu kumpa pole sana Mbunge mwenzetu John Heche kwa kufiwa na mdogo wake kwa kuchomwa kisu na Polisi kule Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kuchangia Wizara hii muhimu ambayo inahusisha Habari, Michezo, Utamaduni na Sanaa. Jambo la kwanza ambalo ningependa kuchangia leo ni kuhusu suala la Bunge *Live*. Bunge ni chombo muhimu sana cha uwakilishi, chombo kikuu cha uwakilishi wa wananchi hapa Tanzania na tunaamini Bunge ni kama mkutano wa wananchi wote kwa sababu kuna wawakilishi kutoka pande zote za Tanzania humu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo nadhani ilikuwa ni muhimu sana Serikali yetu iliangularie upya hili suala la kuondoa Bunge *Live* ili wananchi waweze kutuona wawakilishi wao tunavyowawakilisha ndani ya Bunge ili iweze kuwafikia moja kwa moja na kujua vitu gani vinavyoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi inaongozwa na Mihimili mikuu mitatu, kuna Serikali Kuu, Mahakama na Bunge. Tumeona jinsi ambavyo viongozi wa Serikali wakifanya ziara mara kwa mara na wanaoneshwa *live* maeneo mengine. Hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo ni muhimu sana kwa

wananchi kuweza kuona viongozi wao wanafanya na kutekeleza vitu gani ambavyo wametutuma.

## T A A R I F A

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kumfahamisha mchangiaji anayechangia hivi sasa kwamba Bunge *Live* inaoneshwa saa tatu mpaka saa 4.30 (*Makofii*)

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kuijibu hiyo taarifa kwa sababu mimi naongelea Bunge *Live* yaani hapa ninavyoongea watu wawe wanashuhudia *live* kule, Dada yangu vipi? Hiyo saa tatu watu wanakuwa wamechoka, watu wanaangalia Bunge hadi usiku mkubwa na siyo *live*, hiyo ni *recorded*. Kwa hiyo, hilo liliikuwa jambo langu la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wiki iliyopita niliongea jambo la msingi sana kuhusu Chama cha Mapinduzi kupora viwanja vingi vya michezo ambavyo vimekuwa vikimiliikiwa na Serikali lakini sasa vinamiliikiwa na Chama cha Mapinduzi na wameshindwa kuviedeleza. Hapa ninavyoongea na wewe ni kwamba hapo kwenye Kata ya Ruaha kwenye Jimbo la Mikumi kuna utata mkubwa na tararuki kubwa sana kati ya wananchi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambao kwa kutumia mabavu wameupora uwanja wa shule ya msingi Ruaha 'A' ambao pia unatumia na Ruaha 'B' pia unatumika na shule ya sekondari ya Kidodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya elimu inasema kwamba kila shule lazima iwe na uwanja wa michezo. Pale Ruaha wanafunzi wa shule ya msingi Ruaha 'A' na Ruaha 'B' pamoja na shule ya sekondari ya Kidodi wanatumia uwanja huo, Chama cha Mapinduzi kimeupora na kinaanza kusema sasa hivi ni wa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huo ulijengwa mwaka 1986 ambapo wananchi walijitokeza na kufanya

### **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

harambee kwa ajili ya huo uwanja na wakajenga vibanda pemberi ambapo mkataba walioingia na mkataba wanao mpaka leo inasema kwamba Serikali itamiliiki ule uwanja lakini yale maduka ya pemberi yatakuwa ni haki ya wamiliki au wananchi ambao walikuwepo na mkataba wamesaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha ajabu juzi Chama cha Mapinduzi wamekuja pale Ruaha wakiorodhesha majina na kuwaambia wale wananchi waondoke. Kwa kweli kuna hali mbaya sana na niwambie kitu kimoja, iwapo Chama cha Mapinduzi kitafanikiwa kuchukua ule uwanja maana yake tunakwenda kufunga shule ya msingi Ruaha 'A', Ruaha 'B' pamoja na shule ya sekondari ya Kidodi kwa sababu hawana uwanja wa michezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka niongee kuhusu suala la BASATA, inasikitisha sana hii Wizara kwamba hadi sasa imetimiza asilimia 59 tu ya bajeti yake na asilimia 41 mpaka leo tunavyoongea haijakamilika. BASATA ni chombo cha msingi na tunaichukulia BASATA kama wazazi lakini BASATA imegeuka na kuwa kama chombo cha hukumu kwa Wasanii wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, BASATA ni kama mlevi na mtoto akijisaidia kwenye mkono wako huukati, unauosha na unaendelea na shughuli zingine. Niliamini kwamba BASATA inatakiwa iwape elimu hawa wasanii wa Tanzania waweze kujifunza, waweze kupata ushauri lakini pia waweze kuangalia jinsi gani ambavyo wanawenza kuisaidia tasnia ya muziki hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie wenzetu wamefanyaje, Uingereza kwa mwaka 2015 muziki peke yake umechangia *GDP* paundi bilioni 4.1 katika Pato la Taifa la Uingereza. Marekani mwaka 2015 muziki peke yake umechangia *GDP* ya dola milioni 15. Kwa hiyo, naamini kabisa kama Wizara inataka kuwekeza kwa vijana maana huwezi ukamkamua ng'ombe ambaye hujamlisha majani.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwaambia Serikali waweke bajeti kwa wasanii, wana matatizo makubwa tofauti na hayo wanayoyafanya maana wanadhani kwamba kuwasaidia wasanii wa Tanzania ni kuwaalika sehemu za maofisi zenu kupiga nao picha, kupiga *selfie* na vitu vingine. Wasanii wa Tanzania wana matatizo makubwa, hawahitaji kula ubwawa na wao. Wanahitaji wawasaidie masuala ya kazi zao zinazoibowi, wanahitaji wasaidiwe masuala ya masoko na mitaji. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie ndugu zangu, BASATA mpaka sasa katika hali ya kustaajabisha ndiyo imepewa mamlaka ya kusimamia hii kitu lakini bajeti yake ni milioni 23 kwa mwaka mmoja, mwaka 2016...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, dakika tano zako zimekwisha. Mheshimiwa Balozi Mwamoto, Mheshimiwa Tauhida na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami nianze kwa kuwapongeza vijana wana Paluhengo Lipuli *Sports Club* kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Bila kuwasahau Dar *Young Africans*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda zaidi kwenye ushauri na mchango wangu utakuwa kwenye ushauri zaidi. Kwanza kabisa nianze kuishauri Serikali kwamba chombo kikuu ambacho kinasimamia michezo ni Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Kwa mujibu wa sheria na taratibu, Sheria Na. 12 ya Mwaka 1967 ndiyo ilianzishia chombo hiki cha michezo maana yake Baraza na ikafanyiwa marekebisho mwaka 1971.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki ndicho ambacho kinapaswa kusimamia, kuendeleza, kustawisha, kuratibu aina zote za michezo kwa kushirkiana na wadau. Ukiangalia chombo hiki kinategemea fedha kutoka Serikalini, sasa ukiuliza wanazo shilingi ngapi utashangaa.

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiria, either tuletewe hapa tubadilishe sheria au ikiwezekana Baraza la Michezo livunjwe kwa maana ya kuanzisha kitu kingine ambacho kinaweza kikajitegema, tukaanzisha labda Shirika la Michezo la Taifa badala ya Baraza kwa sababu ukileta likawa Shirika la Michezo la Taifa na kuna neno wadau pale wanaweza wakafanya biashara. Fedha zile ambazo tunasema ziende kwenye michezo ambazo ni za *gaming* za mambo ya michezo ya kubahatisha zingeweza kwenda kule wakawa na uwezo wa kujidesha wenyewe kwa vyanzo mbalimbali ili sasa tukienda kwenye kutayarisha timu zetu tuwe na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ambayo Mheshimiwa Mwakyembe amepata, kwanza nimpongeze sana kwanza kwa kazi nzuri ni fedha ambayo tungeweza tu kuiweka timu ya Taifa kwenye matayarisho ya michezo siyo ya Wizara. Kwa hiyo, akisema kwamba ataweza kufanya vizuri ni kujidanganya na ndio maana niliwahi kuuliza hapa siku moja kwa nini tusiifute michezo Tanzania? Hata hivyo, swali hili lilikuwa gumu kujibiwa. Maana yangu ni kwamba unataka kukamua maziwa wakati hujamlisha ng'ombe majani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba tukae chini, tufikirie kitu gani tukifanye ili Baraza liwe na meno, uwezo kama tunataka kuendelea na Baraza, lakini kama haiwezekani tulivunje kwa sababu leo kazi kubwa ya Baraza la Michezo ni kusajili vyama vipya na kuvifunga na kuvifungia vile ambavyo vimefanya makosa, kazi ambayo siyo nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa michezo ya *AFCON* wa vijana chini ya miaka 17 itafanyika hapa, maandalizi sina hakika kama yameanza na hayawesi kuanza kwa sababu hamna fedha, kama yapo ni yale ya mechi hizi ambazo zinaendelea. Wasiwasi wangu ni kwamba inawezekana tukatumia fedha nydingi sana na gharama kwenye vikao kuliko maandalizi ya timu, matokeo yake tutakuja kutoa visingizio vingi, ningeomba Serikali iangalie uwezekano wa hilo.

### **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, medali nyingi Tanzania tulianza kuzipata kwenye michezo mbalimbali, mwaka 2003 tulipata medali 12 za wanariadha kwenye *Special Olympic* Ireland. Bahati nzuri fedha zilikuwa hamna tukatayarisha mechi kati ya Mabalozi na Wabunge, fedha iliyopatikana tuliwasafirisha wale watoto kwenda Ireland na walileta medali 13. Baada ya hapo hakuna medali ambayo imeletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanapokwenda kwenye riadha bahati nzuri Filbert Bayi yupo nimemwona, wanapokwenda kuwakilisha nchi, hawaendi watatu au wanne. Sisi tumepeleka wanariadha timu nzima nafikiri hawazidi 50, wanariadha waliotoka Kenya walikwenda 200 hawawezi kukosa medali, lakini sisi utapeleka wote hao kwa maandalizi gani? Kwa hiyo, naomba kama kweli tunataka michezo ya nchi iendelee basi tujipange. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri ajaribu kwa sababu Mabaraza hayapo yamekufa kama yapo hayana uwezo, akae na wadau tena aanzie hapa Bungeni, akae na wadau wa michezo tuko wengi tu halafu tuone tunatokea wapi ili tusimwache peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Cosato Chumi amelizungumza na mimi niliwahi kuzungumza hapa, kwamba sisi tunataka timu ya Taifa ifanye vizuri. Timu zetu zimesajili wachezaji wengi wa kigeni kutoka nje ambao hawana uwezo. Kwa hiyo kinachofanyika wachezaji wetu wanakosa nafasi. Unasajili wachezaji ambao hata kwenye nchi zao hawana nafasi, unakuja inakuwa dampo. Kwa hiyo, ningeomba Ndugu yangu Karia yupo, hebu waangalie uwezekano wa kupunguza idadi ya wachezaji, ikishindikana basi angalau wale watakaokuja kucheza wawe ni watu ambao wana uwezo kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Timu ya Taifa inapocheza, jezi zile inazotumia hazina hadhi ya nchi yetu kwa sababu hazina bendera, rangi zetu zinafahamika za bendera yetu lakini leo tunavaa jezi nyeupe wapi na wapi, tumekosa rangi.

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kwa hiyo, niombe Karia yupo hapo, Kiganja nimemwona, ndugu yangu Tandau nimemwona, hebu wakae wafikirie, tusitie aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia najua sana kwamba Wizara kwa kushirikiana na *TFF* watapita kuangalia viwanja vyenye hadhi vitakavyotumika Kimataifa ili viweze kutambulika na *FIFA*. Uwanja wa Samora Iringa hebu wapite pale waone umetengenezwa kisasa, uko vizuri na watu wako radhi wana uwezo wa kwenda kuangalia mpira na wameona timu ya Lipuli mambo ambayo inafanya, unaweza ukawauliza watu wa Singida wanaweza kueleza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ningependa kumpongeza sana Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* ndugu yangu William Ngeleja. Baada ya Wabunge kushiriki michezo tumepata faida kubwa sana; moja, ukiangalia idadi ya watu wanaokwenda hospitali kutibiwa imepungua. Idadi ya watu wanaokwenda kwenye sehemu za starehe kunywa pombe imepungua, ndiyo maana umeona hata walioitwa kwa Mheshimiwa Paul Makonda walikuwa wachache kwa sababu wamekuwa na shughuli sasa nyingine mbadala ya kufanya ambayo ni mazoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Spika amwangalie Mheshimiwa William Ngeleja amwongeze fungu kwenye fedha zile ili wanamichezo wengine washiriki, lakini sitaacha pia kumshukuru Mwenyekiti pamoja na Majimarefu ambaye kwa kweli wanasaidia kwenye yale mambo mengine na kufanya timu yetu iweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji aliyemaliza amechangia vizuri sana, niombe badala ya kulalamikia viwanja vile ambavyo vina wenyewe, tuangalie uwezekano wa kuomba vingine kuna nafasi, ombeni CHADEMA muweze kupata viwanja vingine ambavyo...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto umemaliza? Wewe huwezi kukaa mpaka nikwambie ukae wewe endelea

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe wenzetu wale ambao wana nia ya viwanja vya michezo waje waombe, Iringa tuna maeneo, Kilolo tuna maeneo, waje waombe ili nao wamiliki badala ya kugombea hivi ambavyo viro, kwa sababu hivi tumerithi zamani Chama kilikuwa kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
*(Makof)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto sasa ungependekeza rangi gani za timu ya Taifa ili wakusikie hapa, basi kaa lakini, najua lengo lako kulikuwa kuna rangi ulitaka kuitaja tu hapa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Tauhida, Mheshimiwa Amina Mollel atafuatia.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa jioni hii kuweza kuchangia Wizara hii ya Habari na Michezo. Kwanza kabisa nichukue fursa hii ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake lakini kwa umuhimu mkubwa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayofanya. *(Makof)*

Mheshimiwa Waziri, naamini kwamba anafahamu na anaelewa kwamba yeche ni baba na baba siku zote kazi yake ni kulea, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nichukue fursa hii kumshukuru kwa sababu anajua kwamba ni wajibu wake kulea. Wizara alionayo takribani vijana wengi wa Tanzania wapo hapo. Vijana wa Tanzania shughuli kubwa wanazozifanya kwa sasa wamekimbia kwenye suala la sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajielekeza zaidi kwenye vijana nizungumzie chombo chetu cha *TBC*. Chombo cha *TBC* kiumri mimi siwezi kuipata lakini inafikia wakati

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

inatubidi tuzungumze na nategemea kwamba kuna baadhi ya Viongozi wa *TBC* watakuwepo mahali hapa. Kwa kweli mfumo wao wa kazi wengine hauturidhishi na maeneo hususan yasiyoturidhisha *TBC*ni pale ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wanapokuwa na mambo mahsusii kwenye taarifa za habari niliwahi kuzungumza miaka mitano nyuma iliyopita, lakini sidhani hili kama nina hoja ya msingi kuishawishi Serikali yangu iwaongezee bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi suala la kukaa la kupanga vipindi vipi wafanye, hili linahitaji bajeti gani kwa sababu mimi ninavyofikiria, nadhani kwamba ni suala la karatasi na peni na kukaa na Watendaji Wataalam wakajipanga. Sidhani hili kwamba linanishawishi kuishawishi Serikali kwamba waongeze fedha ili kuweza kullfanikisha hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu ni jambo la aibu, tena ni aibu kweli kukuta chombo kama cha *TBC* tunachokitegemea wanafanana na vyombo vingine vya habari ambavyo vinamilikiwa na watu binafsi au wao kupitwa na vyombo vya watu binafsi. Hivi leo *TBC* Rais amekwenda kufungua miradi tofauti na mikubwa, kweli kwenye taarifa ya habari unachukua dakika tatu, anasimama Mheshimiwa Tauhidha leo kaenda Jimboni kwake dakika tatu, akisimama sijui nani dakika tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais ni Rais wa nchi hii tuwape fursa viongozi wetu hususan Rais wetu, apewe fursa na hakuna chombo kinachoweza kumpa fursa zaidi ya *TBC*. *TBC* wametutia aibu, chombo chao tulitegemea ndiyo kiwe mkombozi wa Watanzania kwenye kutoa habari, hivi leo *TBC* nikwambieni ukweli...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nishasema hakuna taarifa tena, kaeni chini wote, muda tulionao ni mdogo sana.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli leo Wabunge tukasimame hapa tukaisifie *ITV*, Azam tena na Wasafi TV sasa wanaikimbiza *TBC*, kitu ambacho kwangu ni aibu najisikia vibaya kusimama hapa kuizungumza *TBC*. Hamu yangu na shauku na niliwahi kuzungumza kwenye Bunge, siyo vibaya *ku-copy* kwa ndugu yako. Leo Zanzibar wanaweka vipindi wanaweka mpangilio wa *TV* kujua sasa taarifa ya Rais inatoka kwenye chombo cha habari. Leo unakuta watu wanakimbia wanaenda kuwahi kufungua taarifa ya habari anafungua *TBC*, baada ya dakika tatu anaona sherehe ya harusi ya mfanyakazi wa *TBC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Azam, mmoja wao niliangalia katika shughuli ya Ali Kiba niliangalia, walifanya vizuri walijua muda wa kutenga kuweka shughuli ile. Leo *TBC* tunategemea waweke vipindi vyao vizuri wapange mpangilio kwa itifaki kwamba inakuja ripoti ya Rais, inakuja ya Makamu wa Rais, inakuja Waziri Mkuu tunakwenda kwa itifaki hii, nchi inaongozwa na itifaki. Huwezi kumpangia Rais anazungumza kwenye taarifa habari dakika tatu au dakika nne siyo kitu kizuri, *TBC* kwa hili naomba wabadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri alichukue, nililizungumza miaka mitano nyuma imepita, naomba alichukue alifanyie kazi. Hivi hili niliombee bajeti gani, lionezwe bajeti gani, hivi Rais anaongelea masuala ya ndege, anaongelea masuala ya Tanzania kwenye miradi ya reli, anaongelea wananchi jinsi gani wanaweza kunufaika na mazao yao, anapewa dakika tatu kwenye taarifa ya habari na hizo *TV* nyingine zinafanyaje? Naomba Mheshimiwa Waziri walifanyie marekebisho hili. Bajeti ijayo nafikiri nitakuwa namba moja kukamata shilingi ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri tuje kwenye suala la sanaa, kwa wasanii limekuwa sawa na ng'ombe wa nyuma kutandikwa bakora, wakati ngombe wa mbele hatembe. Kwa kweli, Mheshimiwa Waziri inatubidi tuseme, atusamehe watoto

wake, wasanii wanaonewa, tufike wakati tuseme wanaonewa. Hii BASATA inafanya kazi gani? BASATA kabla ya nyimbo ya msanii kutoka wao ndiyo wanaotakiwa kujua anaimba nini, kwa sababu kwenye Kiswahili kuna kitu kinaitwa tungo tata. Sasa inawezekana wasanii kuna maeneo wanatumia tungo tata, kama wanatumia tungo tata Baraza lipo, wanafanya kazi gani? Mheshimiwa Waziri hebu atupe mfano hii BASATA hebu awatoe, wanachokifanya wanawaonea wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wapewe posho, mishahara, kazi wanayotakiwa kuifanya hawaifanyi matokeo yake msanii ameshajituma, ndani ya mwaka mmoja ndio anakuja kufungiwa nyimbo yake. Hatumaanishi kwamba kila kinachofanyika ni kizuri hapana, nyimbo inawezekana ikawa mbaya na inawezekana maneno yaliyotumika yakawa mabaya na wanavyofanya baadhi ya wasanii na sisi haturidhiki navyo, lakini kuna chombo kinatakiwa na wao wawajibishwe ili twende sawa. Asipigwe bakora ngombe wa nyuma wakati wa mbele hatembei. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie vilevile kitu ambacho dada yangu Devotha hapa alizungumzia, Waziri aje na sheria, aje na kanuni kila kinachohusu sheria kama kuna sheria zimekaa upande huko atuletee maana Mheshimiwa Devotha anavyozungumza kazungumza kwa kujua anakizungumza nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hili kwa sababu sheria lazima zije Bungeni tuziweke sawa. Haiwezekani Mmiliki wa Vyombo vyaa Habari akaamua kufanya anachokitaka yeye mwenyewe kisa tu kwamba wana uhuru, uhuru usiokuwa na mipaka una tatizo. Uhuru wowote anaopewa binadamu ukiwa hauna mipaka unakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo utamkuta mmiliki wa chombo binafsi kakorofishana tu. Nimtolee mfano Ali Kiba samahani kama italeta shida. Leo anaenda kuimba kakosana na mmiliki wa vyombo anafunga hata nyimbo zake

kutokuimba, sidhani kama ina tija, sidhani kama ina faida. Sasa hizi sheria anazozzungumza dada yangu zije Bungeni hii ni nchi inaongozwa na watu makini. Sheria Waziri alete Bungeni tuzifanyie kazi lazima watu wote tufuate sheria twende na utaratibu, siyo kila mtu aamue anavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii ya kuwapongeza wasanii wengi wanaofanya vizuri kuliwakilisha Taifa letu. Kwa siku ya leo nimpongeze dada yangu Monalisa amefanya vizuri, amevaa bendera ya Tanzania na picha zake zote ukiziona nyigi takribani ana bendera ya Tanzania. Siyo yeye tu na wengi wapo wanaofanya kwa ajili ya kutetea Tanzania. Hili linaonesha sura fika kwamba sanaa ni faida kwetu, sanaa ina uwezo wa kuongeza kipato kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee kidogo Waziri atakapokuja kufanya majumuisho siyo mtaalam sana kwenye mambo ya michezo, lakini kipindi cha nyuma tulikuwa Zanzibarsana tunalamikia masuala ya michezo ila kwa sasa shwari imepatikana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amina Mollel

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa, pili naomba nifafanue na kuweka taarifa sahihi kwenye *Hansard*. Nilimaanisha saa tatu asubuhi mpaka saa nne na nusu kipindi cha maswali na majibu ndiyo lilikuwa lengo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kama sijaenda mbali zaidi naomba nizungumzie kidogo alichozungumzia mwenzangu aliyemaliza kuongea. Katika habari lengo kuu la tasnia ya habari ni kuelimisha, kuhabarisha na kuburudisha. Kwa hiyo katika TV kuna vipindi vya kuelimisha, kuna vipindi vya kuburudisha na kuna vipindi ambavyo vinajumuisha

kwenye michezo, burudani lakini nya kuhabarisha ni kama habari. Kwa hiyo, allipozungumzia kuhusu taarifa ya habari dakika tatu, taarifa ya habari unakuta ni nusu saa na inajumlisha matukio yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya habari, habari nyingine kwa mfano habari kubwa kama ya Rais itakwenda dakika tatu mpaka dakika tano, lakini habari nyingine zitakwenda dadika moja moja au dakika mbili na kama kuna tukio maalum la Rais wanachofanya ni kusema kwamba kutakuwa na kipindi maalum na katika kipindi hicho maalum wanarudia hiyo taarifa katika kuelezea. Kwa hiyo, nataka tu kuweka ufanuzi huo kwa sababu *TBC* hawana nafasi ya kuja kujadili hapa na kwa sababu na mimi pia ni mwanataaluma na nimetoka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda pia nimshukuru Mwenyekiti wa Bunge wa Michezo, Mheshimiwa Ngeleja na Kamati yake kwa ujumla kwa kunitfea kuwa Msemaji wa Timu ya Bunge, kwa hili nashukuru sana na mimi nasema kwamba kipele kimepata mkunaji na mimi nitakikuna sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nianze na maswali kwa Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*windup* aje kutufahamisha. Mheshimiwa Waziri timu yetu imekwenda kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola kule Australia. Taarifa nilizonazo mpaka hivi sasa ni kwamba mionganoni mwa wachezaji waliokwenda huko mmoja ametoroka kambini na amezamia huko nchini Australia. Jina lake nimelipata anaitwa Fathiya kutoka Ukonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*windup* atufahamishe kwamba hizi taarifa je, zina ukweli wowote kwamba huyu mchezaji ametoroka kambini na kuzamia huko nchini Australia? Pia nataka kujua kwamba kama ni kweli ametoroka ni vipi mahusiano yetu kati ya Tanzania na Australia, hili haliwezi kututia doa kwa sababu sisi tunafahamu Tanzania ni mionganoni mwa nchi

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ambazo zimekuwa zikipokea sana wakimbizi, lakini siyo Watanzania kutorokea kama huyu mwenzetu alivyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo kwa sababu dakika ni chache, moja kwa moja niende kwa maslahi ya Waandishi wa Habari. Tunafahamu kwamba tuna mhimili mitatu, Mhimili wa Bunge, Mahakama na Serikali lakini tasnia ya Habari pia ni mhimili ambao tunauhesabu kama mhimili wa nne, lakini waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana. Wengi wao hawalipwi ipasavyo na hata katika ile mikataba yao, ukienda kwa mfano anapofanya miaka miwili hakuna chochote kinachoingizwa katika mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mifuko kabla haijavunjwa sasa hivi na kuwa mifuko miwili; tunafahamu kulikuwa kuna *PPF* na mifuko mingineyo, illkuwa haipelekwi huko. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba atakapokuja atufahamishe hapa ni vyombo gani ambavyo vimeduwa haviwalipi Waandishi wa Habari ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waandishi wa Habari wanafanya kazi kubwa sana. Popote pale ulipo Waandishi wapo na ndiyo wanaowahabarisha wananchi, matokeo yake hawapati hiyo mishahara kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atufahamishe amechukua hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nivipongeze vyombo ambavyo vimeduwa mstari wa mbele katika kuwalipa na hasa mimi nitolee mfano Azam, nawapongeza sana *TBC*, lakini pia, hata *ITV*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje atueleze, mwaka jana nakumbuka mwenzangu ambaye sasa hivi ni Naibu Waziri alishika shilingi kwa ajili ya kutaka wakalimani katika taarifa za habari. Naomba kufahamu mchakato huo umefikia wapi?

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanamuziki wetu tunafahamu kwamba, muziki wa dansi tulikotoka mpaka hivi sasa, lakini kwa mfano kwa hivi sasa kumbi nyingi za burudani zinatakiwa zifungwe saa sita kamili usiku, kama unavyofahamu saa sita kwetu watu wazima ndiyo kumenoga kwelikweli, lakini hawa pia ndiyo ajira yao wanaambiwa kwamba muda huo wafunge. Mpaka wamefikia kuwaweka wasanii ndani kwa mfano mwanamuziki mkongwe *King Kikii* aliwekwa ndani. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aje kutufahamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu lingine ni kwamba, Maafisa Utamaduni, tunafahamu wapo chini ya TAMISEMI. Nataka kujua hivi sasa je, ule ufanyaji kazi wao ukoje na Wizara husika kwa sababu, mambo ya sanaa, utamaduni na michezo yako katika Wizara yake, aje kutuambia kwamba, wamefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maadili, naomba Waziri aje kutufahamisha, Mheshimiwa Waziri nimemwonesha katika *Night Clubs* zetu kumekuwa na mchezo ambao wanahamasishwa labda kama ni mwanamke au mwanaume kucheza na wakati mwininge mpaka kufikia kuvua nguo na kufanya tendo la ndoa na Mheshimiwa Waziri nimemwonesha kilichotokea hivi karibuni. Nataka atakapokuja hapa aje atueleze wamechukuliwa hatua gani na ni mikakati gani ipo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, utamaduni wetu na maadili yetu tunayalinda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TBC*, naweza kusema ni mielongoni mwa mashirika ambayo yana wataalam wallobobe, wakongwe tangu miaka hiyo. *TBC* tunafahamu popote pale katika shughuli zote za Kitaifa, *TBC* ndiyo ambao wamekuwa wakitegemewa sana, lakini wakati mwininge tunawalaumu *TBC* wakati makosa siyo ya kwao. Makosa siyo ya kwao kwa sababu hatujaliangalia ni kwa jinsi gani tunawekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni shirika la umma, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ni kwa jinsi gani analiwezesha Shirika la Utangazaji (*TBC*) ili basi liwe kweli ni Shirika la Umma, liwe kweli shirika ambalo linaweza kufanya majukumu yake na hizi lawama zinazotokea zote ni kwa sababu, tumelisahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika taarifa kwamba, wamesema wanakuja kujenga studio ya kisasa hapa MJINI Dodoma, lakini je, kwa wakati huu ambapo bado wapo Dar es Salaam tunawawezesha vipi? Naomba kwa sababu ndiyo shirika tunalolitegemea sana katika utendaji wa kazi wamebobe. *TBC* ndiyo ambaao wamefunga mitambo ya vyombo vingine vyote, kwa maana kwamba, wamewatoa wataalam *TBC* na wamekwenda kufunga huko. Kama wanaweza kufunga huko kote kwa nini washindwe wao kufanya vizuri? Ni kwamba, hatujaamua kuwekeza ipasavyo katika Shirika la Utangazaji (*TBC*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, leo hii mimi najivunia uwepo wangu hapa ni kwa sababu nimelelewa katika taaluma, nimetoka huko ndiyo maana najivunia uwepo wangu hapa bila kusahau nilipotoka, siku zote tulipotoka ndipo ambapo pameweza kutufikisha hapa. Naipongeza sana *TBC* na naomba tuwawezeshe ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie *Online TV*. Nafurahi kwa sababu, vijana wengi wamepata ajira hivi sasa, lakini katika kila kitu kisipowekewa msingi mzuri ni dhahiri kabisa kwamba hata maadili wakati mwengine yanaweza kukiukwa, ndiyo maana hata ukiangalia nyingine zinafanya vizuri sana, lakini sasa utaratibu ambaao amekuja nao Mheshimiwa Waziri, nafurahi kwamba, tutaweka sasa zile *guidelines* na kuwafahamisha vizuri ili wasiweze kwenda kinyume na maadili ya Mtanzania, kwa sababu ile ni njia mojawapo pia ya habari, tuone kwamba ni kwa jinsi gani wanafuata misingi, sheria na taratibu zilizopo katika kuhakikisha kwamba, wanaendelea kuuhabarisha umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu sanaa na

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

utamaduni. Sipingani na maamuzi ya Serikali katika kuwafungia Wasanii. Hapa kuna sehemu tulikosea kwa sababu haiwezekani mwanamuziki anatoa *single* yake, ametoa wimbo wake unapigwa halafu wanakuja kumfungia! Hili haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujikumbushe siku za nyuma wanamuziki wengi, wakati huo Redio Tanzania Dar-es-Salaam, walikuwa wakitoa nyimbo zinakuwa *edited*, baada ya hapo ndiyo zinapigwa. Je, hawa wataalam sasa hivi wako wapi? Tuweke misingi mizuri tuwasaidie wasanii wetu ili wakikiuka baada ya kupewa hiyo misingi mizuri na kulelewa vizuri, hapo ndipo tunaweza tukawahukumu. Kwa hiyo, nawapongeza akina *Diamond*, nampongeza Monalisa na wengine wote ambao wameweza kupeperusha vizuri bendera ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa pia ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu Mkataba wa *Star Media* pamoja na *TBC*. Nafurahi kwamba, mkataba ule umekuwa *renewed* hivi sasa na kwamba matakwa yamezingatiwa, lakini sikubaliani na walichosema kwamba kwa miaka yote saba *Star Media* wamepata hasara! Hii naona kwangu ni aibu kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbuka mwaka 2013, *TBC* na *Star Media* ndiyo walikuwa wa kwanza kuanza kuuza ving'amuza, wote ni mashahidi na tunajua...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje dakika tano, Mheshimiwa Nkamia dakika tano.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie Wizara hii.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni Vyombo vya Habari. Vyombo vya Habari ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi hii na uchumi wa nchi hii. Serikali ilikuwa hasa vyombo vya Habari vya Umma tulishalamika hapa Bungeni kwamba habari nyingi zinazoandikwa ni za mjini tu, lakini vijijini ndiyo kuna taarifa nyingi, tulishaari Serikali kwamba, kila Wilaya iwe na Mwandishi wa Habari. Kwa hiyo, huo ni ushauri wangu Mheshimiwa Waziri, kule habari nyingi hazifiki kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, maslahi ya vyombo vya habari. Vyombo vya habari vya umma kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge mmoja vyombo hivji vinafanya kazi nzuri sana na vinailetea sifa nchi yetu, wanaandika taarifa kila siku tunasoma magazeti, habari tusingezipata bila yale magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari kwa mfano *TBC*, *TBC* ni chombo cha umma, lakini *TBC* inafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kwanza vyombo vyaao vimechakaa, baadhi ya vyombo kwa hiyo, kuna baadhi ya maeneo katika nchi hii *TBC* haisikiki. Kwa hiyo, Serikali ijitalidi kuongeza bajeti ili tuboreshe *TBC* iweze kusikika nchi nzima hasa *TBC One* pamoja na *TBC Taifa*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi. *TBC* wanafanya kazi usiku na mchana. Hapa tunaona wanavyohangaika usiku na mchana wanafanya kazi, lakini maslahi yao ni kidogo sana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aboreshe maslahi ya watumishi wa *TBC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, viwanja vya michezo. *Pitch* ikiwa nzuri na timu itacheza vizuri mpira...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nkamia dakika tano.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru. Sana nitatoa ushauri tu kwa sababu na mimi nimeshawahi kukaa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hakuna nchi yoyote duniani inaweza kuendelea kimichezo bila kuwa na makocha wake wazawa. Ni aibu kubwa kwa Taifa la Tanzania leo kuchukua makocha kutoka Burundi kuja kufundisha timu zetu za *Premier League*. Kocha Msaidizi wa Simba anatoka Burundi, Mbeya City - Burundi, Mbao FC – Burundi. Katika *FIFA ranking* Tanzania iko juu kuliko Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani ni wakati wa Serikali sasa kuwekeza ku-*train* makocha. Hata kwenye michezo ya *Commonwealth* juzi, mabondia wetu walikuwa wanasmamiwa na makocha kutoka Kenya kwa sababu makocha wetu hawana sifa za kukaa kwenye *ring*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni viwanja vya michezo. Ni kweli viwanja vyetu katika mikoa yetu vingi, hivi vya mpira wa miguu vinamiliikiwa na Chama cha Mapinduzi, lakini havipo kwenye hadhi nzuri. Ushauri wangu ni kwamba ili utoe *product* nzuri ya wachezaji lazima uwe na viwanja vizuri. Nliombe Serikali, wala siyo dhambi, kila mkoa Majimaji, Mbeya, hebu ikiwezekana wakae na Jeshi, *JKT* wanaweza ku-*maintain* hivi viwanja na vikawa katika ubora mzuri zaidi, wao wakawa wanachukua kamisheni kama Chama cha Mapinduzi. Viwanja hivi vitakuwa na ubora sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Misri, ukienda *Port Said*, ukienda Ismailia, viwanja vyote ni vizuri kwa sababu vinakuwa *maintained* na Jeshi. Badala ya *JKT* kushughulika na mikopo ya matrekta, huu ni wakati sasa wa ku-*maintain* viwanja hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tatu. Leo tuna wachezaji wengi sana wa kigeni hapa Tanzania na tuna

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mokocha wengi wa kigeni hapa Tanzania. Kama kuna kosa ambalo mchezaji anayecheza kwenye nchi nyingine *as an International Player or Profession* anaweza kupata kosa kubwa sana kama atakwepa kodi. Lionel Messi alipata matatizo, Cristiano Ronaldo alipata matatizo kwa sababu ya kukwepa kodi, Tanzania wachezaji wetu hawa wa kigeni hawalipi kodi na hata *registration fee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchezaji anasajiliwa kwa milioni themanini lakini anachukua hiyo fedha anaondoka nayo kwenda nyumbani kwao, Serikali inakosa mapato. Niwaombe *BMT* hili jambo waliangalie. Kuna wachezaji wamesajiliwa hapa kutoka Zimbabwe, kutoka Uganda, kutoka Kenya, kutoka *Ivory Coast*, kutoka Benin na wengine hawana hata kiwango, lakini fedha anayolipwa kama *registration fee* haitozwi kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, leo hata ukimuuliza Mheshimiwa Waziri pale kwamba, hebu tuambie tu wachezaji wa kigeni kwenye *registration fee* walilipa kodi kiasi gani? Sidhani kama ana majawabu? Huu ndio ushauri wangu ambao nimependa niutoe leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nchi zilizoendelea kimichezo duniani fainali za *FA* zinafanyika Makao Makuu ya nchi ile husika, lazima tuwe na huo utamaduni kuliko mwaka jana tumecheza Dodoma, mwaka huu Arusha, keshokutwa utasikia Chemba, kutoka Chemba utaenda kucheza wapi, Mafia, eeh! Au kwa Mheshimiwa Kakoso kule. Tuwe na msimamo kwamba fainali ya *FA* inachezwa kwenye Makao Makuu ya Nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Waziri Mwakyembe kwa hotuba nzuri na yenye kutia matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchezo wa mpira wa miguu bila shaka ndio mchezo unaopendwa na Watanzania wengi kuliko mchezo mwingine wowote hapa nchini. Ni ukweli usio na shaka shirikisho linalosimamia mchezo huu *TFF*, lina changamoto nydingi zinazohitaji kurekebishwa ili kuleta faraja na furaha kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganii mwa changamoto hizo ni Katiba ya *TFF* ina mapungufu mengi sana, mojawapo likiwa ni hili la uchaguzi wa kumpata Rais wa *TFF*. Ushiriki wa wadau ni mdogo sana na vigumu kuamini Rais wa *TFF* Taifa anapigia kura na Wajumbe 128 tu nchi nzima. Kuminywa huku kwa demokrasia kunasababisha kupata viongozi wabovu. Tatizo hili linaanzia kwenye ngazi ya chini kabisa mpaka Taifa. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya Katiba ya *TFF* kufanyiwa marekebisho makubwa ili kuongeza ushiriki mkubwa wa wadau kwenye chaguzi za ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuanzishwa kwa kituo kikubwa na cha kisasa kwa wanariadha Wilaya ya Mbulu, Mkao wa Manyara ni jambo muhimu katika kukuza vipaji vya wanariadha wetu. Nchi yetu miaka ya 1970 na 1980 ilikuwa haikosi kwenye orodha ya nchi zinazopata medali kwenye michuano ya Kimataifa na kwa kiasi kikubwa wanariadha hao walikuwa wanatoka maeneo ya Mkao wa Manyara, hivyo ni muhimu Waziri ukalifanya kazi wazo hili ili tuwe na chuo ama kituo cha kisasa cha michezo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzorota kwa michezo katika Majeshi yetu ni jambo ambalo Mheshimiwa Waziri alitupie macho vilevile. Zile zama za kina Willy Isangura, Nassoro, Michael, Kingu na kadhalika zimeyeyuka na tumekuwa wasindikizaji kwenye michezo ya Kimataifa. Ipo haja ya kuliangalia jambo hili kwa undani kujua chanzo chake na kupata ufumbuzi ili turudi kwenye zama zile michezo wa ndondi na mingine iliyokuwa inatuletea sifa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.  
Ahsante.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanja vya michezo. Serikali ije na mkakati kabambe wa kupatikana viwanja vya Serikali vya michezo. Mfano katika Mkoa mpya wa Geita, Mkoa mzima hakuna viwanja vya *football, basketball, netball* na hata riadha. Pia nataka kufahamu mkakati wa Wizara kuhusu bima ya wanamichezo wote kwa kuwa hivi sasa mchezaji anapopata tatizo dogo la kiafya maisha yake yanakuwa ya kuombaomba. Kwa nini Wizara isipitie upya sera yake ili kuwafanya wanamichezo wote kuwa na hifadhi maalum ya fedha na bima kwa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina mbalimbali za michezo. Limekuwepo tatizo la Watanzania kuwekeza zaidi katika mpira wa miguu na kidogo ngumi ili kuongeza wigo au chaguo la aina ya michezo. Mfano shule ziache kuweka sharti la uwanja wa mpira wa miguu kama ishara ya kuwepo kwa michezo, ikiwezekana michezo kama kuogelea, ngumi, *basketball, volleyball, table tennis na squash* na mingine mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushirikiane na Wizara ya Elimu kuratibu wamiliki wa shule kutoa *proposal* ya aina ya michezo ambayo shule itau-*promote* kwa nguvu zake zote kwa kuweka miundombinu yake badala ya kuweka mkazo kwenye masharti ambayo yamebaki kuwa mapambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vazi la Taifa, naishauri Serikali badala ya kulifanya vazi la Taifa kuwa moja kwa nchi nzima, vazi hili lianzie kwenye Wilaya, Mikoa na baadaye Taifa. Iwapo Wilaya kutakuwa na vazi lake na baadaye Mkoa mwisho wa siku Taifa litakuwa na vazi lenye kujumuisha Mikoa yote.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kodi zinazokusanywa kuititia sanaa nchini bado Serikali hii ya Awamu ya Tano imeshindwa kuwasaidia wasanii.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kupata stika za *TRA*; ili kumwezesha msanii kuuza kazi yake kwa halali ni kwa nini Serikali inashindwa kuweka ofisi za usajili kila Wilaya na Mkoa ili kuondoa usumbufu kwa wasanii kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa kazi za wasanii na hati miliki. Mpaka sasa Serikali imeshindwa kuwasaidia wasanii, wanafanya kazi katika mazingira magumu mpaka akamilishe kazi yake sokoni, lakini kazi hiyo inaibiwa, inampelekea msanii kutopata faida na kufaidisha wezi wa kazi hizi. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa wasanii pamoja na kulinda kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa viwanja. Changamoto za viwanja vya michezo vingi vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi. Ni kwa nini Serikali inatumia kodi za wananchi hovyo kukarabati viwanja vya CCM ilihali viwanja hivi vingi nchini vina migogoro na kwa nini Serikali isichukue hatua ya kujenga viwanja vya michezo katika mikoa ili kuondoa ubaguzi huu na badala yake ijenge viwanja vya michezo katika mikoa na kuleta ajira, afya na michezo inawaweka watu pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bunge *Live*; Serikali ya CCM imeshindwa kutetea hoja ya kwa nini Bunge halioneshwi na kupelekeea wananchi kutoendelea kuiamini Serikali hii ya CCM kwa sababu inaficha mambo yake kupitia Bunge. Pia uminywaji wa demokrasia nchini kupitia vyombo vya habari kama radio, magazeti na kufungia nyimbo zinazokosoa Serikali, je, hawaoni kwa kufanya hivi ni kuonesha wamefeli.

**MHE. ZAINABU M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu nashauri Serikali iwekeze katika mchezo wa mpira wa miguu pia isisahau

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kuwekeza katika michezo mingine ambayo tayari imeshiriki katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi yetu na imesajiliwa, kufuata taratibu zote za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Roll Ball* – Timu hii ya mchezo wa *Roll Ball* imeshindwa kushiriki kwenda kuwakilisha nchi katika nchi ya Kenya kwa sababu ya kukosa wadhamini. Hivyo Serikali ione haja ya kusaidia mchezo huu ambao utasaidia kuleta ajira pia kusaidia nchi kujitangaza Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu itolewe kwa wasanii wetu hususan wanaoimba muziki wa kizazi kipyra, kuweza kutunga na kuimba nyimbo zenyne maadili yanayoendana na utamaduni wa nchi yetu. Serikali itunge sheria ya kudhibiti vijana ambao wanavaa nguo fupi (nusu uchi) ambazo haziendani na maadili yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali, iweke mkakati maalum wa kuhamasisha michezo mashulenii, kuanzia shule za awali, shule za msingi, sekondari hadi katika vyuo ili kuweza kuibua vipaji kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Taifa upo katika Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam, hivyo pindi mechi zinapochezwa katika uwanja huo wananchi wa Wilaya ya Temeke hawafaidiki na fedha zinazopatikana katika viingilio. Hivyo naishauri Serikali kwa kushirikiana na *TFF* iweze kutoa kiasi cha fedha kwa Wilaya ya Temeke ambayo itasaidia katika kuboresha miundombinu na shughuli nyingine za kijamii katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mungu awape afya njema Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake ili kuweza kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpira wa miguu na

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

udhamini wa Serikali, Mpira wa miguu katika nchi yetu ya Tanzania ni mchezo unaopendwa lakini kwa bahati mbaya tumeshindwa kuwekeza katika michezo ipasavyo. Mfano katika *Academy*tupo nyuma sana, vilabu havina *academies* na shuleni hakuna mipango (*mission wala vision*) na hata ikiwepo dhaifu. Angalau tungeweza kuviardaa vilabu vyetu viwe na *academies* zao, hili nashauri vilabu vyote vilivyo katika *VPL – Vodacom Premier League*vielekezwe kuanzisha *academies* na Wizara ichangie. Vilabu nya Simba na Yanga kupewa mabasi na vilabu vingine kuachiwa huu utaratibu mbaya, vilabu vyote vinavyoshiriki *VPL*, vipatiwe usafiri (*Buses*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu wachezaji kukatwa kodi ya mapato. Wachezaji wa vilabu vyetu kukatwa kodi ni utaratibu mzuri lakini bado tuko mbali sana, kipato chao ni kidogo. Pawe na utaratibu wa kiwango fulani cha malipo na kwa muda maalum ukifika ndio wachezaji hawa wakatwe kodi. Mfano, mchezaji anayekuwa na mkataba unaoanza Tsh. Milioni 100 kwa miaka mitatu mfululizo huyu akatwe kodi angalau asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja nya kisasa nya michezo, Jiji la Tanga lipo eneo la uwanja wa kisasa unaotaka kujengwa kwa ufadhili wa *FIFA*, hadi leo hakuna hata uzio na matokeo yake uwanja unaanza kuvamiwa na wajenzi holela. Je, Serikali katika ujenzi wa uwanja huu na udhamini wa *FIFA* inawaeleza Watanzania, mikataba ikoje, lini uwanja utaanza kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ya Kimataifa; michezo wa *boxing* ndiyo michezo pekee ambao unadiriki kututoa kifua mbele, lakini michezo huu Wizara (Serikali) imeutupa, katika mikoa na wilaya ambazo michezo huu unaendelea kuchezwa wapatiwe vifaa nya kisasa na nya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uibuaji vipaji shuleni, nashauri Serikali itilie maanani masuala ya michezo ya aina zote kuanzia *primaries, secondary's* hadi *Universities*, Serikali ianze kuwekeza kwa dhati.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ya Wabunge; pamekuwepo na mashindano ya Wabunge wa Afrika Mashariki, lakini maandalizi na stahiki za Wabunge wa Tanzania hazieleweki, wanadai kuanzia mashindano ya Mombasa (Kenya) hadi iliyofanyika Dar es Salaam (Tanzania). Ushauri, namwomba Waziri atulipe Wabunge.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Michezo, imekuwa ikikumbwa na changamoto ya gharama kubwa ya vifaa vyta michezo inayotokana na kodi inayotozwa hasa vifaa vinavyotolewa kama msaada kwa mfano kulikuwa na nyasi bandia ambazo hadi sasa sijui suala hilo limefikia wapi kwani zilizuiliwa bandarini. Waziri atupe majibu ya suala hilo. Kuna uvamizi na kubadilishwa kwa matumizi ya viwanja vyta michezo. Serikali itupe majibu na pia kuna uvamizi wa maeneo yaliyotengwa kwa burudani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni biashara, hivyo ni lazima tufanye uwekezaji kama biashara yoyote inavyotakiwa ifanyike. Uwekezaji lazima uanzie katika ngazi ya chini kwa kutayarisha watoto wetu kuwa wachezaji wazuri kwa michezo mbalimbali au sanaa na utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za michezo na utamaduni katika halmashauri zinakuwa chini ya Idara ya Elimu msingi ambayo ina majukumu mengi ya kushughulikia elimu na sehemu kubwa ya bajeti yake matumizi ya kawaida inatoka Serikali Kuu. Kitengo cha michezo kinamezwa na shughuli za elimu, hivyo kushindwa kutimiza wajibu na majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri zile asilimia 10 za wanawake na vijana ziwekezwe kwa kuwapa mafunzo vijana na wanawake katika vyuo mfano, TASUBA ili wapate ujuzi na wawekeze katika sanaa. Halmashauri zinaweza kusomesha hata vijana wawili kila mwaka. Hii ni sawa na

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kuwapa ndoano badala ya kuwapa samaki. Tusiwape fedha tu, mafunzo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Kilimanjaro *Marathon*. Michezo hii ilianza kufanyika Mkao wa Kilimanjaro lakini pia Mkao wa Mwanza wameanzisha *marathon*. Mapendekezo au ushauri wangu ni kuwa; Serikali iangalie namna watakavyogawa mikoa na shughuli mbalimbali na tofauti ili iweze kuwa tulivu. Mfano, Mikoa ya Kusini wanaweza kuwa na mashindano ya vifaa vyaa majini kama vile mashua na boti na mikoa mingine itafutiwe michezo kulingana na mazingira yake kama vile mashindano ya magari na kadhalika hii itasaidia wananchi kujua na kutilia maanani sehemu ambayo mchezo anaoutamani na mahali atakapokwenda kufanya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada ya Serikali chini ya Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote ndani ya Wizara hii wanafanya majukumu yao kwa tija na ufanisi katika kurejesha heshima na sifa za Kitaifa kwa nchi yetu. Napenda kupata ufahamu kwa nini bajeti ya 2018/2019 imepungua kwa asilimia 15.4 kwa Sh.5,136,989,000/= kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, bajeti ya mishahara ya mwaka 2018/2019 imepungua kwa asilimia 11.7 kutoka Sh.17,276,616,000/= na kufikia Sh.15,253,265,000/= je, ni kutokana na punguzo la watumishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kilichosababisha bajeti ya matumizi mengineyo kuongezeka kwa asilimia 50.8 ya Sh.4,780,331,000/= kutoka lengo la 2017/2018. Wakati bajeti ya miradi ya maendeleo ni Sh.8,700,000,000=, pungufu ya Sh.696,410,000/= ya bajeti ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunahitajika kuendeleza na kuimarisha maendeleo ya utamaduni na

sanaa, maendeleo ya sanaa na maendeleo ya michezo na kutuwezesha kuibua vipaji vya aina zote na kuitangaza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Wizara. Hongera sana kwa timu nzima kwa kazi nzuri, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, wataalam na wasaidizi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeneo ya Kihistoria, Utamaduni, Mila na Desturi. Eneo la Masonya Wilayani Tunduru ni tajiri sana kwa mahitaji haya. Ni ombi langu eneo hili liboreshewe miundombinu yake, kutangazwa na kuendelezwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya mallikale na utalii ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kushirikisha machifu katika Wilaya ya Tunduru. *Chiefdoms* bado zina wazee wenye taarifa kubwa na muhimu, licha ya taarifa kutoka halmashauri ya wilaya; *Chief Mataka, Chief Ntalika, Chief Kanduru, Chief Mbalamula, Chief Nakoko*, kwa kuanzia. Ni vizuri hatimaye huko siku zijazo tukawa na orodha, *directoryya* maeneo haya muhimu yote na ikazinduliwa kwa matumizi ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Ukombozi wa Kusini mwa Afrika hauwezi kuzungumziwa ukakamilika bila kutaja Wilaya ya Tunduru. Kituo cha Masonya ni maarufu kama kambi ya kimkakati kwa harakati za ukombozi wa Msumbiji. Yapo makazi na maficho ya Samora Machel, Mwalimu Nyerere na wengineo. Nashauri Mheshimiwa Waziri atembelee kambi hii tukiongozana nami, ili aone umuhimu wa eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usikivu wa Redio (*TBC*). Kukatikakatika na kupotea kwa matangazo, pia usikivu hafifu katika baadhi ya nyakati ni mambo yanayowakera wananchi wa Tunduru. Tunaomba ufuatilaji na ufumbuzi wa tatizo hili.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili, utamaduni, mila, desturi katika Wilaya ya Tunduru huenda hili likawa ni tatizo la Taifa zima. Vinaathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, hususan, simu za viganjani, *TV* na kadhalika, kiasi ambacho hata vijiji ngoma za asili zinapotea maadili ya Mtanzania na makabila unapotea. Nini mkakati wa Serikali?

**MHE. DEO F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*). Matangazo ya shirika hili la utangazaji la Taifa hayafiki katika Wilaya ya Ludewa na maeneo mbalimbali ya Ludewa. Hivyo tunaiomba Wizara kuangalia suala hili ili Ludewa ipate matangazo ya *TBC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa wa kuwa na utaratibu wa mpango wa kujua matangazo ya *TBC* juu ya uwekaji wake awamu kwa awamu katika maeneo mbalimbali ya nchi. Hii itaondoa usumbufu wa kuulizauliza lini itakuwa ni zamu ya maeneo fulani na pia kujua *TBC* itachukua muda gani kufika nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vazi la Taifa. Kuna mchakato uliana wa Vazi la Taifa, lakini mpaka sasa hakuna mwendelezo wowote wa kupatikana kwa vazi hilo. Vazi hilo ni muhimu kwani linaweka utambulisho wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maandalizi ya Timu Zetu katika Mashindano ya Kimataifa. Serikali itenye pesa za kutosha katika maandalizi ya michezo mbalimbali katika fani za mpira wa miguu, pete, wavy na kadhalika kabla ya kwenda katika mashindano mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ajira za Maafisa Michezo na Utamaduni. Serikali haitengi bajeti kwa ajili ya ajira za Maafisa Utamaduni na Michezo katika kuibua aina mbalimbali za michezo. Ukitoa soka na riadha bado tuna michezo mingi sana, ipewe kipaumbele. Kwa mfano *volleyball*, *tennis*, *basketball*, tufe na kadhalika.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongeza Waziri wa Habari, Naibu

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, watendaji wote walio chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuhakikisha sekta zilizoko katika Wizara hiyo zinasongea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo kuna changamoto kadhaa ambazo zinatakiwa kufanyiwa maboresho. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha karibu miaka 30 iliyopita kumekuwa na ulegevu kwa kiasi fulani kwa Serikali yetu kwa kutokuwa karibu na vijana (rika la miaka 12-35), kundi ambalo linahitaji kuelewa, kuelimishwa na kuthaminiwa kwa kuwa vijana ndio nguvu kazi ya nchi yoyote duniani hususan Tanzania. Kwa kuwatumia vizuri vijana wetu watasaidia kuongeza uchumi wa nchi na pia watajajiri wao wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii wetu wanahitaji elimu ya ujana, mila zetu, utamaduni wa Mtanzania, staha, heshima, nidhamu, utu, utaifa na uzalendo kwa nchi yetu. Haya yote yanahitaji fedha za bajeti katika Baraza la Michezo (BASATA) ili zitumike kwa kuwapatia elimu, mafunzo, warsha, semina, hamasa, matangazo mbalimbali ambayo yatasaidia kuwaelimisha wasanii/vijana wa Kitanzania kuelewa na kujiheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ijpange upya katika kutambua na kusimamia vijana wasanii wa aina mbalimbali yaani *music*, ngoma za jadi, wachoraji, waimbaji injilli, muziki wa dansi, waigizaji, wanamichezo na wengine wanaojihuisha na sanaa. Kwani wasanii wana mchango mkubwa katika ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu enzi ya kutafuta uhuru wa nchi yetu ya Tanzania. Kwani wasanii wetu walikuwa bega kwa bega katika kutafuta Uhuru wa Tanganyika kwa kuimba na kucheza ngoma za kudai uhuru wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba tena

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Serikali kutoa fedha za bajeti za kutosha kwa ajili ya kuelimisha wasanii kwani mtoto umleavyo ndivyoakuavyo. Tukiri eneo hili tulilisahau likajilea lenyewe. Tukumbuke vijana ni kundi lenye nguvu na pia wana muda mwingi wa kuishi hapa duniani, tulilee na kulielekeza vema. Msanii Diamond anaiwakilisha Tanzania anahitaji kuelimishwa na kulelewa vema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri pamoja na *team* yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lushoto ni eneo lenye milima na mabonde mengi na kwa hiyo tullomba mnara kwa ajili ya kupata matangazo ya Redio ya Taifa yaani *TBC*. Hivyo basi tunaomba mnara huo ujengwe haraka. Pamoja na kwamba Serikali imetuahidi kutujengea mnara katika maeneo ya Kwebusani katika Kijiji cha Kwemashai, na tuliambiwa ujenzi huo umeanza lakini mpaka sasa bado ujenzi huo haujaanza. Naomba tufanyiwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba kuna vijana wengi sana ambao wana vipaji mbalimbali hasa katika michezo, sanaa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Lushoto ina vijana wengi ambao ni wachezaji wa mpira wa miguu. Cha kusikitisha vipaji vya vijana vinapotea bure na Serikali kupoteza nguvu kazi ya vijana hao. Hivyo basi niiombe Serikali ijenge chuo cha michezo katika Wilaya ya Lushoto pamoja na kiwanja hata kimoja tu. Sambamba na hilo kuna hawa vijana ambao ni wanasanaa na utamaduni. Lushoto ni Wilaya ambayo imebarikiwa kwa vipaji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu Tukufu itume wataalam kwenda vijiji na wilayani kwa nia ya kwenda kuwabaini vijana wenye vipaji na kuwapa au

kuwajengea uwezo ili waweze kutoka vijiji na kuwaleta mjini na kuwapa msaada ili nao waweze kujajiri. Kama inavyojulikana kuwa michezo ni ajira, kwa hiyo tukwasaidia vijana hawa Serikali itakuwa imepunguza asilimia kubwa sana ya tatizo la ajira hasa kwa vijana wetu hawa wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuwekeza katika michezo kuanzia shule za msingi hasa kwa kupeleka vifaa vyta michezo katika shule zetu. Sambamba na hayo niiombe Serikali itoe VAT katika vifaa vyta michezo ili vijana wetu waweze kumudu gharama za kununua vifaa hivyo vyta michezo, kwa sababu ukizingatia Tanzania imeamka sana katika tasnia hii ya sanaa na michezo. Ni imani yangu kubwa kuwa tukiwatumia vizuri wasanii wetu hawa tutakuwa tunaingiza pesa nyingi hasa kwa kuwatumia kutangaza utalii wetu nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niiombe Serikali kuwasimamia wasanii wetu ili wasidhulumiwe na matajiri ambaao hawana nia nzuri na wasanii wetu. Msisitizo, tunaomba mnara wa Lushoto ufanyiwe bidii ili uweze kuisha haraka kwa sababu tumechoka kusikiliza redio za Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanja vyta michezo. Viwanja vyta michezo vingi katika halmashauri mbalimbali hali yake ni mbaya sana, ili kuboresha michezo ni lazima tuboreshe viwanja vyetu katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukuza vipaji kuanzia shulenii tuwe na matokeo chanya ni lazima tuwekeze kwa watoto wadogo hasa kuandaliwe *syllabus* maalum zitakazowajenga wanafunzi wakiwa mashulenii ili kuwakuza kulingana na vipaji walivyonavyo ili kulisaidia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vazi la Taifa. Kulingana na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

umuhimu wa jambo hili ni vyema suala la Vazi la Taifa lipewe kipaumbele kwani kutokuwa na Vazi la Taifa ni vigumu kumhukumu kwa kosa la mavazi, sio sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suala la Kufungia Magazeti; jambo hili liangaliwe upya kwani magazeti yanasaidia kufikisha ujumbe kwa jamii. Naiomba Serikali ibadilishe utaratibu, badala ya kufungia gazeti apewe adhabu Mhariri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii kufungiwa wakati nyimbo tayari zimepigwa kwenye redio na *TV*, jambo hili si sawa kwani huwezi kufuta wakati wimbo huo unakuwa umesambaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo irejeshwe mashulenii, UMISETA na UMITASHUMTA miaka iliyopita vyombo hilvi villichangia sana kukuza michezo na kuibua vipajji vingi kwa wanafunzi wetu shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya michezo ifanyiwe marekebisho ili kuleta ufanisi katika michezo nchini kwani tumekuwa tukifanya vibaya mara kwa mara katika Taifa letu.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumbukumbu zangu kuna kauli alioitoa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano kwamba *COSOTA* na BASATA ziunganishwe pamoja ili kuboresha utendaji kazi na ku wahudumia kwa ubora zaidi wasanii wote. Hii ni kutokana na *COSOTA* kushindwa kabisa kuwasaidia wasanii na kulinda kazi zao, kiasi kwamba zinaibiwa kila kukicha ilhalii *COSOTA* wapo. Je, ni lini *COSOTA* na BASATA zitaunganishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali au Wizara inatamka nini juu ya *Msama Production* ambaye yeze amekuwa akifanya kazi ya *COSOTA* ya kuzuia wizi wa kazi za sanaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kuwa *TRA* wanapoteza mapato mengi sana kwa kutodhibiti wizi wa

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

kazi za sanaa? Kwa sababu kudhibiti wizi huu na kazi zote zikauzwa kihalali, Serikali itapata na msanii atapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kuwe na *one stop center* ya wasanii pamoja na vyama mbalimbali vinavyoanzishwa, lakini kuwe na mahali pamoja ambapo msanii au chama cha sanaa kingeweza kuripoti kwa maana sasa hivi Maafisa Utamaduni wako TAMISEMI, COSOTA iko Viwanda na Biashara na BASATA iko Wizara hii ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hii kero na usumbufu wa TRA kuchelewesha kutoa *sticker*, kitu ambacho kimekuwa ni usumbufu mkubwa na kurudisha maendeleo ya wasanii wetu. Je, Serikali inalisaidiae hili maana hizo ndizo kero za kutokana na kutokuwepo kwa *one stop center* ya wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma COSOTA walikuwa wakiwalipa wasanii mirabaha ya kazi zao ambazo COSOTA hukusanya kupitia TV, Radio na kadhalika, lakini siku hizi hawalipi na kama wanalipa nadhani wanawalipa wasanii wachache sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kumnyang'anya COSOTA jukumu hilo na kutafuta chombo kingine kifanye kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu COSOTA hawawezi, hata ukienda kuuliza wanadai kuwa mashine ya kufanya mahesabu ya mgao wanasema mpaka wapate mtaalam kutoka Uswisi. Je, hivi ni kweli hii nchi hakuna mtaalam wa hiyo mashine mpaka wamsubiri kutoka Uswisi? Kama ni kweli jambo hilo naomba kupatiwa majibu. Pia ningependa kujua hizo fedha zipo na ziko ngapi na ziko wapi? Hapa naomba majibu ya kina ama lah, nitashika shilingi na naweza kubaki nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya COSOTA imetoea muda wa kugawa hiyo mirabaha kwa wanamuziki lakini utaratibu huo haufuatwi. Katiba inasema mgao utakuwa Desemba lakini hautazidi mwezi wa Pili, lakini hadi sasa hawajalipa kwa muda mrefu sasa. Kauli yao ni mashine mbovu, mtaalam aletwe toka Uswisi! Jamani, Please!

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu warejee enzi za Mzee Steven Mtetewaunga alikuwa Afisa wa *COSOTA*, malipo yalikuwa mara mbili kwa mwaka mwezi wa Sita na Desemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasita sana kuunga mkono hoja. Naomba tu ielevweke wazi kuwa na mimi ni msanii wa muziki wa Injilli Tanzania hivyo na-*declare interest* kuwa ni mdau wa sanaa ya muziki na nimesajiliwa *COSOTA*, BASATA na kadhalika.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Viwanja vya Michezo. Mkao wa Kilimanjaro kila mwaka wiki ya kwanza ya mwezi wa tatu panakuwepo na mbio za *Kilimanjaro Marathon*. Mbio hizi kwa sasa zimezidi kukua mwaka hadi mwaka na zinahusisha wageni kutoka nje ya nchi na wenyeji Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbio hizi zinachangia sana uchumi kwa wakazi wa Moshi na Taifa kwa ujumla kwa sababu wageni zaidi ya kukimbia pia hufanya utalii wa kupanda mlima na kutembelea mbuga zetu za wanyama. Mbio hizi kwa sasa kuanzia uwanja wa Chuo cha Ushirika Moshi na kumalizikia pale. Hata hivyo, kwa jinsi mbio hizi zilivyopata umaarufu uwanja ule unalemewa na wingi wa watu ambao ni hatari kwa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Moshi tuna uwanja mkubwa wenyewe michezo zaidi ya saba unaoitwa *King Memorial Stadium*, lakini uwanja huu hautumiki ipasavyo ukizingatia kuwa hakuna viwanja vya michezo Moshi na huu uwanja unamilikiwa na mkoa. Kwa sasa ni sehemu ndogo tu inayotumiwa na wauza nguo za mitumba. Je, ni kwa nini Serikali isitafute watu binafsi kwa kushirikiana na Serikali wakakijenga kile kiwanja ili kiweze kutumika hata kwa michezo mingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa kilipewa jina la mfalme wa Uingereza naamini likiandikwa andiko zuri mfalme anaweza kukijenga kiwanja kile na tukaendelea kukiita *King Memorial Stadium*. Hii itachangia Serikali kupata

mapato yatokanayo na uwanja huu, itatengeneza ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utamaduni; hivi utamaduni wa Mtanzania ni upi? Ni siku nyingi tumekuwa tukilizingumzia Vazi la Taifa na kuna wakati ilitolewa mifano ya Vazi la Taifa lakini hadi leo hatujaelezwa mchakato ule ulifikia wapi. Ni lini tutapata Vazi la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi ya utamaduni wetu Watanzania ulijengwa tuwe na utu, upendo, amani na utulivu lakini kwa sasa nchi yetu tunaelekea kupoteza vyote hivi na mpaka sasa hivi Serikali haijaweza kutueleza hao watu wasiojulikana ni akina nani? Watu wamekuwa wanatekwa, wanauawa na kuokotwa baharini kwenye viroba, waandishi wa habari wanatekwa, yote haya ni amani, upendo, utu na utulivu kutoweka. Je, Serikali inatueleza nini kuhusu utamaduni wetu huu kupotea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Haki ya Kupata Habari. Hii ni haki ya msingi ambayo ipo kikatiba kabisa ya watu kupata habari; lakini tumeshuhudia sasa hivi Serikali imekuwa ikivifungia vyombo vya habari pindi wanapoikosoa Serikali. Pia ni haki ya Watanzania kuona wawakilishi wao Bungeni kama wanazitungumzia kero zao, lakini haki hii wamenyimwa kwa kuzuiwa kwa Luninga (*TV*) kutokuwa mubashara (*Live*) wakati vipindi vya Bunge vikiendelea. Huu ni uvunjwaji wa sheria, inapelekeea nchi kuendeshwa bila kufuata sheria.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kazi nzuri iliyotukuka. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri, hotuba na Mipango mizuri, hivyo naunga mkono hoja hii kwa furaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chemchemi ya michezo ni vijana wetu vijiini. Chemchemi hii ikihifadhiwa, ikaendelezwa huliletea Taifa sifa na faraja ya kushinda katika mashindano

ya Wilaya, Mkoa, Taifa na Kimataifa. Kwa sababu hiyo niliomba na bahati nzuri nikaahidiwa na Waziri tangu Mei, 2016 mipira 100 *football* kwa ajili ya kuendeleza mpira wa miguu ngazi ya Kata. Mipira hii niliahidiwa na Waziri wakati huo 2016 kama mchango wa kuendeleza *League* ya mpira wa miguu Wilayani Mwanga (*Maghembe Cup*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anikumbuke kutekeleza ahadi yako hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu kidogo katika Wizara hii muhimu katika kuendeleza michezo na utamaduni katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Sera ya Sheria ya Utamaduni inayotumika nchini kwa sasa imepitwa na wakati ndiyo maana tunashuhudia migongano na mivutano hasa katika tasnia zingine sanaa zikifungiwa kwa maelezo ya kufanyika kinyume na maadili tuliyokubaliana ambavyo vinatumika kuamua huyu kakiuka maadili na huyu hajakiuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumeona hata baada ya baadhi ya kazi za sanaa kufungiwa kumekuwa na malalamiko kuwa mbona baadhi ya kazi za sanaa ambazo zinaonekana kuwa na migogoro kuliko zilizofungiwa bado zipo na zinatumika. Hii inaonesha upo umuhimu wa kupitia upya sheria na sera za utamaduni nchini ili kulinda na kutunza utamaduni wetu na kazi zetu za sanaa bila uonevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, ipo haja ya kupitia upya sheria na taratibu zinazotumia mwenendo wa vyombo vya habari vya *ki-electronic* yaani *TV* na *Radio* katika mazingira ya teknolojia ya leo unapofungia *TV* na *Radio* za nchini kwetu kwa sababu ya kupiga muziki fulani (kutumia kazi fulani za sanaa) wakati huo huo ving' amuzi vyetu nchini vinaonesha *channels* za nje ya nchi ambazo hatuna uwezo wa kuzuia uoneshwaji wake nchini ni sawa na kuvinyima vituo

vyetu vya TV hapa nchini vishindwe kushindana kwenye ushindani wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kama kweli tunataka nchi yetu tusomeke kwenye dunia kwenye michezo ni lazima Serikali ikubali kuwekeza katika michezo, tusipofanya hivyo tutaendelea kuwa wasindikizaji katika michezo tutakayokuwa tunashiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali lazima tukubali kushirikiana na Wafadhili wanaofadhili timu zetu kuhakikisha timu zetu zinapata muda mrefu wa kukaa kambini ili waweze kufanya mazoezi ya pamoja. Tusipofanya hivyo tutaendelea kuwa wasindikizaji kwenye kila mashindano. Pia tuwatie moyo wachezaji na wasanii wetu tusiwakatishe tamaa maana wengi wamefika hapo kwa juhudui zao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. GEORGE M. LUBELEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenyе ufanuzi. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono naomba nichangie maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya mpira (*football*) kwa kuwa viwanja vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) hivyo vina hali mbaya sana vinatakiwa ukarabati na CCM haina fedha za ukarabati. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku kwa Chama cha Mapinduzi ili kuvikarabati viwanja vyake hasa ukuta eneo la *Pitch* ili timu zetu za ligi kuu ziweze kuchezea viwanja hivyo bila shida yoyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waandishi wa Habari wa Umma (Serikali) kwa kuwa sekta ya habari ni muhimu sana kwa maendeleo na uchumi wa nchi yetu, Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Waandishi wa Habari kila Wilaya ambako wapo wananchi wengi na wanafanya kazi za kilimo na shughuli nyingi za maendeleo kwa ajili ya kuinua uchumi

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

wa wananchi. Vyombo vingi vya habari vinahamasisha sana wananchi kushiriki shughuli nyingi za maendeleo badala ya Waandishi wa Habari kujazana Mijini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyombo vya Habari hasa vya Serikali havipati maslahi ya kutosha kama vile *TBC* maslahi ni kidogo sana ndiyo maana watumishi wengi wanahamia vyombo binafsi ambaao wanalipwa vizuri. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya watumishi wa *TBC* na Waandishi wa Habari wa Serikali ambaao wapo chini ya Idara ya Habari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu nyingi za mpira wa miguu zina migogoro mingi sana. Je, ni sababu zipi zinazosababisha migogoro hiyo na kusababisha kushuka kiwango cha mchezo wa mpira wa miguu hapa Tanzania? Je, Serikali itasaidiaje kupunguza mlgogoro hiyo ili kuboresha soka la Tanzania hata Kimataifa.

Mheshimiwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya michezo mashulenii, viwanja vingi vya michezo nchini hasa viwanja vya shule vimechukuliwa na taasisi mbalimbali wakiwemo wanachama wa CCM, matokeo yake shule zinahangaika hakuna sehemu ya kuchezea watoto wa shule. Naomba Serikali ihakikishe viwanja hivyo vinarudishwa kwenye shule ili wanafunzi wetu waweze kuvifurahia. Kwa mfano, uwanja wa sabasaba ulioko Njombe uliochukuliwa na CCM, uko kwenye eneo la shule ya msingi ya Sabasaba na Mpechi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo mashulenii watoto wetu wa shule za msingi na sekondari wamelemaa, awali kulikuwa na michezo hata mchakamchaka lakini hivyo vyote vimefutwa, naomba Serikali irudishe mchakamchaka mashulenii na itiliwe mkazo somo la michezo na mazoezi.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili katika nchi yetu yameporomoka, naomba somo la maadili lifundishwe mashulenii kuanzia shule za msingi hadi vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwasaidie wasanii kuboresha kazi yao badala ya kuwaadhibu kwa kuwafungia. Tutoe maelekezo vizuri badala ya kutumia nguvu, pia tusiache wasanii kuonesha sanaa zao kama nyimbo kwa muda mrefu halafu baadaye tunawafungia wakati tayari watu wamekwisha sikia nyimbo hizo, tuwasaidie wasanii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. KHADIJA H. ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali, Wizara ya Habari pamoja na Mheshimiwa Waziri na wasalidzi wake wote katika Wizara hii kwa jitihada zao wanazofanya kuhakikisha wanafikia malengo waliyojipangia katika kuendeleza sekta zote zilizomo ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri yafuatayo:-

(i) Wizara iongezewe fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake.

(ii) *TBC* inahitajika nchini kote hivyo Serikali iendelee na juhudii za kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waendane na hali ya sasa ya teknolojia ya habari. Aidha, *TBC* ipatiwe mitambo ya kisasa na yenyewe nguvu ili iweze kusikika na kuonekana ndani na nje ya nchi kwa muda wote.

(iii) Wizara iweke msukumo na mkakati maalum katika kuiendeleza lugha ya Kiswahili ikiwemo shughuli zote za kiserikali itumike lugha ya Kiswahili, mikutano yote inayofanyika nchini itumie lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuongeza ajira kwa Watanzania, kuongeza idadi ya watumiaji wa Kiswahili na kuifanya lugha yetu hii itumike duniani kote.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(iv) Wizara kupitia taasisi zake zote iendelee na juhudzi zake wanazochukua kuhakikisha maadili, mila na desturi za Watanzania zile zilizo bora zinalindwa na wasisite kuzuia au kufungia nyimbo, michezo, filamu na sanaa zote zinazokiuka maadili ya nchi yetu na Watanzania kwa ujumla.

(v) Wizara ihamasishe na kufufua michezo ya zamani ambayo imepotea ambayo inaweza kuongeza tija kwa Taifa na wananchi kwa kuongeza kipato na kulinda isipotee kabisa.

(vi) Sanaa na utamaduni ni vyombo vyenye nguvu sana katika kuitangaza nchi. Hivyo juhudzi za Wizara za kuitangaza nchi yetu kupitia sanaa mbalimbali ziongezwe kwa lengo la kuitangaza zaidi nchi yetu ya Tanzania duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kupiga kazi kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuongelea kuhusu madeni ya matangazo kwenye magazeti ya Serikali. Sikuona busara kulisema hili hadharani, kiukweli Wizara na Taasisi za Umma zinadaiwa mamilioni ya fedha za matangazo kwenye magazeti ya *Daily News* na *Habari Leo*. Je, huko kwenye *private media* kama *Mwananchi*, *The Guardian*, *The East African* ni kweli kuwa Wizara na Taasisi hazilipii hayo matangazo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nyakati hizi ambazo *social media* imekuwa *fast* kueneza na kusambaza taarifa ipo sababu kuyawezesha magazeti ya Serikali kwa kulipa madeni ya matangazo ili vyombo hivyo viweze kuendelea kuwekeza na kukabiliana na *private media* ambazo kwa nguvu ya fedha zinaweza kuwa chanzo cha upotoshaji wa taarifa. Nyote mnajua nguvu ya *media*, hatuwezi kukwepa kuwezesha vyombo vyetu japo kwa kulipa madeni.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ving'amuvi Vs *free channel*. Kwa nini wenyewe ving'amuvi hawaachii *free channel* tano kama miongozo inavyoelekeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuchangia kuhusu usikivu wa Redio Tanzania. Nkasi Kusini eneo Tarafa ya Wampembe kandokando ya Ziwa Tanganyika hawapati matangazo ya *TBC* na hali hii inawasononesha sana. Naomba Serikali ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nashauri gharama za matangazo mbalimbali ipungue kwani wananchi wangependa kutangaza matukio mbalimbali lakini tatizo ni gharama. Hata biashara hazikui kwa kasi bila matangazo. Kumbe gharama zikipungua uchumi wa wananchi utaweza kukua na kuwezesha nchi na wananchi wake kuishi maisha yaliyo bora.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia kwa maandishi katika hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika na kuiwasilisha kwa umakini wa hali ya juu hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni Shirika la Utangazaji Tanzania. Napenda kuipongeza Wizara kwa kuendelea kuliboresha Shirika hili la Utangazaji, ni shirika linalopiga hatua katika utangazaji. Ushauri wangu kwa Wizara, iendelee kutoa mafunzo kwa watendaji wa shirika hili ili kwenda na wakati. Bado kuna wafanyakazi hawaoneshi

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mabadiliko ya kiutendaji kutokana na pengine kukosa elimu na maelekezo ya kikazi. Mfano kwenye mavazi ya mtangazaji baadhi ya watangazaji hawaoneshi kuwa na elimu ya mavazi (*dressing code*). Aidha, naomba Wizara iboreshe usikivu katika maeneo ya vijijini, bado kuna maeneo ambayo usikivu sio mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, viwanja vya michezo. Bado viwanja vyetu nchini haviko vizuri. Tunaendelea na kuwa na viwanja vya kurithi, vya karne zilizopita. Ushauri wangu kwa Wizara ni kuboresha viwanja vya michezo ili viwe vivutio kwa wachezaji na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu muweza wa yote kwa kuniwezesha kuwepo mahali hapa. Nami niungane na wenzangu kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hotuba hii imekuja na majibu ya kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo. Hotuba hii inakwenda kutekeleza llani yetu ya Chama cha Mapinduzi katika nyanja zote muhimu zinazohusika katika Wizara hii, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kuendelea kuhakikisha masuala mazima ya michezo yanakwenda vizuri na kuhakikisha timu zetu za michezo mbalimbali zinashiriki mashindano ya kimataifa na kupata ushindi. Hata hivyo, kuna changamoto mbalimbali katika sekta ya michezo, naomba kuzungumzia uwakilishi wetu katika michezo wa soka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika matokeo ya uwakilishi wetu kimataifa katika soka umekuwa si wa kuridhisha kabisa. Timu zetu kuanzia kwenye vilabu na timu ya Taifa tumekuwa ni wasindikizaji katika mashindano ya kimataifa. Serikali imekuwa ikijitahidi sana kuwekeza katika

mpira wa miguu lakini bado tumeshindwa kuwa na matokeo chanya pindi tunapokwenda katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuja na mkakati kabambe wa kuanzisha shule za mpira wa miguu na michezo mingine kuanzia mashulenii mpaka vyuo vikuu. Hii itatusaidia kupata na kukuza vipaji tangu vijana wetu wakiwa bado wadogo na kupelekea kupata wanamichezo wa michezo mbalimbali ambao sasa watakuja kuwakilisha nchi na kutuletea vikombe mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirikisho letu la Mpira wa Miguu liangaliwe kwa jicho la karibu ili kuondoa dhana ya viongozi wake kuona kwamba ni mahali pa kwenda kujipatia fedha zisizokuwa halali yaani fedha chafu. Wajikite katika masuala ya mpira wa miguu kuhakikisha wananyanyua kiwango cha mpira kwa namna ambayo itatutangaza kama Taifa, lakini siyo kila kukicha ni migogoro tu inatokea kwa kutofautiana kati ya kiongozi na kiongozi na kuacha dhana nzima na malengo ya Shirikisho la Mpira wa Miguu. Serikali kupitia Wizara ichukue hatua kali pale inapoona kuna upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali sasa tuangalie michezo mingine au kitu kingine kitakachotutangaza kimataifa kwa upande wa sanaa, utamaduni au sanaa ya muziki ama inavyoitwa na vijana wetu wa sasa Muziki wa Kizazi Kipywa. Tumejionea baadhi ya wasanii wakifanya vizuri kimataifa na kulitangaza jina la nchi yetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wanavyofanya vizuri kimataifa wanaitangaza nchi na kuiwezesha kupata wageni kwani wageni hutaka kuijua zaidi nchi husika baada ya kuona wimbo au msanii husika katika nchi zao akipewa heshima na taasisi mbalimbali. Hata hivyo, tumeshuhudia wasanii wetu wakikosa kuungwa mkono, baadhi ya watu kutokuona yale mazuri yote wanayoyafanya tena kwa juhudii zao wenye kula tangaza Taifa na Wizara kuja na kuwafungia.

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kupitia Wizara wakumbuke kuwa vijana hawa wanatumia nguvu nyingi na gharama kubwa kujitangaza na kultangaza Taifa. Ni vyema wawe wanakaa nao na kuwashauri, Wizara igeuke kuwa mlezi wa wasanii wetu na siyo kuwa mkandamizaji. Leo wasanii wetu wanapata nafasi ya uwakilishi wa ufunguzi wa Kombe la Dunia kule nchini Russia kwa kwenda kutumbuiza. Mashindano yale ni makubwa duniani, dunia nzima watakuwa wanatazama na watataka kujua msanii huyu anatokea wapi. Wakijua Tanzania watataka kujua Tanzania kuna nini mpaka Shirikisho la Soka Duniani liweze kumchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mwanzo mzuri wa kuanza kupokea wageni kuja nchini kwa shughuli mbalimbali za kiutalii, hata uwekezaji. Je, wasanii wetu kama hawa ambao wanapambana kwa hali na mali na kupata fursa kama hizo tunawaunga mkono kwa kiwango gani? Ni lazima Wizara itambue ni wapi kuna fursa ya nchi kutambulika kisanaa, kimichezo na kadhalika na kuhakikisha inashikamana na wahusika katika kuleta malengo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kupitia Wizara kuendelea kuvisimamia vyombo vyahabari kwa mujibu wa sheria ili vitekeleze majukumu yao kwa utaratibu uliopangwa, kanuni na maadili ya uandishi wa habari. Kufanya hivyo kutasaidia sana kuwa na vyombo bora vyahabari na uhakika wa habari zenyewe kwani tunajua umuhimu wa vyombo vyahabari na waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tasnia ya habari inapotumika vizuri katika kutoa habari basi Taifa hubaki salama, lakini pale itakapopotoka na kutoa habari za kichochezi basi Taifa lazima litaingia katika machafuko na amani kutoweka. Wizara iwe inavikumbusha vyombo vyahabari wajibu wao ili navyo vitekeleze majukumu yao kwa uhuru na haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wageni walioko Bungeni jioni hii ni:-

Wageni 88 wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu ha Dodoma wanatokea Mkoa wa Simiyu. (*Makofi*)

Pia kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Mhagama ambao ni rafiki zake kutoka Jiji la Dar-es-Salaam. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wageni 17 wafugaji kutoka Chama cha Wafugaji Tanzania wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho ndugu Ester Laban. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninawakumbusha tena semina siku ya Jumapili juu ya Uvuvi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 15.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuweza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia uzima pamoja na afya njema, sote kuweza kuwepo katika Bunge hili Tukufu. Vilevile nichukue nafasi hii kuweza kumshukuru Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa njoo hapa mbele, unajibu hoja, huchangii.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue nafasi hii kuweza kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa miongozo yote ambayo amekuwa akinipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Vilevile nichukue nafasi hii kuweza kuwashukuru akinamama wote na wanawake wote wa Mkoa wa Songwe

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kwa imani yao kubwa kwangu ambayo inaniwezesha katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue nafasi hii kuweza kuwashukuru Wabunge wote ambao wameweza kuchangia na hoja yetu, nami niseme kwamba, michango yao yote imekuwa ni michango ambayo ina tija sana na tunaahidi kwamba, tutaichukua na kuweza kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu baadhi ya hoja ambazo zimeweza kuzungumzwa, kwanza nianze na kujibu hoja za Kamati. Hoja ya kwanza ambayo imeibuliwa na Kamati ni juu ya usajili wa magazeti kwamba uko chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yetu ya mwaka 2018/2019, Wizara tumejipanga kuendelea kusajili magazeti yote nchini, lakini vilevile kwa sababu ni takwa la kisheria chini ya Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 tumepokea ushauri wa Kamati na Wizara tutaendelea kuhakikisha tunaendelea kusajili magazeti ambayo yapo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema pia tukubaliane na Waheshimiwa Wabunge katika jambo hili kwamba, katika suala zima la usajili wa haya magazeti Wizara imefanya kazi kubwa sana kwa sababu ukiangalia ndani ya muda mfupi katika kipindi cha mwaka mmoja magazeti ambayo yamesajiliwa ni magazeti 169 ukilinganisha na magazeti 400 ambayo yamesajiliwa tangu kuanzishwa kwa sheria hii mwaka 1976.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba, jitihada kubwa zinahitajika, lakini pamoja na hayo, Wizara imefanya kazi kubwa sana na tunaahidi kwamba usajili wa magazeti tutaendelea nao katika mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili pia ambayo imeweza kuibuliwa na Kamati ni kuhusiana na Serikali

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

kufanya kazi andiko la *TBC* kwamba wanahitaji shilingi bilioni 80 kwa ajili ya kuboresha usikivu wa *TBC*. Serikali imeendelea kusaidia shirika hili la *TBC* katika kuboresha usikivu katika nchi yetu ya Tanzania, hilo limejidhihirisha kwa sababu ukiangalia bajeti ya mwaka 2016/2017, fedha ambayo ilitengwa ilikuwa ni shilingi bilioni moja, lakini kwenye bajeti ya mwaka wa 2017/2018, bajeti hiyo ya kuboresha usikivu ilipanda na kuweza kufika shilingi bilioni tatu. Kwenye bajeti hii sasa ambayo tunaomba leo Waheshimiwa Wabunge muweze kuipitisha Shirika la *TBC* limetengewa shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa kwamba kwa kuwa, Serikali katika fedha ambayo ilitenga mwaka uliopita shilingi bilioni tatu na fedha hiyo imeshatolewa yote, ni imani yetu kabisa kwamba, katika bajeti hii ambayo imetengwa ya shilingi bilioni tano kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019, Serikali tunaahidi kwamba hiyo fedha itatoka na kwa namna moja au nyingine itasaidia sana katika kuboresha tatizo la usikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii vilevile iliweza pia kuchangiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo ambaye alisema kwamba fedha hii ambayo imetengwa ni ndogo sana. Niseme tu kwamba Mheshimiwa Mbunge naomba tukubaliane kwamba Serikali ina nia ya dhati kabisa katika kuboresha usikivu na kulisaidia Shirika la *TBC*. Wanasema kwamba safari ni hatua, kwa hiyo tumeanza kidogo kidogo na sasa hivi tunaendelea vizuri kuhakikisha kwamba tunamaliza kabisa tatizo la usikivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imeibuliwa na Kamati ni kutoa ushauri kwamba Serikali iweze kutoa fedha kwa *TBC* Redio ili iweze kusikika nchi nzima. Waheshimiwa Wabunge katika mwaka wa fedha 2017/2018 Shirika la *TBC* limefanya kazi kubwa sana katika kuboresha usikivu hasa katika maeneo ambayo ni ya mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukienda maeneo ya kule Namanga, Tarime, Kankoko, Nachingwea, Mtwara *TBC* inasikika vizuri sana. Hiyo yote ni kazi ambayo imefanyika

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

katika mwaka huu wa fedha na bajeti ambayo ilitengwa katika mwaka huu ambao unaenda kumalizika, bajeti ya 2017/2018, maboresho hayo yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 *TBC* ilikuwa inasikika katika Wilaya 81 tu, sasa hivi tumefikia Wilaya 100 ambazo *TBC* inasikika vizuri. Kwa hiyo, niseme kwamba, ushauri tumeupokea lakini kama ambavyo nimezungumza awali kwamba fedha inaendelea kutengwa na sasa hivi bajeti ya maendeleo ya *TBC* imepanda kufikia bilioni tano tunaamini kwamba tatizo hili litaenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge ambayo imezungumziwa na Wabunge wengi ni kuhusiana na suala zima la Wasanii pamoja na BASATA, kwamba BASATA inafungia nyimbo pale ambapo nyimbo zinakuwa tayari zimekwishapigwa, halafu BASATA inakuja kufungia nyimbo hizo baadaye. Hoja hii imejadiliwa na Mheshimiwa Tauhidha na pia Mheshimiwa Amina Mollel ameizungumzia vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Filamu kwa maana ya Bodi ya Filamu, Sheria ya Bodi ya Filamu pamoja na kanuni zake inataka wasanii wote ambao wanatengeneza filamu kabla hawajapeleka filamu zao sokoni wahakikishe kwamba filamu hizo zimepita Bodi ya Filamu kuweza kuhakikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwa Bodi ya Filamu hata kanuni ambazo tunazo katika chombo ambacho kinasimamia sanaa kwa maana ya BASATA, tuna kanuni ambazo zinawataka wasanii wote kabla hawajapeleka nyimbo zao kuanza kurushwa katika vyombo mbalimbali vya habari, wahakikishe kwamba nyimbo hizo wanazipeleka BASATA ili ziweze kupitiwa na kama zina marekebisho ziweze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo tunayo katika nchi yetu lakini kwa wasanii ni utii bila shuruti. Wasanii wengi hawapeleki kazi zao, nyimbo zao BASATA wala hawapeleki filamu zao. Hii ndiyo sasa imekuwa

changamoto inapelekea BASATA wanakuja kushtukia tayari kazi imeshaingia sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue nafasi hii pamoja na changamoto mbalimbali ambazo tulikuwa nazo BASATA, lakini Serikali haina ugomvi wowote na wasanii. Ugomvi ambao Serikali inao na wasanii ni juu ya mmomonyoko wa maadili. Nichukue nafasi hii kusema kwamba Serikali na Wizara hatutaacha kulisimamia niwaombe wasanii wote kuhakikisha kwamba kazi zao kabla hawajazipeleka sokoni wanazipitisha katika vyombo hivi ambavyo nimeweza kuvitaja ili kazi hizo ziweze kuhakikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo limezungumziwa pia na Kaka yangu 'Profesa J' Mheshimiwa Joseph Haule amesema BASATA imekuwa haina mahusiano ya karibu na wasanii badala yake sasa BASATA imekuwa kama chombo cha kuwachukulia hatua na adhabu wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, BASATA imekuwa ni chombo ambacho kipo karibu sana na wasanii. Katika kudhihirisha hilo kuanzia mwaka 2010 BASATA imeandaa makongamano na matamasha mbalimbali ambayo wasanii wengi wamekuwa wakishirikishwa. Mpaka sasa wasanii zaidi ya 30,000 wameweza kushiriki makongamano hayo ambayo kwa namna moja au nyingine yamewasaidia wao kama wasanii pia kuweza kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mwaka huu wa fedha BASATA imeweza kukutana na wasanii zaidi ya 2,000 na kuweza kujadili changamoto zao mbalimbali. Tatizo linalojitokeza ni kwamba baadhi ya wasanii ni kutokushiriki pale ambapo hivi vikao vinaitishwa na hivyo wanakuwa hawajui kwamba BASATA ina msimamo gani na mambo gani ambayo wao kama wasanii wanapaswa kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna hoja nyingine pia imeibuliwa hoja ya uhakiki wa video. Waheshimiwa Wabunge suala la uhakiki wa video ni suala ya Bodi ya Filamu kama ambavyo nimezungumza awali

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kwamba Bodi ya Filamu imekuwa ikifanya kazi nzuri sana kuhakikisha kwamba inaendelea kuhakiki kazi zote za sanaa. Mpaka sasa hivi tunavyozungumza katika mwaka huu wa fedha zaidi ya filamu 689 za Kitanzania na 155 filamu ambazo zinatoka nje zimehakikiwa. Kwa hiyo niendelee tu kusisitiza kwa wasanii kuhakikisha kwamba wanapeleka kazi zao ili ziweze kuhakikiwa na kuepusha matatizo ambayo yanaweza kuwapata hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imezungumziwa ni kuhusiana na vazi la Taifa. Hii ni hoja ambayo imeibua mjadala mkubwa, Mheshimiwa Lucy Owenya ameweza kuchangia pia kwa maandishi na kudai kwamba ni lini sasa mchakato wa vazi la Taifa utaweza kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa Vazi la Taifa ni mchakato ambao tayari ulikwishaanza tangu Serikali ya Awamu ya Nne ikiwa madarakani. Changamoto kubwa ambayo ilitokea katika mchakato huo ni ulipofika katika Baraza la Mawaziri na kama tunavyojua kwamba nchi yetu ni nchi ambayo ina makabila zaidi ya 120, hivyo inakuwa ni vigumu sana kuweza kujua kwamba ni vazi gani ambalo Watanzania tunaweza kulitumia kama vazi letu la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni vigumu kuweza kuamua kwamba ni vazi gani ambalo linafaa kuweza kuwa Vazi la Taifa, hivyo maamuzi ambayo yalifikiwa ni kwamba ni vema kwamba vazi la Taifa likatokana miongoni mwa mavazi ya jamii husika. Mpaka sasa hivi mchakato huo umeachwa kwa Watanzania wenyewe ili waweze kuamua kwamba ni vazi gani ambalo litawafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara tumeendelea pia kutoa taarifa mbalimbali kwenye vyombo vyahabari, lakini vilevile kwa kutumia tovuti yetu ya Wizara ili kuwapa nafasi sasa Watanzania waweze kujadili namna gani ambavyo wanadhani kwamba vazi gani ambalo litafaa kuwa ni Vazi la Taifa, lakini mpaka sasa hivi ni mchakato huo umeachwa kwa jamii yenyewe kwamba vazi litokane na jamii.

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imezungumziwa ni suala la usikivu wa *TBC* ambapo Mheshimiwa Ramo Makani Mbunge wa Tunduru Kaskazini amezungumzia tatizo la usikivu wa *TBC* eneo la Tunduru. Napenda tu kuchukua nafasi hii kuweza kumhakikishia Mheshimiwa Ramo Makani kwamba katika Wilaya ya Tunduru tayari mtambo wa *TBC* umekwishafungwa na sasa hivi maboresho yanaendelea kufanyika. Tunaamini kabisa kwamba maboresho hayo ifikapo mwezi wa Tano maboresho hayo yatakuwa yamekwishakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna tatizo pia la usikivu wa *TBC* katika Wilaya ya Lushoto ambapo Mheshimiwa Shaabani Shekilindi pia ameweza kuzungumza. Niseme kwamba katika Wilaya ya Lushoto wote tunafahamu kwamba kuna changamoto ya milima ambayo kwa namna moja au nyingine imekuwa ikiathiri mawimbi ya *TBC FM* pamoja na *TBC Taifa*. Mpaka sasa hivi ninavyoongea tayari tumeshapata eneo ambalo litatumika kufunga huo mtambo na tunaamini kabisa kufikia mwezi Mei, tatizo la usikivu wa *TBC* katika Wilaya ya Lushoto litakuwa limeshakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Machano Othman Said pia amezungumzia tatizo la usikivu Zanzibar. Nichukue nafasi hii kuweza kumhakikishia tu Mheshimiwa Machano kwamba katika bajeti hii ya mwaka 2018/2019, tayari Zanzibar imewekwa kwenye kipaumbele katika kuonesha kwamba tunaboresha usikivu wa *TBC* na siyo tu kwa Zanzibar peke yake, kuna mikoa mitano ambayo ni Mkoa wa Songwe, Mkoa wa Simiyu, Katavi pamoja na Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine pia ambayo imeibuliwa na Mheshimiwa Rhoda Kunchela ambaye amesema kwamba Serikali iweke ofisi za usajili kila mkoa kwa ajili ya wasanii kuweza kununua *sticker za TRA*. Ni kweli Mheshimiwa Rhoda kwamba mpaka sasa hivi *sticker za TRA* zinapatikana katika Mkoa mmoja tu ambao ni Mkoa wa Dar es Salaam.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tayari jitihada za makusudi zimeanza kufanyika na mpaka sasa hivi ninavyoongea Kamati ya Urasimishaji imekwishakaa na sasa hivi tunaandaa utaratibu mzuri kabisa ili kwamba *sticker* hizo hata wasanii ambao wanapatikana mikoani waweze kuzipata kwa njia ya kununua hizo *sticker* kwa njia ya mtando. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba hili litakapokamilika itakuwa ni njia mojawapo ya kutatua tatizo la usumbufu wa kuwatoa wasanii kutoka mikoani kuja kununua *sticker* hizo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge ambayo imejadiliwa ni hoja ambayo ameizungumza Mheshimiwa Peter Lijualikali ambaye amesema kwamba kama Chama cha Mapinduzi kimeshindwa kukarabati viwanja vyake ni vema viwanja hivyo vikarejeshwa Halmashauri. Mpaka sasa hivi Chama cha Mapinduzi hakijashindwa kukarabati viwanja vyake na nasema hilo nikiwa na ushahidi na uhakika kwa sababu hata ukiangalia katika Mkoa wa Singida kiwanja ambacho kinamiliwi na Chama cha Mapinduzi Kiwanja cha Namfua kimeshakarabatiwa na kipo kwenye ubora wa kisasa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Uwanja wa Sokoine Mkoa wa Mbeya ambao nao upo kwenye ukarabati. Vilevile kuna uwanja mwingine ambao pia Mheshimiwa Mbunge ameweza kuuzungumzia Uwanja wa Samora Iringa. Kwa hiyo, siyo Chama cha Mapinduzi kimeshindwa kukarabati viwanja vyake, nasi ndani ya Chama cha Mapinduzi kuna msisitizo kuhakikisha kwamba chama kinakarabati viwanja vyake, lakini ni vema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA  
MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof/Kicheko*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwashukuru Wabunge wote waliochangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ya mwaka 2018/2019 kwa kauli na maandishi. Naishukuru Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge ya Huduma ya Maendeleo ya Jamii kwa maoni na ushauri walioutoa kuptitia hotuba ya Kamati hiyo ambayo imewasilishwa mapema leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni muhimu sana kwa maendeleo ya sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Juliana Shonza kwa kuyatolea maelezo baadhi ya maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu lmechangiwa na jumla ya Waheshimiwa 41, ambapo waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa 23 na kwa kauli ni Waheshimiwa 18. Wabunge hawa 41 wamezalisha hoja na maswali 214, hivyo basi majibu na ufanuzi tutakaotoa utajikita kwenye baadhi tu ya hoja za Kamati na baadhi tu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na nitaeleza kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati ya kwanza ambayo nimeona ni muhimu kuijibu ni kwamba, lini Serikali itakamilisha uundaji wa Bodi ya Ithibati na Baraza Huru la Habari. Ningependa nieleze tu kwamba pamoja na kwamba mwaka huu wa fedha tumeshaomba fedha kwa ajili ya uanzishwaji wa Bodi ya Ithibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado mchakato huu unavihu sana vyombo vya habari vyenyewe, kwa sababu Serikali ikikimbia sana ikaanzisha Bodi ya Ithibati, ikaanzisha Baraza Huru la vyombo vya Habari, kesho tutaambiwa hilo ni baraza lenu nyie wenyewe, sisi haituhusu. Naviomba vyombo vya habari vijitokeze na vyombo vyao mbalimbali ili tuweze kukamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa la hii sheria ni

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kutaka vyombo nya habari vijendeshe vyenyewe, viwe *self governing*, tunataka tuwe na *self governing media industry* na itaunda Baraza Huru la Habari. Kutakuwa na Bodi ya Ithibati na Kamati ya Malalamiko na Mfuko wa Habari kwa ajili ya Maendeleo ya hii Tasnia. Inaitambua tasnia hii sheria mpya, kuwa ni taaluma na wana taaluma hawa wawe na sifa stahili kuanzia Diploma na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa liliopokuja hapa Bungeni, ndipo utata ukajitokeza kwamba sasa hawa waliosoma hawapo, lakini tunajua wapo wengi, ndipo kikatolewa kipindi cha miaka mitano kuruhusu Waheshimiwa ndugu zetu Waandishi wa Habari wawewe kusoma, lakini nina uhakika hata tukianza kesho Waandishi wenye *Diploma*, wenye *Degree* wako wengi sana. Nawaomba Waheshimiwa Waandishi wa Habari wenyewe wawe mstari wa mbele. Tuklunda sisi, zitaanza hizo ngonjera za kwamba hiyo ni Kamati ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilikuwa Kanuni za Sheria za Habari hazijatungwa mpaka leo. Hii ni hoja ya Kamati, lakini kwa heshima kubwa kabisa naomba kusema kwamba Wizara ilishakamilisha Kanuni za Sheria ya Habari na kanuni hizo zilichapishwa kwenye Gazeti la Serikali mwaka jana mwezi Februari tarehe tatu na zilishaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali iweke mkakati wa kuwa na Kanzidata Wataalam wote wa Kiswahili nchini ili watumike kama Wakalimani katika maeneo mbalimbali hasa mikutano ya Kimataifa. Kwenye hotuba yetu iko wazi na huu ni ubunifu mkubwa wa Wizara ambao tayari tumeshaanza kuutekeleza. Tunachotaka tu ni kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge ambao tunaelewa, baadhi yenu hapa ni mabingwa wa lugha ya Kiswahili kwa kusomea, naomba na ninyi m jitokeze kujisajili katika tovuti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwepo na suala la wizi wa kazi. Suala hili tumelifanyia kazi sana na nimelieleza

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

kwenye hotuba yangu kwamba tumefanya kaguzi mara kwa mara katika sehemu mbalimbali korofu na tumeweza kukamata kazi nyingi za sanaa ambazo zinaingia kinyemela kuweza kuumiza vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam tuna kesi tunayoisema sana ambayo tulifanikiwa kesi ya jinai namba 414 ya mwaka 2011 ambapo Mahakama ya Wilaya ya Ilala ilitoa hukumu ya kutaka kazi ambazo zilikuwa zimeingia kinyemela, zinauzwa kinyemela kuwaumiza wasanii, ziweze kuharibiwa chini ya usimamizi wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tulilipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa iliyofanyika na Mahakama kufanya uamuzi huo haraka. Kwa hiyo, tunafanya hiyo juhudu kubwa kuhakikisha kwamba wasanii hawaendelei kunyonywa. Sasa hivi tunaipitia Sheria ya Haki Miliki na nina uhakika italeta sura nzuri tu baada ya muda siyo mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwepo na suala la mapato ya Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru kwamba yasichanganywe. Kamati kwa kweli tunashukuru sana kwa hoja hii, lakini ningependa tu nisisitize pengine tupate maelekezo mengine ya wazi kabisa ya Kamati pesa yote inakusanya kwa njia ya kielektroniki. Mapato yote ya hivi viwanja na kwa sababu fedha yote hii inakwenda Mfuko Mkuu, wahusika kule wanaona kabisa hii ni Uwanja wa Taifa, hii ni Uwanja wa Uhuru kwa sababu hakuna anayeshika hela taslimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoomba tu ni kwamba kama Wizara kwa kweli tuna kifungu kimoja tu cha kukusanya mapato hayo kwa jina la Uwanja wa Taifa na *code* yake tena ni 140259, lakini kama ni muhimu sana tupate *code* ya pili itawezekana, lakini kwa kweli tunakusanya hiyo pesa lakini imetoka wapi, inaeleweka kabisa kwa mtu anayepokea kwenye Mfuko Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala kwamba uchunguzi ufanywe kuhusu fedha za Mchина, yaani kuna Wachina wanapewa fedha zinazokatwa katika kila mchezo na Bunge lako Tukufu lipewe taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja imesisitizwa sana na Kamati yangu. Ningependa nilieleze ili pengine nieleweke vizuri pole pole, kwamba katika mgawanyo wa fedha unaofanyika kwa asilimia, hakuna kipengele cha fedha ya Mchина au Wachina, sijawahi kuona mimi tangu nlingie kama kiongozi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila ninaambiwa huko nyuma kulikuwepo na utaratibu wa kuwalipa Wachina. Kuna *technical team* ipo pale uwanja wa Taifa ilikuwa inalipwa kwa kazi iliyokuwa inafanyika, ni huko nyuma, lakini sasa hivi sijaona wala Afisa Masuuli wangu Katibu Mkuu hajawahi hata siku moja akaidhinisha hela iende kwa Mchина au Wachina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishuhudie tu kitu kimoja, kwamba tukishapata mapato mgawanyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunatoa asilimia 18 ya VAT na asilimia tano ya *Selcom* ambao ndio waliokuwa *service providers*. Ikishatolewa hii kinachobaki ndio asilimia 100. Sasa mgawanyo unakuwa kama ifuatavyo:- asilimia 15 ni ya uwanja ambayo pia hatukai nayo tunaipeleka Mfuko Mkuu, asilimia tano ni ya *TFF*, asilimia 40 ni ya timu mwenyeji, asilimia 20 ni ya timu ngeni, asilimia tisa ni bodi ya ligi, asilimia saba gharama za mchezo na hizo gharama za mchezo na hiyo pesa inakwenda *TFF* huko huko, asilimia moja inaenda *BMT* na asilimia tatu *DRFA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pengine nitumie nafasi hii vile kumwelezea Mheshimiwa Kadutu, alisema sana kwamba *BMT* inapata hela nydingi hapo. Hapana si asilimia 15 ni asilimia moja tu na kwamba hiyo moja pengine tuipe *TFF* lakin *TFF* hapa wana asilimia tano kuna asilimia saba

gharama za mchezo; ndio hao *TFF*, kuna asilimia tisa bodi ya ligi; hao hao ndio *TFF*, *BMT* asilimia moja. Kwa hiyo, nafikiri nimejieleza, limeeleweka kuhusu hayo malipo ya Mchina; hayapo tena na kama yalikuwepo hapo nyuma ilikuwa ni utaratibu wa kuwalipa wale *technical team* ya kichina iliyopo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilikuwepo lingine la uwepo wa udhibiti wa mapato yatokanayo na uuzaji wa tiketi kwa njia ya kielektroniki. Nashukuru sana, hili wazo zuri, Kamati yangu kwa kweli ni makini sana. Wizara kwa kutambua umuhimu wa kudhibiti mapato imeshakamilisha mchakato ulio wazi wa kumpata mtoa huduma ya kukusanya mapato kwa mfumo wa kielektroniki katika uwanja wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huo tutauunganisha na mfumo wa Serikali wa ukusanyaji mapato (*Government Payment Gateway System*) ili kuimarisha udhibiti wa mapato. Hili tunaahidi na nadhani tutakapokutana na Kamati tena wataona hicho kimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa maandalizi mazuri ya Timu ya Taifa ili ziweze kushiriki kikamilifu kwenye mashindano na kurudi na ushindi. Waheshimiwa Wabunge wengi sana nitashindwa wengine kuwataja, wengi kwa maandishi na kwa kuongea hapa, wamelalamikia sana hilo na kwamba Serikali ipo ipo tu, hatufanyi chochote kuhusu hizi timu zinaenda tu; hiyo si picha ya kweli. Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Sima na Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea hilo na wametoa na mfano vilevile kuhusu timu yetu ilipokwenda Australia kwenye Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba ukichukulia michezo iliyokwisha juzi ya riadha, ndondi na michezo mingine Australia, wawakilishi wetu waliandaliwa vizuri, hivyo naomba niwasitizie hilo na tumeiandaa sisi Serikali. Tulipewa

nafasi 34 lakini tukaamua sisi wenyewe kwa ajili ya kujali viwango waende 22 tu. Kushindwa kupata medali ni kawaida ya mchezo, asiyekubali kushindwa si mshindani. Tulishindwa na timu ambazo zilijiandaa vizuri kutupita sisi, lakini tulijiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano wa timu ya *table tennis*. Ilikuwa na wachezaji wanne; watoto wa kike wawili na watoto wa kiume wawili, wazuri sana. Wamefanya mazoezi hapa nyumbani, tukawapeleka China ambako kuna mabingwa wazuri sana wa *table tennis*, wamekaa China kufanya mazoezi kwa siku 80. Jamani kama Serikali tufanye nini zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewapeleka wameenda wamerudi, wameenda huko Australia; na watoto hawa wamecheza vizuri wameenda *round* ya kwanza, ya plii, *round* ya tatu ndiyo wameondolewa. Tusiwalauku, tusiwakatishe tamaa kwa kauli zinazotoka kwenye hili Bunge kwamba tulipeleka vilaza kule. Hapana ni vijana waliokuwa wameandaliwa vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mwanariadha mmoja wa mbio, Ally Gullam nafikiri kutoka Zanzibar, ambaye mbali na mazoezi hapa nchini ilibidi tumpeleke Brunei kwenda kufanya mazoezi ya ziada chini ya mwanariadha maarufu nchini hapa Suleiman Nyambui. Suleiman Nyambui sasa hivi ni kocha wa Taifa wa riadha wa hilo taifa la Brunei. Kafanya mazoezi huko, kijana wetu amejitahidi ameshindwa. Nina uhakika tutaendelea kufanya hivyo huyu bwana mdogo hatimaye atashinda, *practice makes perfect*. Tutaendelea kufanya mazoezi, atashinda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanariadha wetu wa mbio za *marathon*, bwana Said Makula nafikiri wote mlimuangalia. Mimi nilikuwa naangalia sana pale amekuwa wa tatu mpaka kilometra 41 *marathon*, tumepata sasa na sisi *bronze*, akaanguka. Amemaliza kilometra 41, kabakiza tu kilometra 42.2 akaanguka bahati mbaya. Akakimbizwa hospitali kuangalia *oxygen* ilikuwa imepungua kichwani.

Hakuanguka peke yake, walianguka wengi wa Ireland na kadhalika kutohana na *attitude* ya sehemu hiyo. Kwa hiyo, ni kijana alijitahidi, tulikuwa tuwe namba tatu pale lakini sijui shetani gani aliingia pale, basi kijana wetu akaanguka akakimbizwa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwagine Kassim Mbwana aliyejewa tegemeo letu kubwa sana kwenye *boxing* na alisema anaahidi kwamba akifika atatuletea *gold*. Amefika kule bahati mbaya sana wenzake wote waliokwenda kule Kenya, Uganda na *South Africa* wakapewa wapiganaji wa ajabu ajabu huko; yeye peke yake mchezo wa kwanza akapewa apambane na bingwa wa *Commonwealth* ambaye alipata dhahabu mchezo uliopita na huyo kijana ana *silver* ya *Olympic*, ni bingwa kutoka India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wakasema ni maafa wengine wakaanza kusema jitoe wewe cheza cheza kidogo tu ukimbie lakini yule kijana amecheza mpaka *round* ya mwisho, ametolewa kwa *point* za Majaji. Yule mshindi amepata Majaji watatu wa kwetu amepata Majaji wawili. Anastahili pongozi za hili Bunge badala ya kuwakatisha tamaa hawa vijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa sababu wamelalamika sana Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme zaidi hapo. Hata soka la Tanzania linapanda, soka linapanda. Mimi naona kabisa kuna maendeleo makubwa. Msisahau *Serengeti Boys* mwaka jana ilituinua kwenye viti hapa Watanzania, ilifuta mkosi wa nchi hii, miaka 37 hatuendi hata *semifinals* za *AFCON*. Hawa vijana wameenda fainali za *AFCON* mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu angalia dozi wanayotoa kwa timu, sita bila, Serengeti hao; sasa hivi ni mafanikio tu. Kwa kweli tuwape nguvu hawa vijana; kwa sababu tumegundua kwamba kufanikiwa katika michezo ni mazoezi na kuwekeza. Hakuna tena kwenda sijui wapi mkachezeshe usiku na hirizi, hamna. Ni mazoezi tu na ndio maana tunafanikiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimbie tu kueleza vile vile kwamba pengine Wizara mwaka huu itaongeza zaidi kampeni ya kueleza mafanikio yetu. Kwa mfano mwaka jana tulifanya vizuri sana, katika riadha. Ukimwacha mwanariadha wetu huyu Simbu ambaye alipata medali ya shaba *London Marathon* mwaka jana, lakini tulikuwa na kijana ambaye nimeona *ni-note* hapa niwaeleze Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kuna kijana anaitwa Cecilia Panga, ambaye *Beijing International Marathon* alipata *gold medal*. Ni binti, sawa yupo jeshini lakini ndiye aliyetuletea Tanzania hiyo *gold medal*. Kuna binti mwingine Madgalena Shauri alikuwa wa tano *Hamburg Marathon* ambayo ilihusisha wakimbiaji 25,000. Ukiwa wa tano hapo lazima ushikwe mkono kusema kijana umefanya vizuri. Tulikuwa na mwingine Emmanuel Giliki Gesamuda alipata *gold medal Shanghai International Marathon*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushindi wote huu tunapata lakini huwa tunakaa kimya, safari hii sikai kimya itabidi tu tupige *sound* sana hapa tunapopata mafanikio yoyote. Hii ni kwa sababu tukikaa kimya tutaonekana kwamba hakuna kinachofanyika, mengi yanafanyika na yote ni juhudhi ya Serikali si kama, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja anasema kwamba hiyo ni juhudhi binafsi, hapana. Juhudi binafsi gani, Serikali ndio ina-create hiyo *enabling environment* tunafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya kufufua vyuo vya michezo nchini ili viweze kuendelea kutoa mafunzo kwa Walimu wa michezo. Vyuo vya Ualimu vya shahada na stahada ya elimu ya michezo na sanaa viro chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tunaongea vizuri sana na Wizara ya Elimu na Mheshimiwa Waziri kuhusu kuvirejesha angalau tuenze polepole baadhi ya vyuo sasa viendelee na ile mitaala ya nyuma ya michezo na sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa kuwa *very proactive* na tayari tumeshakaa mara ya kwanza, wanaendelea wataalam wetu kuliangalia hili suala kwa undani. Wizara ya Habari sisi tuna chuo pekee cha Maendeleo ya Michezo, Malya kinachotoa stashahada ya michezo katika nyanja za uongozi na utawala katika michezo, elimu ya ufundishaji michezo na elimu kwa michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tu Mheshimiwa Waziri wa Elimu aliposikia ametajwa kuhusu chuo hiki ambacho wala hakisimamii, lakini tayari amesema kuna umuhimu sana watendaji wetu wakae chini waangalie hiki chuo kama Wizara ya Elimu nayo ifanye nini. Kwa hiyo, yote haya ni maendeleo makubwa na nina uhakika tutafika mbali sana katika ushirikiano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nydingine, iliyotolewa na Mheshimiwa Silafu Maufi kwamba kwa nini bajeti ya Wizara imeshuka sana na vilevile Kamati yangu ya Bunge nayo imeongelea hivyo hivyo. Naomba niseme hapana. Nafikiri pengine ilikuwa ni makosa tu ya kuandika kwa sababu Kamati hii ya Kudumu ya Bunge imenisaidia sana, imeisaidia sana Wizara kupata bajeti kubwa zaidi. Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 ni shilingi bilioni 33.35 ikilinganishwa na ya mwaka jana iliyokuwa shilingi billioni 28.21, ni ongezeko kubwa, ongezeko la asilimia kumi na nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilikuwepo suala pia ambalo ameuliza Mheshimiwa Maufi kwamba sababu za bajeti ya mishahara ya Wizara kupungua. Nimewaelezea kwa kirefu kwenye hotuba yangu ukurasa wa 14 kwamba sababu ni kuhama kwa Idara ya Maendeleo ya Vijana kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado watu wengi wanadhani Idara ya Vijana ipo Wizara ya Habari, hapana imeenda Ofisi ya Waziri Mkuu. Kutokana na kuhama kwa ile

idara ambayo ilikuwa kubwa ndiyo maana kumetokea kitu kama hicho. Vile vile kuna mambo mengine pia ya vyeti feki na wengi wametoka kwa hiyo lazima mishahara itaonesha upungufu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chaneli ya Bunge ionekane mubashara kwenye chaneli zote. Hii hoja ni ya Mheshimiwa Devotha Minja na imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wengi tu, lakini kwa ajili ya muda nashindwa kupanga majina sasa hivi hapa. Ningombu tu nisitizie kwamba wahusika wa hii Chaneli ya Bunge ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nina uhakika anayehusika zaidi hapa ni Spika si mimi, kwa sababu ndio anayesimamia hiyo chaneli, ni ya kwake, ni ya Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Mbunge akihoji kukosoa Serikali baadhi ya taarifa zinahaririwa na kutoonekana kwenye chaneli hiyo wakati zinaonekana kwenye *hansard*. Lah! Hii ni tuhuma nzito sana Mheshimiwa Devotha Minja, hili haliko kwangu, vile vile bado linalekezwa kwa Mheshimiwa Spika ninyi ndio mwenye *hansard* na hiyo Chaneli ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini magazeti yanjasajiliwa upya kila mwaka. Nataka niseme tu kwa kifupi sana kwamba chini ya Sheria mpya ya Magazeti, Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016, kwa kweli magazeti husajiliwa mara moja tu na kupewa leseni ya uchapishaji kila mwaka. Pengine alikuwa ana maana hiyo kwamba leseni ya uchapishaji kwa nini iwe kila mwaka. Sheria hii ilipitishwa na Bunge hili Tukufu kwa lengo la kuimarisha sekta ya habari na kuondoa ubabaishaji uliokuwepo. Kuna watu walikuwa wanakaa tu na vichwa vyaa majina ya magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilibidi Mkurugenzi wa Maelezo mwaka jana afute vichwa vyaa magazeti 200, vimekaa tu ooh "Mwakyembe Leo" sijui 'Devotha Kesho' yaani jina tu la gazeti liko pale wakati halina kazi. Ndiyo

maana tunasema kwamba kuonyesha upo *live* na uko *serious*, si kwamba inatokea *opportunity* imetokea sasa nafasi uanze kuandika mambo yako kumshambulia mtu ndio unaanzisha hilo gazeti, unaanza kulifanyia kazi. Ndio maana tukasema hapana kama upo *serious* basi hata kama ada ni ndogo lakini kila mwaka ulipe, lakini leseni unabaki nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kwa nini vyombo vya habari vinavyokosoa Serikali vinafungiwa, Serikali ingalie upya suala la kufungia magazeti. Ukweli kwa heshima na taadhima, hili suala limeulizwa vilevile na Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani. Sheria ya Huduma za Habari imeeleza wazi makosa yanayostahili kupewa adhabu iwapo vyombo vya habari vitakiuka sheria hiyo. Vyombo vya habari vinavyofungiwa vimekiuka sheria na ni pale ambapo suala la usalama wa nchi limeguswa. Hata Dkt. Ally Yusuph anasema Serikali isifungie magazeti na radio, Waziri avilee vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa. Nataka nimweleze kwamba tunawalea vizuri waandishi wa habari kwa sababu hatujawahi hata siku moja kuchukua hatua bila kukaa na vyombo vya habari mara tano, sita, saba; ndugu zetu angalieni hiki sio sahihi. Kulikuwepo na aina fulani ya fikra katika nchi yetu kwamba uhuru unaweza ukawa usiwe na mipaka. Sasa hao tunaona sasa wamezidi kiasi lazima sasa tuwafundishe kwa kuwafungia kwa muda na wengi wanaporudi wanaenda vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kulea vile vile tunapeleka waandishi wa habari nje ya nchi kwenda kusoma. Kwa mfano mwaka jana tumepeleka vijana 10 China waandishi wa habari, wawili kutoka Serikali na wanane kutoka *private media*, kwenye hilo hatufanyi kabisa upendeleo. Mwaka huu tumeshapata nafasi za masomo China na Sweden na nawahakikishia tutakuwa na waandishi wa habari wa vyombo binafsi wengi zaidi kupita wa Serikali kwa sababu wote wanatimiza lengo kubwa la kikatiba la kuhabarisha umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Devotha Minja vile vile na Mheshimiwa Lucy Owenya wanasema kwa nini Serikali haitoi tamko pale waandishi wanapotekwa na wengine kupotea. Lah! Sasa Mheshimiwa Minja ananipa mtihani mgumu sana na ametoa mfano kwa mfano mwandishi wa *Guardian*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwa mfano huu alioutoa wa mwandishi wa *Guardian*; hebu naomba yeye mwenyewe aulizie vizuri alikuwa wapi maana nisingependa mimi kuwa sasa chanzo cha kuharibia majina watu hapa. Yeye mwenyewe aulizie alikuwa wapi, atapata majibu tu huko *Guardian* maana yupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana tumefika kipindi ambacho kuna watu wengine wanajiteka wenyewe. Sasa mimi Waziri mzima nikakurupuka kutoa *statement* wakati suala lenyewe ni la jinai linahusu polisi, nafikiri polisi wakishapeleze basi na sisi tunaweza tukatoa kauli. Tunaheshimu na kuthamini sana waandishi wetu, mchango wao ni mkubwa katika maendeleo ya Taifa hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, anasema Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa *TBC* na Maafisa Habari wa Idara ya Habari Maelezo. Mheshimiwa Lubeleje, kaka yangu namheshimu sana, namshukuru sana kwa mapenzi makubwa aliyonayo kwa waandishi wa habari wa *TBC* na wengine wa Idara ya Habari Maelezo. Nadhani tuwe wakweli; watumishi wa Idara ya Habari Maelezo, watumishi wa *TBC*, hawa ni waajiriwa wa Serikali ambao maslahi yao huboreshwa sambamba na watumishi wengine wa Serikali. Mimi sioni kama wana matatizo makubwa hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwe mkweli na nilishashutumiwa sana katika Bunge hili kwa kusema ukweli, kwamba watu ambao ni wa kuwaonea huruma ni waandishi wa habari ambao wako kwenye vyombo binafsi.

Kuna waandishi wanapata, si kima cha chini, ni chini ya kima cha chini cha mshahara, ni mishahara ya kitumwa wanayopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili, mwandishi wa habari abishe aende nyumbani kwake mke wake atamkuta amekasirika kwa sababu nyumbani hajaacha kitu. Hakuna mkatuba wa kazi, vijana wangu wanachezewa sana, hawawekewi bima, hakuna kuwekewa pesa kwenye Mifuko ya Jamii; ndiyo maana sheria hii mpya, nawaomba waandishi wa habari jitokezeni mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoogopa sisi tukiunda *Media Council* hapa watasema ni ya kwetu Serikali; waunde *Media Council* yao tutawasaidia. Chini ya sheria hii wana uhakika wa kuwa na ajira inayowalinda wao wenyewe. Waandishi wa habari wengi hawalewi wanapiga kelele ya wamiliki, ndiyo shida hiyo tuliyonayo. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lijualikali anasema kuna ubaguzi mkubwa katika kutoa adhabu katika baadhi ya magazeti, magazeti mengine yanafungiwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari, kama nilivyo sema, kuna namna mbili za utoaji wa adhabu; kama kosa linaathiri usalama wa Taifa kwa kuihusisha Serikali au viongozi wa kitaifa ambao hawawezi kujitetea, Waziri anaweza kutumia kifungu cha 59 cha sheria dhidi ya gazeti husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni mtu binafsi, akidhalilishwa na gazeti hiyo ni kesi ya kudhalilishwa, ni kesi ya *defamation*, anaweza kulalamika Idara ya Habari Maelezo ili hatua za kimaadili zichukuliwe, lakini vile vile anaweza kabisa kwenda mahakamani kupitia kifungu cha 41 cha sheria kudai fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa si Maelezo wala Wizara ambayo imepokea malalamiko rasmi ya viongozi au mtu ye yote kunyanyaswa na gazeti tusichukue hatua. Tulipata kesi moja ya gazeti moja linasemwa sana hapa, tuliwaita

Wahariri, tumewaandikia onyo la mwisho lakini haikuwa onyo kwamba wametishia kitu chochote, walimchafua mwenzao kwamba utapelekwa mahakamani na hii ni kinyume cha maadili; huo wajibu tunaufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usikivu wa *TBC* Nkasi Kusini, kandokando ya Ziwa Nyasa; namwomba Mheshimiwa Desderius John Mpata kuwa ndugu yangu akae mkao wa usikivu mzuri tu kwa sababu katika bajeti tuliyoweka sasa hivi tunaweka *transmitter* mpya Mbeya, *transmitter* mpya Dodoma, lakini vilevile namhakikishia kwamba katika bajeti hii inayokuja eneo lake pia lipo kati ya maeneo ambayo tumeyapa kipaumbele, ikiwemo Zanzibar na Simiyu vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usikivu wa Redio Zanzibar, Mheshimiwa Machano Othman; kama nilivyo sema katika bajeti ya mwaka huu ambayo naomba aipitishe leo Mheshimiwa Machano Othman, tuna Zanzibar, Songwe, Simiyu, Njombe, Katavi kuweza kuyafikia na nina uhakika tutayafikia. Tumeshapata uzoefu wa maeneo tuliyopitia sasa hivi; Rombo, Kibondo, Nyasa, Longido na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusajiliwa na kulipwa tozo kwa blogu; Mheshimiwa Devota amelalamikia kuhusu suala la kulipa tozo kwa blogu mbalimbali kwamba tunaonea; lakini si yeye tu, Waheshimiwa Wabunge wengi wamelalamikia sana hizi kanuni mpya tulizo zitoa. Nataka nitoe taarifa tu kwamba wakati humu sisi tunaongea, taarifa nimeipata dakika kumi zilizopita kwamba usajili wa watoa huduma za maudhui mtandaoni, maombi tuliyopokea mpaka sasa ni 86 na tumesha-*approve* moja ambayo vigezo vyote vimekamilika. Wengine wanaendelea kusaidiwa, kuelekezwa ili warekebishe karatasi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumechukua hatua hiyo? Waheshimiwa Wabunge naomba kwa sababu ninyi ndio wawakilishi wa wananchi, vyombo hivi sasa duniani vinabeba nafasi sawa na vyombo rasmi vya habari katika kuhabarisha. Nina uhakika ndani ya mwaka mmoja, miwili,

mitatu ijayo, vitakuwa vyombo vikubwa zaidi nya kuhabarisha kuliko hata vyombo rasmi tulivyonavyo kama *TV*, magazeti na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu Tanzania vyombo hivi; blogu, majukwaa mitandaoni, redio na *TV* mtandaoni vimeanza pole pole kuwa vyombo muhimu na vikubwa nya kuhabarisha na kuhabarishana na kutaarifu na kutaarifiana. Leo hii itisha *press conference* Mheshimiwa Mbunge, vyombo vitakavyokuwa mbele yako pale, vyombo rasmi vitakuwa vinne, lakini utashangaa *microphones* mara nne ya pale au mara tatu, mara mbili ni vyombo hivi nya kimtandao. Vimeanza kuwa ni vikubwa, vimeanza kuwa ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba tofauti na wenzao wale wachache, hawana utambulisho rasmi kuwa ni wanahabari, hilo la kwanza. Hawana miiko wala masharti rasmi ya kazi, wao ilimradi kimetoka, wapo pale wanachukua habari. Hawabanwi na maadili yoyote katika kazi wanayofanya; hawalipi kodi pamoja na kwamba wanashindana na vyombo rasmi vinavyolipa kodi kugombea matangazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, tuwe *fair, let us be fair*. Tunachokifanya sisi sio peke yetu, tumefanya utafiti nchi nyingi zimefanya hivyo na lazima tuwahi, tusije tukajikuta tumetengeneza dude kubwa likatushinda mbele ya safari. Watu wengi siku hizi ndugu zangu, si Tanzania tu, wanaweza akakaa siku moja, mbili, tatu, hata wiki nzima hajasoma gazeti wala hajaangalia *TV*, yeye yuko bize na *twitter*, anaangalia tu kuna nini kwenye *instagram*, kuna nini kwenye mitandao, inamtosha, imemhabarisha, sasa hivi ndiyo imeendelea hiyo *trends*sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vyombo vina changamoto kubwa vile vile, vimeduwa sasa *mainstream* katika kuhabarisha umma, lazima viwe na maadili, viwe na miiko. Sababu, tatizo kubwa la vyombo nya mitandaoni ni *fake news*, kama wanavyosema Wamarekani, ni taarifa za

upotoshaji, za uongo, kwa sababu hao watu wamechukua, ni kikundi tu cha kuongea, unaongea unachotaka, lakini kuna watu wanachukulia kwa nguvu sana kwamba ni ukweli. Kuna nchi zimekaribia kwenda vitani kwa ajili ya taarifa *fake*, taarifa za uongo katika vyombo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, na kwa mujibu wa taarifa ya mwaka 2017 ya *Freedom House*, wote mnajua hiyo; ni chombo cha wanaharakati wa kidemokrasia, wanasema asilimia 75 ya nchi duniani zote zimechukua hatua kudhibiti maudhui katika mitandao; lazima zidhibiti. Wao wanasema wanalinda watoto, sisi ndio hatuna watoto? Nasi tuna watoto. Kwa hiyo na sisi tumesukumwa na sababu hizo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine upande wa Tanzania ni hitaji la wanahabari mitandaoni kutaka nao watambuliwe kama wanahabari. Imetoka wakati amekuja Rais wa *FIFA* hapa, Infantino, anataka waandishi wa habari 20 tu wenye *press cards*, hawa hawana. Wakasema, Waziri tunataka na sisi tutambuliwe, tukasema lakini ninyi sijui ni watu gani, sijui na ninyi ni waandishi, nao wanataka watambuliwe kama ni *formal media institutions*. Sasa tulichokifanya ni hicho, ni kuwaweka nao kuwa wanatambuliwa kama wanahabari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii uksoma taarifa ya *Reporters Without Borders*, nao ni wanaharakati wa demokrasia hawa, wanataja nchi nyingi ambazo zimeweka masharti katika kutumia mitandao. Nchi nyingi ambazo ni kongwe kidemokrasia zimo humo; Marekani, Australia, Uingereza, Canada, India na kadhalika, ambao hoja yao kuu ni kuwalinda watoto. Sasa sisi hatuna watoto jamani, sisi ndio hatuna watoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi Tanzania tuna wajibu wa kuweka mazingira ya matumizi salama ya mitandao ama sivyo, kama nilivyosema kwenye kitabu changu, ukurasa wa 64, teknolojia badala ya kuitumia, itatutumia na ni madhara makubwa sana mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu vyombo hivi vinafanya kazi ya Kikatiba ndiyo maana kwa kweli tumesema tuchukue hatua. hivyo basi, kanuni zetu zinatambua kazi yao, hawa wenzetu wa blogu na kadhalika na zinawaingiza kwenye mfumo ule ule wa maadili wa vyombo vingine vya habari na kama kuna tatizo tuongee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye mitandao ni kwamba tunawatoza dola 925 kwa mwaka, hapana, kiingilio ni shilingi laki moja. Sema muda sina, lakini naweza kuonesha tunavyowatoza wale wenye vyombo vyenyewe vilivyokaa, wao tunawatoza shilingi laki moja, lakini vyombo rasmi tunavitoza, kama *TV*kweli iko pale, ni dola 5,000, hawa laki moja, wengine dola 5,000. Sasa tufike tu-*argue* lakini tukiwa na *facts* tayari. Baadaye nikiulizwa nitatoa, ninazo hizo *figures* tayari lakini nikizitoa sasa hivi nitatumia muda mrefu mno na nafikiri sasa hivi nitapigwa kengele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naambiwa fungiafungia kwa wasanii, msanii mzuri, anafanya kazi nzuri, akikosea mnampfungia. Mimi nashindwa kuelewa, hivi tungefungia wasanii 20, nafikiri hii nchi ingepasuka. Sisi ni walezi, kama wenzetu ni walezi ninyi ndani ya nyumba, mtoto anakosea unamuimbia nyimbo kumsifu, sisi wengine ni walezi ambao mtoto akikosea lazima ajue kwamba kuna adhabu. Kwa sababu wengine wataendelea kufanya hivyo na hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri hapa; tuna utaratibu mzuri sana kisheria, usitoe wimbo wowote bila kwanza kupata *opinion*, ushauri wa BASATA, BASATA ni walezi; hakuna anayefanya. Nchi hii imezoea, utii wa sheria bila shuruti ni kitu cha ajabu, siku hizi imekuwa yaani lazima mtu afanye anavyotaka. Sasa tukiingia kwenye sheria maneno yanaweza kuwa mengi sana. Hakuna mtu tuliyemfungia tukasema wewe sasa sio msanii tena, tunataka vijana waelewe wana wajibu kwa hii jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Amina Mollel ameeleza hapa, jana amenionesha picha ya ajabu

sana inazunguka kwenye mitandao. Wako kwenye steji jamaa anatoza pesa nydingi, laki mbili watu kuingia mle ndani lakini mule wanaitwa watu wasimame wavue nguo, mengine siwezi kusema, hii ni *TV*, lakini hayo mambo hatuwezi kukubali nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuja hapa na kitu *very controversial* tunakifanya utafiti ndani ya Wizara yangu. Wenye pesa Ulaya wengi ni mashoga, wameanzisha *foundations*, yametawanywa kila nchi Afrika. Sasa hivi Tanzania tumekuwa *earmarked* kama kitovu kizuri cha kuwa ndiyo *centre* ya huduma za mashoga katika Bara la Afrika, hatuwezi kukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upuuzi huu upitie kwenye mitandao, usipitie kwenye mitandao sisi tutadhibiti; wakubwa wakasirike, wasikasirike, hili ni Taifa letu lina maadili yake na utamaduni wake. Mwalimu alisema; sitasahau hilo; Taifa lisilo na utamaduni wake ni taifa mfu na sisi sio taifa mfu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la visimbazi, imetoka kwa Mheshimiwa Chumi, kwamba ni kwa nini havioneshi hizi *TV stations* zetu tano, sita, saba ambazo ni *Free to Air*. Hili suala liko Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa harakaharaka, naona kengele ya kwanza imelia. Mheshimiwa Shekilindi amesema Serikali iwasimamie wasanii wasidhulumiwe. Kwa kweli dhuluma ilikuwepo kubwa sana kwa kutumia *middlemen*, watu wenye pesa wamewachezea sana wasanii wetu Tanzania. Hili limeanza kubadilika, tumeanza kuwa-*empower* wasanii wetu kwa kutumia TEHAMA, wasitumie *middlemen*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msome kitabu change nimeeleza vizuri njia tulizotumia, lakini wachukulie vijana wazuri kama akina marehemu Kanumba, amefariki Kanumba kila mtu anajua ni milionea, hapana, waliotajirika ni wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mwanasanaa mzuri mzee Majuto anaumwa, anaomba pesa mimi nachanga kutoka mfukoni. Leo hii nusu ya mabango ya biashara ni ya Majuto, matangazo ya biashara kwenye *TV* ni Majuto. Naomba sasa nitumie nafasi hii kusema nimeunda Kamati ya Wanasheria, tunaanza na kesi ya mzee Majuto. Mashirika yote, kampuni zote zilizoingia mkataba na Majuto tutapitia hiyo mikataba kama ameonewa lazima ilipwe familia yake; tumeshachoka. Tukishamaliza Majuto tutarudi kwa Kanumba, na msanii ye yeyote ambaye anaona aliingia mkataba wa kipumbavu aje atuone. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaudhi lakini ndiyo hivyo. Leo mzee yuko hospitali anakosa shilingi laki tano, mimi Waziri nitume, pesa yenye we ndiyo hiyo mnaelewa maisha yalivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja tu nitakalolaumiwa na wananchi, kwamba Mheshimiwa Amina Mollel amesema kuna Mtanzania aliyetoroka kambi. Ni kweli kabisa, tume pata aibu, kati ya vijana wetu waliokwenda Australia kwenye mashindano ya *Commonwealth* mmoja amejongo huko, amepotea huko, hakurudi na jina lake kweli kama alivyosema Mheshimiwa Amina Mollel, ni Fatihya Hassan Pazi wa Ukonga, Dar es Salaam, ambaye alikuwa mmoja wa wachezaji wetu wa *table tennis*, mzuri sana katika *table tennis*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimpeleka China kama nilivyosema siku themanini kuimarisha kazi yake na walifanya kazi nzuri sana, baada ya kumaliza mchezo tarehe 11, Aprili, tarehe 12 hakuonekana. Kiongozi wetu, Dkt. Singo ambaye alikuwa nao alijua kabisa huyu hajapata ajali maana alikuwa ametoatoa nguo zake zote safi akaacha tu traksuti mle ndani, na vile vile jana yake alikuwa amenunua pia na *sim card* ya kule, kwa hiyo ilikuwa ni maandalizi tu ya kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini alivyokwenda polisi kuripoti akakutana na wenzetu wa Kenya wakisema nao wawili wamepotea; Uganda nao wawili wamepotea. Aliyekuja ameinamisha shingo kabisa alikuwa ni mtu kutoka

Cameroon, wanane walikuwa wameondoka kwenye kambi yake. Tumesharipoti hili suala mambo ya nje na uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hujajibu hoja ya mwanaume mashine. (*Kicheko/Makofii*)

Hoja imeungwa mkono. Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kif 1001 – *Adm. and HR Management.....Sh.4,053,953,000/=*

**MWENYEKITI:** Haya, tuko katika mshahara wa Waziri, nina majina hapa ya CHADEMA na nina majina ya CCM. Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

**MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupewa nafasi hii. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini nasikitika sana. Nina hoja kama tano nimejibowi hoja moja tu na Naibu Waziri, ya *TBC* ya bilioni tano; Malya sikujibowi amepita kama upепo, *TOC* hakunijibu, Sera ya Michezo hajasema. Sasa nina moja ambalo nataka majibu yake na hii akikataa kujibu vizuri tutaenda mpaka mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza; nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Kuna Maafisa Utamaduni wangapi ndani ya ajira 52,000 katika nchi hii ambao wametengewa

nafasi hiyo? Kuna Maafisa Michezo wangapi katika ajira hizo? Kwa sababu ndani ya halmashauri zetu zote nchini kunatakiwa kuwa na Afisa Utamaduni na Afisa Michezo. Naomba majibu yangu. Hivi vingine nimesamehe kwa sababu namheshimu, lakini hapo nataka majibu sahihi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Abdallah Bulembo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nisamehe sana, nimesema toka mwanzoni kwamba tumepata hapa hoja zaidi ya 211, sasa hatuwezi tukajibu zote za kwake peke yake, kama amejibiwa moja ana bahati sana. Kwa sababu kuna Waheshimiwa Wabunge wengi na ni kutokana na muda tu wakitaka twende mpaka kesho asubuhi nitajibu yote.

Mheshimiwa Mwewayekiti, hata hivyo Maafisa Utamaduni wote na Maafisa wa Michezo wote wako chini ya ajira ya TAMISEMI, sisi tunawasimamia wao kisera. Ni ajira ya TAMISEMI na ndiyo maana nilikuwa nachungulia kama Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pengine lingekuwa swali maalum kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tuna ushirikiano mzuri sana kati ya TAMISEMI na Wizara yangu; na siwezi sasa hivi nikasema; maana kuna mapengo mengi sana upande wa Wilaya nimeyagundua nikafanya ziara upande wa Maafisa Michezo na Maafisa Utamaduni lakini kama nilivoyosema Maafisa hao wa Utamaduni wako chini ya ajira ya TAMISEMI sio Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa, Michezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ALHAJI A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu nilionao wa kawaida, hii Serikali si ni moja? Serikali ni moja, majibu haya hayawezi, katika eneo hili nataka majibu, kwa sababu halmashauri ziko zaidi ya 185, Maafisa Utamaduni wako wangapi, tunawekezaje kwenye michezo Maafisa Vijana wako wangapi? Mzee

Mkuchika alikuwepo pale, nikasema ndani ya 52 nataka niambiwe nafasi za Maafisa Utamaduni ni ngapi na Maafisa Michezo ni wangapi. Sasa kama Serikali haiwezi kunipa majibu na mimi ni Serikali fulani, lakini nataka kuondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri, nataka majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa Mheshimiwa Bulembo kwa sababu kiukubwa zaidi hoja yake imelenga namna ya kuhakikisha nchi inafanyaje katika haraka za michezo kwa kujuu kwamba ajira nydingi zinapatikana huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili ni kwamba tuna jumla ya halmashauri 185 ukijumlisha Jiji la Dar es Salam; lakini halmashauri nyingine ziko 184. Bahati nzuri tuna Maafisa Utamaduni katika kila mkoa na katika kila halmashauri. Inawezekana kwamba tuna upungufu, kwamba idadi inawezekana haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwa *ratio* tuliyo nayo hivi sasa halmashauri zote 185 zina Maafisa Utamaduni ambao wanahudumu katika maeneo hayo. Kikubwa zaidi ni juu ya changamoto; kwamba tufanyeje ili kuweza kuhakikisha tunaongeza idadi yao kwa kadri iwezekanavyo ili kwamba weledi wa michezo unapatikana.

Mheshimiwa mwenyekiti, hata hivyo, nataka nimhakikishe Mheshimiwa Bulembo kwamba mwaka huu 2018 tuliweza kukutana nao mara mbili. Juzi juzi nilikutana nao wakati tukiwa na wenzetu wa *Coca Cola* katika uzinduzi wa ugawaji wa vifaa vyta michezo ya UMISETA katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niMhakikishie kwamba hawa maafisa tunao, changamoto kubwa jinsi

gani tutafanya ya kuwawezesha kuwa na weledi mpya zaidi ili kazi zao wazifanye vizuri kwa ajili ya kuhakikisha Taifa letu linakwenda mbele katika suala zima la michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulembo nafikiri majibu sahihi.

**MHE. ALHAJI A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa Mwanasimba mwezangu nimekubali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hapo ndiyo huwa naipenda Serikali, majibu yao ni *perfect*, Mheshimiwa Munde, hayupo, Mheshimiwa Devota Minja.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama sitaridhika na majibu ya Waziri ifahamike wazi kabisa kwamba nitaendelea kuishikilia shilingi. Tukisoma katika katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya (18), nanukuu:-

*"18. kila mtu-*

- (a) *ana uhuru wa kuwa na maoni ya kueleza fikra zake;*
- (b) *anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila kujali mipaka ya nchi;*
- (c) *anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki na kutoquingiliwa katika mawasiliano yake; na*
- (d) *anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni baada ya Serikali kutunga hii Sheria Huduma za Habari ambapo kusajili magazeti ipo kwa mujibu wa sheria; lakini Serikali imekuwa

na mkakati mwingine eti wa kutoa leseni upya kwa vyombo  
vya habari kila mwaka. Jambo hili linakwenda kinyume  
kabisa na Katiba yetu, linaendelea kutoa usumbufu kwa  
wamiliki na waandishi wa magazeti na redio na mitando  
mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona mkakati huu  
ni madhubuti kwa ajili kufunga midomo ya vyombo  
vya habari, kwamba kama hawataandika habari za kuisifu  
Serikali basi baada ya mwaka leseni zao hawatakuwa na  
fursa ya *ku-renew* naomba ufanuzi kwenye jambo hili.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI, NA  
MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu  
Mheshimiwa Devota Minja swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu tunaoufuata ni  
utaratibu ambao unatumika hata upande wa *radio* na  
*television* na vyombo vingine; kwamba unapopewa leseni  
ile ya mwanzo hiyo ni leseni ya kudumu. Lakini kila mwaka  
lazima tuwe na uhakika kama utaitumia hiyo leseni. Kwa  
sababu tumekuwa na uzoefu sisi hapa kwamba gazeti  
linasajiliwa Nuru ya Kesho, kwa mfano, lakini litakaa bila  
kuchapishwa kwa miaka kumi lakini tunajua tuna magazeti  
500 Tanzania. Mwaka jana 2017 Mkurugenzi wa Habari  
imebidi afute magazeti 200, yalikuwa yamekaa tu stoo  
namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanakuja wenye nia  
njema kutumia hilo jina wanaambiwa hapana hilo kuna  
gazeti sasa. Vile vile tumekuja kugundua kuna nia moja  
ambayo si nzuri, wanaokusanya idadi kubwa ya majina ya  
magazeti na kuyasajili, wanasubiri fursa za kisiasa fursa zingine  
tu, anapopata hiyo fursa sasa aweze kumsema mtu fulani  
au kuwashambulia wengine basi hapo anachomoa. Nami  
nawafahamu nina majibu ya hao watu ambao magazeti  
ya msimu yako mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ili kukomesha mchezo huo, kama wewe una gazeti unalitumia kila mwaka basi wewe huisha uchapishaji wake ni uchapishaji tu lakini bado leseni unakuwa bado unayo, uchapishaji wake ambao kila mwaka lazima useme mimi nina dhamira ya kuendelea kuchapisha mwaka huu, kuna shida gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devota.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba nitoe hoja iungwe mkono. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devota watu wengi hizi kanuni hamzisomi, huna haja kutoa hoja wala una haja ya kuungwa mkono, wewe endelee tu kama kuna mtu mwingine anaruhusiwa kusimama *much as* wewe umesimama, mnashindwa kuzielewa hizi kanuni.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mimi nasema nawajengea hoja ninyi, tulieni. Nasema, mara nyigi Wabunge wote wanafikiri kama hakutoa hoja hamna fursa ya kuchangia; si hivyo, hata kama hakutoa hoja akisimama ye ye na wewe unaruhusiwa kusimama.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mnaona mmezoa fujo basi hata hamjielewi wakati mwingine. Haya, Mheshimiwa Salome, Mheshimiwa Jitu na Mheshimiwa Anatropia. Tunaanza na Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Devota Ninja. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri anasema hoja yao ya kutaka ku-renew magazeti eti ni kuangalia magazeti ambayo yanaendelea kufanya kazi. Hapa kuna ajenda imejificha. Kama inavyofanyika kwenye

makampuni, kwa nini wasifanye kuwe kunafanyika *annual return* yaani ripoti ya mwaka ya magazeti kupeleka Wizarani ili kutoa taarifa kwamba sisi tumeendelea hivi changamoto zetu ni hizi, tunatamani tupate msaada wa Wizara namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ajenda hapa ya kusema kwamba wanataka kuangalia utendaji kazi wa magazeti, ajenda iliyojificha ambayo sisi tunaiona hapa ni kutaka kufungia magazeti ambayo yanaipinga Serikari. Hilo limefanyika mahali pengi na tumetoka kulalamika, kwamba gazeti ambalo linaonekana linaisifu Serikali hilo gazeti hata kama linaandika taarifa mbaya kuhusu upinzani au viongozi wa dini halishughulikiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti linaloshughulikiwa ni lile ambalo linaandika kinyume. Hata kwenye mitaandao makosa ya mitandao watu wanaotoa maoni mbadala kwa Serikali wanashughulikiwa; lakini wale wanaoisifu; tumeshtaki mara nyingi na hata kwenye Bunge hili tumesema kuna watu wanatuchafua kwenye mitandao, kuna watu wanatukana viongozi wa upinzani hawashughulikiwi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ajenda hii ya kusema kwamba wanafanya hivyo kwa ajili ya *regulate* magazeti ambayo yako *dormant* siyo kweli, kinachofanyika hapa ni kujaribu kuzuia. Ahsante (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nadhani hapa Waziri awe *very clear* kwamba kuna magazeti tunayalenga, kuna na magazeti tunayaacha ili yaweze kutusaidia kuchafua watu kadha wa kadha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *annual returns* naongelea kama alivyosema Mheshimiwa Salome kama akiongelea hapa itakuwa ni sahihi sana. Hata hivyo, kusema unampa mtu leseni ya muda mrefu halafu baadaye kila baada ya

mwaka mmoja, huo ni usanii na lengo kubwa ni kuondoa baadhi ya magazeti ambayo wanaona yanawakwaza. Magazeti kama Jamvi la Habari, Tanzanite, hatuoni yakionya, hatuoni yakiguswa na badala yake tunaona kama yanapongezwa kwa kazi mbovu inayofanyika kila siku ya kuchafua watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri, ye ye ndiye anasema anajua sana haki ya watu kupata habari; na alivyokuwa anaongoza Mawaziri kujibu taarifa ya CAG alisema wanatumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kujieleza; vivyo hivyo atumie Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuyaacha magazeti yafanye kazi yake badala ya kuwaingilia, badala ya kuwachomoa na kuwaingiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikasema hiyo ni *system* ya chomoa, ingiza, weka, *edit, paste*, magazeti yanayoisisia CCM, magazeti yanayopambana na upinzani ni sahihi, lakini magazeti yanayoisisia CCM ndiyo magazeti ambayo ndiyo yanatakiwa yawepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na naunganana na hoja ya Mheshimiwa Devota. Kimsingi ni kutaka *ku-filter* haya magazeti yale yote ambayo yanajaribu kuikosoa Serikali; na naomba Serikali hapa isiwe *double standard*. Nimemsikia mara Waziri wa Mambo anasema hata nchi zilizoanzisha demokrasia huko haziruhusu mikutano, lakini kwa nini hamjifunzi kwa nchi hizo hizo mlizojifunza hiyo kuzuia mikutano ambayo wao wanadiriki kusema kwamba waandishi wa habari muhimu namba nne? Tumeona mataifa makubwa ambao wanakubali kukosolewa na mhimili mwингine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sheria inapanga kabisa kudhibiti upinzani na naomba hili suala lieleweke kabisa,

kwamba sisi kama Serikali mbadala mawazo yetu lazima yapitie kwenye vyombo vyahabari... (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ninyi ni Serikali mbadala?

**MHE. PETER MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo *unless utuambie kwamba hii siyo Westminster ya Bunge hili ni Bunge la Westminster na sisi hapa ndio Government on wait unless tumepingana na katiba hiyo ndiyo maana hatueshimiwi hapa kama tunafuata Westminster.*

**MWENYEKITI:** Endelea na mchango wako Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. PETER MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nachangia hivyo. Sisi ni *Government on wait* tunatakiwa tuheshimiwe tutoe mawazo yetu, lakini vyombo vyote ambavyo vimekuwa vikitoa maoni yetu mbadala vinadhilita, *TBC ambacho ni chombo cha humu amesema mwenyewe Mheshimiwa Waziri kwamba wanafanya hivyo kwenye television, TBC kimegeuka kuwa kiperushi cha Chama cha Mapinduzi, kuanzia asubuhi mpaka jioni anaongea Mheshimiwa Polepole kukashifu wapinzani, vile vyote mnadhibiti.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi *television* za watu binafsi tukipeleka taarifa za mawazo mbadala wanazidhibiti. Kwa hiyo sheria hii Mheshimiwa Waziri kama kweli wanataka mawazo mbadala ili waonekana wanavyofanya kazi; siku zote tumesema hapa, sisi ni kioo na ukimya huu wa Bunge wa Chama cha Mapinduzi nao wanaona wanakubaliana kwa sababu ni kweli mnadhibiti vyombo vyahabari upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri huo utaratibu ubadilishwe; kama katiba inavyosema maana inakiukwa, hebu turuhusu huu... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jitu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nitofautiane na hoja ya Mheshimiwa, kwa sababu kama tulivyo kwenye biashara yoyote ile tunajua kabisa kwamba unapata leseni *next year* una *renew*; hata vibali mbalimbali na kila mwaka kutakuwa na ada ndogo. Pamoja na hiyo utakuwa unaleta *performance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna hoja kwamba kuna gazeti fulani limefungiwa kimakosa, wote si tumo humu ndani, si tuje tulitete, tusimame kwa kanuni? Halafu hata hii wakati inapitiwa tungeikuta kwenye hii taarifa ya Kamati, taarifa ya Kamati ingeleza kwamba hoja hii hawakubaliani nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kabisa kila jambo liwe linakuwa *censored*. Hata duniani kote hakuna leseni ya kudumu kwamba ukishakata jambo fulani inakuwa ni ya kudumu. Mambo *annual returns* ni sahihi, kabisa kwenye makampuni unakataa leseni ya biashara lakini *annual returns* unalipa, usipopeleka *annual returns* unafutiwa, lakini pia na leseni ya kila mwaka iko palepale. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala la leseni kama unafanya kazi yako vizuri weka *constructive criticism* hukatazwi kabisa, lakini ukienda kinyume na maadili, ukienda kinyume na masuala mbalimbali ambayo tunapigia kelele kwenye hii mitandao ambayo inawekwa hata sisi wote tunapiga vita, si suala la Serikali peke yake sisi wenyewe hatutaki mambo hayo; jenga *constructive criticism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona watu wanajenga hoja vizuri na inakubalika? Naamini kabisa kila mmoja, hata kwa upande wenu tungakuwa tunafanya *constructive criticism*, si kulaumu tu lakini ingekuwa tunajenga hoja pia ya kutoa mawazo mbadala; huwa sioni mawazo mbadala naona ni kulaumu tu, kila siku ni kulaumu toeni mawazo mbadala halafu tuone nini kinafanyika, naamini tutafanikiwa. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI, NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kama nilivyosema mwanzoni, kwamba hatuna ajenda kama Mheshimiwa Salome Makamba alivyosema hapa ya kufungia magazeti fulani ndiyo maana tumekuja na utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, sheria hii imepishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano hapa hapa mwaka 2016 wote mkiwepo. Ni aibu sana leo Mheshimiwa Mbunge unasimama unasema hii ilikuwa na lengo fulani wakati wewe mwenyewe uliipitisha. Sasa lete mabadiliko ya hii sheria tuweze kuyajadili, lakini siyo unatoka tu hapo kwa sheria mliyotunga wenyewe mnaanza kusema kwamba ilikuwa na lengo fulani baya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize, hivi Mawakili ambao kila mwaka pamoja na kwamba wamesajiliwa kama Mawakili, kila mwaka lazima *wa-renew practice license* bila kufanya hivyo huingii mahakamani; nao kuna mchezo hapo wa *control*. Jamani! hao ndiyo mabingwa wa sheria hawalalamiki leo nyie mliopitisha sheria yenu yenu wenyewe mnalalamika. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Devota.

**MHE. DEVOTA W. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kabisa, Mheshimiwa Waziri nimemsikiliza lakini ikumbukwe kwamba haya magazeti kusajiliwa ni kwa mujibu wa sheria, lakini pia ndiyo maana wakati wa kuhitimisha hajaweza kunipa ufanuzi kwa sababu nilimwambia Mheshimiwa Waziri kwa nini wanapata kigugumizi cha kuanzisha yale mabaraza ambayo kwa mujibu wa kanuni yatakuwa mabaraza mojawapo ya ithibati na yale mengineyo ambayo kazi yake ni kucheki hiyo mienendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa kama kuna hayo mabalaza ambayo yanapaswa kuwepo ambayo

yataangalia vyombo vya habari na utendaji wake wa kazi kunakuwa na haja gani kama watu wanalipwa, huku mnawataka wajisajili kila mwaka wakati suala la kupata habari na taarifa lipo kwa mujibu wa Katiba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalionia kama ni utaratibu ambao unataka kuhakikisha unakata mikono vyombo vya habari, ni mkakati madhubuti kabisa wa kutisha vyombo vya habari. Mathalan wale wandishi ambao wataandika habari za kuikosoa Serikali wanakuwa mashakani, kwa maana hawana uhakika wa leseni yao ku-renew tena kwa mara nyingine. Hii vile vile... (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devota muda wako unakwenda kipindi hiki sasa mimi ndiye ninaye-*control*, sasa wewe kubali *either unaing'ang'ania shillingi au unamrudishla shillingi*. Waziri amekueleza vizuri sana, hii ni sheria wala hakuitunga yeye, Bunge ndilo limetunga sheria hii. Kama unaona sheria hii haifai unao wajibu wa kuleta *amendment* ili Bunge iljadili vinginevyo, *simple as that*. Sasa ni mawili unaishika shillingi yake au unamrudishia? Umemsikia kasema masharti anayokwenda nayo sasa hivi.

**MHE. DEVOTA W. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaendelea kuishikilia kwa sababu hii haipo kwenye sheria... (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DEVOTA W. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *regulations* ambazo wameziweka. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Basi kaa, Waheshimiwa sasa nitahoji wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Devota waseme ndiyo, wasiokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Devota waseme siyo. Hoja yako imekufa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja illamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto, hayupo. Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna timu zetu za Taifa ambazo ni za *football*, lakini vile vile tuna timu zetu za Taifa za mashindano ya Jumuiya ya Madola na *Olympic*; lakini Wizara yetu hii pamoja na mambo mengine inasimamia mambo yetu ya michezo, sanaa na utamaduni. Katika bajeti ya Waziri, sioni namna gani Serikali inagharamia timu zetu zinazowakilisha nchi na kupelekea wakati mwingine tuna miaka 20 kwenye soka hatujafika *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwenye Olimpiki hatupati medali kwa sababu wanainglia hakuna maandalizi, hamna kambi, wanakata tamaa. Namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze sasa Serikali inatuhakikishia vipi kugharamia timu zetu za Taifa ili tuweze kupata medali na asipofanya hivyo naweka nia ya kukamata shilingi ya Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mtulia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka Serikali ifanye kila kitu kwenye michezo sidhani kama hiyo nchi unaweza kuipata duniani hapa. Ni kwamba kwa mfano, michezo ya *Common Wealth* ni michezo ya kiserikali, naomba nthibitishe kwamba ni Serikali ambayo imewapeleka wanamichezo kwenda *Common Wealth-Australia*. Tuna *All African Games* ni michezo ya Serikali, michezo hiyo huwa inagharamiwa sehemu kubwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye michezo kwa mfano ya mpira sisi tunatengeneza tu ile *enabling environment*

kwa sababu vyama vilivyopo vya mpira kwa mfano wa miguu vinapata pesa ya kutosha na vinapokwama vinatufuata. Tuna matatizo hapa Tanzania kwa sababu tulifanya mambo ya hovyo hovyo kidogo, tukasimamishiwa pesa ambayo kila chama cha mpira au Shirikisho la Mpira Duniani kinapata, mwanachama wa *FIFA*, sisi tumefungwa kwa ajili ya miaka minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na kifungo cha miaka minne basi isianze kulaumiwa Serikali kwamba kwa nini haioneshi hapa sasa kwamba itatoa pesa kwa Simba, Yanga kwenda huku, hapana, hiyo hatuwezi kupanga namna hiyo kwa sababu utaratibu wa timu au michezo ambayo sisi tunaigharamia uko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokwenda Olympic, *Rio de Janeiro*, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge ni kwamba Serikali iligharamia ile safari vile vile ya wanariadha wetu ambapo Simbu aliweza kushika nafasi ya tano kwenye olimpiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwamba timu ya Taifa mfano ya mpira wa miguu (*Taifa Stars*) anataka Mheshimiwa Waziri kwamba twende tukacheze na kugharamiwa na Mashirika ya Kimataifa ya *FIFA* ilihali sisi tunatoa bendera zetu, hivi mpira wetu sisi Tanzania ataugharamia nani kama Serikali inashindwa kugharamia angalau timu zake za Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono ili Serikali ijue hili ni jukumu lake la msingi, wahakikishe timu zetu hizi zinapata bajeti na Wizara inapotenga bajeti yake iweke na bajeti ya kugharamia timu zetu ili tupate mafanikio kama nchi nyingine.

**MWENYEKITI:** Anza mwenyewe kuchangia.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nayasema haya, mimi nimezungumza na viongozi wa *TFF* lakini nilizungumza nao kwa ajili ya kutaka kuuliza tu kwamba gharama ya timu yetu kwenda kucheza tu mechi za *trial* kwa mwaka, Timu ya Taifa *Stars* inafika mpaka bilioni mbili, bilioni tatu kama tunakwenda mechi za mbali kama vile Algeria na kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu tu ya timu za Taifa (*Taifa Stars*) hujazungumzia Ngorongoro, hujazungumzia *Olympic*, hujazungumzia timu ya Madola. Sasa ninachokiomba kwa mtazamo wangu, Serikali tusifanye mambo ya kubahatisha. Katika bajeti ya Waziri kwenye utekelezaji wa kazi zake tutengete fungu angalau kwa ajili ya timu yetu ya Taifa ili iweze kufanya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tukitegemea, Congo juzi wamekuja kucheza na sisi hapa wamepewa Dola milioni moja...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi, jiandae Mheshimiwa Mwamoto

**MHE. COSSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maulidi ana hoja ya msingi kwa maana ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Waziri anasema Serikali haiwezi kubeba mzigo wote huu katika ujumla wake, lakini tukumbuke kwamba hizi timu zinapokwenda tumeshaziita ni Timu ya Taifa iwe inakwenda Madola, iwe inakwenda timu ya mpira wa miguu haiendi kama vile *TFF Stars*, hapana, ndiyo maana inaitwa Taifa *Stars*. Kwa hiyo, nadhani kwamba ushauri wa Mheshimiwa Maulid Mtulia tunapozungumzia dhana nzima ya michezo kwamba kama ni sehemu ambayo inakuwa pia ni chanzo cha ajira, chanzo cha mapato, unaanzaje kutangaza Taifa katika

masuala ya utalii? Ni pamoja na timu kufanya vizuri, unafanyaje vizuri? Ni pamoja na kuandaliwa vizuri, unaandalilwaje vizuri? Ni pamoja na kuwa na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani Waziri pengine alichukue hili na ufile wakati kwamba Serikali iwe kiasi fulani inatenga kwa ajili ya kuhudumia timu za Taifa. Kwa hiyo Mheshimiwa Mtulia nimwombe kwamba amrejeshee Mheshimiwa Waziri shilingi lakini Waziri ajipange kwa wakati ujao kuweka fedha kwa ajili ya timu za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Mheshimiwa Mtulia lakini nimwombe amuachie Mheshimiwa Waziri shilingi kwa sababu tumesema waangalie chombo ambacho kinasimamia michezo. Kwa mfano, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), ile sheria iliyopitishwa inatakiwa ibadilike, iletwe hapa tuibadilishe ili Baraza la Michezo sasa liwe lina fedha ya kutosha kwa maana ya kulibadilisha muundo wenyewe, kwa sababu sheria zile zimepitwa na wakati bila kufanya hivyo itakuwa ni shida na pia tuangalie uwezekano wa kumwongezea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na kusema kwamba tunafanya vizuri kwenye timu zetu za Taifa, lakini bado unahitaji upate maandalizi ya kutosha na fedha za kutosha. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mtulia amwachie Mheshimiwa Waziri shilingi yake ili twende mbele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa michango yote na nimwombe Mheshimiwa Mtulia ambaye anasema ameongea na viongozi wa *TFF*. Mimi nina uhakika alipoongea na viongozi wa *TFF* hajauliza Serikali inatoa

mchango gani katika kufanikisha masuala ya mpira. Nitoe mfano mmoja tu; safari ya *DRC* ya Ngorongoro *Heroes* bila Serikali isingefanikiwa kwa sababu kama imefadhiliwa na Mamlaka ya Ngorongoro ile ni mamlaka ya Serikali siyo lazima iitwe Wizara ya Habari, *facilitation* tunaifanya sisi kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema hili suala ni suala ambalo ni pana na sisi tunaelewa, tutafanya nini katika mazingira mbalimbali lakini nikuhakikishie tunaleta kwa mfano, mwezi wa Sita, kuna mabadiliko ya Sheria ya BMT, Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono, hiyo nayo ni sehemu moja ambayo inatusaidia sisi tuweze kupata pesa kuingia BMT kuitia michezo ya kubahatisha ambayo hatupati senti tano mpaka sasa. Sasa hayo ndiyo maeneo ambayo wanaweza kutusaidia ili tuweze kusaidia zaidi na zaidi timu zetu za Taifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtulia umeombwa urudishe shilingi ya Waziri

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme yafuatayo halafu nitoe uamuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia Mheshimiwa Waziri suala la michezo, sanaa, utamaduni kwetu sisi watu wa Dar es Salaam ni ajira na si suala la michezo kama watu wanavyofikiri. Ukitikia habari, tuna vyombo vya habari vingi sana Dar es Salaam, ukisikia utamaduni tunaufanya sana, ukisikia sanaa na michezo pale ndiyo nyumbani kwao. Kwa hiyo suala hili anapouliza Mbunge kama mimi wa Kinondoni namaanisha na nategemea Mheshimiwa Waziri mwakani atakuja na jambo hili kwenye bajeti yake, hatutaki suala la kubahatisha. Namrudishia shilingi yake kwa ahadi kwamba mwakani asipokuja na bajeti inayoonesha tutaonana hapa.

**MWENYEKITI:** Ahsante na umevaa koti zuri leo.  
(*Kicheko*)

Mheshimiwa Mtata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nionyesha masikitiko yangu kwa Waziri kwa sababu nimechangia kwa maandishi na nimezungumza suala ambalo linahusu utendaji kazi wa *COSOTA* lakini hajanijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya *COSOTA* inaielekeza *COSOTA* na inatoa utaratibu wa muda wa kugawa ile mirabaha ambayo *COSOTA* imekusanya kwa ajili ya wasanii. Mirabaha hii *COSOTA* wamepewa mamlaka ya kukusanya kwenye taasisi mbalimbali kwenye *radio*, kwenye *TV* ama hoteli na maeneo mengine; lakini sasa hivi imeshakuwa muda mrefu *COSOTA* hawagawi mrabaha huo kwa wasanii. Ukiwaliza, wanasema mashine ambayo inatambua *ratio* yaani mgao wa fedha hizo mtaalam wake hayupo mpaka atoke *Swiss* na imeshakuwa muda mrefu. Kwanza inashangaza, ina maana kweli Tanzania hatuna mtalaam wa kuweza kutambua au kutumia mashine hiyo mpaka sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri alete ufanuzi, hizo fedha ambazo *COSOTA* wamekusanya kwa miaka mingi na naomba ku-*declare* mimi pia ni mnufaika wa makusanyo ya mrahaba huo; ni miaka mingi imepita wasanii hawapati, hizo pesa ziko wapi na zimeshakusanya kiasi gani? Kwa nini zisitoke? Naomba ufanuzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Martha Mlata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala analoliongelea ni moja ya changamoto ambazo tunazipata sasa kwamba *COSOTA* iko chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na haiko chini ya Wizara yangu, sasa tunapigana sasa hivi tuweze kuirekebisha hiyo hali. Naomba nikiri kwa Mheshimiwa Mlata kwamba hili analolisema ndilo nalisikia kwa mara ya kwanza,

naomba nilibebe niweze kukaa na Waziri mwenzangu niulize kwa nini imetokea hali hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlata hukutoa shilingi hoja yako imekufa, imekwisha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitoi nataka tu nishukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ili mradi ameshasema, ameshakujibu wewe sasa umeshakuwa *redundant*, sasa nakuomba ukae chini. Haya mishahara ya Waziri imekwisha, Mheshimiwa Naibu Waziri. Hii nyimbo jamani hii nyimbo ya mpira na sisi tunafurahi mpirani, anatajwa Kichuya, anatajwa Msuva tatizo ni nini? Hebu tuambie Mheshimiwa Waziri mwanaume mashine ikoje?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kufafanua wimbo ambao umeimbwa na Msagasamu unaitwa Mwanaume Mashine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeonyesha kwamba una *interest* kubwa sana ya kuweza kujua kwa sababu gani huu wimbo umefungiwa; mimi niseme kitu kimoja kwamba wimbo wa mwanaume mashine haujafungiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kaa chini imekwisha. (*Makofi/ Kicheko*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002-Finance and Accounts .....	Sh.331,978,000/=
Kif.1003-Policy and Planning.....	Sh.367,680,000/=
Kif.1004-Government Communication Unit....	Sh.111,427,000/=
Kif.1005-Proc. and Mgnt Unit.....	Sh.178,705,000/=
Kif.1006-Internal Audit Unit.....	Sh.112,139,000/=
Kif.1007-ICT Unit.....	Sh. 276,476,000/=
Kif.1008-Legal Service Unit.....	Sh.90,924,000/=

*Kif.6001-Culture Development Division.....Sh.3,951,416,000/=*  
*Kif.6002 – Youth Development Division.....Sh.0/=*  
*Kif.6004-Sports Development.....Sh.2,253,492,000/=*  
*Kif.7003-Information Service.....Sh.12,921,485,000/=*

*(Virfungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 96-Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

*Kif.6001-Culture Development Division.....Sh.1,000,000,000/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika *sub-vote 6001* kwenye *Cultural Development Division*, kwenye miradi ya maendeleo hapa tunaona kwamba *Rehabilitation of Bagamoyo College of Arts*. Tunafahamu umuhimu wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo na hapa ndipo ambapo pia tunapoweza kuwajenga vizuri wasanii wetu. Katika mwaka huu wa fedha hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya Chuo cha Sanaa Bagamoyo; sasa naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwa nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri sanaa zero zero.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hatujatenga pesa ya maendeleo kwenye Chuo cha Bagamoyo kwa sababu mwaka jana tulikuwa ni kipindi ambacho tumefanya mabadiliko makubwa pale Chuoni *in terms of development*. Vile vile tulikuwa tunajiruhusu mwaka huu kutokana na ufinyu wa bajeti na *ceiling* tulizonazo tuweze kupeleka pesa nydingi zaidi *TBC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya pesa yote ya *development* sasa hivi ambayo tumepangiwa Wizara ya

Haari inakwenda *TBC*, kuna umuhimu ambao Waheshimiwa Wabunge wameonyesha kuhusu umuhimu wa *TBC*. Tutaangalia mbele ya safari jinsi ambavyo na sisi tutaangalia namna ya...

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif.6004-Sports Development.....Sh. 1,650,000,000/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kwa mamlaka ya kiti...

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Kifungu 6523...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri kwanza. Kwa mamlaka ya Kiti naongeza nusu saa. Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba *sub-vote 6523* ambayo inahusiana na *National Sports Complex* ambayo ni kile Kijiji Dar es Salaam lakini hapa wamesema pia na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua umuhimu wa michezo nami kwa kuwa niko kwenye Kamati ya Huduma za Jamii kitu cha msingi ambacho nataka kuuliza ni kwamba mwaka jana tulitenga bilioni moja na milioni mia nane na ishirini, lakini mpaka mwezi Machi zilikuwa zimeenda shilingi milioni mia sita sabini na tisa tu, sawa na asilimia 37 na mwaka huu tena wanatenga shilingi bilioni moja na milioni mia tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la msingi ni kwamba, kama mwaka jana wameshindwa kupeleka hela kwa asilimia hiyo ndogo, je, kwa tengeo hili wanataka kutuhakikisha kwamba fedha hiz zitakwenda ili vijana wetu waweze kushiriki kwenye michezo kikamilifu? Kwa sababu

naamini kabisa viwanja hivi viwili au kile Kijiji cha Dar es Salaam na hapa Dodoma itasaidia sana kuinua viwango vyta michezo vyta watoto wetu, je, hizi hela zilizotengwa zitakwenda au zitakuwa kama za mwaka jana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nijibu hoja ambayo amei-raise Mheshimiwa Susan Lyimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ni kweli kwamba katika bajeti ya marekebisho ya uwanja wa Taifa ya mwaka jana imepungua. Hata hivyo, ambacho tunajitahidi kufanya sisi kama Wizara ni kuangalia zaidi ni kutenga bajeti ambazo zinakuwa kiuhalisi zaidi. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kumhakikishia Mbunge kwamba hii fedha ambayo imetengwa ambayo ni bilioni 1.5, nimhakikishie kabisa Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hii tuna uhakika kabisa kwamba katika mwaka huu wa fedha, fedha hii itatolewa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa inafanana na ya Susan Lyimo kwa hiyo na-withdraw.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 7003-Information Service.....Sh.6,050,000,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Mtoa hoja.

## TAARIFA

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Mapendeleko ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuyapitisha. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makof)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono sasa nitawahoji.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda na bajeti imepita.

Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wako pamoja na timu yako uliyokuja nayo hapa na una timu nzuri sasa ya BMT, Tenga ni mtu mzuri sana, Karia ni *President* mzuri wa *TFF*. Kwa hiyo nategemea sasa mabadiliko makubwa sana yatapatikana kwenye mpira na kwenye michezo nchini mwetu. Pia nawapongeza Wabunge kwa michango yenu, kwa ukomavu wenu, kwa kuelewa na Kiti kimeridhika na nyimbo ambayo itaimbwaa Jumapili itaimbwaa, kwa hiyo tunashukuru sana.

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu Saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 30 Aprili, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*

